**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 20 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mbele yetu leo tuna wageni wengi, wengine ni wageni wa kawaida ambao wanaruhusiwa kuja hapa Bungeni. Lakini nitawatangaza wachacha tu. Tuna Wabunge, wa Bunge la Afrika Mashariki wako pale wasimame, ambao ni Mheshimiwa Hafidha Ally Khamidy, Mheshimiwa Kate Kamba, Mheshimiwa Hulda Kibacha na Mheshimiwa Noman Sigara.

Wakati huo huo tunao wanafunzi ambao ni viongozi wa umoja wa wanafunzi wa Vyuo Vikuu Duniani. Wao ni viongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wamekuja hapa kwa ajili ya kujaribu kutafuta fedha kwa ajili ya kuendesha mkutano wa umoja wa *World Universities* ambao utafanyika Dar es Salaam, kuanzia tarehe 13 Agosti, 2006. Kwa sasa wanajaribu kutafuta *resources* hapa na pale. Wanaongozwa na Ndugu Edward Mgelea, akiwepo na Ndugu Leonard Kiswaga, Ndugu Suzan Bundala na Ndugu George Liego.

Sasa hii ni Kamati ya Uongozi, lakini umoja wao watakuwa na Mkutano wa Umoja wa Vijana wa Vyuo Vikuu Duniani kote, na wao wakiwa wenyeji wao.

Kwa hiyo, sasa hivi ziara yao ni kutafuta *funds* kokote kunakohusika, pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Spika ataongea na nyie wakati muafaka. Baada ya kusema hayo tunaendelea na *Order Paper*. *(Makofi)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:**

Taarifa ya Mwaka wa Hesabu za Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka Ulioishia Juni, 2005 *(The Annual Report and Accounts of the National Environment Management Council (NEMC) for the year ended June*, 2005)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 242

**Daraja la Losavana – Siha**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH (K.n.y. MHE. AGGREY D. J. MWANRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa kijiji cha Kashashi na cha Manio katika Jimbo la Siha wamekuwa wakitaabishwa sana na tatizo la daraja la Lasavana ambalo halipitiki wakati wa mvua na kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Hai imewataka wananchi wa vijiji hivyo wachangie gharama za utengenezaji wa daraja hilo lakini wanashindwa kufanya hivyo kwa sababu wanatakiwa pia kuchangia shule ya sekondari ya Suumu na zile shule za msingi zilizopo katika maeneo hayo:-

Je, ni kwa nini Serikali isishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Hai katika ujenzi wa daraja hilo hasa ikizingatiwa kuwa linachangia sana katika kukuza uchumi kwa upande wa zao la Kahawa na lile la Ndizi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Losavana – Siha linaunganisha Vijiji vya Lawate na Kashahi ambavyo vipo katika Kata ya Siha Mashariki. Daraja hili ni muhimu kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Vijiji vya Lawate kwa kuwa linawaunganisha na soko la Lawate ambapo huuza mazao yao kama vile mahindi na ndizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama zinazotakiwa kukamilisha ujenzi wa daraja hilo ni shilingi milioni 38. Halmashauri kwa mwaka 2006/2007 imetenga shilingi milioni 20. Fedha hizo zitapatikana kutoka *Local Government Capital Development Grant* (*LGCDG*) na ujenzi utaanza baada ya mvua zinazoendelea kunyesha kukatika.

Aidha, kwa kuwa daraja hili ni la Kata ya Siha, ujenzi wake umeingizwa kwenye mpango wa maendeleo wa Kata. Wananchi hadi sasa wameshakusanya vifaa vya ujenzi kama vile mchanga, mawe pamoja na nguvu kazi yenye thamani ya shilingi milioni 2. Kwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Hai inaendelea kushirikiana na wananchi wa Kata ya Siha kuimarisha kivuko cha muda kinachotumiwa na wananchi wa Vijiji vya Lawate na Kashashi. *(Makofi)*

Na. 243

**Uundaji wa Mamlaka za Miji Midogo**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilishaahidi Bungeni kuanzisha Mamlaka za Miji midogo ikiwa ni pamoja na Miji Midogo ya Kongwa, Kibaigwa, Mlali na Mkoka, Wilayani Kongwa na kwa kuwa hadi sasa jambo hilo halijafanyika:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hili?

(b) Je, mgao mpya wa Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji nao Unasubiri nini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndugai, Mbunge wa Kongwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imeahidi kuanzisha Mamlaka za Miji Midogo nchini. Aidha, Miji Midogo ya Kongwa, Kibaigwa, Mlali na Mkoka imetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 20 la tarehe 4/2/2000 kuwa Miji Midogo.

Miji midogo ya Kongwa na Kibaigwa imepandishwa hadhi kuwa Mamlaka ya Miji kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 353 la tarehe 17/9/2004. Mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Miji hiyo miwili umeanza kwa kufanya yafuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira na Mwanasheria wa Halmashauri ya Kongwa wamefanya ziara katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa kujifunza uanzishwaji wa mamlaka za Miji Midogo mwezi Julai, 2005.

Baada ya ziara hiyo hoja za uanzishwaji miji hiyo ilijadiliwa katika Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya Halmashauri na kuwasilishwa katika Baraza Kuu la Madiwani mwezi Machi, 2006. Baraza limeazimia kuanzisha kwanza Mamlaka ya Mji wa Kibaigwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi yangu imepokea maombi ya kuanzisha Kata 8, Tarafa na Vijiji toka Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa. Uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala inahitaji gharama kubwa. Hivyo gharama zake, Kata mpya za Mkoka, Ugogoni, Mkinga, Kibaigwa, Moleta, Chamae na Chamkoroma, zitaanzishwa hapo hali ya fedha ya Serikali itakapokuwa nzuri. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na ya kweli. Kwa kuwa katika maelekezo ambayo TAMISEMI wameyatoa, kwa Halmashauri za Wilaya, ikiwa ni pamoja na wilaya ya Kongwa kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka za miji midogo. Maelekezo yale yanaelekeza kwamba Mwenyekiti wa Mamlaka hiyo awe ni mmoja wa wenyeviti wa vitongoji, jambo hilo linamwondoa Diwani, linaondoa Wodi C iliyokuwepo Diwani anabakia kuwa mwalika tu.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba iko haja ya kuangalia upya maelekezo hayo ili ikiwezekana Diwani ndiye awe Mwenyekiti wa Mamlaka hiyo ndogo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria kama ilivyo sasa sheria namba 7 ya mwaka 1982, Mwenyekiti wa Mamlaka ya mji mdogo ndiye anakuwa Mwenyekiti ambaye anatokana na wale wajumbe ambao ni wenyeviti wa vitongoji.

Lakini madiwani si kwamba wanaondolewa katika zoezi zima la kushirikishwa katika mamlaka hiyo. Ukisoma sheria hiyo hiyo inaeleza bayana kabisa kwamba watakuwepo madiwani ambao watakuwa wamechaguliwa kutoka miongoni mwa Baraza la madiwani, ambao wanatokana na eneo hilo ambako Mamlaka ya mji mdogo imeanzishwa.

Lakini kamwe na mimi nafikiri si sahihi kabisa kumfanya Diwani sasa kuwa ndio Mwenyekiti ya Mamlaka wa mji mdogo kwa sababu walengwa pale ni wale Wenyeviti wa vitongoji. Hata hivyo, naomba kuliharifu Bunge lako Tukufu kwamba Sheria hiyo hata hivyo kwa sasa inatazamwa, ili tuweze kufanya marekebisho yatakayoweka bayana mambo ambayo bado yanaonekana kama vile hayako wazi.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, kwa kuwa tangazo hili la kuanzisha miji midogo nchini limejumuisha mji wa Kongwa na miji mingine mingi tu Tanzania ikiwemo kwa mfano mji mdogo wa Nzega, Kahama na Mpwapwa.

Je, kwanini Serikali inashindwa kusema neno moja tu ili hii miji iweze kuwa Halmashauri kamili na kuzipatia pesa kama ambavyo inakuwa na fedha katika Halmashauri zingine za Wilaya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA M ITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naheshimu sana mawazo ya Mheshimiwa Selelii na amekuwa kwa kweli akiomba mara nyingi, mji wake uweze kupandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji. Sasa ninachoweza kumwahidi tu kwamba tuko kwenye mchakato huo na pengine nimwahidi tu kwamba kwa upande wa mji wake nina hakika kabisa utatangazwa kwa sababu ni kati ya miji michache tuliyoilenga.

Na. 244

**Vivutio vya Utalii Mwambao mwa Ziwa Nyasa**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa ni sera ya Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania ili kupunguza msongamano wa watalii na uharibifu wa mazingira sehemu za Kaskazini mwa Tanzania:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa kuna vivutio vizuri sana vya utalii katika mwambao wa Ziwa Nyasa na hasa katika maeneo ya Wilaya ya Ludewa?

(b) Je, ni lini na kwa utaratibu gani vivutio hivyo vitaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Wizara yangu ni kuendeleza utalii nchi nzima. Hata hivyo kwa sababu ya ukubwa wa nchi yetu tulilazimika kuanza uendelezaji kwa kanda kufuatana na mpango kabambe wa uendelezaji utalii ulioandaliwa mwaka 1996.

Kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1990 Wizara imeelekeza nguvu zake katika kutangaza vivutio na kuvutia wawekezaji Kanda ya Kusini. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa wa Iringa na Wilaya ya Ludewa imeainisha vivutio vya Utalii na kuviorodhesha. Katika zoezi hili tumebaini kuwa kuna vivutio vizuri sana vya utalii katika mwambao mwa Ziwa Nyasa na katika maeneo ya Wilaya ya Ludewa. Vivutio hivyo ni pamoja na Mandhari ya kuvutia, fukwe nzuri, samaki wa mapambo na safu za milima ya *Livingstone*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vivutio vilivyoko mwambao mwa Ziwa Nyasa na Wilaya ya Ludewa vimekwisha ainishwa na kuorodheshwa, hatua inayofuata ni kuvitangaza kupitia Bodi ya Utalii, Balozi zetu za nje na Mawakala katika nchi mbalimbali.

Aidha, ni imani ya Wizara yangu kuwa matengnezo ya barabara kuu yanayoendelea nchini pamoja na ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Songwe yatachangia kwa kiasi kikubwa katika kurahisisha usafiri na kazi ya kukua kwa utalii Kanda ya Kusini hususan mwambao mwa Ziwa Nyasa na maeneo ya Wilaya ya Ludewa.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru majibu yanaridhisha, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa vile vivuti hivyo vimehorodhoshwa na vinajulikana na Wizara imeanza kuvitangaza, na hasa hivyo vya Kusini, lakini kwa vile wawekezaji na hasa sekta binafsi wanakuwa wazito, wanasita kuwekeza kule, bila shaka hawana uhakika kwamba miradi yao uwekezaji wao utakuwa endelevu. Je, si busara kwa Wizara na Taasisi zake kuanza zenyewe kuwekeza huko, ilikuwavutia na kuonyesha mfano na kisha wakishajiingiza sekta binafsi Wizara ikajitoa?

(b) Kwa kuwa Naibu Waziri amezungumzia suala la samaki wa mapambo, kwa sababu uvunaji, uvuvi unaoendelea wa samaki hao katika ziwa Nyasa, nitaita ni holela, na bila shaka wenzetu wa ziwa Nyasa nao wanavua samaki hao, na hatujui kuna samaki kiasi gani, uwezekano wa kuwamaliza samaki wale ni mkubwa na wanafaida kubwa sana. Je, Wizara haioni umuhimu wa kusitisha kutoa ruksa au vibali vya kuvua samaki hao mpaka *assessment* ya uwingi na mazaliano ya samaki hao ijulikane?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema kweli wawekezaji mpaka sasa wameonesha ari na nia ya kuwekeza katika maeneo ya ukanda wa Kusini. Mimi nilikwenda Dubai, mwezi Mei, ambako kulikuwa na *Conference* iliyokuwa inahusisha wawekezaji katika masuala ya utalii na palikuwa na kampuni tatu ambazo zimeonyesha nia kabisa ya kuja kuwekeza, hasa katika Ukanda wa Kusini. Lakini vilevile Wizara kwa kupitia *TANAPA* nayo ina mpango wa kununua ndege *SESI* na *CALVAN* ambayo inaweza kuchukua watu 14. Ikishanunuliwa itaanza safari yake za kwenda Kusini, kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Samaki wa Mapambo, nakiri kwamba kweli tathimini ya kujua kuna samaki wangapi wako katika hao wa mapambo wako katika Ziwa Nyasa haijafanyika, lakini ni imani ya Wizara kufanya hivyo. Naona kwamba itakuwa sio busara kwa kweli sasa hivi kusitisha kuwavua samaki hao. Kinachofanyika sasa hivi ili kuhakikisha kwamba hao samaki hawatamalizika ni kwamba wavuvi wameshauriwa kuvua samaki madume zaidi, kuliko samaki wa kike. Hii inamaana kwamba samaki wa kike wakibaki wengi wataendeleza kizazi.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini pamoja na kuwa iko haja ya kuendeleza vivutio katika ziwa hilo na kwa kuwa sasa kuna utata wa muda mrefu sasa, kuna utata wa umiliki wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi kwa muda mrefu, Tanzania wakisema katikati ndio mpaka katikati ya Ziwa na Malawi wakisema mwambao wa ziwa Nyasa, upande wa Tanzania ndio mpaka. Serikali ione sasa imefika wakati wa kutatua tatizo hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulikuwepo na mgogoro juu ya mpaka huo lakini kimataifa inajulikana kwamba mipaka siku zote ni katikati ya yale maji na ndivyo tunavyotambua, na ndivyo mataifa yanavyotambua lakini tutaendelea kuzungumza na wenzetu wa Malawi ili tuelewane, kwa hiyo tunaelewana vizuri, lakini kimsingi, mpaka siku zote upita katikati ya ziwa.

**MHE. SUZAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, kwa kuwa lengo la sera la Utalii ni kuendeleza Utalii katika nchi yote ya Tanzania. Je, ni kweli kuwa mikoa ya Kaskazini imekuwa na watalii wengi kiasi cha kuharibu mazingira, na kama ni hivyo, ni kwa kiasi gani basi wameharibu mazingira?

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, unataka kusema kwamba wakienda Kusini nao wasije wakaharibu mazingira au vipi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, cha msingi hapa nadhani ni kuonyesha maeneo yote ambayo yanavutia watalii kwa sababu kila mtu ana *interest* tofauti. Kaskazini wengi watapenda kuona mlima, na wengine wanataka kuona wanyama. Sasa wanyama unaweza kuwaona Katavi, ukawaona sehemu nyingine ambazo ni za Kusini, Mikumi na kadhalika.

Kwa hiyo, tunachotaka kufanya ni kwamba tuwe na maeneo mengi moja wapo ya sababu pia ni hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameieleza kupunguza *pressure* upande wa Kaskazini, na kupunguza nadhani ulisikia juzi tulipokuwa tunatoa hoja yetu ya Bajeti kwamba kuna muda fulani magari yanakuwa mengi sana.

Mfano kama Serengeti na kadhalika, lakini wote wanakwenda kuona wanyama, sasa kama kuna sehemu nyingine ya kuona wanyama, nadhani itasaidia sana kupunguza hiyo *pressure*.

Na. 245

**Uvunaji wa Misitu na Mazao ya Misitu**

**MHE. FELIX KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imepiga marufuku uvunaji wa misitu na mazao ya misitu kama miti, mbao, kuni na mkaa na kwa kuwa, Watanzania wengi Vijijini na Mijini hususan wale wa Wilaya ya Kibondo wanatumia kuni na mkaa hasa ikizingatiwa kuwa, hata nishati mbadala ya umeme na mafuta haijaweza kuwafikia wananchi wengi:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa wananchi nishati mbadala kwa matumizi yao ya kila siku?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, ilipaswa kuwaandaa wananchi kabla ya kusitisha ghafla matumizi ya kuni na mkaa ili kupunguza usumbufu kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Felix Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikupiga marufuku moja kwa moja uvunaji misitu na mazao ya misitu, bali imesimamisha kwa muda uvunaji katika misitu ya asili kwa wafanyabiashara. Ilibidi hatua hiyo ichukuliwe kwa nia ya kuiwezesha Serikali kuboresha taratibu za matumizi ya miti na misitu yetu ili kuweza kusimamia ipasavyo Sheria ya Misitu ya Na. 14 ya mwaka 2002.

Hatua hiyo haikuhusu uvunaji mdogo mdogo unaofanyika vijijini kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kama vile kuni. Pia, hatua hiyo haikuhusu uvunaji wa miti iliyopandwa. Kwa hiyo, watu waliendelea kuvuna miti waliyoipanda hata kama ni kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mheshimiwa Kijiko Mbunge wa Muhambwe, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkakati wa nishati mbadala Wizara yangu inawahimiza wananchi, hasa wanaoishi mijini, kutumia nishati mbadala kama vile umeme, gesi, bayogesi, pumba, mafuta ya taa, umeme wa *solar*, pumba zilizounganishwa yaani brikwiti na kadhalika.

Shughuli za kuhamasisha na kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya nishati mbadala zitafanywa mwaka huu wa fedha na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, pamoja na wadau mbalimbali. Matatizo hayo yatafanywa kwa muda wa mwaka mmoja hadi mwili kabla ya kusitisha kabisa matumizi ya nishati itokanayo na maiti ya asili mijini.

Maandalizi ya kampeni hiyo ambayo itafanyika kwa njia ya vyombo vya habari na mikutano yanaendelea. Na tayari Serikali imepunguza kodi ya mafuta ya taa, imefuta gesi ya nyumbani na hatua zaidi zitaendelea kuchukuliwa ili kuondoa makali ya matumizi ya nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwaandaa wananchi kabla ya kusitisha matumizi ya nishati itokanayo na miti nikuwa, kama nilivyojibu katika sehemu (a) ya jibu, maandalizi hayo yatafanyika kwa kipindi nilichokieleza.

Katika kipindi hicho cha maandalizi, nishati itokanayo na miti itaendelea kutumika mijini lakini kwa kufuata utaratibu mpya ambao utadhibitiwa ipasavyo vilevile utengenezaji wa mkaa mbadala (Brikwiti) utahamasishwa zaidi.

Kwa mfano wachoma mkaa wote watapaswa kujiandikisha kisha watumie njia za kisasa za kufanya shughuli hizo ambazo zinatoa mkaa mwingi kwa kutumia miti michache. Kanuni mpya za utaratibu wa kuchoma na kuuza mkaa zimo k atika Tangazo la Serikali Na. 69 la 9 Juni, 2006.

Hata hivyo, Wizara yangu inawahimiza wananchi wanaoishi vijijini kujijengea tabia ya kuhifadhi misitu na kupanda miti kwa manufaa yao mbalimbali. Wananchi

wataweza kuitumia miti wapendavyo bila usumbufu kama wataistawisha kama zao la kilimo. *(Makofi)*

**MHE. FELIX W. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na nashukuru na kwa majibu mazuri ambayo Naibu Waziri ametoa. Lakini kwa kuwa zuio hilo limeweza kuathiri sana wananchi na hasa wale wananchi wa jimbo la Muhambwe na Watanzania kwa ujumla, nilikuwa napenda nijue.

Je, Serikali ina mpango gani kwa sababu wananchi hao wanatumia mavuno ya misitu, kwa sababu hawana jinsi nyingine hawajawahi kuona umeme ambao unaweza ukatumika kama njia mbadala ya kuweza kutumia badala ya mkaa na kuni?

Sasa je, Serikali imejipanga namna gani Kuhakikisha wananchi wanapata njia nyingine ya kuweza kuwasaidia katika kufanikisha zoezi lao la kila siku kama njia moja wapo ya kupunguza ajira ambayo Serikali imeahidi itatoa ajira nyingi? Lakini nao wananchi wameweza kutumia njia hiyo kama kuiongezea sifa Serikali kwamba wamejiajiri wenyewe na hasa wanavijiji, naomba jibu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo kuhusu jitihada gani Serikali inafanya kwenye maeneo ya Nishati mbadala ili wananchi waweze kunufaika nayo na waepukane na uharibu wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetangaza hapa Bungeni kuhusu matumizi ya gesi asilia na juzi wakati wanawasilisha Bajeti hapa tulizungumza juu ya makampuni ambayo sasa hivi tayari yamejiingiza nchini kuweza kufanya utaratibu wa kusambaza au kufanya biashara ya kusambaza gesi, hiyo moja.

La pili, tuliwahi kuzungumza hapa Bungeni juu ya umuhimu wa kutumia makaa ya mawe niliwahi kusema hapa tuliwahi kuzungumza makampuni kama Kiwira na mengineyo kutengeneza hizi *brickets* za kuweza kutumia majumbani.

La tatu, ni umuhimu wa mafuta ya taa ambayo Serikali pia imepunguza hata kodi yake, sasa nafamu kwamba sasa hivi kuna upungufu wa mafuta ya taa nchini lakini nataka niseme kwamba Serikali imechukua hatua na leo kuna Timu ya Serikali inakwenda kusaka mafuta ya taa ambayo pengine inawezakana yanafichwa kwa kuhodhiwa katika makampuni mbalimbali ya mafuta kwa nia ya kutaka kujitajirisha zaidi ili mafuta haya yatolewe kwa wananchi waweze kununua na waweze kuyatumia.

Lakini hatua nyingine ambazo zimewahi kuchukuliwa na Serikali ni hatua mbalimbali, ni Serikali ambayo imechukua hatua kupunguza kodi ya vifaa vya *solar* na mengineyo na miradi ambayo tumeitangaza ya kusambaza umeme vijijini ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Kigoma ambao kwa miaka mingi haujawahi kuona umeme kwa maana ya umeme wa gridi umekuwa na umeme wa *diesel*. Lakini mwaka huu Serikali imetenga fedha nyingi ya kuanza kupeleka umeme kwenye Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nisisitize jambo moja na liko katika sehemu nyingi za nchi yetu matumizi ya *biogas*. Nimeshawahi kusema kwa mfano kwenye maeneo ya watani zangu Wasukuma kuna *biogas* ya kutosha na Wizara yangu inahitaji kuhakikisha kwamba tunashirikiana na wananchi katika maeneo haya ili *biogas* ile ambayo ipo kwa wingi kwa wanyama na kwa binadamu iweze kutumika katika uzalishaji wa umeme. (*Makofi*)

Na. 246

**Kuanzisha Hospitali ya Majeruhi wa Ajali Chalinze.**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Dar es Salaam – Morogoro na Chalinze - Segera ni barabara kubwa ambapo suala la ajali za magari ni jambo linalotokea mara kwa mara: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga hospitali ya majeruhi Chalinze ili kuokoa majeruhi wa ajali za barabarani ambao husafirishwa umbali mrefu kwenda Hospitali za Tumbi, Muheza na Morogoro?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara haina mpango wa kujenga hospitali ya majeruhi Chalinze. Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na hospitali kubwa katika Mkoa wa Pwani, na katika kutekeleza azma hiyo Serikali inatarajia kufanya upanuzi wa hospitali ya Tumbi kuanzia kipindi cha mwaka huu wa fedha. Upanuzi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, hospitali hii itakuwa na chumba cha huduma cha kisasa kwa wagonjwa wa dharura yaani *casualty*, vyumba vitatu vya upasuaji wa kisasa, chumba cha wagonjwa mahututi yaani *Intensive Care Unit*, maabara ya kisasa na wodi ya majeruhi yenye vitanda 100. Ni matarajio yangu kuwa upanuzi wa Hospitali hiyo utakapokamilika utaboresha utoaji huduma za afya bora kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Pwani ikiwemo Chalinze, ikiwa ni pamoja na huduma kwa majeruhi wa ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuongezea, kuna mpango wa kupanua Kituo cha Afya cha Mlandizi kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kibaha Vijijini. Upanuzi huu utasaidia pia katika matibabu ya majeruhi wa maradhi mengine. Aidha, Zahanati ya Chalinze imepanuliwa kutoka hatua ya zahanati hadi hadhi ya kituo cha afya na kupewa Gari la Wagonjwa. Wizara itaendelea kushirikiana na Mkoa katika kutoa ushauri wa kitaalamu unaolenga kuboresha huduma za afya sambamba na utoaji wa matibatu kwa majeruhi. Kwa kupitia mpango wa *Emergency Preparedness* uliofadhiliwa na Serikali ya

Marekani, Mafunzo yametolewa ya jinsi ya kushughulikia majeruhi kwa wafanyakazi katika Hospitali za Tumbi na Morogoro.

heshimiwa Spika, pamoja na kupanua upatikanji na ubora wa huduma za afya kwa nia ya kunusuru majeruhi, naomba nitumie fursa hii kutoa rai kwa Wizara mbalimbali, watumiaji wote wa barabara, wakiwemo waenda kwa miguu, wapanda baiskeli, wachungaji wanaoswaga mifugo barabarani pamoja na wadau wengine kwamba tushirikiane na kuwa waangalifu ili kuzuia ajali zisitokee. Ajali nyingi zinaweza kuepukika kwani utafiti unaonyesha kuwa agali nyingi zinatokana na uzembe, barabara mbovu, ulevi, magari mabovu na mwendo wa kasi. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri yenye kuleta mafanikio mazuri katika Mkoa wa Pwani, pamoja na kuwa matatizo yanayojitokeza ya ajali za barabarani husababisha majeruhi wengi kupoteza maisha wakati wanasafirishwa kwenye hizo hospitali nilizozitaja.

(a) Serikali haioni umuhimu sasa wa kuongeza idadi ya madawa kwenye vituo vya afya kama Chalinze, Miono na Lugoba ili kukabiliana na tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa, vituo vya afya nilivyovitaja vya Miono, Chalinze na Lugoba vina wakuu wa vituo wenye ngasi ya *Clinical Officer*. Je Serikali haioni umuhimu sasa wa kupeleka *Ma – assistant Medical Officers* ili kukabiliana na tatizo hilo kwa sasa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maneno kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ambao tumekuwa tukiufuata sasa hivi ni kupeleka vifungasho yaani *kits* za dawa ambazo zinafanana kutoka kituo hadi kituo tumeona utaratibu huo haufai kwa sababu mahitaji yanatofautiana kati ya mahali na mahali lakini pia katika msimu na msimu. Kwa hiyo, sasa hivi tunaanzisha utaratibu tunaita *Indent System* ambao wahusika watakuwa wanaleta mahitaji kufuatana na misimu jinsi inavyobadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili tunafanya tathmini ya wafanyakazi kwani tuna uhaba mkubwa sana wa wafanyakazi nimewahi kusema hapa Bungeni na hivi sasa tuko katika mchakato wa kuongeza wafanyakazi itakuwa mradi mkubwa kabisa lakini nia yetu hatua kwa hatua na kwa jinsi tutakavyopata pesa nina imani kwamba tutapunguza matatizo hayo na hayapo katika eneo la Chalinze peke yake ni nchi nzima.

**MHE WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Waziri wa Afya napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika barabara inayotoka Dar es Salaam – Kibaha – Chalinze – Lugoba – Mkata – Segera huduma za afya ziko mbalimbali je, Waziri haoni sasa ni wakati wa kuanzisha *mobile health or first aid service* kwa sababu tatizo ni kuwafikisha majeruhi kwenye maeneo yenye huduma, nchi nyingine zinafanya hivyo nadhani hilo hata kuchangia tungeweza hata kuchangia sisi wengine ambao ni wadau wa barabara hiyo.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu swali la msingi nilitoa rai au ombi kwa watu wote tunaohusika kutumia barabara kwamba tuwe waangalifu nadhani Serikali hata ikiwa na pesa kiasi gani tukijenga hospitali nyingi na ajali zikaendelea kila wakati maombi yatakuwa yanakuja hapa kwamba tuendelee kujenga hospitali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninachoomba ni kwamba tupunguze ajali tujipange vizuri tupunguze ajali na ningependa kutoa taarifa kwamba umbali wa vituo tunavijua kwa sababu tumeshatengeneza *atlas* inayoonyesha vituo vya kila aina vinavyotoa huduma ya afya kwa nchi nzima na hii ni katika kujipanga kuongeza vituo mahali ambapo tunaona vipo mbalimbali.

Na. 247

**Maandalizi ya Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu.**

**MHE. MARGRETH AGNESS MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna mchakato unaoendelea Kimataifa kuandaa Mkataba wa Haki za watu wenye ulemavu.

(a) Je, Serikali ina habari juu ya mchakato huo?

(b) Je, ni kwa kiasi gani Serikali imewashirikisha watu wenye ulemavu katika ushiriki wa nchi katika mchakato huo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusahihishe kidogo Mimi ni Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ndiyo maana hili swali ni la Ustawi wa Jamii kwa hiyo tusisahau hicho kipengele.

**NAIBU SPIKA: -** Unapunguza muda. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:-** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali naomba nimpongeze Mama Mkanga, kwa kuwa mtetezi mkubwa wa watu wenye ulemavu hapa Bungeni. (*Makofi*)

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo habari kuhusu mchakato wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za watu wenye Ulemavu kwa kingereza unaitwa *The Comprehensive and Integral International Convention on the Protection and Promotion of the Rights and Dignity of Persons with Disabilities.*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa mkataba unaohusika, Chama cha Mapinduzi kimeainisha katika kipengele chake kutambua haki za Walemavu na vilevile Umoja wa Mataifa uliunda Kamati iliyoitwa *Ad Hoc Committee* kwa lengo la kufanikisha uandaaji wa Mkataba huo. Kamati hiyo tayari imetayarisha Kanuni za Msingi kuhusu Haki na Usawa wa Fursa kwa Watu wenye Ulemavu, (*The Standard Rules on the Equalization of Opportunities for Persons with Disabilities.*

Kamati hiyo ya Umoja wa Mataifa ilianza kukutana mwaka 2002 na imeendelea kukutana mara moja au mbili kila mwaka. Kikao cha karibuni kilichofanyika mwezi Februari 2006 mjini New York ambapo nchi yetu iliwahilishwa na Ubalozi wetu uliopo *New York.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vikao hivi muhimu sana na Serikali inapaswa kuhudhuria ndiyo maana ubalozi wetu ukapata maagizo kupeleka mawazo ya Serikali katika vikao hivyo, Serikali haijapeleka ujumbe kutoka hapa nchini lakini baadhi ya watu wenye ulemavu kwa kufadhiliwa na Shirika linaloitwa *Pro – disability* wameweza kuhudhuria vikao hivi.

Kikao cha mwisho cha mchakato huu na ambacho kitatoa maamuzi kuhusu mkataba kitafanyika mwezi Agosti yaani mwezi ujao na Serikali inakusudia kutuma ujumbe. Ni matarajio yetu kwamba ujumbe wa Tanzania kwenye mkutano huo utashiriki watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba matayarisho yamekamilika kwa Tanzania kuridhia kanuni hizi. Katika matayarisho hayo wadau mbalimbali walihusika, wakiwemo Shirikisho la Watu wenye Ulemavu Tanzania, Umoja wa Walemavu Zanzibar, Chama cha Wasioona Tanzania, Chama cha wenye Ulemavu wa Viungo Tanzania, Chama cha Viziwi Tanzania, Chama cha Maalbino Tanzania, Chama cha Viziwi na Wasioona na Chama kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu wa Akili.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Margreth. Hicho kikao katika mikutano ya Walemavu walioomba waheshimiwa Wabunge waliopo humu ndani walihudhuria hicho kikao cha mwezi Agosti nadhani hiyo mtaikumbuka.

Mheshimiwa Anne Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa walemavu ni kundi kubwa sana na wako nchi nzima ya Tanzania vijijini, milimani na tambarare na mimi mara kwa mara ninapoona ninaona vizawadi na misaada ikitolewa kwa walemavu haifiki vijijini na milimani.

Je, Serikali itafanya mikakati gani ya kuwafikia walemavu wote ili fursa iwe ni sawa kwa wote?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika huu mkataba umeaisha kabisa kutuelekeza namna ya kufanya lakini sisi wenyewe tunao utaratibu ambao umeshaanza kufanyika wa kufanya utambuzi wa walemavu na mayatima katika nchi nzima, kwa hiyo ni mategemeo yetu kwamba tutakapopata takwimu ndiyo tunaweza tukajipanga sawasawa ili hii tunayoizungumzia fursa sawa kwa wote iweze kuwafikia walengwa.

Na. 248

**Mahusiano ya Biashara na Msumbiji**

**MHE. MOHAMMED S. SINANI** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu ina mahusiano mazuri na nchi jirani ya Msumbiji na kwamba, Daraja la Umoja nalo linajengwa.

Je, Serikali inachukua hatua gani hivi sasa ya kuanzisha mahusiano ya biashara kati ya nchi hizo mbili ili kusaidia wananchi kiuchumi hususan waliopo Mikoa ya Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niamba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko napenda kumjibu Mheshimiwa Mohammed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania na Msumbiji zina mahusiano mazuri katika sekta zote za kiuchumi na kijamii, hasa tukizingatia kwamba Tanzania ilitoa mchango mkubwa katika harakati za kuipatia uhuru wa Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuona umuhimu huo, pande hizi mbili zilikubaliana kuanzisha Tume ya Pamoja ya Ushirikiano yaani *Permanent Joint*

*Commission on Cooperation*. Ushirikiano huu ulikuwa katika nyanja za Biashara za mpakani, kushiriki katika maonyesho ya biashara, Madini, Nishati, Elimu, Habari na Miundombinu. Kwa kipindi kirefu Tume hii ya Ushirikiano haijakutana hivyo ipo haja ya kufufua ushirikinano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia ukaribu uliopo baina ya Tanzania na Msumbiji, Mtu Ruvuma umekuwa ni kikwazo kikubwa kibiashara baina ya Tanzania na Msumbiji. Ujenzi wa Darala la Umoja litaunganisha nchi hizi mbili na litasaidia sana katika kukuza biashara za mikoa ya jirani na majimbo ya Msumbiji yanayopakana na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano wa Marais wa Nchi mbili hizi, uliofanyika tarehe 7 Januari, 2005 walikubaliana kuanza utekelezaji wa kujenga Daraja yaani *Unity Bridge* hatua kwa hatua kwa kutumia fedha za nchi mbili bila kuomba pesa za wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa daraja hili la Umoja kutatimiza ndoto ya Marais wanzilishi wa nchi hizi mbili, yaani Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere na Rais wa kwanza wa Msumbiji na FRELIMO Hayati Samora Michael waliotaka kujenga daraja hili wakiwa Marais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *Mtwara Development Corridor* uliozinduliwa tarehe 15 Desemba 2004, huko Lilongwe. Utekelezaji wa mambo yote yaliyoainishwa yatachochea biashara kati ya Msumbuji na Tanzania.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu vizuri swali husika lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Mtwara – Kitaya imekuwa ikitumka sana na wananchi wa nchi hizi mbili kibiashara na uchumi, je Serikali ina mpango gani wa kutengeneza kwa lami barabara hiyo ili kuvutua mahusiano ya kibiashara baina ya nchi hizi mbili?

**NAIBU SPIKA:** Lakini swali hili ni jipya kabisa, sasa naomba uliandike vizuri kwa sababu hizo barabara siyo kwamba anazijua *automatic*.

Kuna Waziri wa Miundombinu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ndani ya wiki moja nitatoa kwa kirefu jibu hapa Bungeni kuhusiana na barabara hiyo kwa hiyo naomba avute subira atapata hilo jibu rasmi kutoka Wizara ya Miundombinu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhagama swali la pili la nyongeza.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, sasa mahusiano ya Tanzania na Msumbiji yameshaanza kuelekezwa katika madaraja ya Umoja yote mawili, *Unit Bridge* namba moja ya Mtambaswala na *Unit Bridge* namba mbili ambayo inapita katika Kata ya Mhukulu Wilaya ya Songea vijijini.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami sasa hivi anapozungumzia maendeleo ya kibiashara anatakiwa pia agusie na ukanda huo wa *Unit Bridge* namba mbili ambao unapita katika Wilaya ya Songea Vijijini na siyo Uniti Bridge namba moja tu?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Mtwara Development Corridor kuna miradi mingi ambayo imehusishwa ambayo ina jukumu ya kuendelezwa katika ndani ya Mtwara Development Corridor. Katika miradi hiyo ni pamoja na Daraja la Umoja ambalo linahesabika kama Unit Bridge Number one pamoja na hilo Unit number Two ambalo analizungumzia Mheshimiwa.

Kwa hiyo, ndani ya Mradi wa *Mtwara Development Corridor* miradi hiyo yote inahusishwa na itakuwa inatekelezwa awamu kwa awamu. (*Makofi*)

Na. 249

**Upatikanaji wa PASSPORT**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, *passport* ni haki ya kila raia na kwa kuwa upatikanaji wahati hizo hapa nchini umekuwa wa urasimu kiasi cha mtu kulazimika kutoa rushwa ili aipate kwa urahisi.

Je, ni lini Serikali itaweka mazingira yaliyo rahisi ya upatikanaji wa hati hizo kwa wananchi wake na kuondoa mwanya wa kutoa rushwa?

**WAZIRI WA MAMBO YA DANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwia Ali Said Salum, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge *Passport* ni haki ya kila raia wa Tanzania na kwamba raia yeyote anayetimisha masharti ya kuomba *passport* anastahili apewe *Passport* kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo suala la utoaji wa *Passport* na hati za safari linatawaliwa na Sheria ya *Passport* na hati za safari Na. 20 ya mwaka 2002, ikisomwa pamoja na kanuni zake Na. 197 za mwaka 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya *Passport* na kanuni zake inatoa masharti na utaratibu wa kuomba na kupatiwa *Passport* kwa kila raia wa Tanzania, kwa mfano, kuwa na *affidavit* au cheti cha kuzaliwa cha mwombaji wa *Passport* na wazazi wake, ushahidi wa safari za nje na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kufuata taratibu za utoaji wa *Passport* sio usumbufu bali ni kuepuka kutoa *Passport* kwa watu wasio raia wa nchi yetu. Aidha, nia nyingine ya utaratibu huu ni Serikali kuchukua tahadhari dhidi ya watu wanaoweza kutumia vibaya *Passport* kama kutumika katika biashara ya madawa ya kulevya, usafirishaji haramu wa watu yaani *human t rafficking*, ugaidi na uhalifu mwingine wa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati zoezi la ubadilishaji wa *Passport* mpya lilipoanza mwezi Machi 2005 ulitokea msongamano na usumbufu uliosababishwa na waombaji kuwa wengi kupita kiasi kilichotarajiwa.

Hata hivyo kwa sasa msongamano na usumbufu huo haupo kutokana na ukweli kwamba maombi ni machache hivyo *Passport* hutolewa katika muda wa siku saba kwa Dar es Salaam, siku 14 Mikoani na siku nne kwa Zanzibar. Kwa safari za dharura, *Passport* inaweza kupatikana ndani ya siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba upatikanji wa *Passport* kwa wananchi wanaotimiza masharti hivi sasa hauna usumbufu, hauchelewi na hakuna kudaiwa rushwa. Iwapo kuna mwananchi mwenye malalamiko dhidi ya zoezi hili alete malalamiko Wizarani ili hatua zichukuliwe mara moja.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, utaratibu wa sasa wa kupatikana hii *passport* hauishii Halmashauri za Wilaya kufika Mkoani mpaka Taifa. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba ni wakati muafaka wa taratibu zote za kupatikana kwa *Passport* zikamalizikia Wilayani badala ya utaratibu wa sasa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo.

Ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa sasa hivi mwombaji anaomba anajaza fomu katika Wilaya yake zile Wilaya ambazo zina ofisi ya Uhamiaji baadaye yale maombi yanakwenda Mkoani na kutoka Mkoani ndiyo yanakuja Makao Makuu kwa ajili ya *Passport* kutolewa. Sasa Mheshimiwa Mbunge anasema utaratibu huu uishie kulekule wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili haliwezekani kwa sababu tu za udhibiti, kule nyuma tuliwahi kutoa *Passport* katika kila mkoa, utaratibu ulikuwa unaishia mkoani, udhibiti ukawa hafifu, *Passport* zikazagaa kwa watu ambao hawakustahili kupata *Passport*. Ndiyo maana sasa hivi tumeacha utaratibu huo na tunatoa Makao Makuu kwa ajili ya udhibiti.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, *Passport* siyo kama kitambulisho cha kazi au makazi bali hutolewa kwa raia wa Tanzania ambao wana nia hasa ya kusafiri kwenda nje ya nchi na kwa vile kumejengeka hofu katika baadhi ya waombi ya *Passport* kwamba unapoomba *Passport* ni lazima utoe rushwa na kwa hiyo mara nyingi hutumia maajenti wa katikati yaani *middle men.*

Je, hali hii siyo inasababisha kwamba wale maajenti ndiyo wanaoomba rushwa halafu wakaamua kuwashawishi baadhi ya Maafisa Uhamiaji ili wawape rushwa hiyo ili kusudi *Passport* zipatikane mapema?

Kwa nini hawa wananchi wasiende Ofisi za Uhamiaji mahali ambapo hawatapata usumbufu hata wa kuombwa rushwa kama wanavyoombwa na ma *middle men*?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba *Passport* ni waraka kwa ajili ya safari, maana yake baadhi ya Watanzania wanataka *Passport* waziweke tu nyumbani kama kitambulisho chake lakini kwa kweli *Passport* ni *document* inayokuruhusu uende nchi za nje sasa wanaozitafuta *Passport* Mheshimiwa Nyami anasema kwamba wanatumia mawakala nataka niseme kwamba suala la Mawakala tumeshalipiga marufuku. (*Makofi*)

Tunataka kila anayeomba *Passport* yeye mwenyewe afike katika ofisi ya Uhamiaji yeye mwenyewe na kwa utaratibu wa sasa hivi tunataka tuchukue mpaka na alama za vidole sasa sidhani kama atamleta mtu mwingine aje amwekee alama ya kidole katika *Passport* yake. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba suala la mawakala tumelipiga marufuku tunataka yeye mwenyewe aje katika Ofisi ya Uhamiaji tutamchukua alama ya vidole na picha yake ili kuzuia hiyo mianya ya rushwa inayotokana na hao mawakala.

**MHE. MANJU S. MSAMBAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri ametuambia huko zamani *Passport* zilikuwa zinatolewa mkoani lakini kwa sababu kumetokea kutokuwa na uaminifu kwa maafisa wale ndiyo maana sasa *Passport* zote zinatolewa Makao Makuu ya Uhamiaji.

Hivi Mheshimiwa Waziri anataka kuliambia Bunge hili kwamba Maafisa Uhamiaji waliopo Mkoani sasa siyo waaminifu na siyo *Vetted Officers*?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu haumaanishi kwamba hatuwaamini wale Maafisa wa Mikoani kwamba wao sio waaminifu wala hatusemi kwamba pale Makao Makuu ya Uhamiaji ndiko kuna malaika watupu, hapana. Isipokuwa ni tahadhari kwamba hii huduma ukiisambaza sana kama tulivyofanya mwanzo uwezekano wa mtu ambaye si muaminifu kujipenyeza akaharibu upo na tulishauona ndiyo maana tukachukua hii hatua. Hata pale Makao Makuu ya Uhamiaji bado kuna vijana ambao sio waaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mwaka jana hapa palitokea kesi mbaya ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, rafiki zake mwuliza swali Ali Said Salum, ambao walitumia vibaya ile fursa ya *Passport* na wakawarubuni baadhi ya vijana wetu wawili ambao sasa hivi wako Mahakamani na wenyewe kwa ajili ya kosa la kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge kufanya kosa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Manju Msambya, kwa kweli ni tahadhari tu, tunawaamini sana wenzetu wa Mikoani na wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Na. 250

**Kikosi cha Kuzuia Ujambazi Zanzibar**

**MHE. FATMA OTHAMN ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa hali ya ujambazi imeshamiri Zanzibar; na kwa kuwa, ujambazi unaofanyika ni wa kutumia bunduki na bastola:-

Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuunda kikosi cha kuzuia ujambazi kama kilichopo Dar es Salaam, chenye silaha za kutosha, usafiri na redio za uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Fatma Othman Ally, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Jeshi la Polisi lina kikosi cha kupambana na ujambazi katika Visiwa vya Unguja na

Pemba. Kikosi hiki kimepewa jina Kikosi Maalum *Special Squard* na kinaendelea na shughuli zake za kupambana na uhalifu katika Mikoa yote ya Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikosi hiki kimekuwa kikiimarishwa kwa kuongeza idadi ya Askari wake, kupewa mafunzo maalum sambamba na kuwapatia magari, pikipiki, *radio call*, na vifaa vingine ili kudhibiti vitendo vya uhalifu vilivyojitokeza kwa kasi hivi siku za karibuni.

Aidha, Inspekta Jenerali wa Polisi alifanya ziara ya dharura Mjini Zanzibar kuzungumza na kubuni mikakati ya pamoja na vyombo vya usalama vilivyopo Zanzibar na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushughulikia suala la ujambazi na uhalifu Visiwani Zanzibar Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, anatarajia kufanya ziara fupi wakati wowote kutoka sasa akiongozana na Inspekta Jenerali wa Polisi na viongozi wengine wa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba Wizara yangu na Jeshi la Polisi haitavumilia kuona vitendo vya uhalifu vikiendeshwa na majambazi na wafadhili wao na hivyo kuhatarisha maisha ya raia, wageni na watalii wetu na kuathiri uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

**MHE. FATMA OTHMAN ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, ujambazi unaharibu amani katika jamii na ili majambazi hao wafichuliwe kwa wingi. Je, Serikali haioni haja hivi sasa ya kuanzisha Mfuko Maalum wa Zawadi kwa wale wote watakaotoa taarifa na kuwafichua majambazi hao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Serikali imeona umuhimu wa kuanzisha Mfuko huu na kwa bahati nzuri imewashirikisha wananchi na wananchi wameitikia vizuri katika kuimarisha Mfuko huu. Kinachoendelea sasa hivi ni hatua za kuimarisha zaidi na wale wote ambao wanatoa taarifa wanapata zawadi nzuri. Ningependa kuwaomba wananchi waendelee kutupa taarifa ili tushughulikie jambo hili kwa ukamilifu wake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Ninayo matangazo machache.

Kwanza kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri Daniel Nsanzugwanko ana mgeni wake hapo Katibu wa Vijana wa Mkoa wa Kigoma Ndugu Mperi. Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa Capt. John Komba, wanao mgeni wao Mheshimiwa Koneli Msuha, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbinga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Job Ndugai, anapenda kuwatangazia Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo tarehe 20 Julai, 2006 Chumba Namba 133 saa 5.00 asubuhi.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo tarehe 20 Julai, 2006 saa 5.00 asubuhi katika ukumbi Namba 231 katika ghorofa ya pili. Halafu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Mussa Zungu anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo tarehe 20 Julai, 2006 chumba namba 428 saa 5.00 asubuhi, kwenye shughuli ya kuzungumzia taarifa ya Bunge la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ni kazi muhimu wakutane chumba Namba 428 ghorofa ya nne, saa 5.00 asubuhi.

Halafu Kamati ya Uongozi kwa maana ya Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge za Kudumu, pamoja na wajumbe wa Tume ya Bunge watakuwa na Kikao saa 7.30 leo. Ndiyo maana hizi Kamati zinakaa saa 5.00. Kwa hiyo, mnapokuwa huko mjue kwamba saa 7.30 pia kuna kikao hicho. Mtakutana kwenye Chumba cha Mkutano cha Spika, kama kutakuwa na mabadiliko taarifa mtaipata pale. Baada ya kusema hayo, tunaendelea na shughuli za leo. Katibu endelea. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007
### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji nilionao hapa ni 25 na kwa sababu ya umuhimu wa Wizara hii tumejifunza kwamba ni vizuri tukatoa muda mrefu sana kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge watakaochangia ni mpaka saa 7.00, na baadaye jioni tutawaita watoa hoja waanze kujibu hoja kwa muda wa saa moja. Halafu tutakuwa na muda mzuri wa kuendelea na Kamati ya Matumizi.

Kwa hiyo, watakaoweza kufikiwa kuchangia kwa nafasi hii ya kubanabana hapa ni Waheshimiwa Wabunge 11. Kwa hiyo, sasa tunaendelea na Waheshimiwa Wabunge waliochangia mara moja na wakimalizika, tutaendelea na Waheshimiwa Wabunge waliochangia mara mbili ambao watakuwa wachache na wengine watabakia. Sasa nitamwita Mheshimiwa Anastazia James Wambura. Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi wajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza asubuhi hii leo. Awali ya yote napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na vilevile kutuwezesha kumaliza salama Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi na Jumuiya ya UWT kwa kuongeza nafasi za Viti Maalum ambazo ndizo zimeniwezesha kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kuchukua nafasi hii kuwashukuru akinamama wa Mkoa wa Mtwara kwa kunichagua niwe mwakilishi wao katika Bunge hili. Vilevile nawashukuru wananchi kwa ujumla wa Mkoa wa Mtwara kwa kunipa ushirikiano wao mkubwa sana katika kazi zangu za Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri ambayo inafanya kwa kasi kubwa kupitia Wizara mbalimbali. Kwa mfano, katika kutatua matatizo ya uhaba wa chakula, upungufu wa shule na vilevile kukabiliana na tatizo la mgao wa umeme. *(Makofi)*

Naomba nitoe mfano, kwamba hata juzi tuliweza kwenda na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mkoani Mtwara kutembelea machimbo ya gesi ya *Mnazi Bay,* na kwa kweli wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwa ujumla wanashukuru wamefarijika na wanampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na wanamwomba aendelee na kasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Mtwara wanasema kwamba kwa hatua hizo ambazo Serikali inafanya kuhakikisha kwamba maendeleo ya Mikoa ya Kusini yanapatikana ni ishara kubwa kwamba sasa Mikoa ya Kusini kumeanza kupambazuka na wana imani kwamba itakapofikia hatua ya barabara ya Kibiti-Lindi kufunguliwa mwakani, basi kutakuwa kumekucha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe na Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri ambazo mnafanya kwa *speed* na *standard*, ninawatakia kila la kheri katika kazi zenu na kwa kushirikiana na Serikali katika kazi hii. Nina imani kubwa sana kwamba Taifa letu sasa litakuwa na maendeleo ya kasi kubwa labda tutakuwa na *super sonic speed* katika maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi nyingine tena kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara zilizotangulia kuwasilisha Bajeti zao. Vilevile kwa namna ya pekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na ofisi yake nzima kwa hotuba nzuri ambayo wameiandaa kwa umakini mkubwa. Kwa sababu hiyo basi, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Sasa naomba nitoe mchango wangu kwa kuanzia na tatizo la upungufu wa walimu katika Mkoa wa Mtwara. Mkoa wa Mtwara kwa kadri ya takwimu zilivyo una upungufu wa walimu wapatao 884. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kutupatia walimu 155. Lakini nasikitika kusema kwamba walimu ambao wameweza kuripoti ni 34 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi afuatilie suala hili, ili kusudi aweze kuhakikisha kwamba tunapata walimu na kuhakikisha kwamba tunakuwa na maendeleo katika elimu katika Mkoa wetu wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi pengine labda nichukue nafasi hii kuwaomba hao walimu 121 ambao wamebaki hawajaripoti, niwaombe waweze kufika katika Mkoa wetu ili tushirikiane katika maendeleo ya elimu. Kwa sababu kwa sasa nawahakikisha kwamba hakuna tena shida kubwa kama walivyokuwa wakidhani katika Mkoa wetu wa Mtwara. Kuanzia suala la umeme, sasa hivi umeme hauna shida, kuna gesi ambayo inaweza ikatumika katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo. Vilevile mwakani tumehakikishiwa kwamba barabara yetu itapitika. Kwa hiyo, kutakuwa hakuna shida ya usafiri na masuala mengi tu ya kimaendeleo, nadhani sasa hivi kutakuwa hakuna shida. Kwa hiyo, naomba niwakaribishe sana hao walimu 121 waweze kufika katika Mkoa wetu ili tushirikiane kuliendeleza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwaombe walimu hao waelewe kwamba wamesomeshwa kwa kodi za wananchi na hasa wametumia uchumi mkubwa kutokana na zao la korosho ambalo linalimwa katika Mikoa ya Kusini ukiwemo na Mkoa wa Mtwara. Kwa hiyo, naomba walifikirie hili na waweze kuitikia huo wito wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kwenda kuripoti katika Mkoa wa Mtwara. Hata wale ambao watapenda kwenda kuripoti basi mimi naomba wafike hata kama hawakupangiwa wanaweza kutuambia sisi Waheshimiwa Wabunge na tukashirikiana nao kuhakikisha kwamba wanapangiwa nafasi katika Mkoa wetu wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia suala la pili katika elimu nalo ni kuhusu Elimu ya UKIMWI mashuleni. Nilikuwa napenda sana kuiomba Wizara iangalie kwa makini na ipitie upya zile *contexts* ambazo zinafundishwa kwa wanafunzi hasa wale wadogo wa darasa la nne na darasa la tano. Kwa sababu upo uwezekano kwamba yale wanayofundishwa hayawiani sana na umri wao. Pengine kunaweza kukawa na kitu kwa wale watoto ambao ni watundu, kunaweza kukawa na ile haja ya kutaka kujua zaidi kuhusu hayo ambayo wanafundishwa na pengine kuliangamiza Taifa kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ijaribu kuangalia zile *contexts* na hasa yale matumizi ya vifaa mbalimbali ambavyo vinaagizwa vitumiwe katika kujikinga na UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu suala la michezo na hili limejionyesha pia katika hatua mbalimbali ambazo zimepangwa kuchukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Lakini nilikuwa napenda kusisitiza kwamba walimu wetu wapewe mafunzo ya kutosha katika fani ya michezo ili waweze kufundisha michezo kitaaluma na hapo labda tunaweza tukafanikiwa kuitumia hii fani katika ajira ya vijana hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu suala la maadili. Nadhani wote tunatambua kwamba lipo wimbi sasa hivi katika Taifa letu la mmomonyoko wa maadili. Nadhani tunajua kwamba vijana wengi sasa hivi wamejiingiza katika utumiaji wa madawa ya kulevya, wasichana wanafanya shughuli ya kuuza miili yao, kuna tatizo la wizi, kuna tatizo la ujambazi, kuna tatizo la ubakaji, rushwa, uzururaji na kutopenda kufanya kazi. Lakini haya yote yanafanywa na vijana ambao wamesoma katika shule zetu, na hawa vijana wana wazazi na pengine wana walezi ambao wana shughuli zao na wengine ni wakulima na wengine ni watumishi wa kawaida. Vilevile wengine wanaweza wakawa hata ni viongozi. Wazazi hawa hawapendi tabia za hawa vijana wanazozifanya na si kwamba wazazi wanazifurahia. Sasa je labda tujiulize nani anayewajibika kuhakikisha kwamba watoto wanakuwa na maadili mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tunatambua kwamba Taasisi ya kwanza katika maadili ya vijana ni familia, ikifuatiwa na shule na baadaye Taasisi za Kidini. Lakini nizungumzie kidogo kuhusu familia. Kwa sasa kuna mabadiliko makubwa ya kijamii na ya kiuchumi katika familia zetu na hili linaweza kusababisha familia hizi kushindwa kutekeleza wajibu wao wa malezi kwa watoto ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine labda nianzie mabadiliko ya kijamii katika familia. Kwanza, katika siku zilizopita kulikuwa na huu mfumo wa *extended family* ambapo katika familia utakuta kwamba walikuwa wakiishi ndugu, jamaa na wazazi wa watoto na hao wote walijishughulisha moja kwa moja katika malezi ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sasa kuna mabadiliko makubwa kwamba familia ina baba na mama na ni hao wawili tu ambao wanashughulika na malezi ya watoto. Labda niseme kiuchumi pia yapo mabadiliko kwamba zamani alikuwa akijishughulisha tu baba katika kutafuta kipato cha familia. Lakini kwa sasa hivi baba na mama wote wanajishughulisha katika kutafuta kipato. Hivyo, kwa muda mwingi sana utakuta kwamba mama hayupo nyumbani na baba hayupo nyumbani na hivyo kuwaacha watoto pekee yao. Kutokana na hili basi mimi nadhani ni vizuri sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikaangalia kwa umakini na ikafanya utafiti wa hili ili kusudi sasa mashule yaweze kuchukua hili jukumu la kuwalea watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na pengine nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika bajeti yake awasaidie wale akinamama ambao ni wafanyakazi katika mabenki kwani wao huwa wanarudi usiku nyumbani labda saa 2.00, wengine ni wafanyabiashara wanasafiri katika sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, muda mwingi hawako nyumbani na wengine ni viongozi hawapo nyumbani. Naomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie kwamba watoto wao watakuwa salama kimaadili kwa kupitia Bajeti hii ili kusudi kuweza kusaidia kupunguza hili wimbi la mmomonyoko wa maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine kwa pendekezo tu naomba utafiti ufanywe wa kina na vilevile mashindano labda yafanyike ya kihusisha walimu kama vile yanavyofanyika mashindano ya kitaaluma. Lakini yafanyike sasa mashindano ya

nidhamu na maadili kwa walimu na kwa wanafunzi kwa mashuleni. Nadhani tumesikia jana kwamba kuna walimu ambao wanajihusisha na vitendo ambavyo ni ukiukwaji wa maadili. Kwa mfano, ubakaji, wapo walimu pia ambao ni watumiaji wagogo na walimu wengine wamekuwa wakituhumiwa kwa tuhuma za wizi mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili nilikuwa naomba sana liangaliwe ili kusudi tuweze kuirudisha jamii yetu ya Kitanzania katika maadili ambayo yanastahili. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuchukua nafasi hii kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na nasema tena naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Mheshimiwa Margaret Sitta. Nami naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja Manaibu Waziri wake Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kipindi hiki cha miezi sita. Pia nachukua fursa hii kuwapongeza wataalam waliohusika na maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua fursa hii kuwapongeza watumishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Makao Makuu katika kada mbalimbali kwa ushirikiano wanaotupatia Waheshimiwa Wabunge wakati tunapokwenda kufuatilia masuala mbalimbali ya Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi nilionao sana katika Wizara hii sasa hivi ni kwamba wengi wao ambao wanatupa msaada ni watu ambao rika yao wanakaribia kustaafu. Sina uhakika kama Wizara imejiandaa vilivyo kuleta watu wengine ambao watakuja kuchukua nafasi zao katika ari ile ile na nguvu ile ile ambayo sasa hivi tunaiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru sana kama Mheshimiwa Waziri wakati wa ku-*wind up* atasema kwamba Wizara yake inaliangalia hilo kwa makini ili tuendelee kupata elimu bora katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na pia naipongeza Serikali kwa kuwa na Mipango mizuri ya kuendeleza elimu nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu nilionao mkubwa hasa ni katika maeneo yafuatayo:- Hebu tuangalie ni namna gani ya kufanya kwa kuwa sasa hivi lengo kubwa ni kufanya vijana wafaulu mitihani yao na wanafunzi wakishamaliza shule

ni kwenda kuangalia *results* zao. Hapo ndipo tunapotengeneza makundi mawili, kundi lile ambalo wamefaulu ambao wanajua njia ya kwenda na kundi lile ambalo hawakufanya vizuri ambao hawajui ni wapi pa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Wizara iweke mikakati au itafute uwezekano hata kama wa kiushauri kuwapa wale ambao hawakufanya vizuri katika mitihani yao warudi tena shuleni wapatiwe ushauri maalum wa namna gani ya kuendelea na maisha yao. Maana yake vinginevyo tutakuja kuwatengeneza vijana wa aina mbili, kesho na kesho kutwa vijana hao ambao wanashindwa kufanya vizuri katika mitihani yao wanaweza wakawa ni kero kubwa kwa nchi yetu. Sasa naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliangalie hilo ni namna gani wanaweza kuwasaidia vijana ambao hawakufanya vizuri katika mitihani yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma kulikuwa na *system* ya kuwa motisha walimu au Idara hiyo ya walimu kwa kuwapa *study tour* kwa mfano, Ma-*headmaster* au walimu wa kada mbalimbali walikuwa wanapelekwa nje angalau kuangalia nini kinachoendelea katika maeneo ya wenzetu ili wanaporudi waweze kutekeleza yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pamoja na kwamba Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni finyu lakini utaratibu huu ulikuwa ni nzuri sana. Wapo ma-*headmaster* wa zamani sana ambao waliwahi kupelekwa nje ya nchi na baadaye wakaendeleza elimu katika kasi nzuri sana. Kwa hiyo, naomba utaratibu ule pale inapowezekana uweze kurejewa kila baada ya muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninashukuru kuona kwamba maandalizi yanaendelea kufanywa ya kuboresha hali za walimu. Walimu wengi wako Vijijini na baadhi ya walimu hao kusema kweli wako katika maisha magumu, na baadhi yao wakipata ajira ya mwanzo inawachukua muda mrefu sana kupata mishahara yao na wale walimu wanaohamishwa inawachukua muda mrefu sana kupata mishahara yao. Naomba utaratibu ufanywe kuona hayo yote yanarekebishwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza pia kuona kwamba Wilaya kama ile ya Liwale sisi hatuna *DEO* mpaka leo hii, lakini unaweza ukakuta mwalimu amekaa mahali pamoja kwa muda wa miaka 20. Sasa sielewi kwa nini tunashindwa kumhamisha mwalimu ambaye amekaa mahali kwa muda wa miaka tano katika kituo kimoja na kumpeleka katika kituo kingine, lakini tukaweza kumhamisha *DEO* aliyekaa sehemu kwa muda wa miaka miwili na wakati mwingine mwaka haumalizi *DEO* anahamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba utaratibu huu uangaliwe upya kuona kwamba walimu wanakwenda katika *rotation* za uhamisho vizuri. Vinginevyo wengine wanakuwa ni kero katika maeneo yale walipo. Kwa mfano, katika Wilaya yangu kuna mwalimu wa *Primary School* katika Kijiji cha Lilombe amekaa miaka 20. Sasa ningetegemea kwamba hata Wizara yenyewe kwa kuwa ni hodari kwa kupata takwimu ingeweza kuzitumia. Sasa hizo takwimu ambazo inazipa Wizara ingeweza kuzitumia katika kutoa maamuzi mbalimbali inayoyaona pale Wizarani. Badala ya kungojea tu

Mbunge aende na suala moja la kushughulikia masuala hayo. Naomba sana Wizara itumie takwimu inazozipata kuhusu Idara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kurudi katika Jimbo langu la Liwale. Jimbo la Liwale lina eneo la *square* Kilomita 39,000 na asilimia 53 ya eneo hilo ni Hifadhi ya Wanyamapori. Naomba sana tunapojaribu kujenga Sekondari za Kata, eneo kama la Liwale Serikali izingatie matatizo tuliyonayo ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Hivi leo ninavyozungumza katika kipindi hiki tu cha Bajeti kuna wanafunzi wawili wamepoteza maisha yao nao ni wa darasa la saba. Mwanafunzi mmoja ni wa Mkundi ambaye aliuawa na simba akiwa darasa la saba 12 Mei anaitwa Mohamed Lipuka. Hivi karibuni tarehe 10 Julai, mwanafunzi wa kike darasa la saba pia Tumaini Ahmad naye ameuawa na simba katika kijiji cha Mtawatawa. Huu ni ushahidi tosha kwamba walimu wanaokaa katika maeneo wanahitaji majumba mazuri ya kuweza kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hivyo tu katika Shule za Sekondari ambazo tumezijenga kwa bahati Liwale tumejenga Shule za Sekondari nyingi sana sasa hivi ziko tano ambazo zinafanya kazi na tukichanganya na ya awali ziko jumla sita. Lakini hizi tano ambazo tunazungumzia hazijakamilika zina mapungufu mengi sana. Kwa bahati mbaya au kwa bahati nzuri kwa namna nyingine nafasi kwa wanafunzi waliomaliza darasa la saba Liwale wote wamepata nafasi ya kwenda Shule ya Sekondari. Lakini tatizo kwamba hatukuweza kujaza nafasi hizo zote, kilichojitokeza ni kwamba wanafunzi wa Wilaya jirani tumejaribu kuwapa nafasi hizo ili wajaze. Lakini wanafunzi hawa sasa hawana mahali pa kukaa ni wageni, hakuna hosteli na hali ya wanyamapori kama nilivyokuwa nimeieleza badala ya kuwasomesha wanafunzi au hawa watoto au hawa vijana wetu tutakuwa tunawahatarisha vijana wetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali isaidie na Halmashauri zetu na pia itoe mchango mkubwa wa kuona namna gani ya kuweza kudhibiti kwa kujenga hosteli. Wananchi tuko tayari kusaidia lakini na Serikali pia iwe tayari kutusaidia na kutoa mwongozo na kuharakisha ujenzi wa hosteli kwa ajili ya shule hizo tano ambazo sasa hivi zinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya walimu katika shule hizo pia hatuna nyumba za kutosha. Kwa kuwa shule hizo ziko katika vijiji au ziko kwenye Kata matatizo ni kwamba hakuna hata sehemu wanafunzi wanaweza kukaa kama wengine wanakaa kwenye madarasa ambayo sasa hivi hayatumiki.

Sasa watoto wanaotoka mbali hawana uwezo wa kupata *accommodation* nje ya shule. Kwa kuwa maisha ya maeneo hayo ni ya vijijini huwezi kupata nyumba ya kupanga kwa ajili ya mtoto wako. Sasa hiyo inahimiza kabisa kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kujenga hosteli haraka iwezekanavyo kwa kusaidiana na Halmashauri zetu. Naomba sana suala hili litekelezeke mapema iwezekanavyo kabla hatujaanza kuhesabu idadi ya wanafunzi walioathirika na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hivyo tu baadhi ya hizi Sekondari tulizokuwa tunajenga hakuna hata zahanati. Matokeo mtoto anavyoumwa usiku inabidi apelekwe

katika kijiji jirani kilomita kama kumi hivi kwenye dispensari, hakuna usafiri wa uhakika. Sasa hii pia inaleta matatizo na inahatarisha maisha ya vijana hawa. Naomba sana Serikali izingatie hayo yote ili mnapokuwa mnachukua takwimu za kila mahali na nyie muweze kuweka mwelekeo nini la kufanya katika kila Wilaya.

Hali ilivyo sasa hivi katika Wilaya ya Liwale ukiangalia Ofisi ya Wilaya ya Elimu kusema kweli inahitaji iboreshwe nadhani hivyo ndivyo hali ilivyo katika Wilaya zingine. Nawashukuru Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Sitta alivyotembelea Liwale ameona hali hiyo na pia sio mara yake ya kwanza kufika pale. Pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mwantumu Bakar Mahiza ambaye pia amefika ameona hali halisi ya Liwale. Tegemeo langu ni kwamba atalipa mchango mkubwa sana wa yale waliyoyaona na kujaribu kutusaidia namna gani tuyarekebishe kwa ushirikiano wao mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashukuru kuona kwamba Mama Mwantumu naye ni mlezi wa mkoa ule, kielimu. Kwa hiyo, naomba hilo pia ulitilie maanani ili uweze kuona kabisa hali halisi ya Liwale. Vinginevyo hali ya Liwale kielimu itaendelea kuwa duni au wanafunzi pamoja na kufungua hizo shule zote za Sekondari lakini watakuwa wanaogopa kwenda kusoma katika shule hizo. Kwa hiyo, naomba sana msaaada wa Wizara katika mazingira hayo tuliyonayo ya wanyamapori. Hayo nimetaja tu kwa ujumla, lakini wapo baadhi ya Walimu katika kijiji cha Ndapata kwa siku za nyuma ambao aliuawa na simba maana sio tembo sikumbuki vizuri. Lakini hiyo ndiyo hali halisi ya vijiji vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Liwale ni eneo kubwa lina *square meters 39,000*. Mkoa wa Lindi ina Wilaya sita. Ukichukua Wilaya tano zingine ukiziweka katika Wilaya ya Liwale bado Wilaya ya Liwale ni kubwa. Kutoka Liwale kwenda Lindi Makao Makuu ya Mkoa ni kilomita 250 kwenda na kurudi ni 500 gharama ni kubwa mno. Hata *REO* akitaka kufunga safari na kuanza kutembelea Wilaya zake pamoja na vijiji au Shule za Msingi ni kazi kubwa sana. Hata hizi Sekondari ambazo sasa hivi tunazifungua baadhi ya Kata itakuwa ni kazi kubwa sana. Naomba kabisa kwa dhati baada ya Waheshimiwa Mawaziri hawa kutembelea pale naomba *OC* inayokwenda Liwale iongezwe maradufu. Vinginevyo tutakuwa tunawalaumu Watendaji kwa kutotembelea maeneo yao kumbe hawana uwezo. Na sio hivyo tu hata bei ya mafuta sasa hivi imepanda. Bei ya mafuta Liwale nadhani sasa hivi imeshafikia zaidi ya 1,500 kama ni dizeli. Sasa hayo yatiliwe maanani kusudi Watendaji wetu wawe na uwezo wa kutembelea maeneo yao vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya walimu katika Wilaya yangu wamekuwa na matumaini makubwa sana hivi sasa kutokana na uongozi wa Mheshimiwa Waziri Sitta. Wanasema Waziri Sitta kabla ya hapo ndiyo aliyokuwa anafuatilia matatizo ya walimu. Kwa hiyo, wanaamini kabisa kwamba sasa hivi matatizo yale hayatakuwepo tena. Kwa hiyo, naomba sana kwa kutumia *standard* hiyo hiyo ujaribu kutusaidia wananchi wa Liwale ili tuweze kuokoka na matatizo ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Liwale kuna vijiji 42 na kuna Shule za Msingi zaidi ya 40. Shule hizo hazifikiki kirahisi wakati wa masika. Ninaomba basi

Wizara iwasaidie kwa kushirikiana na Halmashauri zetu waweze kupata gari la uhakika. Gari kule likitumika miaka miwili, mitatu basi litakuwa limeshachakaa kutokana na umbali na barabara zetu zilivyo. Sio hivyo tu kwa hizi Shule za Sekondari ambazo zimefunguliwa hivi karibuni pamoja na shule Kongwe ya Liwale Mjini tutashukuru sana kama Serikali au Wizara itatusaidia kupata angalau *school truck* moja ya kuweza kuangalia masuala mbalimbali katika shule hizo za Sekondari ambazo ziko sasa hivi. Vinginevyo wanategemea sana malori ambayo yanakwenda kuchukua nafaka mbalimbali. Kazi yenu kubwa sana itakuwa……..

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba yao nzuri ambayo imegusa karibu kila eneo. Pia nawapongeza Watendaji wote wa Elimu kwa kusaidiana na Mawaziri, Manaibu Waziri katika maandalizi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu ni machache tu kwa sababu mengi yameshazungumzwa na wengi waliotangulia na matatizo ya walimu pamoja na wafanyakazi wa elimu ni yale yale, mimi nina sehemu tu chache ambazo nitazizungumzia hapa. Kwanza nitazungumzia upungufu wa Walimu wa Sekondari. Kwa kweli katika Wilaya yangu ya Kilwa ni aibu kusema. Siwezi hata kusimulia maana yake ni aibu. Walimu walio wengi ambao ninasema ni idadi kubwa kidogo wako katika Shule ya Sekondari ambayo iko pale Wilayani ambayo kidogo inaridhisha kwa sababu pale wafanyakazi wengi wana wake zao ambao ni walimu kwa hiyo hii shule ina walimu wengi.

Lakini shule zilizobaki kwa mfano Mitole, Kipatimu pamoja na Matanda ni aibu. Matanda imediriki kubaki na Mwalimu mmoja ambaye alitoka Mtwara *Technical* kwenye fani ya umeme. Shule ambayo ina wanafunzi mpaka Kidato cha Nne Mwalimu mmoja tu alikuwa amebaki, wengine wote hawapo pale. Jamani hii ni shule nao wanafunzi wa madarasa hayo yote wanafundishwa na nani? Imefika hatua hata ya yule Mgavi ambaye ana *supply* chakula pale aingie darasani walau hata wanafunzi wapate elimu. Kwa hiyo, mimi hapa sina maelezo zaidi nategemea Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake, wataliangalia hili, ili waweze kutuletea Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni matatizo ya nyumba za walimu. Matatizo haya yamekuwa makubwa sana na nafikiri sio Kilwa tu ni sehemu zote. Lakini hivi karibuni nataka kusema kulikwenda Waandishi wa Habari kwa shughuli zao wakapitia baadhi ya shule. Waandishi wa Habari hao ni ndugu Mashaka na Ndomba walipitia pale hapa wakaangalia hali halisi. Kwa kweli nyumba walioipiga picha haifanani kukaa mwalimu ni nyumba hata kuku huwezi kumuweka. Kama alivyoeleza

mwenzangu kutoka Liwale Mheshimiwa Kigwalillo kule ni vijijini kuna wanyama wakali na hali hizo zote. Jamani nyumba ile iliyopigwa picha hata nyoka anaweza kupenya, hata kama hatapita mnyama mkali. Naomba liangaliwe hili. Mimi naahidi kulisaidia hili kwa njia moja. *(Makofi)*

Nilipokuwa naishi Mkoa wa Mtwara kuna Wilaya ya Masasi walikuwa na ONJAMA. ONJAMA maana yake ni Ondoa Njaa Masasi ambayo walikuwa wanashiriki wanakijiji wote kwa ajili ya kulima eneo moja kwa siku maalum ambayo imepangwa. Naomba utaratibu huu tuuangalie. Wananchi wa Kilwa tutajaribu kuwaelimisha ili kila eneo ambalo lina shule tuweze kukusanyana wanakijiji ambao wanafunzi wetu wanasoma pale, tupange siku maalum ya kuweza kujenga nyumba moja baada ya nyingine kwa kuweza kuwasaidia hawa walimu waweze kukaa mahali pazuri. Ninaamini nyumba za udongo ni nyumba sisi wote tumekulia kwenye nyumba za udongo. Kwa hiyo, tukiweza hata kuwasaidia kujenga moja baada ya nyingine kwa kusaidiana na walimu wenyewe, wanakijiji pamoja na wanafunzi nategemea kwamba walimu watakaa sehemu nzuri ukilinganisha na nyumba zile ambazo zipo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu huduma za matibabu kwa walimu. Walimu wanakaa sehemu ngumu sana na mazingira magumu. Lakini walimu hao hupoteza maisha kwa kukosa huduma. Kwa maana kwamba wanapotoka kule kijijini labda anaugua anakwenda ofisi ya elimu inakuwa ni taabu sana kupata fedha za kuweza kuwapeleka hospitali za rufaa. Kama wanapata basi hawapati kwa wakati muafaka mpaka hali ile ya ugonjwa inazidi. Hata kama wanapata basi ile fedha ndogo sana ambayo haikidhi mahitaji. Sisi wananchi wa Wilaya ya Kilwa tunategemea hospitali kubwa ni Ndanda pamoja na Dar es Salaam. Lakini mtu anapopewa shilingi 30,000 aende akajitibu Ndanda nauli kwanza kutoka Kilwa mpaka Ndanda ni kubwa, bado hajalipia matibabu yake au kwenda Dar es Salaam. Naomba Ofisi ya Elimu mliangalie hili kwa kweli wanapata taabu sana na ndiyo maana wanashindwa kukaa kijijini, fedha watapata wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia kwanza natoa shukrani kwa Wizara ya Elimu kwa kutoa magari ya Wakaguzi wa Shule. Nashukuru sana. Vile vile hapo hapo nataka kuzungumzia hali nyingine ni kwamba mimi Wilaya yangu ya Kilwa Mkaguzi wetu wa Wilaya hiyo amerudisha gari Wizarani lakini hadi sasa hajapata gari, sijui kama katika utaratibu wa haraka huu na yeye atapata au vipi? Lingine ninataka kuzungumzia hapo hapo kwenye Ukaguzi mazingira ya Kilwa. Kilwa ni eneo kubwa ingawa lina wakazi wachache. Kwa hiyo kwa ukubwa huu wa eneo hawa Wakaguzi wa Shule wanakosa ile fedha ya mafuta inakuwa ni ndogo kiasi kwamba wanageuka viombi wakati mwingine kwa sababu wanahitaji kutekeleza kazi zao na fedha ya mafuta ni ndogo. Naomba Wizara ya Elimu iwaangalie hawa watu ili waweze kuwaongezea isiwe bajeti hii hata bajeti ijayo walau iongezewe ongezeko la fedha ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia kuhusu magari ya Sekondari. Shule za Sekondari nyingi zilikuwa na magari lakini haya magari mengi yamekufa na shule hizi zinahitaji pia kupata huduma ya usafiri hasa zile ambazo ziko mbali na Wilaya kwa mfano za Bweni ambazo wanafunzi wanahitaji kupata huduma ya

matibabu na kadhalika. Kwa hiyo ningeiomba Wizara pia hili ilifikirie kwa baadaye hata kama sio bajeti hii kuweza kutengeneza hayo magari ya hizo Shule za Sekondari au kupata magari mengine ikiwezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuzungumzia hili suala ambalo nilizungumzia wakati wa semina pale Ubungo Plaza kuhusu nidhamu za wanafunzi na walimu. Kama alivyozungumza mzungumzaji aliyepita jana kuhusu Mwalimu ambaye alimpa ujauzito mwanafunzi. Mimi nalizungumzia kwa njia nyingine. Katika Wilaya ya Kilwa kuna shule hiyo ya Mitole ambayo wanafunzi wali-*miss behave* kwa kuonekana kwamba walikuwa wanadai chakula. Chakula kile wanafunzi sisi tunawapa fedha au tunawabebesha vyakula vile kwa hali ngumu kwenye mabaiskeli kila mtu kiwango ambacho anatakiwa apeleke shule. Chakula kikifika pale kinapikwa kwa wanafunzi wote. Lakini kile chakula kuna Mwalimu ambaye amekiiba kikaisha kabla ya wakati wanafunzi wamepeleka chakula cha kutosha. Hii ikatokea *scandal* kubwa ya kudai chakula chao hawapewi majibu ya kutosha matokeo yake wanafunzi wakaanza fujo zilizowapelekea kuingia kwenye nyumba ya Mwalimu. Fujo hizi zimekuja kuwa-*cost* wanafunzi lakini yule Mwalimu hivi ninavyosema bado yupo. Wanafunzi walisimamishwa kwa miezi kadhaa wale wazazi wenye uwezo wa kuweza kuwapeleka watoto *tuition* wao ili waweze kufanya mitihani yao ya Kidato cha Pili na Nne waliwapeleka lakini wenzangu na mimi walibaki kama walivyo watoto wao wakisubiri matokeo ya kurudishwa watoto shuleni. Baada ya hapo wanafunzi wachache walirudishwa shuleni wengine lakini wachache hadi leo hii bado wanalalamika kuhusu kurudi shuleni.

Nataka kuzungumza kwamba hili kosa ni kosa la Mwalimu wa pale na wanalitambua na Wilaya nzima pia inalitambua. Naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hili suala na ikiwezekana tuma watu ukaangalie huo ushahidi wa hilo eneo kuhusu hao wanafunzi hadi sasa hivi wanahitaji kusoma. Sisi tuko hapa kuwasaidia wanafunzi wanaopata ujauzito mashuleni waendelee kupata elimu. Je, wengine hawa ambao wanafukuzwa tu bila ya kupata ujauzito Mheshimiwa Waziri naomba hili uliangalie. Sisi Wilaya ya Kilwa ni maskini lakini umaskini wetu unatokana pia na kukosa elimu. Sasa watu wanapojitokeza kwamba wanahitaji kupata elimu halafu wanafukuzwa kiholelaholela hii naona itakuwa ngumu sisi tutaendelea kuwa maskini wa kutupwa milele. Naomba Mheshimiwa Waziri ulifuatilie hili suala na ikiwezekana hao wanafunzi warudi shule. Sihitaji kwamba huyo Mwalimu afukuzwe shule pengine naye kuna tatizo lakini nahitaji wanafunzi warudi shule na muangalie hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pia ningependa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa mlezi wa Mkoa wa Lindi. Pia namshukuru kwa juhudi zake ambazo amezifanya za kuzungukia katika maeneo ya Kilwa na kujua ugumu na na hali halisi ya walimu wanayoipata. Pia nazidi kumwomba pindi apatapo nafasi azungukie pia maeneo yale ambayo hajawahi kuzungukia aangalie hali halisi ambayo wanaipata walimu wa Kilwa.Mimi sina maelezo mengi zaidi ila naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa juhudi zao zote wanazozifanya nikitegemea kwamba Mheshimiwa Waziri alikuwa Rais wa Walimu na anajua mazingira

yote yanayowakabili Walimu nina hakika kitengo hiki cha Elimu pamoja na wafanyakazi wake kimepata mtu na kitafaidika vya kutosha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTH M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninayo heshima kubwa kutoa pongezi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba yao nzuri ambayo wameiwakilisha ni hotuba ambayo inatia matumaini makubwa hasa kwa upande wa elimu. Nampongeza Waziri na Manaibu Waziri, Makatibu na Watendaji wote wa Wizara. Pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya wananchi wa Mkoa Singida kwa imani yao kubwa ambayo wamenipa ili niweze kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Nami ninawaahidi kwa hofu kubwa ya Mungu kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kuchangia mambo machache sana katika hotuba hii ili kuweza kuboresha Wizara hii katika utendaji wa kazi. Napenda kuzungumzia hasa mazingira ya walimu walioko vijijini. Nadhani kila mtu anaelewa vijijini tunapozungumza kuna vijiji ambavyo viko katika mazingira mazuri na kuna vijiji ambavyo viko katika mazingira mabaya. Mazingira mabaya hayo kwanza ni vijiji ambavyo unatembea zaidi ya kilomita 15 ndipo upate usafiri au ukutane na barabara. Vijiji hivyo pia utakuta hata njia kwenda kwa baiskeli zingine inakuwa ni matatizo. Utakwenda kwa baiskeli lakini baadaye inabidi ushuke utembee kupisha vigogo au michanga.

Kwa hiyo ni mazingira magumu sana. Vijiji vingine vimezungukwa na mito. Mvua inaponyesha basi vijiji vingine vinakuwa kama kisiwa, walimu hao wapo katika maeneo hayo. Lakini pia wamekuwa wakifundisha katika mazingira magumu maisha wanayoishi nyumba zao zinakuwa ni nyumba ambazo kwa kweli hazistahili kama mwalimu. Nakumbuka wakati mimi nasoma ukiiona nyumba ya mwalimu unamheshimu yeye mwenyewe kama mtoto. Lakini sasa hivi mtoto anapoangalia nyumba ya mwalimu anaangalia na alikotoka hawezi kuona tofauti kwamba huyu ni mwalimu au ni mkulima wa kawaida. Hivyo naiomba sana Wizara iangalie kwa makini ili kuwafanya walimu waishi katika mazingira mazuri.*(Makofi)*

Mheshismiwa Naibu Spika, lakini bado pia kuna matatizo ya matibabu. Vijiji vingine unakuta hakuna hata dispensari hata kama ipo basi haina muuguzi, haina dawa, haina kitu chochote. Ni Mwalimu yule yule anahitaji pia kupata huduma. Basi unakuta wengine wanafunga safari kwa ajili ya kwenda kupata matibabu sehemu zingine kwa shida sana. Hivyo ninaomba bado tuone kwamba ni mazingira yaliyo magumu sana. Pia katika ufuatiliaji wa mishahara yao wanafuatilia katika mazingira magumu. Anamaliza wiki nzima akiwa anafuatilia mshahara wake na huko anapofika …hii kengele mbona imelia mapema sana. Hapana.

**NAIBU SPIKA:** Ya kwanza ya pili itakuja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Basi mimi ninaomba niishauri Wizara kwamba iboreshe mazingira haya kwa kutoa motisha kwa walimu wanaoishi katika mazingira magumu hasa kwa kuweka kitengo kitachofuatilia walimu hawa wanaofundisha katika mazingira hayo magumu. Kwanza ninashauri itoe mikopo ya pikipiki pamoja na mafuta kwa ajili ya walimu wale ili kuweza kujikimu na shida zao hizo na wengi wataweza kuvutika na kutokujisikia kwamba wametengwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda nizungumzie kwa haraka suala la upungufu wa walimu. Suala hili limekuwa la nchi nzima. Leo asubuhi nilikuwa nasikiliza taarifa ya habari kuna shule moja ya Kasinde Kapala Mbozi ambayo nimeiona kwenye televisheni kuku wako darasani pamoja na wanafunzi lakini walimu hakuna. Yuko mwalimu mmoja tu na ni shule ambayo imekuwa ya mwisho kitaifa na hiyo ni mfano karibu wa nchi nzima kwenye vijiji, shule zimekuwa hazina walimu. Ninaomba Wizara ielekeze nguvu zote katika shule zilizoko katika mazingira magumu iache kuanzia mijini.

Lakini pia labda nizungumzie kuhusu suala la majengo ya shule. Wizara ilipiga marufuku majengo ya Shule za Msingi kufanywa Shule za Sekondari. Kuna shule ambazo tayari zilishachukuliwa kuwa Shule za Sekondari. Zile shule wale watoto wamekuwa wakihangaika kufuata shule zingine. Hivyo ninaiomba Wizara si kwamba ifunge shule ambazo zimeshafanywa Shule za Sekondari lah!! Wizara simamie ujenzi wa shule zingine mbadala ili kuepusha matatizo ya watoto kwenda katika shule zingine mfano ni iliyokuwa Shule ya Msingi Kibaya wamehamishiwa Songambele. Sasa hivi imekuwa ni Shule ya Sekondari Ndago. Ninaomba Wizara ifuatilie kwa sababu kiwanja kimeshapatikana itoe fedha ili shule nyingine ijengwe. Hatusemi kwamba Shule ya Sekondari ambayo ilishaanzishwa pale ifungwe, hapana ijengwe shule mbadala. Wananchi wasitwishe mzigo wa kujenga ile shule nyingine. Wizara ifuatilie hilo. *(Makofi)*

Lakini pia napenda kuzungumzia suala lingine la Vyuo vya Ualimu kufanywa Vyuo Vikuu. Hivi walimu wale ambao walikuwa wakisoma pale watakwenda wapi, kuna upungufu. Shule za Sekondari kufanywa Vyuo Vikuu mfano Mkwawa wanafunzi wale walisambazwa nchi nzima kufanya Chuo Kikuu. Sasa kwa nini Serikali isiache yale majengo yaendelee kutumika kama Sekondari na yajengwe majengo mengine kwa ajili ya Vyuo Vikuu. Mimi naona ni usumbufu mkubwa hasa kwa wanafunzi wanaokuwa wanasoma katika maeneo yale. Sasa hivi tunasikia *Mazengo Secondary School* na yenyewe inataka kufanywa kuwa Chuo Kikuu. Sasa tunapunguza ile idadi ambayo tunasema kwamba tupige mbio ili tuongeze idadi ya wanafunzi halafu bado tunataka kupunguza idadi kama wanafunzi walikuwa ni 500 je, wale 500 watakwenda wapi, kuna mbadala. Kwa hiyo, ninaomba Wizara au Serikali iweke mpango na utaratibu mzuri wa kutokupora majengo ijenge majengo mengine yale yaachwe yaendelee. Vyuo vya Ualimu Chang'ombe sasa hivi kimekuwa Chuo Kikuu sasa wale walimu waliokuwa wakipata elimu pale ina maana ile idadi tayari imeshapungua na tuna tatizo la walimu. Hivyo ninaomba sana Wizara au Serikali iweke mpango mzuri kwa ajili ya kuendeleza fani ya elimu kwa kutokupora majengo mengine.

Lakini pia nataka kuzungumzia juu ya ujenzi wa hosteli za Wasichana wa Sekondari. Watoto wa kike wamekuwa wakipata shida sana, wanapanga kwenye nyumba za wenyeji maana Shule ya Sekondari ya Kata inakuwa mbali na mahali walikotoka inabidi wapange karibu. Mle wamekuwa wakiolewa matokeo yake wanashindwa kuendelea na elimu ya sekondari. Hata kwenye *data* zile tukiangalia watoto wa kiume wako juu zaidi kuliko watoto wa kike. Basi ninaomba Serikali iweke mkazo au iweke kipaumbele, itoe ruzuku kwa ajili ya hosteli za watoto wa kike ili tuweze kunusuru watoto wetu wa kike tuweze kuwa na akinamama wengi ambao wamepata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia suala la chakula shuleni. Sasa hivi tulipata takwimu kuhusu hali ya chakula. Ni baada ya muda mfupi sana watoto watakuwa wanashindwa kwenda shuleni kutokana na hali ya njaa. Basi yale maeneo yaliyobainishwa kwamba yana upungufu wa chakula. Wizara tafadhali ninawaomba muweke utaratibu katika shule ambazo zitaonekana zina shida kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwanza kabisa napenda kuwapongeza watendaji wote waliohusika kwa njia moja au nyingine ndani ya Wizara kutengeneza Bajeti hii. Bajeti ni nzuri na ikitekelezwa basi inaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kuleta maendeleo katika elimu. Napenda niwapongeze Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mahiza na Mheshimiwa Mwananzila kwa kuonyesha umahili mkubwa katika utendaji kazi. Hawa Manaibu Waziri ukiwaomba *data* au taarifa siku hiyo hiyo unaipata. Ni kwamba nawapongeza sana na hasa hasa kwa uwezo wenu wa kumudu maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Elimu Mheshimiwa Margaret Sitta, kwa kuteuliwa kuwa Waziri, walimu na watanzania kwa ujumla walifurahi waliposikia kwamba umechaguliwa kuwa Waziri wao, kwa sababu walijua kwamba wewe unayafahamu matatizo ya Wizara ya Elimu na ninaomba niwahakikishie walimu hawa na Watanzania hawa kwamba Serikali haikufanya kosa, kwa sababu kwa miezi michache uliyokaa Wizarani, tumeona kwamba sasa upele umepata mkunaji.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ni mengi yaliyokatika Wizara hiyo la kwanza ninalotaka kuzungumzia ni upungufu wa walimu. Kuna upungufu mkubwa wote wameongea, lakini upungufu mkubwa huu unachingia kwa wale wachache waliobaki sasa wana mzigo mkubwa sana. Mwalimu wa kawaida anayepaswa kufundisha vipindi 24 kwa wiki. Sasa hivi mwalimu anafundisha vipindi 50 mpaka vipindi 70, haiwezekani. *(Makofi)*

Mwalimu kazi yake si kufundisha tu darasani yeye anapaswa vilevile kusimamia *Extra Curricular Activities.* Anafundisha mwanafunzi nje ya darasa. Mwalimu mzuri baada ya hapo anapaswa kuondoka na madaftari aende kusahihisha nyumbani,

anakwenda kuandaa kwa siku inayofuata. Kwa hiyo, mwalimu hana muda zaidi wa kuweza kujifanyia kazi zake nyingine za kumletea kipato. Lakini mwalimu huyu huyu mshahara wake ni mdogo. Sasa naomba wakati watakapokuwa wanajadili jinsi ya kuongeza mishahara ya wafanyakazi mwalimu afikiriwe kwamba hana mahali popote pale ambapo anaweza kujipatia kipato cha ziada. Hata hizo kazi ya mwalimu wa kawaida huwa anakaa shuleni mpaka saa kumi na mbili, *boarding* wanakaa mpaka saa nne usiku lakini wanasema ualimu ni wito, hawalipwi hata *over time*. Kwa hiyo, tunaomba mishahara yao ipandishwe ilingane na kazi wanayoifanya.

Kuna matatizo makubwa kuna madai ya walimu makubwa sana, mlijaribu kulipa lipa lakini bado yapo. Hivi Wizara ya Elimu inakuaje tofauti na Wizara nyingine. Mtu alihamishwa tangu mwaka 2002 mpaka sasa hivi hajalipwa hizo gharama za kumhamisha. Aliajiriwa au alipandishwa cheo tangu mwaka 2003 mpaka sasa hivi hajapewa hiyo nyongeza, kwanini inakuwa tofauti kwenye wizara moja tu.(*Makofi*)

Nawashukuru Wizara ya Elimu sasa hivi wanajitahidi kuongeza namba ya walimu wanachukua vijana waliomaliza *Form Six* wanawapa *training* ya muda mfupi halafu wanawa-*post*. Lakini wakishawapeleka kule wanawatelekeza hawawalipi mshahara mfano ni wale walioajiriwa mwaka jana waliomaliza *form six* wakaajiriwa mwaka jana *August* mpaka sasa hivi hawajalipwa mshahara. Hivi mnafikiri hawa Wakuu wa Shule wanawatunza walimu hao kwa tumia kasma gani? (*Makofi*)

Hii inachangia watu wasipende ualimu wanahama ndiyo maana tunapata upungufu mkubwa wa walimu. Halafu walimu wengine mkiwapeleka kwenye maeneo kama ya Kagera wanarudi na visingizio, Wizara hiyo hiyo, mnawapangia kwenye mashule ambayo yako karibu. Ninaomba kama huo mchezo utaisha mwalimu akipangiwa kwenda Lindi au Kagera akikataa muacheni. Mkifanya hivyo wataendelea kukaa kule na uzoefu umeonyesha kwamba wale wanaokubali kwenda akishakaa mwaka mmoja anaona kwamba kumbe lile eneo ni sawa sawa na maeneo mengine na anaendelea kukaa. Basi naomba mkiliangalia hilo na mkawaangalia walimu waliorundikana mijini kama Dar es Salaam, *teaching load* ya mwalimu wa Dar es Salaam wengi ni masomo tisa kwa wiki, masomo kumi kwa siku na wale wakisambazwa kwenye mikoa basi utakuta kwamba upungufu huo utakuwa umepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ufaulu mdogo, lakini hebu tuangalie shule ambazo watoto wana-*perform,* ni *Seminaries* ni *private* na shule ambazo tunasema ni za watoto wenye vipaji maalum, wa vipaji maalum *of course* tunajua *brain* iko juu. Lakini hizi nyingine ni kwa sababu wana-*facilities*, wana walimu wa kutosha, wana madarasa ya kutosha na wanavitabu vya kutosha , ndiyo maana wanafaulu. Mashule yetu ya Serikali na ya wananchi hawafaulu kwa sababu hakuna walimu hakuna vitabu ndiyo maana hawafaulu. Lakini sasa kila mnapotangaza matokeo wasichana wanafanya vibaya, ufaulu wa wasichana uko chini. Naishukuru Serikali kwa sababu wamehakikisha kwamba namba ya wanafunzi wanaoingia *form one* wanaoanza darasa la kwanza na kwa kiasi fulani wanaoingia kidato cha tano, wanalingana wavulana na wasichana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hawa wasichana ni watu ambao tumeshasema kwamba wamegubikwa na matatizo makubwa sana tangu walipozaliwa, kwenye malezi na humo humo shuleni. Je, katika Bajeti hii labda Waziri atatueleza atafanya nini cha ziada kuweza kuhakikisha kwamba huyu mtoto wa kike sasa sio kuongeza namba tu katika shule za sekondari ni kuhakikisha kwamba anatoka na ushindi. Tunaomba hiyo mikakati tuisikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka watoto tunaotayarisha sasa hivi waweze kushinda kwenye soko na watoto wa nchi nyingine inabidi ufundishaji wa sayansi uwe tofauti. Nasikitika Waziri Mkuu hayupo, sasa hivi kuna kitu kinaitwa *alternative to practical*.

**NAIBU SPIKA**: Ipo Serikali.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru, kuna kitu kinaitwa *alternative to practical* mwanafunzi anaingia darasani mwalimu anamwadithia tu kwa maneno. Kwamba ukichukua kitu kinachoitwa *wire* ukaunganisha na kitu kinachoitwa *bulb* na nini sijui, ndivyo anavyomfundisha, *spanner* anaiona kwenye ubao tu imechorwa tu picha na sasa hivi tunashangaa kwanini maghorofa yanaporomoka huko Dar es Salaam. Ni watu ambao tumewaandaa tunawafundisha sayansi kwa maneno bila vitendo. Anapofika *form four* na mtihani unakua hivyo hivyo, *alternative to practical* anakaa anaandika wanamwambia ukichanganya kemikali fulani na kemikali fulani unatoka mgando wenye harufu fulani na rangi fulani. Hii ni kudanganyana. Sayansi lazima ifundishwe kwa nadharia na vitendo kama kweli tunataka tuendelee.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madeni makubwa sana ndani ya Wizara hii, hasa hasa mashuleni. Kuna madeni ya wazabuni, Wizara ilijitahidi kulipa. Lakini kwa sababu hawakulipa *on time,* watoto wako mashuleni wanakula mlilipa tangu mwaka jana mwezi wa tano,mmekuja kulipa mwaka huu mwezi wa tano, hivyo madeni ytameongezeka. Walikuwa wanaendelea kula, sasa madeni yamekuwa makubwa sana hata sasa hivi mkija kulipa mtakuta yameshakuwa makubwa kuliko yale mliyoyakuta na ninawahakikishia kwamba madeni yaliyo mashuleni nawahakikishia kwamba hayafahamiki Wizarani. *(Makofi)*

Hakuna taarifa kamili ya madeni, kuna madeni ya umeme, maji, ukarabati, vifaa vya kufundishia na madeni ya walimu, ni makubwa sana. Sasa ninapendekeza kwamba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake waende kwenye shule watumie njia tofuati wakusanye yale madeni kusudi waweze kuomba aidha Hazina iweze kuwapa kifungu cha kulipia haya madeni wakati wanaendelea kutumia fedha za bajeti kwa uendeshaji wa kawaida wa shule. Naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake waanzie Mkoa wa Kagera, na mikoa mingine yenye ina matatizo kama hayo muangalie uchakavu wa mashule na muangalie mrundikano wa hayo madeni na ikiwezekana ujipangie shule utakazo zitembelea. Nazungumza hivyo kwa sababu juzi juzi alikuja kiongozi mkubwa sana katika Serikali akatembelea Mkoa wa Kagera, tulipofika mahali fulani nikaona amechepuka ametoka kwenye barabara ya kawaida. Nikasema mbona sasa

hamkupitisha kule, wakasema ile barabara ni mbaya sana hatuwezi kumpitisha, nikawaambia si huko huko tumpeleke aone. Wakasema ni kiongozi mkubwa sana anategemewa na taifa zima akivunjika kiuno sasa itakuwa kasheshe.

Sasa ninaomba, kusudi usije ukonyeshwa shule nzuri tu ambazo hazina matatizo, chagua mwenyewe mwende mkaone, kuna mambo mabaya sana kule. Kuna kero kubwa sana kwa Wakuu wa Shule kukusanya ada, wao hawataki hii kazi, ila kwa sababu walipewa ndiyo maana wanafanya wazazi wahalipi wengine hawalipi kwa sababu hawana uwezo kwa nia njema kabisa Serikali mlitangaza kwamba karo mmeiteremsha. Kwa *day* mpaka shilingi 10,000, mkasema Serikali itachangia ruzuku ya shilingi 30,000 hamzipeleki. Hivi mnategemea Wakuu wa Shule wanaendeshaje shule kwa shilingi 10,000 kwa *term* inawezekana kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mpaka sasa hivi ninavyozungumza tangu mwaka umeanza Januari hazijapelekwa. Serikali iliahidi kuwalipia watoto ambao wanatoka katika mazingira magumu, ambao familia zao zinakipato duni wengine ni yatima wanamatatizo makubwa hadi leo mashule mengi hawajapata hizo fedha. Waliopata ni *form three* na *form four, form one* na *two* hawajapata watoto wa *form two* wameshindwa kujisajili kwa ajili ya mtihani kwa sababu ya Serikali haijalipa tangu mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamezungumzia chakula cha wanafunzi shuleni. Msipoangalia watoto watapata utapia mlo na watavia akili kwa sababu wali hawali ni *luxury*, nyama ni luxury, samaki hawali, mchicha hawali wanakula ugali kwa maharage kila siku Mkuu wa Shule akibadilisha anawapa makande ambayo ni maharage na mahindi. Kwa kweli ninapendekeza Wakuu wa Shule wameshaleta kwenye Wizara ya Elimu bajeti mbadala ambayo ni ya shilingi 1,260, kusudi waweze kumpa mtoto chakula, uji wa asubuhi, chakula cha mchana na jioni. Ninaomba mtueleza kama Serikali katika Bajeti hii, mtoto ambaye yuko kwenye shule ya bweni, mmemtengea kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu anaitwa Mkuu wa Shule, Mkuu wa Shule huyu ni mtu mwenye digrii, mbili tatu au *Diploma.* Asingekuwa mwalimu angeweza kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Wizara yoyote, angeweza kuwa hata kuwa Katibu Mkuu, angeweza kuwa Mkuu wa Mkoa au *DC*. Lakini anapochaguliwa cheo chake hata hakifahamiki, anaendelea na mshahara huo huo haongezewi hata senti tano. Mnawa-*frustrate* Wakuu wa Shule sasa hivi hata watendaji wa Kata hata makatibu Tarafa wamepewa hata pikipiki yeye hata baiskeli hamjawahi kumpa, na mshahara wake hauna hata *scale* yoyote.

Anachaguliwa Mkuu wa Shule, anajikuta kuna walimu walio chini yake wanaomzidi mshahara pale shuleni, anaendelea kuwa na mshahara huo huo sasa sijui akiishiwa aende kukopa kwa hao walimu anao wasimamia. Hivi kwanini Serikali inapata kigugumizi , inashindwa kutamka kwamba Ukuu wa Shule sasa hivi *it is a substantive post* badala ya kuwa *duty post,* na mshahara wake ukajulikana kuwa Mkuu wa Shule unaanzia kiasi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hili naiomba Serikali na lazima itamke kwanini hiki kigugumizi hakiishi mkatamka kwamba inakuwa *substantive post* na Mkuu wa Shule anaanza kwa kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tunadanganyana, kama tunataka kweli kuleta maendeleo haiwezekani tukaacha ku- *invest* kwenye *education.* Bajeti waliyopewa Wizara ya Elimu ya shilingi bilioni 239.65, ni ndogo sana. Tunategemea kupokea wanafunzi wengi sana, mwaka jana darasa la saba wamemaliza 400,000 hivi baada ya mwaka mmoja watamaliza milioni 1.4. Mwaka jana walikuwa wametengewa shilingi bilioni 109, mwaka huu zimeteremka zimekuwa bilioni 105, na tunasema kweli tunataka kujenga mashule kuwapokea hawa wanafunzi. Tutajenga na nini! Wizara hiyo hiyo imeongezewa na vyuo vya ufundi. Lakini Bajeti ya Maendeleo imekwenda chini, tunadanganyana. *(Makofi/Kicheko)*

Kama kweli tunataka kuleta mapinduzi katika elimu na kama kweli tunataka kuleta maendeleo katika Tanzania na kama kweli tunataka kuondoa umaskini kwa kupitia elimu lazima Bajeti ya elimu iende juu kusudi tuweze kutekeleza kutekeleza hiyo Mipango na Bajeti hiyo nilivyoiangalia asilimia 90 ya Bajeti hii ambayo ni shilingi bilioni 94, mnategemea fedha za nje. Zisipokuja ina maana kwamba hii mipango mizuri ya Bajeti ya ndani, fedha ambazo zitakusanywa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kitu alichosahau kufuatana na Kanuni ni ku-*declare* kwamba yeye alikuwa *Headmistress* wa shule fulani. Basi angesema hivyo wote mngemwelewa vizuri. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwanza kabla sijapongeza Wizara, napenda nipongeze utaratibu wa Ofisi ya Bunge ya kuhakikisha kwamba kila Mbunge anapata nafasi ya kuzungumza katikaBunge hili kwa kuona kwamba nani amechangia mara ya kwanza, nani amechangia mara ya pili na mara ya tatu. Hiyo inatoa nafasi nzuri kwa Mbunge yoyote anayetaka kuzungumza na anataka kuchangia mahali gani. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo na mimi nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo Mheshimiwa Margaret Sitta kwa kazi nzuri ambayo amewasilisha katika Bunge hili. Pia napenda niwapongeze Manaibu Mawaziri wote wawili na Katibu Mkuu wa Wizara, Afisa Elimu Kiongozi na wataalam wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri ambayo wamemsaidia Waziri kuandaa hotuba hii ambayo hatimaye imewasilishwa katika Bunge hili ili kujadiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze kidogo mazingira ya Wilaya ya Ngorongoro ambayo ni kati ya Wilaya ambazo ziko katika mazingira magumu. Kwa kweli Wilaya ya Ngorongoro. Kwanza, kufika Makao Makuu ya Wilaya kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambayo iko kwenye Tarafa ya Ngorongoro ni zaidi

ya Km. 200 na hakuna barabara ya uhakika ya kukufikisha huko. Kama wewe ni mgeni unakwenda, ukifika mpaka wa Serengeti na Ngorongoro unachukua *compus* unakwenda kwa mwelekeo. Unaambiwa utapita milima miwili inaitwa milima Matiti pita kushoto au kulia na kama hujasikiliza maelekezo vizuri unaweza kupotea. *(Makofi)*

Wakati fulani gari la mbio za mwenge lilipotea kabisa. Lilipata hitilafu baada kutengenezwa, ilipotengemaa kidogo dereva alipojaribu kuwafuata wenzake hakuweza kujua wamepita wapi barabara zimekuwa zaidi ya 1000 huko Serengeti. Kwa hiyo, hiyo gari imepotea mpaka leo hatuna taarifa nayo. Kwa kweli hali ya miundombinu ni mbaya sana. Lakini sio hilo tu, mawasiliano. Pia hakuna kwa maana ya simu.

**NAIBU SPIKA:** Hilo gari lilikuwa halina watu?

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwa na watu, lakini baada ya watu hao kuona hali imekuwa mbaya wakaitelekeza gari wakakaa umasaini na walipopata msaada walirudi mjini. Lakini gari ikawa imepotea jumla. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna pia mawasiliano na nilizungumza katika Bunge hili, tunayo mawasiliano ya *TTCL* lakini inaharibika mara kwa mara. Kwa hiyo, tunatengwa na ulimwengu mwingine wa Tanzania. Hakuna umeme, na sio viongozi wengi wanaoweza kufika kule. Lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye mwezi wa tatu alifanya ziara huko na aliona hali halisi na akatuhakikishia kwamba kwa upande wa elimu atamtuma Waziri wa Elimu au Manaibu wake waweze kufika Wilaya ya Ngorongoro na maeneo ya wafugaji kwa jumla kujaribu kuona hali halisi na ugumu wa elimu katika maeneo hayo. Namshukuru sana na nafikiri ahadi hiyo itatekelezwa hivi karibuni nasisi tuko tayari kushirikiana nao. (*Makofi*)

Wilaya hii inapakana na Wilaya Monduli, Wilaya Karatu, Serengeti, katika Mkoa wa Mara, Meatu katika Mkoa wa Shinyanga na Jamhuri ya Kenya hususan Wilaya ya Narok. Lakini pia kwa sababu wameanzisha Wilaya mpya ya Longido, tutapatakana nayo mipaka ikisharekebishwa. Kwa hiyo, ni Wilaya kubwa lakini ina matatizo mengi kama nilivyoeleza. Jambo jingine ambao nataka niliseme, tumesikia kilio cha Wabunge wa Kusini kuhusiana na barabara na mambo mengine kadha wa kadha. Ni kweli kilio chao ni *genuine*. Lakini huko inakoitwa kaskazini na maendeleo yaliyopo kaskizini hii kaskazini ikifunikwa namna hiyo inakuwa kama blanketi tu. Kwa sababu huko kaskazini kuna Wilaya kama ya Ngorongoro, kuna Wilaya ya Longido, kuna Simanjiro na Monduli kwa upande wa maendeleo hizi Wilaya zote si lolote si chochote ziko nyuma kimaendeleo. Kwa hiyo, tukifunika tu blanketi kwamba ni Kaskazini wamepiga hatua kwa kweli Wilaya hizi mnaweza mkasazihau na hivyo mtakuwa hamtutendei haki.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya hizi pamoja na matatizo ya maendeleo, Wilaya hizi zimewahi kutoa viongozi mahiri, viongozi wachapakazi kweli kweli. Mfano kila mtu anajua Marehemu Edward Moringe Sokoine, ambaye alifikia hatua ya Waziri Mkuu na Ndugu yetu Edward Ngoyai Lowassa Waziri wetu Mkuu wa sasa. Kwa hiyo, Wilaya hizi naomba Wizara inayohusika iendelee kuangalia kwa kweli kwa macho ya huruma ili watu hawa wasifunikwe katika blanketi hilo linaloitwa la maendeleo

Kaskazini. Lingine ni upungufu wa walimu suala hili limezungumzwa sana, mimi nina shida sana kwa sababu wakati fulani shule yangu moja inaitwa Mbarueli ni *Secondary School*. Tuliwasiliana na vyuo mbalimbali kuwapata walimu ambao watahitimu katika vyuo hivyo, na tukajaribu kuwashawishi ili wakihitimu vyuoni waweze kuja kufundisha katika shule zetu hizi.

Lakini baada ya kufanya kazi kubwa hiyo na tumekubaliana nao lakini baada ya kuhitimu kwa kweli Wizara iliwapangia katika mikoa mingine na barua tuliandika kwa Katibu Mkuu wa Wizara na kujaribu kuwaambia kwamba tumeomba watu hawa wakihitimu lakini bahati mbaya wamepangiwa kwingine, na hivyo tukawa tumewakosa walimu hao ni walimu nane.Lakini sio hao tu hata kwa shule za msingi, tumejaribu kuwasiliana na *TTC* ya Monduli tukaingia hata mkataba nao tumekubaliana nao kwamba mkihitimu chuo mje kutusaidia mmeshakaa kwenye mazingira haya mnayaelewa. Lakini bahati mbaya Wizara nayo ikawa imeshawapangia kwingine. Mimi mwenyewe nimechukua jukumu la kuwafuatilia hawa lakini nikakuta kwanza wasichana sita katika hao waliohitimu wameshaolewa. Kwa hiyo, nikapata tatizo sasa unafanyaje na mke wa mtu. Kwa hiyo, nikarudi kwa masikitiko.*(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, naomba hapa niseme kwamba kuna barua tumeandika na na nilipokwenda kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, alinisaidia sana, alinisikiliza na ndiyo hilo tukafuatilia lakini tukagundua wasichana hao wameolewa. Lakini baadaye nikamwambia kwamba sasa kwa sababu hawa wameshahitimu na kupangiwa basi katika hawa wanaohitmu sasa wajaribu kutukumbuka, hawa wengine ambao wamekwisha kwenda na haiwezekani tukawapata basi watukumbuke kwa hawa ambao wamehitimu vyuo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo naendelea kuliomba hilo kwamba mtusaidie. Nije sasa katika nafasi za kukaimu limezungumzwa pia hili sana. Nina afisa wangu mmoja huko Afisa Elimu amekaimu nafasi hiyo kwa mwaka mmoja na nusu sasa na aliyekuwa anamsaidia sana ni Afisa Elimu, Elimu ya Watu wazima. Huyu ameshastaafu na kwa hiyo hana msaada wowote. Sasa naomba kule Ngorongoro Loliondo kule huyu afisa aliyekaimu muda wote huo naomba kama ana sifa zinazokidhi matarajio na utaratibu wa Wizara athibitishwe vinginevyo tupatiwe mtu mwingine badala ya kuendelea kukaimu. Najua ukikaimu watu wengi wanasemasema hapa unakosa kujenga ile *confidence* ya kujiamini. Kwa hiyo, kwa kweli utaendelea tu kuwa ni mtu wa kuulizauliza hapa na pale hata jambo dogo ni lazima umuulize *DED*. Kwa hiyo, hilo noamba kwa kweli afisa wangu athibitishwe kwa nafasi hiyo kama sifa za kumwezesha kuchukua nafasi hiyo anazo athibitishwe. Jambo jingine ni tatizo la maabara katika shule yangu moja ya sekonadari inaitwa *Digodigo Secondary School*, ni mbali kidogo na Makao Mkuu ya Wilaya. Lakini uzuri wa hawa wamejitafutia kupita kwa wahisani fulani zana na vifaa mbalimbali vya *Chemistry, Biology* na *Physics.* Vifaa hivyo wanavyo lakini tatizo limekuwa ni jengo la maabara. Sasa hili kwa sababu lina kuwa na *Specification* linakuwa na ramani naomba Wizara itusaidie jengo hili la maabara kuel Digodigo sekondari

Mheshimiwa Naibu Spika, nina tatizo la ujenzi wa sekondari, Serikali imekuwa ikihimiza kwamba wanachi wenyewe wajijengee sekondari zao za Kata. Sasa kule

kwenye Kata yangu Lubalbal na Inekonoka, ni Kata ambazo tumekusudia kujenga sekondari mbili na hii kazi tumejitahidi huu ni mwaka wa pili.

Lakini tumepata tatizo na Baraza lile la mazingira. Baraza hili kwa kweli wahusika kule kila wakija kuchungulia wanaishia Makao Makuu ya shirika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, wanakweda kwenye eneo lile wanaangalia wanarudi. Sasa unakuta shirika linawagharamia lakini hakuna chochote tunachopata, hatupati matokeo tunayotarajia kupata. Sasa sijui kwa sababu tuko kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro tumo ndani ya maeneo ya wanyamapori. Lakini lile eneo siku zote nasema ni *multi purpose*. Kuna matumizi mseto pale, kuna shughuli zote za binadamu za maendeleo zinaendelea pale. Kwa hiyo, na kwa kuwa ndugu yangu Waziri wa Mazingira yupo hapa Mheshimiwa Prof. Mwandosya na kwa sababu ndugu yangu mama Hilda Ngoye, Mbunge na mwenzetu ameteuliwa na Rais hivi karibuni kuwa Mwenyekiti wa Baraza hili la Mazingira, nitaomba suala hili liangaliwe haraka ili wananchi hawa wasiendelee kukatishwa tama katika kujenga shule za sekondari. Nina shule chache sana kwa Wilaya kubwa kama ile nina sekondari nne tu kwa hiyo nataka angalau nifurukute nijenge hizo mbili, nifikishe sekondari sita. Sasa naomba *EIA* ifanywe na *NEMC.* Katika baraza hilo upungue ili tuweze kufanya hiyo kazi.(*Makofi*)

Mheshimiwi Spika, mwisho ni tatizo la mabweni katika maeneo ya wafugaji, watoto wa wafugaji hawa kwa kweli wanakaa mbali na maboma na huko ni kilomita kati ya 15 na 20. Anatembea mtoto anafika huko amechoka, kuna wanyama wakali maeneo yale, kuna baridi, kuna ukungu huoni njia kwa sababu Ngorongoro kule ni ukungu mtupu kwa karibu nusu mwaka mzima. Hakuna uji, hakuna chakula mahudhurio ni hafifu utoro mwingi wahitimu ni wachache na ufaulu kwa maana hiyo ni wachache sana. Lakini si kana kwamba hawana uwezo, wana akili sana. Lakini mazingira yanakuwa magumu sana. Kwa hiyo, tunaomba ruzuku katika chakula kama ipo iongezwe.( *Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu mkubwa wa walimu hasa katika mchepuo wa sayansi katika sekondari hizo. Naomba hilo nalo liangaliwe, lakini mwisho kabisa naomba kuunga mkono hoja.(*Makofi*)

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya elimu na mafunzo ya ufundi. Kwanza kabisa ningependa nianze kwa kumshukuru na kumtanguliza Mwenyezi Mungu kabla sijaanza kuchangia, kwa sababu naamini bila yeye unaweza usifanikiwe na kwa kupitia yeye ndio unaweza ukafanikiwa na hapa nikachangia, nikapata nguvu na ndiye anatuwezesha na sisi Wabunge kuweza kufanya mambo mazuri humu ndani. Kwa hiyo, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya hapo naomba niwapongeze wahusika wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi nikianza na Mheshimiwa Waziri, mama Margaret Sitta, nimpongeze pia Manaibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Mwantum Mahiza, pamoja na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Elimu pamoja na watendaji wahusika wengine wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwani wameweza kuitengeneza hotuba yao vizuri kabisa. *(Makofi)*

Lakini nilikuwa nina ombi moja kabla sijaanza kuchangia, nilikuwa naomba basi kama itawezekana, hizi hotuba angalau tungekuwa tunapewa siku moja kabla ili tuweze kusoma na kujua kile ambacho kimezungumzwa humu ndani na mtu ukisimama unachangia unakuwa tayari umekwishaisoma. Kwa sababu tunapewa vitabu hivi siku hiyo hiyo, na Mheshimiwa Waziri akisimama pale haisomi yote, anaenda tu vifungu vichache. Kwa hiyo, unashindwa kujua kwa haraka haraka kama hiki ambacho nataka kukizungumza kimeshazungumzwa humu na kiko vipo.

Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni ombi kwa mfano kesho ni Wizara ya Elimu ya Juu, tungekuwa tunapewa leo kabisa hotuba hizi ili anapomaliza tu Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, unakuwa tayari ulikwishaisoma kama ni jana yake uweze kuielezea vizuri. Na ombi la mwisho ni kuhusiana na saa kama kungekuwa na uwezo na sisi tukawekewa angalau visaa vidogo katika meza zetu ambavyo vinaonyesha muda unachangia, ukiangalia sasa unajua imebaki dakika moja, unamalizia haraka haraka *points* zako sio tena kugongewa kengele. *(Makifi)*

**NAIBU SPIKA:** Hiyo nyingine ni kazi rahisi sana, vua saa yako weka hapo mezani, angalia.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Sawa sawa!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba nianze kwa kuchangia katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwanza kabisa ningependa kuwazungumzia watoto wa mitaani, watoto wa mitaani, wako wengi sana katika nchi yetu, na wamejaa sana katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mkoa Dodoma, pamoja na mikoa mingine. Nakumbushwa hapa naambiwa pia Morogoro pia ipo, Mheshimiwa Lotto ananikumbusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watoto hawa tukumbuke kwamba ni watoto wa Tanzania. Watoto hawa wanahitaji elimu kama ambavyo anatakiwa apate mtoto mwingine yeyote. Wengi wa watoto hawa wamepoteza wazazi na wengine hawana ndugu na ndio maana wanakuja kukaa mitaani na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ijaribu kupanga mkakati ambao utasaidia kuwachukua watoto hawa wa mitaani na kuwapatia elimu, hata ikiwezekana basi kwa sababu kuna nchi nyingine kwa mfano India pia ina watoto wengi sana wa mitaani, lakini wao wana utaratibu kwamba huwa wanawachukua watoto hawa asubuhi wanawapitia na mabasi, wanawapeleka shule, ikifika jioni wanarudishwa kule kule mitaani. Nadhani wameshakubali kwamba tatizo lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba hii pia ifanyike hapa na kama haiwezekani kwa mitaani, basi Mheshimiwa Waziri angeenda katika vituo vya kulelea watoto yatima au vituo vya kulelea watoto wa mitaani kwa mfano *Dogodogo Centre* ama *Kiwohede,* waangalie ni jinsi gani wanaweza wakawapa elimu ya *MEMKWA,* jinsi gani

wanaweza wakawapatia elimu ya *MEMKWA* yaani Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa Walioikosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hawa ni watoto wetu, kama wataendelea kukaa mitaani na hawapati elimu, hakuna mtu yeyote anayeweza kuwajali, watafikia mahali pabaya kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama nchi yetu itaondokana na umaskini kama watoto wataendelea kukaa mitaani bila kupata elimu, wanajifunza tabia ambazo sio nzuri. Mimi naamini mtoto akashapewa elimu kutoka pale mtaani, basi anaweza akapata elimu ya pia kujua kumbe hapa mtaani ninapokaa mimi hapanifai, nahitaji kuondoka, nahitaji kwenda kufanya kazi mahali fulani. Baada ya kupata elimu anaweza hata akaenda kuomba kazi japo si katika sehemu kubwa sana, lakini kulingana tu na ile elimu ndogo ambayo ameipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri alisikie hilo na atanipa majibu kama inawezekana ama haiwezekani na kama itakuwa haiwezekani, anipe sababu ni kwa nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusiana na usafiri wa wanafunzi. Usafiri wa daladala kwa wanafunzi limekuwa ni tatizo kubwa sana na kila siku linazidi kupigiwa kelele. Hapa nataka nizungumzie usafiri wa daladala kwa wanafunzi hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini vile vile nauli ya mwanafunzi ambayo anatakiwa kulipa kwa Mikoa, kwa mfano Mwanza, Mbeya, Arusha na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa Dar es salaam mwanafunzi akiwa na kitambulisho, analipa shilingi 50/= anaruhusiwa kuingia katika basi. Lakini kwa Mikoa ya Mwanza, Mbeya na Arusha, wanafunzi hawaruhusiwi kutumia vitambulisho na nauli inakuwa ni tofauti. Tunaambiwa kwamba analipa nusu ya nauli ya mtu mzima. Sehemu nyingine yaani hakujawa na utaratibu rasmi ambao umepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ataweza, atutangazie viwango vya nauli vya elimu kwa wanafunzi wote nchi nzima na hili liwe ni tamko rasmi kabisa la Serikali kwamba mwanafunzi anatakiwa alipe nauli kiasi fulani na isiwe Dar es Salaam wanalipa shilingi 50/=, Mwanza wanalipa shilingi 100/=, wengine wanalipa shilingi 150/= na wengine wanalipa shilingi 200/= yaani hakuna utaratibu mzuri ambao umepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Wakala wa Kusimamia Usafiri Majini na Nchi Kavu *(SUMATRA),* watutangazie viwango halali vya nauli ambavyo mwanafunzi anatakiwa alipe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa usafiri wa daladala, Dar es Salaam imekuwa ni kero sana, nilishazungumza na leo nazungumza na nadhani pia kuna Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakizungumza. Mimi nashindwa kuelewa tatizo liko wapi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tatizo ni nini mbona sielewi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda ukurasa wa 77 wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naona hapa ameorodhesha mashirika pamoja na wahisani ambao wanaisaidia Wizara hii ya Elimu. Kwa haraka haraka nimejaribu kuhesabu hapa nimegundua kwamba kuna wahisani 14 na nimegundua kuna mashirika 31 ambayo yanaisaidia Wizara hii ya Elimu na mwisho amemalizia kwa kusema na mashirika mengineyo kwamba yapo na mengine, lakini nadhani labda nafasi ilikuwa haitoshi ndio maana hayakuwekwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wizara hii ina utitiri wa wahisani pamoja na utitiri wa mashirika. Inaamanisha kwamba mnapata misaada mingi sana. Mimi ombi langu ni moja tu kwa Mheshimiwa Waziri, kama misaada ambayo wanapewa ni mingi kiasi hiki, basi hii misaada itumike katika yale maeneo ambayo labda wahisani wetu wameomba, wanataka kuingiza fedha zao hapa. Lakini kuwe na utaratibu wa Wizara kuwaambia sasa hivi madarasa tumeshajenga ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vitabu viko vya kutosha, sasa hivi vile ambavyo tulikuwa tunavihitaji, tunaomba basi mtoe hela zije katika usafiri au kama ile haliwezekani, wakati wao wanaendelea kutoa hela hizi katika maeneo ambayo wanayataka, basi ile bajeti ambayo inatolewa na Serikali, bajeti yenyewe halali kupitia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, muangalie kama inawezekana mkaingiza huko, tuanze angalau hata na mabasi matano ya kuanzia kwa wakati huu ambao tunaanza, wakati tukiwa tunaenda taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, aliangalie hili. Wanafunzi wananyanyasika sana. Labda Wabunge wanaweza wasilione hili kwa sababu baadhi ya watoto wao wanasoma katika shule za Kimataifa ambapo wanakuja kuchukuliwa na mabasi asubuhi, wanarudishwa, wengi wao wanasoma katika shule za *Academy*. Wazazi wengi ambao wana uwezo wanawapeleka watoto wao shule kwa usafiri wao wenyewe. Lakini wanaoathirika zaidi hapa ni watoto wa walalahoi, watoto ambao ni maskini, Watanzania wasiokuwa na uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kama ni jambo la dharura ili aweze kutoa usafiri kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na mikoa mingine ambayo inapata matatizo ya usafiri huu wa daladala.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwafikirie wale watoto ambao wameamka asubuhi, anakaa kituoni kuanzia saa kumi na moja mpaka inafika saa mbili asubuhi hajachukuliwa na basi yaani naongea kwa uchungu mkubwa sana, natumai Mheshimiwa Waziri atalisikia hili na atanipa majibu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiachana na hilo, naomba niingie katika unyanyasaji wa kijinsia na ubakaji kwa wanafunzi wa kike, watoto wa kike wakiwa shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa kike wamekuwa wakinyanyaswa sana na walimu wa kiume, sisemi kwamba ni wote, lakini wapo baadhi ya walimu wa kiume ambao wamekuwa wakiwatongoza watoto hawa wa kike na pindi wanapowakataa, basi

utakuta mwalimu akiingia darasani anamtoa mwanafunzi nje, anampa adhabu za mara kwa mara, viboko haviishi yaani wanakuwa wananyanyasika sana watoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yako sana hata jana Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge, alielezea suala la mwanafunzi wa Jimboni kwake jinsi alivyoathirika. Nina mfano wa wanafunzi kutoka shule ya Ngara, nina mfano pia wa tatizo hili hili kutoka shule ya Ruvu na shule nyingine. Kwa hiyo basi, mimi ninachoiomba Serikali, kwa sababu tatizo hili lipo na limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu sana, naomba Wizara iweke mkakati mzuri, iundwe hata Tume kama inawezekana ya kufanya uchunguzi wa kutosha na iletwe sheria mpya ambayo itakuwa inawabana kwa nguvu kabisa walimu hawa ambao wanawanyanyasa watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikigundulika kweli mwalimu amemnyanyasa mtoto wa kike kijinsia, basi naomba iwekwe sheria kali kabisa ambayo itawabana. Tuwasaidie wanafunzi wa kike ambao nao pia wanahitaji elimu. Nasema zaidi wa kike, wakiume siwataji hapa kwa sababu wao huwa hawana sana tatizo hilo la kutongozwa na wanaume, ndio maana nawazungumzia watoto wa kike zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni tatizo ambalo yaani nimekuwa kila siku nikilifikiria, kila siku naliangalia. Nasema laiti ningekuwa na uwezo, ningeweza kuwasaidia watoto hawa. Lakini uwezo nilionao ni mdogo, sitoweza kuwasaidia wote, ni tatizo la watoto kwenda shule pekupeku, bila kuvaa viatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tatizo lipo, kama unakaa mjini unaweza usilione. Lakini kama umebahatika kupita vijijini na uzuri ni kwamba mimi nikitoka kwa mfano Dodoma kuelekea Dar es Salaam, njia ambayo napita, hii njia ya kutoka Dodoma kulelekea Dar es Salaam, kila si ku napishana na wanafunzi ambao hawana viatu, sembuse ndala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndala tu yaani ndala ni tatizo hata mtoto anashindwa kuvaa, wanapita. Tunasema sawa elimu yetu tunasema ni elimu bora, tunawasaidia watoto. Madarasa ni mazuri, wana vitabu, walimu wapo, lakini, mtoto anapoenda shuleni hajavaa kiatu, hata ndala tu hana, inakuwaje? Serikali yetu inaliangalia suala hili kwa ari mpya, nguvu mpya, kasi mpya, maisha bora kwa kila Mtanzania! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,  mimi naomba nitoe pendekekezo moja, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, izungumze na wafanyabiashara hawa wenye viwanda, basi watengeneze angalau viatu ambavyo ni vya bei ya chini kabisa ambayo hata mzazi wa kijijini anaweza akanunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, utengenezwe tu utaratibu wa kutengeneza viatu ambavyo ni vya bei ya chini kabisa, hata mia tano, elfu moja. Utashangaa kiatu kiuzwe mia tano, lakini kwani Serikali inaona hasara gani kama italipia ile hela nyingine iliyoongezeka. Kama hakuna utaratibu wa kuweza kuwagawia bure watoto hawa viatu wakavaa, lakini basi viuuzwe kwa bei rahisi, kwa sababu mimi naamini mzazi hawezi

kumruhusu mtoto wake aende shule pekupeku. Wazazi tuna upendo sana hasa akinamama. Lakini kama inafikia hivi kwamba mtoto anakwenda shule yuko pekupeku, ni kwamba mzazi hana uwezo kabisa. Basi Serikali tunaomba ijaribu kwasaidia hawa wananchi wa hali ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto akienda kwanza anapokwenda shule akimwona mwenzake ana viatu, yeye yuko pekupeku hata kiatu hana, inamwathiri kisaikolojia mtoto huyo, atashindwa hata kuendelea na masomo vizuri. Kwa hiyo, naomba tuweke utaratibu mzuri, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, mtengeneze viatu vya bei rahisi kwa watoto basi angalau wazazi wao waweze kuwanunulia, wavae, waende shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililonalo ni kuhusiana na elimu ya kujitegemea. Mimi nadhani ni wakati muafaka sasa wa kurudisha elimu ya kujitegemea kama ilivyo kuwa wakati wa miaka ya nyuma. Nalisema hili kwa sababu wanafunzi darasa la saba ni wachache, wamekuwa wakipata nafasi na wengi pia tumeambiwa wanafaulu, lakini kwa sababu nafasi zinakuwa hamna. Wale ambao wazazi wao wana uwezo watawapeleka katika shule za kulipia na wengine watapelekwa hata nje ya nchi. Lakini kwa mtoto ambaye amekosa nafasi yaani hajafaulu kuendelea na kidato cha kwanza na mzazi wake hana uwezo, hatoweza kuendelelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba nitoe pendekezo katika maeneo mbalimbali kulingana na mazingira. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ijaribu kuweka mitaala kwa mfano watoto wa elimu ya shule ya msingi yaani darasa la kwanza mpaka la saba, angalau wafundishwe kupika, wafundishwe useremala. Kama wako maeneo ya maziwa, mito, afundishwe uvuvi jinsi ya kuvua samaki, kilimo, ili mtoto anapomaliza darasa la saba, hajapata nafasi, mzazi wake hana uwezo, aweze kwenda kufanya hizi kazi yeye mwenyewe kutokana na ujuzi ambao tayari amekwisha kuupata katika ile elimu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi aliangalie hili. Wazazi wetu miaka ya nyuma elimu ya kujitegemea ilikuwa inapatikana lakini kwa sasa hivi sijui kimetokea nini, imekuwa haitolewi. Kwa hiyo, naomba Wizara iweke utaratibu huo ili mwanafunzi anapomaliza darasa la saba angalau aweze kwenda kujiajiri mwenyewe kwa kufanya shughuli za useremala au hata akienda kuomba kazi awe na ujuzi kwa sababu si wote ambao wana uwezo wa kuendelea na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni hali mbaya zilizoko katika baadhi ya shule za kulala wanafunzi, kwa mfano kukosekana kwa maji ama wanafunzi wawili kulala kitanda kimoja kutokana na ukosefu wa vitanda kwa mfano shule ya Ruvu Sekondari pale, wanafunzi wanalala wawili wawili, wanaambukizana magonjwa ya ngozi. Naomba Wizara ilitambue hili, maji hakuna, mwanafunzi akiamka asubuhi anaenda kuteka maji, maji anakosa inabidi akanunue. Maji ya kunywa tu yanakuwa hakuna. Naomba tulifikirie mara mbili mbili. Wamekuwa

wakipata matatizo sana na hasa matatizo ya kuhara na kama mtakuwa mnahitaji takwimu na mifano halisi nitaomba mnione.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni moja tu ya shule ambayo nimetolea mfano wake lakini ziko shule nyingi tu za sekondari nyingi tu za Serikali ambazo zinakosa huduma muhimu ikiwemo hata *dispensary* ya pale pale shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, fikiria tu ya kwamba mzazi hata ada ya kumlipia mtoto wake hana, ataweza vipi tena kumuonbea hela ya kununua maji, labda ampelekee tena na kitanda ndiyo ataweza... yaani... Naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, alisikilize hili kwa makini na ajaribu yeye mwenyewe kufanya ziara katika baadhi ya shule na ikiwezekana hapa hapa Ruvu ambapo nimetolea mfano. Akaone hali halisi jinsi ilivyo pale na aone basi ni jinsi gani anaweza akawasaidia watoto hwa ambao wanapata tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwaombea walimu wetu, najua mishahara imepanda lakini naomba ipande zaidi na zaidi. Tuwafikirie walimu ni watu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe naamini umefika hapo kwa ajili ya walimu, walikupa mwongozo mzuri toka ulipokuwa shule. Mimi mwenyewe naamini nimefika hapa kwa sababu ya walimu ambao wamenipa mwongozo mzuri kabisa, wamenifundisha. Wamenifundisha kujiamini na mambo mengi. Wabunge humu ndani ninaamini wote kwa pamoja tumefikia hapa kutokana na msingi mzuri tuliotengewa na walimu wetu.

Basi, naomba muwe mnawakumbuka na kugundua kwamba walimu ni watu muhimu sana tena sana. Wanahitaji kuangaliwa kwa jicho la huruma. Kama msemaji mwingine aliyetangulia alisema hawana marupurupu. Mshahara wao basi naomba uongezwe ili uwe mshahara mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu nao wawe wanapata semina angalau safari za kutoka shule aliko na kwenda sehemu nyingine, shule nyingine kuangalia wenzao wanafanya nini, angalau tu kujifunza na hizi safari za nje pia zinazokuja Wizarani, wasiende watendaji tu nje ya nchi kusoma, walimu pia nao wapelekwe, wapate hizi safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwafikirie sana walimu wetu wana mazingira magumu. Serikali ya Awamu ya Nne ninaamini kwa ari mpya, nguvu mpya, kasi mpya, yote haya yanawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia hapo basi naomba niseme naunga mkono hoja mia kwa mia lakini, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi nitahitaji majibu ya maswali yangu yote ambayo nimeuliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nasikia unaongea kwa haraka, sijui *Hansard* itapatikanaje huko! *(Kicheko)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuwapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Mawaziri wake wawili na watendaji wa Wizara hii, wote kuanzia ngazi ya juu kabisa mpaka wafanyakazi wa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo kioo cha Taifa, Wizara hii ndiyo inaweza ikamwelekeza Mtanzania yuko katika eneo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nayazungumza haya kwa sababu utajua kabisa kwamba ukitaka kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine, lazima upate elimu na wanaofanya kazi hii ni Wizara hii hii. Kwa hiyo, wana kazi kubwa na ni lazima tuwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa muda mfupi, kazi ambayo kwa kweli Watanzania kwa ujumla wameiona na Watanzania wanaisifu. Kwa hiyo, lazima tuwasifu kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kiongozi ni legelege, basi ujue kabisa kwamba hata utendaji kwa watendaji wengine wanakuwa hawawezi wakafanya kazi inayostahili. Kwa hiyo, ningependa nitoe pongezi hii kubwa kwa Wizara hii kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wilaya ya Geita tukitaka kutoka hatua moja, tulikuwa tunazungumza kuhusu elimu na ndiyo maana tunazungumzia umaskini. Umaskini wa Geita umetokana na kutokuwa na elimu kubwa ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo na madhumuni makubwa tuliyojiwekea katika Wilaya yetu ya Geita, tukasema tunaenda kwa muda wa miaka kumi. Miaka kumi, lazima Geita ibadilike na hatutaweza kubadilika, lazima tuwe na elimu na ndio maana mikakati mikubwa ya ziada ikafanyia mpaka ikaishinda Serikali. Kwa hiyo, hiyo ndio mikakati yetu ya kuijenga Geita iwe katika hali nzuri. Lakini tulichokiona ni kwamba msingi mkubwa lazima tu-*invest* kwenye elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba kabisa Waziri atuelewe sisi wana Geita tuna lengo gani na ndio maana unakuta kwamba sasa hivi hatupigi kelele hata masuala ya madini. Tumeona kwamba baada ya miaka kumi, uchumi wote wa Geita tutaushika sisi wenyewe. Sasa Wizara hii isituangushe. Naombeni sana wasituangushe, twende sambamba kuleta elimu katika Wilaya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunazungumza haya muda mrefu na hata katika majukwaa, tulikuwa tunawaambia jamani, ukitaka kujikomboa lazima usome. Walioko wasomi wengi unakuta kwamba ndiyo kuna maendeleo. Ukitaka kuwa na maendeleo, lazima umsomeshe mtoto wa kike. Ukimsomesha mtoto wa kike, lazima utakuwa umeishasomesha watoto wawili, kwa sababu gani! Mwanamke akisoma, akiolewa, hata aolewe Mtwara, basi wa Mtwara atakuja maeneo yale na ndiyo maana wenzetu wa Kaskazini waliwasomesha watoto wa kike na wanaume wengi wakakimbilia huko huko.

Sasa tumeishabadilika sasa hivi, tumewaambia kwamba ndugu zetu wana Geita tuwasomeshe watoto wa kike na sasa hivi kuna mtiririko mkubwa sana na ninawashukuru sana wananchi wa Geita na wazazi wote wa Geita, wameonyesha mfano mmoja mkubwa sana na ndiyo maana unakuta kwamba Wabunge walionitangulia, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, tuliomba kwamba nguvu za wananchi walizozitoa kwa ajili ya kujikomboa kielimu basi izione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga maboma yako pale pale na nasikitika Waziri alinijibu akaniambia kwamba tumeyajenga majengo hayo kwa kiwango cha chini. Siyo kwa kiwango cha chini Mheshimiwa Waziri. Majengo yale, hata kama utaweka gari bila kulifanyia kazi yoyote, utakapokuja kulichukua, siku unalipolichukua, litakuwa ni bovu. Kwa hiyo, hata kama utajenga nyumba yako ya *block* kiasi gani, ukiacha hivi hivi bila kuweka nguvu yoyote pale, kesho na kesho kutwa utakuta kuna ufa. Kwa hiyo, majengo yale tumeyajenga kuanzia mwaka 2003 na 2004, lakini wananchi wanayapigia kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, naiomba Serikali iwaonee huruma wananchi wa Geita kwa nguvu waliyoitoa ili waweze kukamilisha majengo haya. Haya majengo si kwamba wameyaweka tu, wameyaweka kwa ajili ya mikakati ambayo tumejiwekea. Naweza nikatoa mfano mmoja, wakati tunaingia madarakani, tunapata Ubunge mwaka 2000 Wilaya ya Geita ilikuwa na shule za sekondari tisa tu, lakini katika tisa zile, shule za Serikali zilikuwa sita na tatu zilikuwa za wakulima. Tukalazimika kuzihamisha zile za wakulima mbili ziingie kwenye shule za Serikali. Nashukuru Serikali ilikubali. Lakini tukahamasisha kila Kata ijenge Sekondari. Mpaka kufikia mwaka 2005 Wilaya ya Geita mpaka sasa hivi ninavyozungumza, ina shule 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jiulize mwaka 2000 mpaka leo tulikuwa na shule sita tu za Serikali, leo hii tuna shule 34 za Serikali na zote zile zimejengwa kwa nguvu ya wananchi. Sasa naiomba Serikali iwaangalie wananchi wa Geita na kuweza kuwahurumia. Tumejenga maboma katika shule za msingi, lakini hapo hapo tumetoa nguvu, tumeweza kujenga sekondari hizi. Hakuna Wilaya ambayo inaweza ikafanya kazi kubwa kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kazi imefanyika kwa Wilaya ya Geita, kwa nini sasa Serikali isitupie jicho kule ikasema kwamba kwa kweli wana Geita mmefanya kazi nzuri, basi na sisi tumewapa zawadi hii. Kweli mnaleta pesa za *MMEM* au za *MMES,*

lakini pesa za *MMEM* unakuta ni ndogo mno. Mheshimiwa James Musalika, jana alibainisha akasema kulikuwa na maboma 1000 na kitu, Serikali na Halmashauri waliweza kuezeka maboma 200 tu, maboma 800 bado yako pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ili kuweza kuhamasisha na kuweza kutovunja nguvu za wananchi wa Geita, ilione suala hili kama ni suala la kuweza kuwakomboa wana Geita na tusiwe watu wa kuweza kunung'unika kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, waweze kuliona hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mmoja ni mzuri kabisa, kwa sababu unaweza ukasema kwamba labda wana Geita wanajizungumzia tu, wanatafuta msaada wapate Serikalini. Lakini kuna Afisa Elimu Kiongozi, Bwana Mpama, tulimwambia njoo Geita, nashukuru sana alikuja. Tukamwambia orodha ya shule za sekondari kama unataka kuziona ni hizi hapa, chagua sekondari mojawapo au sekondari yoyote, sisi tutakupeleka kwa gharama yetu. Akachagua, tukampeleka. Alienda shule tatu tu, akasema basi tumesharidhika na zote zile alijichagulia mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, ombi maalum, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Serikali imekuwa na kigugumizi kwa kutokutambua kwamba haya tunayoyazungumza ni ya kweli, yanaonekana kama ni ya uzushi, basi afanya ziara maalum aseme kwamba kuna shule iko wapi ya msingi, tutakuorodheshea shule zote za msingi. Achague shule zozote zile kwamba anataka kwenda kuyaona haya maboma, basi, shule yoyote katika Wilaya ya Geita kuna maboma ya madarasa na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na upungufu wa walimu kwa kutokuwa na nyumba, lakini Geita umeishajenga. Sasa ili walimu waweze kukaa pale, basi tumalizie zile nyumba za walimu ili walimu waendelee kukaa katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tena Mheshimiwa Waziri atakumbuka alipokuwa anajibu swali akasema, tuhamasishe wananchi wajenge nyumba za walimu ili waendelee kukaa kule. Sasa Geita tumeshajenga, zipo na maboma yapo. Sasa tunaomba basi, kwa juhudi ya Serikali, imalizie zile nyumba za walimu, walimu waendelee kukaa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, ombi ambalo nimeiomba nafikiri atakuwa amelisikia Mheshimiwa Waziri kama siyo Waziri, basi Naibu Mwaziri wake wote waje Geita. Geita ni kubwa, hawezi akaja mara moja akazunguka sehemu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa sababu sisi tuna ushirikiano, Wabunge wa Geita tuna ushirikiano, huwezi ukaenda sehemu moja, ukamwacha mwingine. Kwa hiyo, naomba kama ni Naibu Mawaziri wawili, wazunguke katika Wilaya ya Geita, ina Majimbo matatu. Naombeni sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ifanye juhudi kuweza kuikomboa au kuiokoa Wilaya ya Geita kuhusu maboma yaliyojengwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kurudisha shule za sekondari, mbili zilikuwa za wakulima ambazo haziwasaidii wakulima wenyewe. Zilikuwa zinawasaidia watu wenye uwezo na ndio maana tukazirudisha Serikalini. Sasa hivi Geita tumebaki na shule moja ambayo imekuwa ni kero. Majengo yake yalikuwa ni ya Serikali, ilikuwa ni *Geita Girls,* sasa hivi inaitwa *Geita Secondary School*. Hii wananchi wengi wamekuwa hawana uwezo wa kwenda pale hasa wa Geita kuweza kusomesha watoto wao pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ichukue shule hii, ni *High School* ambayo itasaidia hata Kitaifa badala ya kuweza kusubiri tu kwamba kuanza kuomba kwamba Geita tunataka *High School,* basi kuna *High School* ile pale, ni wakulima, lakini wakulima wenyewe hawapeleki watoto wao. Ni watoto wa watu matajiri ndio wanaoenda pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni ombi maalum, naiomba Wizara tutakapoleta maombi ya kuirudisha shule hii Serikalini, basi wasiikatae, naomba waikubali shule hii irudi Serikalini ili watoto wa wakulima kweli waweze kusoma katika shule hii, kwa sababu wanaosoma sasa hivi ni mtu mwenye uwezo anayeweza akalipa ada laki mbili, laki tatu, wakati huo inaitwa shule ya mkulima, mkulima gani anaweza aka-*afford* kulipa kiasi kikubwa kama hicho.

Naomba Wizara iichukue shule hii ili wananchi na watoto wa wakulima waweze kusoma katika shule hii. Hakuna kilichoongezeka, bodi ile haijaongeza chochote zaidi ya majengo ya shule ya Zamani ya *Geita Girls*, hakuna kilichoongezeka. Kwa hiyo, bado ile shule iko ndani ya mikono ya Serikali. Naiomba Serikali ichukue shule hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikiwa ziarani katika shule mbalimbali, niliwakuta walimu wa *MEMKWA*. Kweli walimu hawa wamefanya kazi kubwa mno. Kazi iliyofanyika kwa walimu hawa ni kubwa, wamejitolea na sasa huu mpango unakwisha, najua kabisa kwamba hawa walimu watarudi kijijini, watakuwa hawana ajira yoyote.

Naiomba Wizara iwafikirie walimu hawa kuwaweka au waendelee kufundisha katika shule hizo na kuweza kupewa posho maalum au kama siyo posho maalum, basi wapewe kiwango cha kima cha chini cha mshahara wa Mtanzania, siyo hiyo posho ya 20,000/=, kwa kweli haimpeleki kokote, basi tu wanafanya hiyo kazi kwa shida. Naiomba Wizara iwafikirie walimu hawa ili waweze angalau kukidhi maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, katika madai ya walimu, walimu bado wana madai mengi sana. Nimeangalia katika kitabu, Wizara inasema kwamba kuna madai ya shilingi milioni 800, si kweli! Wizara irudie tena madai ya walimu. Nina uhakika kabisa kwa mfano Wilaya ya Geita, walimu wanaidai Serikali zaidi ya shilingi milioni 200 ambazo mpaka sasa hivi bado hawajalipwa. Sasa kwa Tanzania nzima tukisema milioni 800 tu, nimekuwa na wasi wasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba zoezi hili lianze upya kama kuna uwezekano. Kulikuwa na Tume nzuri kabisa ya Mheshimiwa Omar Kwaangw', ambaye alizungukia katika maeneo, aliweza kubainisha matatizo mengi sana na haya yote yalitokana na wewe

mwenyewe kuyaibua wakati ulipokuwa Rais wa Chama cha Walimu. Uliweza kuyaibua matatizo haya.

Kwa hiyo, matatizo haya bado yapo. Naomba hili zoezi halikufanyika vizuri basi lilirudiwe, shilingi milioni 800 sidhani kama kweli ni hizo hizo zinaweza zikalipa madai ya walimu, walimu bado wanadai nina uhakika kuna walimu wengi, Geita wanadai zaidi ya shilingi milioni 200 *and then* mkaangalie katika makabrasha yenu mtaona. Geita tu shilingi milioni 200 Wilaya moja. Je, katika sehemu zingine kuna madai kiasi gani? Lakini naomba kabisa ndugu zangu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tuwaangalie hawa walimu ambao wamekaa wanategemea kwamba wanaweza wakalipwa, wengine wanafuatilia mara kwa mara kwa hiyo, wamefuatilia wamezidi hata gharama ya madeni wanayodai.

Kwa hiyo, sijui wanaweza wakadai na fidia kwamba wamedai kikubwa, nilikuwa naomba Wizara hii iwatambue walimu, iwalipe madai yao ili waendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa kwa dakika hii, pili nakushukuru wewe kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa mambo mawili. Moja ameanza vizuri na timu yake. Siri ya mtungi aijuaye kata na kwamba mchawi mpe mwana alee atamlea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika ina maana gani, Mheshimiwa Margaret Sitta, alipokuwa Rais wa *CWT* alichachafya sana Serikali na alisaidia katika kuongoza katika kuboresha masuala ya elimu. Kwa hiyo, kuteuliwa kwake ninaamini kabisa kwamba ataisaidia sana Serikali ili kutatua matatizo ya elimu na kuleta maendeleo ya elimu. Amepewa wasaidizi wawili ndugu yangu, dada yangu Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza ni gwiji katika elimu. Yeye namwita mwalimu wangu kwa sababu alikuwa anafundisha na alikuwa akiongoza shule wanayosoma watoto wangu wawili na anafahamu sana umahiri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu yangu Mheshimiwa Ludovick Mwananzila ni Mbunge mwenzetu ambaye tunamfahamu uhodari wake kwa hiyo, naamini kabisa kwamba Wizara imepata uongozi thabiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzo wa ndugu zangu hawa watatu na wasaidizi wao wote Katibu Mkuu na Wakurugenzi na wengine wote ni mzuri. Tumekuwa na migogoro mizito sana hapa juu ya maslahi ya walimu. Wameanza kuishauri vizuri Serikali na kwa taarifa ambazo amewahi kuzitoa mwenyewe Waziri hapa migogoro hii sasa itapungua mambo haya yatakwenda vizuri. Tulikuwa na tatizo la shule za mchepuo wa kiufundi na biashara, Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake na timu yao wameweza kubadilisha hali ile na sasa hivi manung'uniko ambayo yalikuwepo shuleni na kwa wananchi kwa ujumla yametoweka. Hongereni sana. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hayo bado zipo changamoto zinazowakabili. Changamoto ziko nyingi, nitajaribu kutoa chache tu na hasa zile zinazohusu Wilaya yangu ya Kisarawe. Tatizo la upungufu wa walimu limezungumziwa sana na Waheshimiwa Wabunge na ndilo kwa kweli lililokuwa kubwa. Pamoja na kwamba upungufu wa walimu ni mkubwa, lakini vile vile lipo tatizo la majengo ya nyumba za walimu. Wenzangu wamesema hapa lakini hali ya kule Kisarawe inatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wakati idadi ya wanafunzi imeongezeka, shule zimeongezeka kama zilivyoonyeshwa katika hotuba hii, ongezeko la walimu bado linakuwa nyuma sana, haliendi sambamba na maongezeko haya. Sasa pana haja ya kuchukua hatua thabiti kabisa za kuhakikisha kwamba tunapata ufumbuzi wa tatizo hili.

Ningependa niwapongeze kwa kutambua kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa ukaguzi. Mwaka huu wamelenga kuongeza idadi ya kaguzi katika shule za msingi na shule za sekondari na mimi nakubaliana nao kwa sababu kule vijijini walimu ambao wako katika mazingira magumu mara nyingi sana wanakata tamaa na kwa muda mrefu hawapo madarasani. Wengine utawakuta kwenye vilabu vya pombe za kienyeji kwa sababu hawana uwezo wa kununua zile pombe nzuri kwa sababu ya marupurupu ambayo ni hafifu. Sasa wakikaguliwa mara kwa mara ninaamini kwamba watakuwa makini zaidi kuhakikisha kwamba wako madarasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu spika, bado najiuliza mwaka uliopita Wizara ilipanga kufanya kaguzi 805 katika shule za sekondari na kaguzi 7018 katika shule za msingi, lakini utekelezaji tunaamini ulikuwa asilimia 98 na 72. Sasa mwaka huu kaguzi zinalengwa katika masafa marefu zaidi wakati ongezeko la walimu ni chache. Je, hili litatekelezwa namna gani? Kuna njia mbili ama itabidi kuathiri mafunzo katika shule kwa sababu wanaokagua ni walimu ili uweze ukakague kule ama uongeze idadi kubwa ili upate wakaguzi au sivyo uwatoe walimu madarasani waende wakakague. Labda pengine wangeliangalia hili vizuri kama hakuna ongezeko kubwa la walimu naona kwamba malengo haya waliyoyaweka ni makubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nyingine nayo mimi kwangu naona ni nzito zaidi ya kutaka kuhakikisha kwamba maeneo yaliyokuwa nyuma kielimu katika Taifa hili yanapewa kipaumbele, nilisema hili nilipokuwa nachangia katika hoja ya bajeti. Lakini nataka nilirudie kwa sababu elimu ndiyo ufunguo wa maendeleo, ndiyo ufunguo wa maisha. Kama kuna maeneo yako nyuma sana kielimu matokeo yake ni kwamba yataachwa nyuma hata kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ujumbe kutoka kwa wananchi wa Kisarawe wamenituma kupitia kwako nimuarifu Mheshimiwa Waziri kwamba Wilaya ya Kisarawe ambayo ina ukubwa wa kilometa za mraba 3500, vijiji vilivyosajiliwa 76 na kuna nane hadi kumi ambavyo vinangojea usajili, Kata 15 zina shule za msingi 75 tu. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba vijana wale wadogo wadogo wa miaka saba hadi kumi hawawezi kwenda hasa nyakati za asubuhi kupita kwenye vichochoro vya misitu kufikia shule ambazo ziko kilometa tano hadi kumi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuziongeza shule ili

kusudi kila kijiji kiweze kupata angalau shule moja na kila kata huko tuendako kwa mpango wa *MMES* iwe imepata shule moja ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu katika kupitia na kuwasilikiza Waheshimiwa Wabunge, wenzangu ni kwamba zipo Wilaya ambazo zina shule mbili hadi tatu katika kijiji kimoja na zina shule mbili, tatu hadi nne kwenye kata moja. Kisarawe ziko shule za sekondari saba tu na katika hizo tano zimejengwa na wananchi katika kutaka kujikwamua, shule za Serikali zilikuwa mbili, tunazo vile vile shule tatu ambazo za binafsi.

Kwa hiyo, nashauri kwa kweli tuangalie na hapa nadhani kuna tatizo kidogo Mheshimiwa Waziri na timu yake maana mwanangu Mabina alipokuwa amesimama hapa amezungumza kwamba wamejenga shule 35 kwa hiyo, mwende mkawaokoe. Kwa hiyo, mimi nasema tumejenga shule tano tu lakini tunahitaji tuwe sawa sawa na wenzetu na tunaweza kufika huko kama Serikali itachukua hatua za makusudi kabisa za kuhakikisha kwamba maeneo yaliyokuwa nyuma yanapewa uzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba msimamo wa Serikali kama alivyoueleza Mheshimiwa Waziri katika ibara ya 31.5 nanukuu: “Wizara yangu imeendelea kuwahamasisha wananchi na wadau mbalimbali kuendelea kujenga shule ili kusaidia Serikali katika kutimiza malengo ya kuwapa watoto wote nafasi ya kupata elimu.” Sawa lakini uwezo wa wananchi katika maeneo mbalimbali unapishana, kuna mahali ambapo wana migodi, kuna mahali ambapo wana viwanda, kuna mahali ambapo wana uvuvi wa Kimataifa, kwa sababu wako karibu na bahari.

Kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri kule Kisarawe tunategemea kilimo tena zao letu la biashara ni moja la korosho na unafahamu jinsi zao la korosho lilivyopata dhoruba katika miaka miwili/mitatu iliyopita. Kwa hiyo, wananchi hawa hawana uwezo sawa sawa na wengine wa kuweza kuchangia ili kusudi waweze kujenga idadi ya shule zile zilizoko mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, nakushauri Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwamba muangalie katika maeneo kama haya pawe na upendeleo maalum ili kusudi kusiwe na kupishana.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niende haraka haraka, vile vile idadi ya walimu nimesema haitoshi kwa Taifa zima tunajua hilo lakini tugawane sawa sawa kile kipanya kidogo dogo. Shule nilizozitaja kule 75 za Wilaya zinahitaji walimu wasiopungua 800 waliokuwepo ni walimu 200 tu kwa hiyo, tuna upungufu wa walimu 600 watafundishaje hawa? Kuna mahali pengine utakuta walimu wawili shule moja yenye madarasa saba na pengine mimi nahesabu moja maana utakuta katika hawa wawili ni mke na mume. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba mafunzo hayawezi kwenda vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la hata wanaokuja wachache wanakimbia kwa sababu ya hali mbaya ya nyumba za walimu yameshasemwa sana na wenzangu sitaki kurudia hapa. Lakini mbinu zinazotumiwa sasa kama kaja mwalimu mwanamke na

anajua hana mahali pa kuishi anachofanya ni kutafuta mume aliye Dar es Salaam au mahali pengine ili aolewe atoe sababu ya kwamba anafuata mumewe. Wengine wanatoa sababu kwamba baba mgonjwa, mama mgonjwa kwa hiyo, lazima niende karibu na hospitali ambayo itatoa matibabu haya. Kwa hiyo, kwa hali hiyo, hali ya walimu katika Wilaya ya Kisarawe na walimu kwa ujumla itakuwa inaendelea kudidimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kengele ya pili inigongee, lakini niseme tu kuona ni kuamini Waingereza wanasema, *seeing is believing*. Kwa sababu hiyo basi, ninayoyasema ili yaweze kuthibitishwa na Wizara namwalika Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake waje Wilaya ya Kisarawe wananchi wanawasubiri sana kule tena tuna mihogo mizuri na machungwa tutawapa na mananasi ili kusudi muweze mkaone hali ya shule zilivyo kule Kisarawe. Mikifanya hivyo mtakuwa mmetusaidia.

Kwa Mheshimiwa Waziri, bahati mbaya Spika hayupo lakini niko tayari kwenda kumuomba ruhusa ili atoe ruhusa ili kusudi Mheshimiwa Waziri, atembelee Kisarawe aone hali halisi ya huko, vivyo hivyo kwa Mheshimiwa Mwantumu Mahiza. Lakini najua Mheshimiwa Ludovick Mwananzila yeye hana haja ya kuombewa ruhusa. Tafadhali karibuni Kisarawe muione hali hii ninayoisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na isinigongee kengele ya pili, napenda niunge mkono hoja hii nikitegemea kwamba hali niliyoieleza ya Kisarawe imesikika na Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake watakuwa tayari kufika Kisarawe wathibitishe hilo na waweze kutusaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa machache niliyonayo katika hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niwapongeze Mawaziri, Naibu Mawaziri kwa hotuba yao hii nzuri, lakini vile vile nimpongeze Katibu Mkuu na timu yake ambayo naamini wamewasaidia hawa makamisaa wa siasa Wizarani kuandaa hotuba hii na mimi nadhani sitakosea kama nitatoa pongezi za kipekee kwa swaiba yangu Ndugu Olvar Muhaiki, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, namfahamu vizuri tangu tuko chuoni. Ni mtu mwenye uwezo mkubwa naamini akiwa anamsaidia Katibu Mkuu wote wawili watamsaidia Waziri na Naibu Mawaziri kuendesha Wizara hii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutamka kwamba naunga hoja mkono na katika machache nitakayoyazungumza, nianze na ukurasa wa tano wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambapo anazungumzia elimu kwa ujumla na hapa ameweka elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasemaji wote waliosimama wamezungumzia tatizo la uhaba wa walimu. Sitokuwa nimevunja kanuni kwamba na mimi nitarudia maana nisipozungumzia uhaba wa walimu, nitakuwa sikuzungumzia namna ya kuboresha elimu

katika nchi hii. Waziri ameweka mipango mizuri sana na nikianza na suala la elimu ya awali, inatakiwa kwa mkakati wa Wizara, kila shule ya msingi iwe na darasa angalau moja la elimu ya awali.

Mimi naelewa si mtalaam wa mambo ya elimu, lakini naelewa kwamba walimu wanaofundisha elimu ya awali ndio wanaokutana na mkiki mkubwa sana ya kuweka misingi mizuri ya mwanafunzi anayekwenda shule ya msingi, hatimaye aende sekondari na aende chuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijui tunayo maandalizi ya kiasi gani kwa mkakati uliowekwa na Wizara kwamba kwa kuanzia mwakani, kila shule iwe na darasa ya elimu ya awali. Tumeandaa utaratibu upi wa kupata walimu wa kutosha wa kufundisha kwenye madarasa ya elimu ya awali, wakati wasemaji wengi wamesema na mimi nikineda hususan kwenye jimbo langu, nitakwenda pale pale waliposema wasemaji wengine uhaba wa walimu kwenye hizi shule za msingi. Sasa ni vizuri Wizara inapoweka maandalizi haya mazuri, iweke maandalizi mazuri zaidi ya walimu wa kufundisha madarasa ya elimu ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia suala la elimu ya msingi na hili nijipeleke kwenye jimbo langu. Wasemaji wengi wamesema na ndio sahihi kwamba shule nyingi zina mwalimu mmoja/wawili. Niliwahi kwenye miaka ya 1990 kusema humu Bungeni na narudia kusema leo, nitaisema kwa kiingereza na tafsiri kwa Kiswahili, *The South is always poor*, igawanye duniani unavyojua wewe, chukua ramani igawanye dunia, Kaskazini mwa dunia ni tajiri kuliko Kusini, igawanye Afrika, ukitoa *South Africa,* Kaskazini kwa Afrika ni tajiri kuliko Kusini, igawanye Tanzania hali kadhalika. Ukija kwenye Jimbo la Kigoma Kusini ndio unakuta ile mantiki ya kwamba Kusini ni maskini kweli kweli, tunazo shule katika Jimbo la Kigoma Kusini, mwambao mwa Ziwa Tanganyika hasa, shule ina mwalimu mmoja na nilijenga hoja hapa wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikaeleza na mwenzangu Mheshimiwa Ludovick Mwananzila tunapakana pakana kule anaelewa mazingira yetu na namsemea na yeye na wala watu wasifikiri kwa sababu yuko pale Wizarani pengine ajipendelee mazingira ndio hayo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zina walimu wachache, halafu tunaambiwa wanapatikana wanafunzi wenye vipaji maalum wanapelekwa kwenye shule za watoto wenye vipaji maalum. Unampataje mtu mwenye kipaji maalum bila kuweka mazingira yaliyosawa ili uwashindanishe sawa sawa. Shule moja ina walimu wawili, lakini shule zingine zina walimu 32 mpaka 40, halafu unapata wanafunzi wenye vipaji maalum.

Mimi nafikiri wale walimu wawili, watatu, ndio wenye vipaji maalum kwa sababu wanafundishwa na walimu wawili hawa wanachagua mpaka wanachagua walimu wa kwenda kuwafundisha, lakini wanafunzi wana walimu wawili halafu unasema unashindanisha watu upate wanafunzi wenye vipaji maalum, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ifike wakati sasa Wizara ibadilishe hii lugha ya kusema kwamba tuna shule za wanafunzi wenye vipaji maalum. Kwanza waweke,

Waingereza wanasema ile kule na *level play ground,* mkishakuwa mnacheza katika mazingira yaliyo sawa sawa, sasa mnaweza kupata watu wenye vipaji maalum na mkasema kweli yule anakipaji maalum.

Kwa hiyo, naiomba Wizara iangalie kufikisha walimu kwenye maeneo yale ambayo mimi nimesema hususan kwenye jimbo langu. Ukienda Kata ya Kalia, kata yenye shule za msingi tano, kwa ujumla wake haina walimu wanaozidi 15. Halafu unataka uandae vijana wafaulu mtihani wa darasa la saba waende sekondari na hatimaye waende Chuo Kikuu na katika kufanya hivyo siku moja mkute mnagawana hizi ajira sawa sawa, haiwezekani, nadhani hilo Wizara imelielewa na si geni kwao, lakini naamini sasa watakuwa wamelielewa kwa sura mpya na watalifanyia kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tatizo la uhaba wa nyumba za walimu na hapa nitazungumza kwa uzoefu wangu nikiwa Mkuu wa Wilaya kwa miaka mitano iliyopita. Nikiwa Mkuu wa Wilaya ya Maswa, nilikuwa kwenye mkutano mmoja wa hadhara nahimiza watu kujenga nyumba za walimu, nikakutana na mtihani mmoja wa ajabu sana wananchi wananiambia mwalimu yeye nani? Mimi nikawaambia kwa kadri ninavyofahamu nitakuulizeni na ninyi na nilitumia hivi hivi maneno makavu kabisa, nikawauliza Mkapa yeye nani? Sasa mimi nawauliza Mkapa ndio ameniteua mimi kuwa *DC*, nikawaambia Mkapa ni Rais wa nchi hii, wewe umejipanga foleni kumpigia kura, mara tu akitangazwa kuwa mkuu wa nchi, anakuta Magogoni pale amepewa nyumba, hamuulizi huyu yeye nani, mwalimu anayekaa na watoto wako kwa zaidi ya saa nane, umuuliza mwalimu yeye nani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sikuishia hapo, nikawauliza huyu Msambya yeye nani, kateuliwa kuwa *DC* na amemkuta *DC* aliye katika nyumba ambayo yeye anataka kuingia hajahama, Serikali imemwekea utaratibu mzuri, tena kwa maneno mazuri ya kiingereza anatafutiwa nyumba inaitwa *rest house,* hamuulize Msambya yeye nani? Lakini huyu anayekuja kuja kukaa na mwanao kwa zaidi ya saa nane unauliza mwalimu yeye nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ni jukumu la Serikali kuona namna gani nyumba za walimu zinapatikana, lakini ni jukumu vile vile la jamii kuona wana kila haja ya kuchangia katika kupatikana nyumba za walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie habari za pesa za *MMEM* na *MMES,* kuna mtu mmoja hapa juzi alisema sio *MMES, MMES* ya *MESS,* ndivyo alivyosema yeye. Wakati nachangia kwenye hoja ya Waziri Mkuu nilieleza, jinsi ubadhirifu ulivyo, nikaeleza kule kwenye jimbo langu Afisa Elimu akishirikiana na baadhi ya walimu wakuu, anatoa maelekezo ya vifaa vya shule vikanunuliwe kwenye maduka ambayo yeye anapenda. Kwa maana ya kufanya hivyo, ni kwamba ana mgao wake na watu wa *PCB* wanatuambia, kudanganya kwa kutumia nyaraka vile vile ni rushwa. Sasa Afisa Elimu anawahimiza maafisa wa chini yake vifaa vya shule vikanunuliwe kwa bei ambayo inapangwa, ni ya juu ili apate mgao wake. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri anatuambia lengo ni kwamba baadaye apatikane mtoto mmoja asome kitabu kimoja yaani kila mtoto asome kitabu chake. Sasa hivi kuna baadhi ya maeneo watoto watatu

wanachangia kitabu, hatuwezi kufikia lengo hilo kama tunao maafisa elimu ambao wanatumia nafasi zao na kuwa-*intimidate* baadhi ya walimu wakuu ili wawaletee mgao kwa kwenda kununua vifaa vya shule kwenye maeneo ambayo wao wanataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri, azamie sana kuangalia pesa zinazopelekwa zinatumika vizuri. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, maeneo mengi sana kuna takwimu na takwimu hizi ni za pesa, ukienda kwa mfano, ukurasa wa 19 zimewekwa takwimu za pesa nyingi sana ambazo zinapelekwa kwenye shule. Sasa kama wasimamizi wa pesa ndio hawa na walimu wakuu ambao wanashirikiana na Afisa Elimu wanaburuza kamati za shule, siamini kama malengo yaliyowekwa na Wizara, yatafikiwa vizuri, kwa sababu pesa hizi zitaishia mifukoni mwa watu badala ya kuboresha elimu ambayo tunasema ndio ufunguo wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi jana nilifarijika sana kwa nukuu mbili alizotoa Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika kuhusu nini hasa elimu ilivyo. Sasa nukuu zile zitafanya kazi vizuri kama udhibiti wa pesa hizi utakuwa ni wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni la Afisa Elimu huyo huyo, nilipokuwa nachangia hoja kwa Waziri Mkuu nilisema, mtihani wa Taifa wa darasa la nne unatakiwa ufanyike kwa siku moja kwa nchi nzima na kama huu mtihani ulifanyika Novemba, 2005, Mkoa wa Kigoma, mtihani umefanyika Januari, 2006 na huu ni kwa uzembe wa Afisa Elimu.

Ningeomba pengine Waziri baadaye akiwa anatoa majumuisho aniambie ni hatua zipi Afisa Elimu huyo amechukuliwa na ni sababu zipi zilizopelekea yeye akawa na tarehe ya kwake binafsi ya kufanya mtihani wa Taifa yeye akateua tarehe yake. Ni vizuri Waziri atakapokuwa anatoa majibu atuambie ni kwa nini na hatua gani amechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la lugha ya Kiswahili na mimi hapa mbele yangu namuona mswahili namba moja, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, mimi namhesabu ni mswahili namba moja. Mimi naweza nikajihesabu pengine ni mswahili namba mbili. Napenda nieleze kwamba wachangiaji wengi wamezungumzia kiingereza kianze kufundishwa tangu shule ya msingi sawa. Lakini mimi siafiki tunavyopeleka lugha yetu ya Kiswahili, tunatakiwa sasa tuweke maandalizi ya elimu yetu ifundishwe kwa Kiswahili tangu darasa la kwanza mpaka elimu juu. Tumewahi kuambiwa kwamba kiingereza ni Kiswahili cha dunia sawa, hivi Mchina anapoamua kuzungumzia bajeti yake kwenye nchi yake, anaizungumza kwenye kiingereza? Mrusi anapoamua kuendesha mambo ya nchi yake anayaendesha kwa kiingereza? Mchina, Mrusi, Mjapani, hawashirikiani na Mataifa yanayozungumza kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema tukaweka mkazo katika kufundisha kiingereza ili tupate wenye kuzungumza kiingereza kizuri. Lakini tuipe hadhi lugha yetu ya Kiswahili na iweze kutumika katika kuendesha mambo ya nchi yetu na ajabu moja inayotokea ni hapa hapa Bungeni tunavyo vitabu hivi vimeandikwa kwa kiingereza, ndiyo kasumba namba moja, tunajadili bajeti katika lugha mbili tofauti, hivi tulikosa wataalam kweli wa kuweza kuandika vitabu hivi kwa lugha ya Kiswahili, kama tunavyojadili bajeti hii kwa lugha ya Kiswahili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nafikiri ifike wakati tusidanganywe kama tulivyodanganywa katika kubadilisha mitaala, kuondoa baadhi ya masomo, sasa twende kwenye kuthmini lugha yetu, imefika wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Msumbiji ndiyo Rais wa kwanza kwenda kuhutubia Kimataifa kwa Kiswahili, halafu Rais wetu akafuata. Lakini sisi katika dunia ndio ambao wenye sifa ya kuzungumza Kiswahili kizuri, kilichonyooka kuliko nchi zingine zote. Sasa ni vizuri sasa uwekwe mkazo wa kufundisha Kiswahili kizuri tangu shule ya msingi, tuweke mazingira ili lugha hii ifundishwe mpaka Chuo Kikuu. Lakini kiingereza kifundishwe ili kitusaidie ili kuwasiliana na dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo narudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii lakini nipate majibu ya lile nililozungumza kuhusu Afisa Elimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu. Tunaomba radhi tunatumia *speed* kali katika kusema kwa sababu tuna mengi tunataka tumalize kwa dakika hizo chache tulizopewa, labda tuzingatie ushauri wa *ZANTEL,* kweli kweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, watumishi wote wa Wizara na wale walio chini ya mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa kazi nzuri waliofanya ya kuandaa hotuba hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote ningependa kutumia nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru walimu wote wanaofanya kazi ya ualimu katika nchi hii popote pale walipo kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuelimisha Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ualimu ni ngumu lakini ni muhimu. Kwa hiyo, nikiangalia kazi nzuri inayofanywa na walimu wa nchi hii katika mazingira haya tunayoyasema, machozi hunilengalenga. Sielewi nani kati yetu hasa anaweza akajilinganisha na kazi wanayofanya walimu ya kulea na kuelimisha watoto wetu. Tunakabidhi watoto wetu walelewe na walimu ambao wana matatizo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi nani kati yetu sisi Wabunge anaweza kupinga maslahi yasiongezwe kwa walimu? Katika vijiji na mijini walimu ni kila kitu. Walimu ndiyo wanaofundisha watoto wetu madarasani, ndiyo wanaondaa mapokezi ya viongozi na mikutano ya sisi Wabunge mijini na vijijini, ndiyo wanaofanya kampeni dhidi ya magonjwa na mambo mbalimbali ambayo yanaamuliwa na Serikali. Ndiyo wanaosimamia chaguzi mbalimbali katika nchi hii. Lakini ukiangalia maslahi yao kama tunazungumzia *equal pay for equal work* kwa kweli ni huzuni kubwa.

Katika kitabu hiki ambacho Wizara imetoa ni kitabu kizuri sana, pale katika marejeo, utangulizi ukurasa namba moja, Rais wetu naye anayaona matatizo ya walimu. Anasema pamoja na mambo mengine kwamba kuboresha maslahi ya walimu katika shule, vyuo hapa nchini kuwepo kwenye mkakati wa Wizara na bahati nzuri Waziri ameyasema haya katika hotuba yake na sidhani kwamba kuna njia ya mkato. Lakini ushauri wa Wabunge wengi unafafana kwa hiyo, nisingependa niende kwenye upande huo. Walimu ni wengi wako kila mahali mjini na vijijini, lakini kuwa wengi au idadi yao isiwe ni sababu ya kupuuzwa, wako wengi kwa sababu wanahitajika au kwa sababu ya umuhimu wa kazi yao. Kwa hiyo, ushauri wao, maombi yao, yasipuuzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua unatoka Wilaya ninayotoka mimi, hebu siku ya kupata mishahara mwisho wa mwezi nenda ukaangalie jinsi walimu walivyorundikana na wanavyobanana katika mabenki ya *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu siku ya mwisho wa mwezi fika hapa Dodoma kwenye ukumbi wa benki ya *NMB* uwaangalie jinsi walimu walivyorundikana ndani ya jumba lile toka asubuhi mpaka jioni na karibu juma zima wanasubiri wapewe maslahi chini ya mazingira magumu sana. Kama ile benki ingekuwa ni ya mtu binafsi kwa kweli hangepokea mzigo wa namna hii. Lakini wapo pale, watoto wa shuleni hawana walimu na wenyewe wako pale bila ya uhakika wa kupata maslahi leo au kesho. Hii ndiyo hali ya mwalimu. *What a poor way of living. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunasema kuwa yale yaliyo chini ya uwezo wetu kwa kweli tujitahidi kuyatatua. Wizara hii peke yake haiwezi na mimi nilikuwa nashauri kwamba pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kufanya Wizara hii isimamie hata elimu ya ufundi kwa matatizo ambayo Wizara hii inayo ya kujenga nyumba za walimu, maabara, ya kusimamia hizi shule za sekondari zinazoota kama uyoga kila siku kwa kweli ni vizuri *VETA* ingekuwa mahali pengine kama ndiyo nia kwamba na *VETA* iboreshwe. Mzigo huu ni mzito mno. Wao hawawezi kusema hivi. Wizara itaelekeza nguvu zake kule inakoona ni kwepesi zaidi na kusahau maeneo mengine. Huu ni ushauri wangu. Ni ushauri, sisi ni washauri lakini tunadhani kwamba ni vizuri mkayaangalia hayo.

Katika Biblia kitabu ambacho Wakristo wanakithamini sana katika sehemu ya Mithali kuna maneno yasemayo: "Watu wenye akili huweka akiba yao katika maarifa au kuwekeza katika elimu."

Nashukuru mkazo ndiyo huu katika Wizara hii ni kuwekeza katika elimu lakini matatizo ni mengi. Hebu tazama matatizo ya maabara kwamba tunajenga shule, maabara 40 kwa kila mwaka na shule ziko zaidi ya 800 hizi mpya na matatizo ndiyo haya na fedha ndiyo hii, tumeletewa na *VETA, the spirit is willing but the fresh is weak.* Nadhani kuna haja ya kutazama upya kama *VETA* inasaidia vijana huenda Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ingekuwa ni nafasi nzuri kwa sababu *VETA* inasaidia ajira ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kunukuu maneno ya mwandishi mmoja katika kitabu cha *Development Out Reach.* Mtaalam huyu anasema hivi, kwa idhini yako

naomba niisome: *"In the next thirty years the population of the world will increase from six to eight billion, virtually all those two billion will be in the poor countries. Whether a large population represents an asset or a set back to progress depends above all on whether people will have the capacity to shape their future. The new economy offers unpresented opportunities but the gains will not be automatic. It will benefit nations in propotion to their success in building human capacity. That is investing in quality education." End of quote.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za Wizara za kujaribu kuboresha elimu ni kubwa lakini zoezi ni kubwa sana na nitapenda kutoa mapendekezo ila kwa sababu ya muda, tukubaliane kwamba chini ya mfumo wa *knowledge economy* nchi zile ambazo hazitilii mkazo katika elimu zitabaki nyuma milele na milele. Kwa hiyo, katika mazingira haya tuliyonayo ambayo tunajaribu kushauri kwa kweli mahali pengine inaonekana kama tunashauri mambo tusiyoyaelewa. Lakini ndiyo ilivyo, sasa mwalimu mmoja atafundishaje *secondary school.* Uwiano wa walimu ndani ya shule unafuata wingi watoto katika shule ile bila kujali madarasa yaliyopo pale, madarasa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni katika matatizo unahangaika kutafuta dawa ya tiba, kama unaumwa unakuwa na waganga wengi, kila mmoja anatafuta uwongo wake. Kwa hiyo, ndiyo matatizo, sasa afanyeje. Kwa hiyo, zinatumika kama *shock-absorbers* kwamba hasa wa Sumbawanga, kwamba hawa watoto waonekane asubuhi wamevaa sare wanarudi jioni, lakini hawana kitu kichwani. Lakini tunawafanyaje? *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nashukuru jitihada zinazofanywa na Wizara za kujaribu kutafuta *programmes* fupi za kutoa walimu kwa haraka, walau kutatua tatizo hili, lakini hata hizo hatua zinapingwa. Sasa wafanyeje? Tuseme miezi 6 haitoshi, sasa ufanyeje? *Psychologically* wewe unafanyaje? *(Makofi)*

Mimi nadhani baadhi ya njia lazima tuzipongeze na tusaidiane. Kwa kuwa muda hauruhusu ningependa kusema kwamba ubora wa Taifa lolote lile duniani hutegemea ubora wa elimu inayotolewa kwa watu wake. Sasa ni aina gani ya Watanzania tutawatoa baadaye katika dunia hii ya mashindano. Huu ndiyo mtihani ambao tunapewa katika shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari, shule za ufundi na vyuo vikuu. Mimi nasema napongeza maamuzi ya Wizara, malengo ya Wizara na hatua zinazochukuliwa. Suala hapa ni kwa namna gani tunaweza kuchangia ili kuboresha njia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kwa sababu ya uhaba wa muda labda nimalizie kwa kusema kwamba kuna matatizo makubwa mawili. Moja pamoja na mikakati hii nadhani tujiepushe kujenga matabaka. Utafiti uliofanywa Morogoro umeonyesha kwamba shule za msingi za mjini hata za sekondari ndiyo wanafaulu zaidi, kwa sababu zina walimu wengi zaidi kuliko shule za vijijini na Mkoa wa Morogoro imeonyesha kwamba *one third* ya watoto wa shule za vijijini ndiyo wanafaulu na mijini ni zaidi ya pale. Tofauti ni nusu. *(Makofi)*

Sasa kama hatuangalii hawa wa mijini katika Tanzania ni asilimia 20 ya Watanzania wote ndiyo wanakaa mijini. Asilimia 80 wanakaa vijijini. Lakini asilimia 20

wanaokaa mjini ndio wanaochukua nafasi asilimia 80 za watoto wanaokwenda *secondary schools* na vyuo vikuu ndiyo watakaokuja kutawala baadaye. Kwa nini mimi nikae vijijini na kuwa *condemned for life* kwamba watu wangu watakaokuwa ni wapiga kura tu, wataingia kwenye uongozi wa nchi hii. Nadhani ni vizuri kama tutapuuzia walio wengi tutashindwa kulinda hata wale wachache tunaotaka kuwalinda. Ni lazima tutoe elimu bora kwa wote na kuwa na msimamo wa makusudi. Pale Morogoro shule nyingine zina walimu zaidi kuliko wanaotakiwa, kwenda vijijini sababu ndiyo hizo ambazo zimeelezwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningependa kupendekeza njia zifuatazo, moja, kama alivyosema Albert Stein, yeye katika kutazama dunia ali-*lament* lakini vile vile alisema kwamba tujaribu kutafuta njia ambazo labda zitakuwa tofauti na zile ambazo zimetumika katika kujenga baadhi ya matatizo, lakini binadamu ni mgumu sana. Kwa maneno yake alisema: *"The world that we have created todate as a result of our way of thinking has problems that can not be solved by continuing to think in the way that we thought when we created them. We have to be radical."* Lakini *radicalism* katika mazingira haya ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo, mimi nilikuwa napendekeza kwamba usambazaji wa walimu uzingatie idadi ya madarasa katika shule badala ya idadi ya wanafunzi kama sasa. Pili, Wizara itaangalia uwezekano wa kuondoa Idara ya *VETA* hii ya ufundi katika Wizara hii kusudi iweze kuelekeza nguvu zake kwenye mzigo huu mkubwa ambao uko kwenye upande wa sekondari.

Tatu, nafasi ya *REO* irudishwe na kwamba majukumu na madaraka aongezewe zaidi ili aweze kusimamia elimu mikoani kuliko kutegemea makao makuu ya Wizara na hatua zinachukuliwa kwenye ngazi ya Wilaya lakini hapa juu ni lazima kwa sababu huwezi kusambaza watu hawatatosha kufika kwenye ngazi ya chini. Lakini naunga mkono lile wazo la kumweka Mratibu wa Sekondari kila Wilaya, lakini yule asaidiwe kwa kuunda Bodi ya Washauri, ngazi ya Wilaya, kwa sababu shule hizi zinatoka madhehebu mbalimbali, mashirika mbali, na Serikali kwa hiyo wale watajenga kiungo muhimu cha kuangalia shule *in totality* ndani ya Wilaya kwa kumsaidia huyu Mratibu ambaye mnampendekeza awe. Naipongeza sana hatua hiyo ndugu Waziri, ni hatua muhimu. Ya nne, tuunde zile Kata za Elimu na Tarafa za Elimu kusudi wewe Mheshimiwa Waziri awe na utaratibu wa kuangalia uhusiano wa hizi shule zinazojengwa na mikakati ya kuandaa walimu ili kuwa na usimamizi, vinginevyo hili zoezi litakuwa gumu sana maana tutaunda Kata za kiutawala, wakati wewe unaangalia kata ngapi na huwezi kuwa na *projection* na kupanga bila usimamizi na kuchukua hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam hizo mimi ningependa kusema kwamba naunga mkono hatua hizi za Wizara lakini upande wa hisabati na lugha za masomo na masomo ya sayansi tusipoangalia tutakuwa tunafanya kazi ambayo tutabaki kuwa manamba na waokota kuni milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, mimi naunga mkono Wizara na kwamba tafuteni kwanza maendeleo ya elimu na mengine yote yatafuata. Nia yetu

nzuri iambatane na malengo yetu mazuri yaambatane na kumwezesha Waziri kutekeleza mipango yake hii mizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niwe kitindamimba katika kuchangia hoja yetu hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote kwa kutayarisha hotuba hii ambayo ni nzuri sana. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri namfahamu siku nyingi na namfahamu miaka mingi sana. Nafahamu yeye ni mpenda kazi, ni mpenda haki na ni mchapakazi. Nawahakikishia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwamba kwa hili Wizara niseme pumu imepata mkohozi. Mtumieni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Serikali nzima kwa juhudi walizofanya mwanzo wa mwaka huu wa kuhakikisha kwamba asilimia kubwa ya vijana waliofaulu shule za msingi wameenda shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu Chunya watoto zaidi ya 1,000 waliokuwa wamefaulu 300 wamekwenda sekondari. Lakini baada ya juhudi ya Serikali waliokwenda sekondari wako zaidi ya 800. Waliobaki hao ndiyo wamekwenda kwenye shule za watu binafsi. Naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mbunge mwingine wa Wilaya ya Chunya, kaka yangu Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, aliongea kwa uchungu sana mambo ya Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chunya kama anavyosema Mheshimiwa Rais au Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kuna Mikoa hapa nchini ambayo ni ya pembezoni, kwa Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Chunya ni Wilaya ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia mwaka 2005 ilikuwa na shule za sekondari nne za Serikali, ina wakazi zaidi ya 200,000 lakini shule za sekondari zilikuwa nne, baada ya juhudi za Serikali za mwaka huu ambazo nimezisifu hapa nyuma, sasa shule za sekondari ziko saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasema ikifika mwaka 2010 angalau kila Kata iwe na sekondari moja. Wilaya ya Chunya tuna Kata 23, sekondari saba, ina maana tuna kazi ya kujenga sekondari 16 ili angalau ikifika mwaka 2010 kila Kata iwe na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri alitupie macho hili atusaidie sana. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, anatoka Chunya. Chunya ni kwao, alizaliwa Chunya na hata katika Baraza la Madiwani, sisi

tumwekea kiti chake kipo. Tunamwomba sana aiangalie Chunya kwa macho ya huruma sana. Tuna kazi ya kujenga shule za sekondari 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba ana majukumu yake Kitaifa na pia ana majukumu yake katika Wilaya ya Urambo anakotoka Spika. Lakini naomba aiangalie Wilaya ya Chunya maana yake hata hiki cheo alichonacho kimetoka Chunya. Namwomba sana aiangalie sana Chunya katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi niongelee Kiswahili. Wabunge wengi hapa wameongelea kwamba Kiswahili, Kiingereza kitafundishwa shule za msingi na sekondari. Lugha ya Kiswahili sasa inakuwa maarufu hapa duniani sana sana. Nchi nyingi zinatumia lugha ya Kiswahili, Ulaya, Asia kote huko, Afrika hii na Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini linaloniogepesha ni kwamba sisi Tanzania hatujalichukua suala la kukua kwa Kiswahili kwa umuhimu wake. Nimewahi kuona mifano, kuna vyuo huko Marekani ambako walimu wanaofundisha Kiswahili ni wananchi wa nchi jirani, ina nchi jirani zimetuzunguka na kupeleka walimu wakafundishe Kiswahili Marekani. Sasa ninaloogopa Kiswahili wanachofundisha huko ni Kiswahili gani, maana yake tunawajua majirani zetu wanaongea Kiswahili gani. Sasa watakwenda huko watafundisha viswahili vya ajabu, baadaye tutakuja kulaumiwa Tanzania. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Serikali kwa ujumla suala hili la Kiswahili tulichukulie kwa mapana yake hii ni *product* yetu nzuri sana tuiuze duniani kama Watanzania kama lugha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu vitabu vya elimu za shule za msingi na shule za sekondari. Hapo zamani ilikuwa vitabu hivi vinanunuliwa na kupelekwa Mikoani na Wilayani kutoka Wizarani baadaye kwa nia nzuri tu Serikali ika-*decentralize* kwa hiyo, vitabu hivi vinanunuliwa kutoka Wilayani na kutoka Mikoani hapa ndiyo imetokea *problem.* Wametokea wafanyabiashara ambao wanavuruga hakimiliki ya wachapishaji, wanakili vitabu hivyo, wanavichapisha wana maduka ya vitabu wanaviuza. Sasa zoezi hilo la kuchukua haki miliki ya watunzi na wachapishaji inawakosesha mapato watu wengi sana.

Kwanza mtunzi anakosa mapato, pili mchapishaji ambaye anakuwa amewekeza muda, amewekeza mali, amewekeza akili, anakosa mapato, tatu, Serikali kwa kuwa hawa *Pirates* hawalipi kodi, Serikali nayo inapoteza mapato na vile vile kwa sababu vitabu hivi vinakuwa *sub-standard* inakuwa na ubora wa chini kwa hiyo, havidumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbaya zaidi, ni kwamba watunzi wanapokuwa wanakosa motisha katika vitabu vyao, wataacha kutunga vitabu na wakiacha kutunga vitabu Taifa litakuwa limepoteza utamaduni wake. Kwa hiyo, naomba sana Serikali na Wizara iliangalie sana suala hili la *piracy* katika biashara nzima ya vitabu vya shule za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kidogo mishahara ya walimu. Wilaya nyingine kama Wilaya ya kwetu, Wilaya ya Chunya ikifika mwisho wa mwezi

walimu wengine huwa wanasafiri kilometa 200 kwenda kufuata mshahara kwenye Makao Makuu ya Wilaya, kilometa zaidi 200. Sasa athari zake ziko nyingi. Moja, inabidi yule mwalimu akope nauli ya kwenda huko Wilayani, apande mabasi sijui malori kwenda kuchukua mshahara wake. Lakini akiwa ni mwalimu wa kiume akifika Wilayani anachukua mshahara wake na kwa kuwa amekaa sijui na kiu mwezi mzima, anaanza kujipongeza kwanza. Anaishia baa anakunywa, anakula, analala *Guest House* kesho ndiyo aangalie usafiri wa kwenda shuleni na nyumbani kwake. Anakuwa amepunguza mapato yake kwa kiasi kikubwa sana na kuweza kuathiri familia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile akiwa mwalimu ni wa kike naye anakopa nauli aweze kwenda Wilayani kwenda kuchukua mshahara wake. Yeye akifika kule wilayani anachukua mshahara wake lakini anakutana na wakware chungu mzima ambao wanamsumbua au wengine wanamnyang'anya, wanamwibia.

Kwa hiyo, ningeomba sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ifikirie njia ya kuweza kuwapunguzia makali walimu katika hilo. Aidha, labda Wizara ikishirikiana na wadau wengine wafikirie namna ya kuhamasisha kuundwa na kuendelezwa kwa Benki Kata ili walimu wapate mishahara yao kwenye Benki Kata hasa kwenye Wilaya ambazo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo haliwezikani, wakati wa operesheni maalum huwa Halmashauri zina-*bolize* magari kupeleka kwenye Kata zilizo pembezoni mwa hizo Wilaya.

Kwa hiyo, ningeomba kama haiwezekani kuunda Benki Kata basi Halmashauri zihakikishe kuwafikishia mishahara hasa walimu ambao wanakaa mbali sana, wanakaa zaidi ya kilometa 200 kama ilivyo Wilayani kwangu Wilaya ya Chunya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nirudie kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na uwezo wa kuandaa Waraka huu, kutoa maoni yangu juu ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio siri kwamba kila mtu anajua umuhimu wa elimu katika kuleta maendeleo, sio tu ya mtu mmoja mmoja, bali hata kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa ambalo halina wasomi (Wataalam) wazuri walioandaliwa vyema, basi litakuwa linasuasua kimaendeleo. Kwa hiyo basi, lazima nchi yetu itilie mkazo wa makusudi na kipaumbele juu ya elimu na hasa kwa kuanzia ile ya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nchi yetu iweze kupiga hatua mbele kielimu, hakuna budi kwanza kutatua matatizo ya Walimu. Ni lazima Shule zetu zipate sio tu Walimu, bali walio bora wenye viwango vya elimu na maadili mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kilio kikubwa karibu kila Jimbo na kila Wilaya. Sasa ili kutatua hilo, ipo haja ya Serikali kupitia Wizara ya Elimu, kufanya kila jitihada ya kupatikana Walimu ambao wanaweza kukidhi haja, maana, kuwa na majengo na wanafunzi tu bila kuwa na Walimu, Shule haijakamilika.

Pamoja na uhaba wa Walimu mashuleni, lipo tatizo kubwa la hao Walimu waliopo kukosa huduma muhimu na za msingi kabisa. Kwa mfano, Walimu wanapata shida sana kwa kufuatilia mishahara yao, inasemekana baadhi ya Walimu wanachukua kati ya siku nne na wiki moja kufuata mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama katika Shule Walimu wataondoka kwa muda wote huo, Serikali haioni kwamba Shule kama hizo zitakuwa zinakosa muda mrefu wa kutoa mafunzo, hivyo kupelekea wanafunzi kutofanya vyema katika masomo yao na hivyo kutofaulu mitihani yao? Ni vyema Serikali ifikirie mipango mahsusi ya kuweza kuwapatia Walimu mishahara yao bila usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia kadhaa zimeshauriwa katika kuondokana na tatizo hili zikiwemo ile ya Serikali kuanzisha Ofisi za Kanda, kwa kuzikusanya Shule tano tano katika Kituo kimoja cha katikati, kati ya Shule hizo. Njia hii itawapunguzia Walimu usumbufu wa kufuata mishahara yao masafa marefu. Vile vile, umetolewa ushauri wa kuwa na *Mobile Office* kwa ajili ya kuwafuata na kuwalipa Walimu mishahara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya kazi ngumu ni kazi ya Ualimu. Kwa kweli Mwalimu aliye makini, hutumia zaidi ya masaa kumi na mbili katika kuandaa na kutekeleza kazi zake. Ni vyema Serikali ilione hili kwa ukamilifu wake na itoe motisha maalum kwa Walimu na hasa wale wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Posho ya Walimu ni kitu cha muhimu sana ikienda sambamba na mishahara mikunjufu. Haya yakitekelezwa, yatawafanya Walimu wajisikie vizuri na kuweza kufanya kazi zao kwa umakini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi katika Majimbo mengi waliitikia mwito wa ujenzi wa madarasa kwa ajili ya kuongeza idadi ya watoto katika Shule za Msingi. Lakini la kusikitisha ni kwamba, majengo mengi sana bado hayajakamilishwa. Yako maboma mengi ambayo kama hapatakuwa na mpango wa karibu sana wa kuyakamilisha, basi kuna uwezekano mkubwa wa maboma hayo kubomoka na kuanguka kabisa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kufanya jitihada kubwa ya kuyakamilisha kuyajenga ili ku-*create* nafasi zaidi kwa watoto wetu na pia kuwapa moyo wananchi kwa kuona kwamba nguvu zao hazikupotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ni muhimu sana kutiliwa maanani, ni ujenzi wa nyumba za Walimu. Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na hili. Ukosefu wa nyumba za Walimu ndilo linalosababisha Shule nyingi kukosa

Walimu, maana Mwalimu anapopata uhamisho ni lazima kule anakokwenda apatiwe nyumba, vinginevyo ni vigumu kuweza kufanya kazi katika Shule ile.

Vile vile, inashauriwa kujengwa *Hostel* maalum kwa wasichana ili kupunguza matatizo ambayo yanaweza kujitokeza kama kutakuwa na mchanganyiko kati ya jinsia mbili (wanaume na wasichana) kwenye *Hostel* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi kwenye Wizara hii. Awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa Bajeti hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iangalie kwa umakini kabisa kuhusu maslahi na makazi ya Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Vijijini kwa ujumla, hakuna kabisa nyumba za Walimu, ndio maana Mwalimu akipangiwa kwenda Vijijini, Walimu wengi wanakwepa kwenda huko. Walimu wasipokwenda huko, wanafunzi hawawezi kupata nafasi wala kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Shule ambazo huko Vijijini hakuna Walimu kabisa. Utakuta Shule nzima ina Walimu watatu. Hapa wanafunzi watafaulu kwa namna gani? Hii inapelekea Walimu kuanza kufanya kazi zao binafsi. Wakisha-*report* Shuleni asubuhi wanaondoka wanakwenda kwenye shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishauri Serikali iangalie ni jinsi gani wanaweza kujenga *at least* nyumba za bei nafuu zenye hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Walimu, kwa kweli Walimu wengi wanakatiwa Bima za Afya lakini wengi wanakatwa kwenye mishahara yao kwa ajili ya Bima, lakini mpaka leo hii wengi wao bado hawajapata *card* zao. Je, walimu hawa wataweza kuwa na motisha ya kufundisha kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wengi hawajapata Elimu ya Msingi nafikiri ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kurudisha ile Elimu ya Watu Wazima ili iweze kuwasaidia hawa ambao hawajapata Elimu ya Msingi. Ukiangalia, wakati huu wa utandawazi, bila elimu kwa kweli maisha yanaweza kuwa magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi, hata wakulima wa bustani za maua wanahitajika wajue kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wengi wakimaliza Shule za Sekondari hawawezi kuongeza lugha za Kiingereza. Ajira nyingi hata ukisoma kwenye magazeti, ili mtu aajiriwe, kigezo cha kwanza lazima aweze kuongeza *fluent English.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana unakuta vijana waliomaliza *Form Six* wanafanya kazi ambazo zingefanywa na mtu ambaye hajasoma kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushahidi wa kijana aliyemaliza *Form Six* lakini anaosha magari. Kwa kweli hili linatia uchungu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kijana amemaliza *Form Six* halafu anakwenda kufundisha. Kwa hakika Shule ile haiwezi kupasisha wanafunzi. Mwalimu lazima awe na maadili na kadhalika. Hawa vijana lazima wapitie *course* ya Ualimu, wajifunze haya yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Taasisi iliyochaguliwa ku-*print* vitabu vya wanafunzi wa Shule za Msingi *(Mture Educational Publisher Limited*), kumekuwa na malalamiko kuna *stationaries* ambazo wanatoa *copy* ya vitabu hivyo na kuviuza kwa bei nafuu.

Tunaomba Wizara ichunguze kuhusu hili kwa sababu Serikali yetu inajaribu kusaidia wazawa au viwanda vya hapa nchini ili kuongeza ajira na uchumi kukua. Sasa ikiwa kama kuna *companies* zinaweza kuchapisha vitabu hivi, ajira itatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Wizara ya Elimu iangalie ni jinsi gani inaweza kuimarisha Kikosi cha *Inspection* kwa kuangalia ni Shule gani hapa nchini hazikidhi viwango vya Shule?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara ijaribu kuweka kalenda moja kwa Shule zote Tanzania ziwe *Private/Public.* Shule nyingi za *Private* zinakuwa na *terms* tofauti hata nne hivi. Wajaribu ku-*create* jinsi ya kupata *School fees* zaidi, lakini Wizara ikisimama kutakuwa na *terms* ambazo zipo sawa kwa wanafunzi wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitaji Waziri atueleze (naomba jibu); Je, ni kweli *tuition fees* imeingizwa katika mishahara ya Walimu? Je, mishahara ya Walimu hawa imebadilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni na maswali yangu haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kujali uwezo wa Mheshimiwa Margaret Sitta na kumteua kuwa Waziri wa Elimu na Ufundi. Nampa Mheshimiwa Waziri hongera sana.

Mchango wangu katika Wizara hii ni kuhusu usajili wa Shule za Msingi na Sekondari za Binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ulio wazi ni kuwa, Sekta Binafsi ya Elimu imechangia kwa kiasi kikubwa sana katika kukuza, kuendeleza na kudumisha Elimu bora katika Taifa letu. Sio siri kuwa Shule nyingi za binafsi za Msingi na Sekondari ndizo zinazoongoza kwa kufaulu wanafunzi. Ikumbukwe kuwa, wengi wa wale wanafunzi

wanaojiunga na Shule Binafsi hasa za Sekondari huwa ni wale waliofaulu lakini hawakuchaguliwa kujiunga na Shule za Serikali. Wengine ni wale waliofeli kabisa na hata wazazi wao huwa wamekata tamaa ya uwezo wa watoto wao na kwa wale wenye pesa, basi hulazimika kuwalipia Shule za Binafsi. Lakini juhudi za wenye Shule na Walimu wao, wanafunzi wale wanaomaliza na kufanya mithani yao ya mwisho, matokeo ni kuwa kufaulu kwao ni kwa kiwango cha juu kuliko wale wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo naliona ni katika kusajili Shule hizo. Urasimu ni mkubwa sana na pengine wa kukatisha tamaa. Urasimu huo unafikia mpaka wale wenye Shule kuingia katika mtego wa rushwa ili Shule yake isajiliwe mapema. Hali hii inakatisha tamaa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni ruzuku kutoka Serikalini ili angalau Shule Binafsi, nazo ziweze kujikimu na ukata ambao Shule hizo hukabiliwa nao. Sio mara moja au mara mbili Serikali inatoa ahadi ya kutoa ruzuku ya kuzisaidia Shule binafsi, lakini hadi leo hii Shule hizo hazijapatiwa ruzuku hiyo. Pamoja na ruzuku yenyewe kuwa ndogo sana ambayo hukadiriwa kulingana na idadi ya wanafunzi, lakini kwa Serikali kutotimiza ahadi yake hiyo, huwa kunaifanya Sekta hii ya Elimu Binafsi kuvunjika moyo na kukakta tamaa. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Waziri wa Elimu ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Sitta pamoja na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mwananzila na Mheshimiwa Mahiza pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii nyeti kwa jinsi wanavyomsaidia Mheshimiwa Waziri.

Naleta maombi mawili kutoka katika Jimbo langu la Moshi Vijiini. La kwanza, upo upungufu mkubwa wa Walimu katika Shule zetu za Sekondari, hasa hizi zilizojengwa karibuni kwa mpango wa MMES na kwa jitihada za wananchi. Naomba sana msaada wa Mheshimiwa Waziri. Najua anajitahidi sana kama alivyoainisha, lakini pale shida zake ni sugu na zinahitaji uangalizi wa kipekee.

Pili, natambua kwamba fedha za MMES hazitoshelezi kujenga madarasa yote yanayohitajika. Katika Jimbo langu, nimehamasisha wananchi, sasa tunajenga Shule moja katika kila Kata, jumla ya Shule 16 za Sekondari.

Namwomba Mheshimiwa Waziri azitupie Shule hizi jicho lake ili mgao wa MMES uende kwa Kata zote hata kama ni kidogo. Naiunga mkono hoja ya Waziri kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa utoaji wa fedha za MMES wa sasa wa Wizara kutuma fedha moja kwa moja mashuleni kwa ajili ya ujenzi na matumizi mbalimbali siyo mzuri.

- Je, Wizara haioni kuwa kwa kufanya hivyo, majengo yamekuwa yakianzishwa nyumba, vyoo na madarasa bila ya ushauri wa Wahandisi na hivyo kupunguza ubora?

- Kwa kuwa fedha hizi hazitolewi taarifa, Wizara haioni kuwa Viongozi na Watendaji katika ngazi mbalimbali hushindwa kuthibiti na kusimamia shughuli na fedha hizo?

- Fedha za Sekondari kupitia kwenye Akaunti ya Sekondari nyingine, Wizara haioni kuwa kufanya hivyo ni kupunguza kasi ya maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Wizara itaimarisha ukaguzi wa Shule za Msingi katika Wilaya ya Meatu na sehemu nyingine? Ilivyo sasa, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikitenga fedha kidogo sana katika Kitengo hiki. Katika Wizara ya Meatu, Idara ya Ukaguzi ilipanga kukagua Shule 64 kati ya Shule 106 mwaka 2005/2006, matokeo wamekagua Shule 19 tu sawa na asilimia 29. Tunakwenda wapi? Je, Wizara inapataje *Quality Education Insurance?*

Kwa nini taarifa za ukaguzi haziletwi kwenye Vikao vya Baraza la Madiwani ili Viongozi nao wafahamu matatizo na mafanikio ya Shule zao?

Ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha katika Kitengo hiki cha Ukaguzi na usafiri wa uhakika ili kuzifikia Shule kwa urahisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongelea kuhusu upungufu wa Walimu. Kwa kuwa Shule nyingi za Sekondari zimeanzishwa Wilaya ya Meatu, jumla ya Sekondari saba, lakini mpaka sasa zina Walimu wawili tu. Ni lini Wizara itatuma Walimu wa kutosha mashuleni Wilaya ya Meatu na sehemu nyingine?

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni yangu kimaandishi. Naomba nijue kuhusu Chuo cha Ufundi Kagera kilichokuwa sehemu ya Gera na Rwamishenye.

Vilikuwa vinafanya kazi vizuri kipindi cha nyuma, lakini kwa sasa hivi, hivyo vyuo havifanyi kazi. Hivi naomba kujua Serikali ina mikakati gani ili kuwasaidia hasa vijana wa sehemu hizo pamoja na Mkoa mzima? Vijana wengi wanapenda kujiunga na ufundi, hivyo kuna Vyuo ambavyo ni vya Makanisa, watu binafsi, lakini vijana wanashindwa kumudu gharama kwa kuwa ni kubwa mno na mtu wa kawaida hawezi kumudu.

Je, Serikali ina mikakati gani katika kipindi hiki cha Awamu ya Nne ya kasi mpya? Naomba nipate jibu. Nikiwa kama Mwakilishi naomba Serikali ifufue kiwanda hiki cha Gera. Nitashukuru Serikali ikijibu vizuri kama inavyostahili. Ahsanteni. Naomba kutoa hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la maandishi haya ni kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Sitta kwa kuwasilisha hoja vizuri. Nawapongeza pia Wasaidizi wake wote, hasa Manaibu Waziri wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu imetafsiriwa kwa namna mbalimbali. Ila wote tunakubaliana kwamba, Elimu ni Ufunguo wa Maisha na kwamba elimu ni mwangaza usiozimika katika maisha ya mwanadamu. Mwenye elimu hata akifa atakuwa bado anaishi kwa sababu mchango wake utaendelea kuonekana japo yeye haishi kimwili tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itusaidie sana sisi tulio na Shule changa. Kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2000 – 2010, tumejenga Shule nyingi za Sekondari, lakini hazina mazingira mazuri ya kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule zetu hazimo kwenye kupewa mgawo wa pesa za *MMES*, wakati huo ndio zenye upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa, Maabara, nyumba za Walimu, Ofisi za Walimu na jengo la Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule hizi pia hazina Bodi za Walimu, kwa hiyo, maamuzi yanaendelea na Kamati za Ujenzi kusimamia Shule hizi hata baada ya kusajiliwa na Serikali. Hali hii inadhoofisha maamuzi rasmi ya kiserikali mfano maendeleo ya Shule na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali isaidie Shule zetu haraka, ambazo naomba nizitaje – Izigyo Sekondari, Kagoma Sekondari, Nyakatanga Sekondari, Ruhanga Sekondari, Kagondo Sekondari na Ibuga Sekondari. Naomba Shule hizi zisaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusaidiwe pia kupata Walimu. Ili tupate Walimu, lazima ziwepo nyumba za Walimu. Tusaidiwe kujenga nyumba za Walimu ili Walimu wakubali kubaki kufundisha katika Shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la vitabu vya kiada na ziada. Naomba yaangaliwe ili watoto wetu ambao ni Taifa la kesho wasome vizuri; Taifa letu lisiangalie kwa kuwa na wengi waliohudhuria Elimu ya Sekondari bila kupata Elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shule za Msingi, naomba Muleba Kaskazini, tuangaliwe kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo Visiwa ambavyo wanaishi watu na wana watoto. Ninashauri na ninaomba tupate fursa ya kuanzisha Shule za *Satelite*. Mazingira ya kule ni magumu ambapo Shule ni chache sana na watoto wanakwenda Shule, wanatembea mwendo mrefu kwenda Shule. Aidha, watoto wengi hawaendi Shule kwa sababu ya umbali na mazingira magumu ya Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na wote walioshiriki katika kuindaa hotuba hii. Hotuba hii nimeisikiliza wakati Mheshimiwa Waziri akiisoma. Kisha, nilipata fursa ya kuisoma na hatimaye nikapata fursa kiasi ya kujisomea. Ni hotuba nzuri sana yenye maudhui yanayotoa matumaini ya maendeleo. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, naomba nichangie na kufanya maombi katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kujiwekea malengo na kuyaweka bayana. Nimeyapitia mara kadhaa na kwa tathmini yangu yote, mkiwezeshwa yanatekelezeka. Ni imani yangu kuwa baadhi ya malengo mtayatekeleza kikamilifu baada ya muda mfupi na inawezekana.

Napenda kuitumia fursa hii pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa watendaji na watumishi wa Wizara hii. Watumishi wa Wizara hii wamenilea tangu nikiwa mwanafunzi, nikiwa Mwalimu mwaka 1974 – 2005. Katika kipindi chote hiki nimejifunza mengi na nimeng'amua mengi katika Wizara hii.

Nawapongeza na kuwashukuru watumishi wa Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa nikiwa mtumishi wa Wizara hii. Sina kitu chochote cha kuwalipa kitakacholingana na mema mengi na heshima waliyonipa katika kipindi chote zaidi ya kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awape heri na mafanikio kwa kila walifanyalo Wizarani na nje, kwa faida yao na Watanzania wote kwa ujumla.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni Wizara muhimu sana kwa uhai, hadhi na maendeleo ya nchi yetu. Wizara hii haizalishi fedha moja kwa moja, ni Wizara yenye Watumishi wengi kuliko Wizara nyingine. Ni Wizara ambayo haina fedha za kutosheleza mahitaji yake. Ili Wizara hii ifanikishe malengo yake ya mwaka huu ya muda mfupi na mrefu nawaomba Watumishi wote wa Wizara hii wazidi kudumisha na kuimarisha umoja. Wawe watumishi wa familia moja *(The Education Community au Education Family).* Njia bora na nyepesi ni kuimarisha mawasiliano kwanza ndani ya Wizara Makao Makuu na Idara au Taasisi nje ya Makao Makuu na muhimu zaidi, kati ya Wizara na Watumishi Mikoani na Wilayani.

Kwa kuanzia, fanyeni tathmini ya dhati ya uwepo wa mawasilisano hayo na ni rahisi. Je, Kurugenzi ziko karibu kiasi gain? Ninachoshauri ni kufanya tathmini ya dhati na uwazi. Mkiridhika yanakidhi haja, yadumishwe na kadri itakavyowezekana yaimarishwe.

Ninaamini kwa dhati kuwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri ambaye ni mzoefu na mkereketwa wa maendeleo ya Elimu nchini, ushirikiano huu ukiwepo watafanya na kufanikiwa katika mengi na makubwa. Cha msingi, kila ammoja atambuliwe na kuheshimiwa katika nafasi yake na aitekeleze vizuri kadri ya uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa kuongeza Shule za Sekondari kwa Kidato cha Tano na Sita, naomba wahusika wapitie, wakaangalie Shule mbili. Nyamilama Sekondari na Mwamashimba ili kuona kama zinakidhi mahitaji ya kupandishwa hadhi kutoka *"O" Level* mpaka *"A" Level.* Ninatambua ya kuwa Shule za *"A" Level* ni za kitaifa, lakini ninaamini kuwa wapo vijana wanaosoma katika Shule hizo na zinazozunguka Shule hizo watakaochaguliwa pamoja na vijana toka sehemu nyingine nchini. Hivyo, vijana hao sio tu watakuwa vijana wa mfano kwa vijana wenzao, bali pia kutokana na ukaribu, itakukwa msaada mkubwa kwa wazazi wao.

Ombi lingine ni kuhusiana na ombi la muda mrefu la Wilaya ya Kwimba la kuibadilisha Shule ya Sekondari ya Kutwa mchanganyiko kuwa ya wasichana tu. Katika Kata hiyo, zipo Shule mbili Nera na Imalilo. Shule ya Sekondari Nera ikibadilishwa kuwa ya wasichana tu, Imalilo itaendelea kuwa ya Kata (kutwa mchanganyiko). Wilaya itafurahi kupata kibali hicho kabla ya uchaguzi wa wanafunzi Kidato cha kwanza mwaka 2007.

Mwisho, ninawatakia heri katika yote mnayoyapanga na kwa vile ninawaamini na Wana-Kwimba wanawaamini. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wana-Kwimba, ninaunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie maeneo yafuatayo: Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Hali ya Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa lolote duniani. Kwenye Jimbo la Vunjo, Shule nyingi za Msingi zimeharibika kwa kukosa matengenzo kwa muda mrefu. Naomba Serikali hata kwa kutumia Wakaguzi watembelee mashule na kutoa maelekezo ya kutengeneza Shule mbovu. Wakaguzi wahakikishe kila Shule ina madawati ya kutosha. Serikali ihakikishe watoto wanapata chakula cha mchana. Serikali ihakikishe vitabu pamoja na madaftari yapo Shuleni. Tujitahidi kuwa na Maktaba ndani ya mashule yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Shule za Sekondari, tumejenga Shule za Sekondari kila Kata lakini kuna upungufu mkubwa wa Walimu na hakuna Maabara kabisa. Serikali kwa kupitia utaratibu kama ule wa *MMES,* ianze kujenga Maabara hatua kwa hatua mpaka Shule zote zienee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hadhi ya Waalimu, Walimu ni kioo cha nchi yetu kwa kuwa wapo kila mahali. Nashauri mishahara yao iongezwe na wapate heshima mbele ya jamii, wawe mfano bora ndani ya jamii ya kitanzania. Naomba Walimu wapewe zana za kufundishia. Pia, wawe na utaraibu wa kujiendeleza unaosimamiwa na Serikali. Kuwe na utaratibu wa matibabu, maana mashule yametapakaa sana na utaratibu wa Bima ya Afya unawaumiza Walimu walio Vijijini. Vile vile, wapewe nyumba nzuri za kuishi na Serikali inaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri pamoja na Manaibu wako na Watendaji nawapongeza kwa Bajeti nzuri na ya kisayansi isiyo na ubabaishaji.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanazofanya kwa niaba ya wananchi katika kutekeleza na kusimamia majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Nchi yetu imepata mafanikio makubwa katika kupanua, kuboresha, kusimamia, na kuongeza Sekta ya Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu na Mafunzo kwa kiwango cha juu tangu mwaka 1996 - 2006. Nawapongeza Watendaji wote waliokuwa mstari wa mbele katika kuinua kiwango cha Elimu ya Msingi, Sekodnari, Ualimu na Mafunzo ya Ufundi. Bado kuna kazi kubwa mbele yetu kufikia malengo na azma ya kuwa na *Secondary School for all,* ikiwezekana asilimia 80. Ili tuweze kufikia lengo la *Univewrsal Secondary Education (USE)* itabidi kila mmoja wetu atekeleze wajibu wake katika utekelezaji wa *MMES*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kama ifuatavyo: Sambamba na utekelezaji wa Mradi wa *MMES* imefika wakati Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ianze kuandaa mpango na makakati wa kutekeleza mafunzo ya *Polytechnic* kama ilivyoainishwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995.

Vyuo vya *Politechinic* ni viungo muhimu kati ya Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu. Kutokuwa na *Politechnic* katika Mfumo wetu wa Elimu, kumesababisha idadi kubwa ya wanafunzi wengi wa Sekondari wanaomaliza masomo yao kutoendelea na Elimu ya Juu. Naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi jinsi alivyoweza kuiwasilisha vizuri mada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza Wizara ya Elimu kwa kupanga hotuba hii ikiwa na malengo na masuala ya kukuza elimu na mafunzo nchini Tanzania ili kumwendeleza Mtanzania kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuchangia maeneo machache tu ikiwa ni msisitizo katika Wizara hii. Kwanza, naomba Wizara itilie mkazo suala la kufundisha Kiingereza katika Shule za Awali ili wanafunzi watakapofika Darasa la Tatu waweze kuzungumza Kiingereza, kwani inapofika wakati wa mtihani wa Darasa la Saba wanakuwa na taabu kufanya mitihani ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wazee wengi wenye fedha wanaangalia Shule Binafsi zinazofundisha Kiingereza, hivyo Shule za Serikali zitakapoanzisha mtindo huo, wanyonge wataweza kufaidika na kushindana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule nyingi zina upungufu wa Walimu. Imefikia wakati Mwalimu mmoja wa fani fulani anapangiwa madarasa mengi kinyume na uwezo wake, mwisho wake wanafunzi hawapati muda wa kumwelewa Mwalimu kwa urahisi. Muda mwingine Mwalimu anaingia darasani kutoa *points* tu na kuwaambia wanafunzi

tafuteni notsi darasa fulani. Hii inawapa shida sana wanafunzi. Mwalimu huyo huyo anatafuta muda wa kwenda *tuition*. Hili naona liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba Wizara iajiri Walimu wenye uwezo mzuri kulingana na fani walizonazo, sio vyeti vya kufoji. Wizara ifanye utafiti wa kina jinsi ya kuajiri Walimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitabu vinavyonunuliwa au fedha zinazotolewa kwa ajili ya vitabu viwafikie walengwa na sio kila siku wanafunzi wanaambiwa vitabu hakuna. Wizara ifanye utafiti wa kutosha kujua vitabu vimefika, sio kufundishia wanafunzi wa *tuition.*

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Kwanza, natoa pongezi kwa Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Margareth Sitta, Naibu Mawaziri wa Wizara hii pamoja na wataalam katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuboresha jamii ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumzia suala la maboma ambayo wananchi walichangia nguvu zao na mpaka sasa hayajakamilishwa kwa hatua mbalimbali. Naomba Serikali na Wizara hii izingatie umuhimu wa kukamilisha maboma haya na wananchi tusiwavunuje moyo katika uchangiaji nguvu kazi katika shughuli za maendeleo.

Naomba Serikali ione ni namna gani tutaboresha elimu ikiwa hatuna madarasa na nyumba za Walimu huku wanafunzi kwa mfano katika Shule ni wengi na wanahitaji huduma kutoka kwa Walimu na hata kukaa chini ya miti kutokana na upungufu wa madarasa.

Hivyo, naomba Serikali ifanye jitihada za aina yake kupeleka fedha za kukamilisha maboma haya hasa katika Mkoa wa Shinyanga na Wilaya zake nane zenye matatizo kama hayo ukizingatia hali ya elimu ni duni sana. (Elimu ya Msingi na pia Elimu ya Sekondari).

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba pia Serikali ifanya juhudi za haraka kupeleka Walimu katika Shule zetu za Msingi na Sekondari zenye upungufu mkubwa wa Walimu kama Shule moja ya Msingi inaweza kuwa na watoto 1200, Walimu wako sita, je, ni kweli watamudu huduma kwa mtoto? Katika Shule za Sekondari, Shule ina wanafunzi 600, walimu wawili au watatu hasa kwa Shule tulizozianzisha, zina hali mbaya ya kutokuwa na Walimu. Hivyo, Serikali ione umuhimu kuharakisha juhudi za kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia ifanye jitihada za kujenga Maabara katika Shule hizi za Sekondari ili wanafunzi hawa nao waende sambamba na ulimwengu wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilete kilio cha pekee na Serikali naomba ione kuwa ni kilio kweli kweli. Kilio hiki ni katika suala zima la Shule hizi za kutwa zilizokwishaanzishwa na zinazoendelea kujengwa. Shule hizi zina wanafunzi wa kike ambao wanaishi katika mazingira magumu na vishawishi vingi na hasa ukizingatia kwamba kuna janga la UKIMWI na uduni wa mwanamke wa Kitanzania kama hatasoma, ni lini jamii hii itabadilika hasa katika Mkoa wa Shinyanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifanye jitihada za kujenga mabweni katika Shule hizi kwani itasaidia na kuwainua wanafunzi wa kike ambao jamii ya Shinyanga haijaona umuhimu wa mtoto wa kike kusoma Shule. Hivyo, hoja ya mwanafunzi kusoma Shule ya kutwa inampa mazingira magumu sana mtoto huyu, mara azuiliwe kusaidia kazi za majumbani, mara anyimwe nafasi ya kujisomea na mambo mengi yanayomkwaza mwanafunzi huyu.

Mwisho, Serikali ione umuhimu wa fedha za *MMES* kuzihusisha rasmi Halmashauri zetu ili ziweze kusimamia suala zima la ujenzi wa madarasa na nyumba za Walimu ili kuzuia na kudhibiti urasimu uliopo sasa hivi kwa Walimu Wakuu/Wakuu wa Shule zetu za Sekondari ambao hawana uchungu na jamii, lakini Halmashauri ndizo zenye kujua matatizo ya jamii na kuhitaji maendeleo katika maeneo yao (Madiwani na Halmashauri).

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo, sina maana ya kuwaondolea mamlaka Wakuu wa Shule, bali ni kuharakisha juhudi za Serikali za Mpango wa *MMES*. Wakuu wa Shule waendelee na mamlaka ya kiutendaji ili Halmashauri zisaide shughuli za ujenzi na kukabidhi Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. KIUMBWA M. MBARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo kuchangia hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Pia, nampongeza Waziri kwa kutuletea kitabu cha aina yake chenye hotuba nzuri inayosomeka na inayoungana na Wizara yake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Baraza la Mitihani Tanzania. Ningeomba Serikali kwa kupitia Wizara hii irekebishe adhabu iliyowekwa ya mwanafunzi anayethibitisha ameiba mtihani. Mwanafunzi kumweka miaka miwili kufanya mtihani ni kumkomaza na kumharibia maisha yake ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wasichana wanaopata mimba Shuleni, lifikiriwe kwa kina na iwekwe sheria kali kwa wanafunzi wote wawili na kisha wanafunzi wa kike wasifukuzwe Shule na akishajifungua aachiwe aendelee na kusoma.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Sitta na Manaibu wake wote wawili Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Mwantum Mahiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nawapongeza Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Prof. Hamis Dihenga na Bwana Oliver Paul Mhaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Namtumbo ni miongoni mwa Wilaya mpya na Halmashauri yake imeziduliwa mwaka huu. Ni Wilaya iliyotokana na iliyokuwa Wilaya kubwa ya Songea Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kugawa Wilaya, zoezi la kugawa Walimu halikutazamwa, matokeo yake idadi ya Walimu wa Wilaya ya Namtumbo imekuwa ndogo kutokana na sababu ya kwamba Wilaya ilipogawanywa, Walimu wengi wa Songea Vijijini walikuwa katika Shule zilizokuwa karibu na Makao Makuu ya Wilaya. Hivyo, upungufu wote uliokuwa unaonekana Songea Vijijini kwa wakati ule ulikuwa kwenye maeneo ya pembezoni na sehemu kubwa ni ambayo ndiyo Namtumbo ya sasa. Hivyo, kufanya kuwa na upungufu mkubwa wa Walimu. Kwa mfano halisi:

| **Wilaya** | **Wanafunzi** | **Walimu** |
|---|---|---|
| Songea Vijijini | (43,000) | (1009) |
| *Average* | (42) | (1) |
| Namtumbo | (44,000) | (679) |
| *Average* | (65) | (1) |

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo inaipelekea Wilaya ya Namtumbo kuwa na upungufu mkubwa wa Walimu na kushindwa kumudu ufundishaji karibu Shule zote za Wilaya. Naomba kuishauri Serikali kwamba Namtumbo iongezewe Walimu wapya kama zoezi la kurekebisha idadi hiyo, isiitazame Namtumbo kwa kufuata mgao wa kitaifa. Naomba Serikali iitazame Namtumbo kwa mapungufu hayo niliyoyaeleza hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa analihutubia Bunge, alisema; naomba kumnukuu: "Hakuna Taifa lililopata maendeleo bila kuendeleza elimu. Hivyo, kuendeleza elimu nchini, itakuwa ni agenda muhimu ya Serikali ya Awamu ya Nne." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo katika Kitabu cha Bajeti katika hotuba yake *Roman (ii)* amesema: Naomba nimnukuu: "DHIMA: Kutoa fursa sawa ya elimu bora kwa wote na kuhakikisha kuwepo mazingira mazuri ya kisheria na kiutendaji." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika karne hii ya 21, tupo katika zama za utandawazi, wanafunzi wengi wa Mijini wanafundishwa namna ya kutumia teknolojia ya kisasa kwa mfano *computer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, wanafunzi wa Jimbo la Namtumbo hawawezi kuwa sawa na wale wa Mijini na Wilaya nyingine ambazo zimepiga hatua kielimu hasa ukizingatia Jimbo la Namtumbo halina umeme na lina upungufu mkubwa wa Walimu, hivyo, kukosa fursa ya kuwa na nafasi ya kupata elimu iliyo sawa na inayoendana na zama za utandawazi katika karne hii tuliyonayo na hivyo, kuendelea

kutengwa na kuwa katika mgawanyiko mkubwa wa kielimu kwa waliopata elimu sana na wasiopata elimu wanayostahili kupata kama Watanzania wa Taifa moja.

Naiomba Serikali ya Awamu ya Nne iangalie suala zima la elimu katika maeneo yaliyo nyuma kielimu ili nayo yaendane na elimu ya wakati tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa kasi mpya, nguvu mpya na Ari mpya, Serikali italivalia njuga suala hili na itaanza na Jimbo la Namtumbo na hasa ni kuzingatia umahiri na umakini wa viongozi wetu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya elimu yanahitaji kuwepo kwa Walimu wa kutosha katika Shule zote.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Vile vile, nampongeza Waziri na Watendaji wake kwa kuandaa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kusimamia vyema Idara ya Elimu ya Sekondari na wananchi wazidi kujenga majengo ya Shule na kuwahamasisha katika masomo na mafunzo mbalimbali kwani wakimaliza wanahitaji kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, utekelezaji wa malengo ya Elimu ya Sekondari yaende sambamba na mazingira ya mwanafunzi yanayomkabili ili aweze kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naunga mkono miradi mbalimbali kama Mradi wa *Prevention and Awareness in School of HIV and AIDS (PASHA).* Mradi utawawezesha watoto kutambua na jinsi ya kujikinga na gonjwa hatari linalotukabili na pia, kuwaelimisha wazazi wa wenziwao popote walipo, kwani wakiwa salama, wataweza kuongoza nchi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitoe pongezi za dhati kabisa kwa kazi nzuri Wizara inayoifanya ikiwa ni kuanzia Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza Wizara kwa kusajili Shule nyingi mpya nchini kote. Ninafahamu kuwa muda wa kusajili Sekondari mpya umeshapita, lakini nina ombi maalum kutoka Jimboni kwangu Hai katika Kata ambayo Vijiji vya jirani na *KIA* vina Shule nyingi za Msingi kama Shule ya Msingi *KIA*, Mtakuja, Tindigani Mashariki, *Sanya Station* na Rundugai Shule ya Msingi. Lakini hakuna Shule ya Sekondari. Baada ya Vikao vya Maendeleo vya Vijiji husika, Vijiji vilikubaliana kusimamisha shughuli nyingine zote na kuelekeza nguvu zao zote kwenye ujenzi wa Sekondari kwa ajili ya watoto wao na hivi sasa majengo ya madarasa na nyumba tatu za

Walimu pamoja na jengo la Utawala yameshakamilika na Halmashauri iko tayari kuweka samani muda wowote kwani ziko tayari.

Kwa kuzingatia jamii husika katika Vijiji hivi ni ya ndugu zetu wa kabila la Wamasai ambapo binti zao huweza kuolewa katika umri mdogo, ninaomba kuwasilisha ombi maalum kwamba Shule hii ipate usajili wa dharura na wa haraka ili kuwanusuru hawa mabinti wasije wakaolewa. Wazazi wa watoto hao wako tayari kutoa ushirikiano wowote utakaohitajika ili kufanikisha kuanza kwa Shule hiyo na hata Maafisa wa Kanda wameshafanya ukaguzi wa awali hapo tarehe Mosi Juni, 2006. Pia ninaomba kusisitiza kuwa, kuna watoto wenye umri mkubwa ambao walichelwa kuanza Shule na wavulana kukimbilia kwenye machimbo ya Mirerani. Ninaomba sana hii Shule isajiliwe na kuanza muda huu kwa *crush programme*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu mafanikio zaidi.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari ya Ganako, Wilaya ya Karatu wananchi walihamasishwa na kujenga vyumba vinne vya Maabara hadi *renter* mwaka 2004/2005 kwa ahadi kuwa Serikali itachukua jukumu la kukamilisha majengo hayo kama ilivyoahidiwa. Wataalam wa Wizara walishakagua majengo hayo na kuridhika kuwa yametimiza masharti. Sasa ninapenda kuhakikishiwa na Waziri wakati wa atakapofanya majumuisho kama majengo hayo ya Maabara yako katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 ili wananchi wasikatishwe tamaa na ahadi hiyo ya Serikali ambayo sasa ni mwaka wa tatu bila kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ukaguzi ni muhimu sana katika kusimamia na kuhakikisha elimu inayotolewa ni bora. Nafurahi kuwa angalau Wizara inanunua magari 18 na *computer* 80 kuimarisha Idara hii. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kuwa Idara hii inakumbana na matatizo makubwa kwa kukosa fedha za *OC*. Wizara au inapeleka fedha kidogo sana; tena hiyo kidogo inachelewa sana au haifiki kabisa. Wakurugenzi Watendaji nao hawatengi fedha kwa vile Wakaguzi hawawajibiki kwao "kiwajibu."

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri fedha za kutosha zitengwe kuwezesha Idara hii kutekeleza majukumu yao na ikiwezekana *OC* inayopelekwa Wilayani itumike pia kwa ukaguzi kuliko safari nyingi za Afisa Elimu Wilaya ambazo mara nyingi hazina tija ya moja kwa moja na ubora wa elimu. Magari ya Idara ya Elimu hutumika katika utawala wakati wa Wakaguzi wanashindwa kufanya kazi hii muhimu. Wizara itoe maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, naomba kurudia hoja ya kuwa na Hosteli katika kila Shule ya Kutwa. Kata ni eneo kubwa sana kwa watoto kutoka na kurudi nyumbani kila siku. Isitoshe, Shule nyingi zimekuwa zikipokea watoto toka nje ya Kata na hivyo kulazimisha watoto kupanga kwenye nyumba za kupanga ambazo mara nyingi hazipo au hazipo katika hali na mazingira mazuri. Hali hii

imewasababisha watoto kuita Hosteli hizo *ghetto*. Maisha katika *ghetto* ni mabaya siyo tu kwa watoto wa kike bali kwa watoto wote. Madhara ya *ghetto* kwa watoto wa kike yanaweza kuonekana haraka sana, mathalan mimba. Kwa watoto wa kiume, madhara kama dawa za kulevya, bangi, tabia za kihuni na kadhalika inachukua muda mrefu kuonekana. Kwa msingi huo, madhara kwa watoto wa kiume ni ya muda mrefu na mabaya zaidi. Hivyo, umuhimu kwa Hosteli uwe kwa watoto wa jinsia zote, vinginevyo athari ni kubwa sana kwa watoto wetu ambao ni raslimali ya siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Wizara iweke mkazo katika kila Shule, kabla haijafunguliwa iwe na Hosteli ya kuwatosha watoto wote badala ya kuwaacha watoto kulala *ghetto*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upungufu wa Walimu hasa wa Sekondari inadidimiza kabisa ubora wa elimu. Nashukuru mwaka huu 2006 wanakwenda Chuoni zaidi ya vijana 7,000 yaani Walimu Tarajali. Naishauri Wizara kwamba kuwe na mpango wa makusudi kabisa kuandaa Walimu na ikiwezekana *Crash Programme* zinazoandaliwa ziwahusishe *graduates* wote ambao hawajaajiriwa kwa utaratibu wa kawaida. Vinginevyo, tuna majengo, tuna watoto, lakini hatuna Walimu na elimu haiwezi kupatikana bila Mwalimu. Shule kadhaa hadi leo zina Walimu wawili tu, hazina Mkuu wa Shule na hata hao wawili ni Walimu wa kushikiza tu kwa maana ya Kidato cha Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukurani za dhati.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kandaa Bajeti nzuri pia na uwakilishaji mzuri.

Nawapongeza kwa maendeleo mazuri ya Elimu kwa ujumla hasa uandikishaji wa wanafunzi na ongezeko la vyumba vya madarasa. Tuendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida kubwa sasa ni Walimu. Naafiki utaratibu wa sasa wa kuwatumia vijana wetu wa Sekondari. Lakini ninashauri lazima tuweke mkakati wa kutatua suala hili ili tuwe na Walimu halisi na wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu kupata Walimu wa vipindi vya Sayansi na Hisabati. Hali inakuwa mbaya zaidi kwetu tuliopo katika maeneo ya pembezoni na ambayo hayana vivutio hususan Jimbo langu, liko mpakani mwa Rwanda na Uganda, Serikali iangalie utatuzi wa suala hili.

Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa Walimu, napendekeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilegeze kwa muda ruhusa ya Walimu kutoka nchi jirani hususan Uganda, hasa kwetu tulio jirani na maeneo hayo ya Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara yake. Nawapongeza pia Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuiomba Wizara hii kuwasaidia Walimu posho za nauli na malazi wanapofuata mishahara yao Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu ni watumishi wa Serikali kama walivyo watumishi wengine wa Serikali; iweje Mwalimu anaposafiri kufuata mshahara wake asilipwe posho ya malazi na nauli? Kwani safari za kufuata misharaka ni safari binafsi kwa Mwalimu au ni ya kikazi? Je, ni lini Serikali itawarudishia Walimu pesa wanazotumia kama nauli na malazi wanapofuata mishahara yao Wilayani? Kama Serikali haiwezi kuwarudishia pesa zao, basi Serikali ifanye utaratibu wa kuwalipa Walimu mishahara mahali walipo (Mashuleni). Walimu wanaonewa katika suala hili ukizingatia kuwa mishara yao ni midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto wa kike anapopata mimba haruhusiwi kuendelea na masomo hata baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali ina nia ya kumwendeleza mtoto wa kike, naiomba Serikali ifikirie uwezekano wa kuwarudisha masomoni watoto wa kike wanaopata ujauzito wakiwa mashuleni, baada ya kujifungua mwanafunzi aendelee na masomo kama kawaida na hii itawawezesha wanafunzi wa kike kujiandaa kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni uonevu kumfukuza mtoto wa kike Shule na kumwacha aliyempa mimba akiendelea na shughuli zake kama kawaida. Adhabu wanazopewa wanaume wanaowapa mimba watoto wa kike, haziridhishi, kwani kwa mwanafunzi wa kike maisha ya baadaye yanakosa mwelekeo. Naiomba Serikali kuwaruhusu watoto wa kike kuendelea na masomo baada ya kujifungua. Katika majumuisho hili lijibiwe tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Elimu kwa kuanzisha mitaala ya Ukimwi mashuleni. Tunajua Ukimwi ni gonjwa hatari na linamaliza nguvu kazi ya Taifa. Naamini elimu kuhusu Ukimwi, ikifundishwa kuanzia Shule za Msingi lengo la Serikali la kupunguza maambukizi litafanikiwa. Katika kitabu cha Bajeti ukurasa wa 38 Wizara imepanga kuwasaidia Walimu na wafanyakazi walioathrika na gonjwa hatari la Ukimwi; kama hilo ndilo lengo la Serikali. Je, wanafunzi walioathirika na gonjwa hili watasaidiwa na nani? Naiomba Wizara ya Elimu itenge fedha kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi watakaogungulika wameathirika, wasaidiwe sambamba na walimu na Wafanyakazi wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waraka *No.3/2000* inaendekeza kuundwa kwa Kamati za Ukimwi Mashuleni; lakini kutokana na utafiti nilioufanya katika Mkoa wa Dodoma, Kamati hizo hazijaundwa katika Shule za Msingi wala Sekondari. Naiomba Serikali kusimamia na kuhakikisha kuwa Kamati zinaundwa na kutekeleza wajibu kama Waraka wa Serikali unavyoagiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzazi wa mwanafunzi anapomwozesha binti yake kabla ya kumaliza masomo anashitakiwa; je, kwa nini mzazi aneyemwachisha mtoto Shule kwa ajili ya kuchunga ng'ombe, kufanya biashara ndogo ndogo na kadhalika, asishitakiwe? Serikali ina mikakati mizuri ya kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata haki zao za msingi na hasa elimu; lakini Serikali haina mikakati ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wote walioandikishwa Shule wanamaliza Elimu ya Msingi.

Naiomba Serikali, Kamati za Shule ziwajibike katika suala hili na wazazi wanaozembea mahudhurio ya watoto wao mashuleni wawajibishwe na wale wanaowaachisha watoto masomo washitakiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza Vyuo vya *VETA* ili vijana wengi wapate Elimu ya Ufundi na waweze kujitegemea kwa kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwa wanafunzi watakaofaulu na kukosa nafasi ya kujiunga na Elimu ya Sekondari wapelekwe moja kwa moja *VETA* ili wakajifunze ufundi na baada ya kumaliza Chuo cha *VETA* wakopeshwe vifaa vya kuanzia kazi baada ya kumaliza na kurudi katika Vijiji na Mijini.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Napenda kupongeza hotuba ya Kwanza ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Ufundi. Imeandikwa kwa ufundi mkubwa halafu hata *quality* ya uchapishaji inafanya mtu apende kusoma kitabu hiki. Hongera sana.

Sasa naomba nisaidiwe katika mambo yafuatayo:-

(a) Sekondari ya Njombe sasa ni ya kitaifa. Lakini majengo ya *Form V* na *VI* walijenga wananchi ambao hivi sasa wanakabiliwa na ukarabati mkubwa wa Shule ya Sekondari Mpechi, ujenzi wa Shule ya Sekondari Maheve na Mabatini pale Njombe Mjini.

Ombi langu ni kuwa, tunaomba mtufidie majengo hayo ili tuimarishe hali ya majengo ya Sekondari Mpechi ambayo ipo katika hali mbaya sana.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Waziri, Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi zao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri imeeleweka na imeandikwa kwa ufasaha, nami naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuanzisha Elimu ya Awali kwa kila Shule ya Msingi. Mpango huu ni mzuri na ndiyo uliokuwa unawapa msingi mzuri watoto waliokuwa wanasoma Shule za Watu Binafsi *(Private)* ukilinganisha na Shule za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, katika kupata Walimu wa Shule hizi za Awali, Serikali isitegemee Shule zake tu, bali iajiri Walimu kutoka kwenye Vyuo vya Walimu vya *private* pia.

Mhesghimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kutekeleza Mpango mzuri wa *MMEM*. Pamoja na kujenga Shule nyingi kwa maana ya madarasa, ni vyema sasa mkazo mkubwa ukawa kwenye ujenzi wa nyumba za Walimu. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambayo tunaitekeleza kwa miaka hii mitano, imeahidi kuwawekea Walimu wa Shule za Msingi mazingira mazuri ya kuishi kwa maana ya nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba nijielekeze kwenye Wilaya yangu ya Kilombero. Wilaya imeitikia wito wa Ilani wa kuanza kujenga angalau Sekondari moja ya Kata kwa miaka mitano ijayo. Wananchi wameitikia wito na katika mwaka huu wa mwanzo wamefungua Shule za Sekondari, nane kati ya Kata 19 za Wilaya yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule hizi zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa Walimu. Kwa vile, kuna mkakati wa kuajiri Walimu wengi, naomba Walimu hao wagawanywe vizuri ili kila Wilaya ipate. Kwa sasa Waratibu wa Elimu Kata, ndiyo wanawafundisha wanafunzi katika Shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za *MMES*, ombi langu ni kuwa, fedha hizo zipelekwe kwenye maeneo ya Shule kupitia Halmashauri za Wilaya kama vile fedha za *MMEM* zilivyopelekwa. Kamati za Shule ziwajibike katika fedha hizi na wawajibike kwa Kamati ya Elimu ya Halmashauri ya Wilaya Husika. Mtindo wa sasa wa kupeleka fedha hizi kwa Wakuu wa Sekondari za Wilaya husika hauleti uwajibikaji na ufanisi wa matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Maabara usiwe tu kwa Shule za Sekondari zenye Kidato cha Kwanza hadi cha sita tu, bali Shule zote za Sekondari hata hizi tunazozianzisha katika Kata zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea katika Wilaya yangu, miaka ya nyuma Wamisionari walitusaidia sana kwa kuanzisha Shule ambazo waliziita *Industrial Schools.* Walengwa walikuwa wahitimu wa Darasa la IV (1950 – 1967) ambao hawakupata nafasi ya kwenda Darasa la V - VIII. Walijifunza ufundi wa Uashi, Useremala, Ushonaji na Umakenika. Sasa hivi, hao Wamisionari hawapo na Vyuo hivi vimekufa kwa kukosa mitaji ya kuviendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kinaelezea ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)* katika kila Wilaya ifikapo mwaka 2010. Naomba mambo yafuatayo:-

Kwa zile Wilaya ambazo hazina Vyuo hivi, (kama Wilaya yangu ya Kilombero) maandalizi ya awali yafanyike. Wizara ishirikiane na Halmashauri ili kutenga maeneo kwenye Wilaya zao kufuatana na michoro ya majengo ya Vyuo hivi yaliyokubalika. Kwa vile mpaka muda huu tuna miaka minne na nusu tu kufikia mwaka 2010, viwanja kwa

ujenzi wa Vyuo hivi vipatikane kwa kipindi hiki cha mwaka 2006/ 2007 ili tubakie na shughuli za ujenzi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari ya Ifakara ilijengwa pamoja na Shule nyingine za mchepuo wa kilimo kama Kibiti na Ruvu. Baadaye hii Shule ikageuzwa kuwa ya Wasichana, kuanzia Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita. Shule hii iko Kilometa 12 kutoka Ifakara Mjini ambako ndiko iliko Hospitali Teule ya Wilaya ya *St. Francis Hospital Ifakara*. Ninashukuru kwa Mheshimiwa Waziri kuyapokea maombi yangu juu ya matatizo yanayoikabili Shule hii hasa juu ya tatizo sugu la usafiri.

Pamoja na kwamba alinishauri niandike barua kwa maandishi, jambo ambalo nimelifanya, maelezo hayo ni kwa ajili ya kukumbusha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Shule hii wapatiwe gari ili wakidhi dharura za magonjwa yanapotokea, hasa nyakati za usiku. Kwa sasa wanatumia baiskeli kukidhi dharura hizi kama zikitokea kwa msaada wa Wasamaria wema.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri na ya kueleweka kwa kila msikilizaji.

Mheshimiwa Naibu spika, pongezi hizo pia ziwafikie Manaibu Waziri wa Wizara hiyo pamoja na Wizara nzima kwa jumla kutokana na maandalizi yao mazuri ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa jitihada zake za dhati katika kutoa kipaumbele kwenye elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawapongeza wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini kwa kuitikia wito wa kujenga Shule za Sekondari katika kila Kata. Pongezi maalum zimfikie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ufuatiliaji wake wa karibu hadi kufanikisha zoezi hili la leo hii matunda tunayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, pamoja na shukurani, napenda sasa nianze mchango wangu katika Sekta ya Elimu hususan Elimu ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kuwa elimu ni muhimu kwa Taifa lolote, lakini tuelewe kuwa elimu hiyo ni lazima iwe ya kumtoa mtu katika umasikni na kumweka kwenye unafuu wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni lazima ipimike ili faida zake zionekane kwa jamii. Sio vizuri elimu ikiwa ni Cheti bila uwezo wa mwenye Cheti husika, elimu ni muhimu ikawa yenye kumpa mtu ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata elimu yenye faida kwa jamii au elimu inayompa mtu ujuzi, ni lazima turejee kwenye Sheria ya Elimu *(education Act)* na jukumu la Halmashauri za Serikali za Mitaa katika Kujenga Shule za Msingi, Vyuo vya

Ufundi *(trade Schools)* na *Regional Schools* au *Local Education Authority Schools (by Act No. 10/1995)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya sheria hiyo ilikuwa ni kwamba, kila Halmashauri ijenge Vyuo vya ufundi vya kuchukua wanafunzi wa Daraza la Saba ambao hawakubahatika kwenda Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Halmashauri zingefanya hivyo wakati huo, hivi sasa tungekuwa na watu wengi Vijijini ambao ni mafundi Uashi, Seremala, Umeme na kadhalika ambao wangejiajiri wenyewe na wengine kuajiriwa rasmi. Kwa hiyo, ujenzi wa nyumba Vijijini leo hii usingetegemea mafundi kutoka Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, laiti sera (Mfumo) wa kujenga Vyuo vya Ufundi ingetekelezwa tangu wakati huo, leo hii Vijijini tusingekuwa na uhaba wa mafundi mbalimbali kama vile mafundi wa zana za kilimo, mafundi wa magari, madereva wa vyombo vya kilimo, ususi, cherehani na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona na tunapongeza juhudi zilizofanya na Serikali kwenye *MMEM* na *MMES*, sasa umefika wakati muafaka kuleta elimu ya ufundi kwa kujenga Vyuo vya Ufundi *(Trade Schools)* ili kuwawezesha vijana ambao hawakupata bahati ya kuendelea na masomo ya Sekondari waweze kujiendeleza na kupata ujuzi kwenye hizi *trade schools.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia kila Halmashauri inaweza kujenga hatua kwa hatua Chuo kimoja katika kila Tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatima ya Vyuo hivi ni:-

- Kupata mafundi wa fani na ujuzi mbalimbali Vijijini;
- Kuwapatia vijana wengi walioishia Darasa la Saba ajira;
- Kuzuia wimbo la vijana kutoka Vijijini na kukimbilia Mijini; na
- Kukuza uchumi, kupunguza umasikini na kuwapatia Watanzania maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme bayana kuwa hakuna uwekezaji wa maana kwa watoto wetu zaidi ya kuwapatia elimu na hakuna urithi wa maana kwa watoto wetu zaidi ya kuwapatia elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Kurasini, Tandika na Mkangalawe zilijengwa kwa operesheni maalum chini ya agizo la Waziri Mkuu. Leo tarehe 19 Julai, 2006 saa 5.00 asubuhi Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke amenipigia simu ananiambia Mkaguzi wa Kanda wa Elimu amekataa kuzisajili Shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili za nyuma tulilalamika kwa Shule za Kinondoni tatizo kama hilo. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri alitoa tamko na Shule hizo zimesajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri katika Kikao chake cha Bajeti atoe tamko kuhusu Shule hizo tatu zipate kusajiliwa. Naomba atoe tamko ili wananchi wa Temeke wasikie na Mbunge wao asikie na Waziri Mkuu asikie na Katibu Mkuu wa Chama cha CCM ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa asikie. Naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni msingi wa maendeleo na adui mkubwa wa ujinga, maradhi na umasikini. Tukielimika na tukiwa na elimu bora tutajenga Taifa bora na lenye uwezo wa kuendesha nchi yetu kwa misingi iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa elimu bora hauji tu kwa dhana, bali ni kuwa na nyenzo. Nyenzo muhimu ya kwanza ni Walimu. Walimu bado ni tatizo sugu, hawatoshi kulingana na idadi ya wanafunzi. Walimu wenyewe pamoja na uhaba, bado wanafundisha katika mazingira magumu, mishahara midogo hata nyumba za kuishi hawana, tena wana uhaba wa vitabu vya kufundishia, havitoshi. Ni budi Wizara itatue tatizo la Walimu ili tupate Walimu bora ili kupata wanafunzi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi anahitaji kusoma katika mazingira mazuri ili kupata elimu iliyo bora. La kushangaza madarasa hayatoshi, madawati hayatoshi, mwanafunzi anakaa chini, vitabu vyenyewe havitoshi. Ni bora kuyaboresha haya ili kupata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la utoro na mimba za utotoni nalo linaathiri elimu kwa vijana wetu, kwa hiyo nalo linahitaji kutazamwa kwa mtazamo wa jicho la huruma na hasa kwa wakati huu wa maambukizo ya *HIV/AIDS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora pamoja na vitabu, majengo mazuri madawati, Walimu, mitaala na mitihani ni kigezo cha kutosha kupata elimu iliyo bora. Kwa hiyo, naomba Maabara ziimarishwe ili kupata elimu kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *MMEM* umefanikiwa kuhamasisha wananchi, idadi ya Shule imeongezeka na wanafunzi wamekuwa wengi zaidi na matokeo yameonekana kuwa mazuri. Ni jambo zuri na ni matarajio yangu kuwa mpango wa *MMES* nao utakuwa tayari kuwapokea wanafunzi wengi waliofanya vizuri kutoka kwenye mpango wa *MMEM.* Kwa hiyo, naiomba Wizara kwamba, mpango huu uende sanjari ili kondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ijitahidi kuviendeleza Vyuo vyote vya Walimu na Vyuo vya Ufundi ili kufikia lengo la madhumuni ya Wizara. Ahsante.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuweza kufika katika Kikao cha leo cha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta kwa hotuba yake nzuri na yenye kuleta matumaini. Pia, nawapongeza Watendaji wengine wa Wizara hiyo kwa mashirikiano yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri ya kuliongoza Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa lolote haliwezi kuendelea bila elimu. Elimu ni Sekta muhimu sana na inafaa ipewe kipaumbele katika kufikia kiwango kikubwa cha maendeleo ya nchi yetu. Elimu bora ndiyo itakayowezesha kuwa na msingi imara ambao utasaidia kuleta maendeleo kamili ya Taifa letu. Serikali lazima ihakikishe kwamba vijana wote wanapata elimu bora na wale ambao kwa bahati mbaya hawakupata nafasi ya kusoma, uandaliwe utaratibu maalum utakohakikisha kwamba wananchi wote angalau wanajue kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu ndio wenye jukumu kubwa na muhimu sana la kuwapatia vijana wetu elimu bora. Kwa hiyo, ni muimu Walimu hao waandaliwe vizuri kitaaluma, kimaisha (maslahi) pamoja na makazi bora. Vile vile, ni muhimu wapatiwe mazingira mazuri ya kazi yakiwa na vifaa muhimu vya kufundishia. Pia, ni muhimu kwa Walimu kupatiwa mishahara yao kwa wakati ili waweze kukidhi mahitaji yao na kuwa na utulivu kazini. Ni muda mrefu sasa mishahara ya Walimu imekuwa ikichelewa sana jambo ambalo linaathiri muda mwingi kuhangaikia mishahara hiyo na hivyo kukosa utulivu kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kuwa na Walimu bora, lakini ni muhimu pia kuwa na Walimu wa kutosha watakaokidhi mahitaji ya utoaji wa elimu kwa mashule yote ya Mijini na Vijijini. Idadi ya wanafunzi inaongezeka mwaka hadi mwaka, lakini idadi ya Walimu inapungua. Kwa hiyo, iko haja ya Serikali kuandaa mpango madhubuti utakaoharakisha kwamba Walimu wa kutosha wanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadui watatu wakubwa katika nchi yetu ni maradhi, ujinga na umasikini. Nchi yetu imekabiliwa na maadui hawa kwa muda mrefu na kwa kiwango kikubwa sana. Naiomba Serikali itilie mkazo mkubwa juu ya suala la elimu bora kwa vijana na Watanzania wote kwa jumla. Elimu ni ufunguo wa maisha. Tuiboreshe kwa maisha bora. Ahsante sana.

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutamka kuwa naunga mkono hoja. Aidha, nawapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi ya Bajeti jadidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, yapo maeneo kadhaa ambayo ninaonelea ni vyema nitoe ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo zuri kuwa na Shule zote zikiwa na madarasa ya Elimu ya Awali. Hata hivyo hakuna uwiano wa elimu, wanafunzi Waalimu na utoaji wa elimu. Elimu ya Awali ndio mahali pa kuanzia kujenga msingi wa elimu bora. Hivyo, ni mahali pa kusaidia kupeleka Walimu makini. Hakuna uhakika wa Walimu wa kutosha kwa Elimu ya Awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Shule zimepata ubora wa majengo kutokana na mpango wa *MMEM*, mazingira ya kusomea yamepewa hadhi inayostahili. Hata hivyo, napenda nieleze wazi kuwa kujisifu alikojisifu Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Kilimo wakati akijumuisha hoja za Wizara yake kwa kudokeza mafanikio yake akiwa Wizara ya elimu, hakuna maana sana maana kupata madarasa mazuri bila kuwa na Walimu sio tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda ifahamike kwamba, Wizara haifuatilii pesa inayopelekwa kwenye Shule, lakini Kamati za Shule zilizo nyingi zinaburuzwa na kudanganywa na Makatibu (Walimu Wakuu) na hivyo kufanya pesa kutumiwa nje ya utaratibu. Lengo la kila mtu kutumia kitabu vila kushirikiana na mwanafunzi mwenzake halitafikiwa kwani ununuzi wa vifaa haufuati taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili lina tatizo la uhaba wa Walimu. Cha kushangaza ni kwamba, tunazo Shule za watoto wenye vipaji maalum. Hawa wenye vipaji maalum wanatoka wapi? Hivi Serikali haioni kama Shule zote kutoka Msingi hadi Elimu ya Juu zingeweza kuwa na wanafunzi wenye vipaji maalum kama Walimu na vitendea kazi vingeweza kupatikana. Huwezi kusema Shule za Watoto wenye Vipaji maalum wakati katika nchi hii yapo maeneo maalum wamelundikana na maeneo mengine Walimu ni wachache? Ni dhahiri pale walipo Walimu wengine hali ya ufundishaji ni ya kuwezesha watoto kuwa na vipaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hapo juu kuwa wapo Walimu wanaoburuza Kamati za Shule. Katika kufanya hivyo, matumizi mabovu ya fedha za umma yanafanyika. Zipo taarifa kwamba ununuzi wa vifaa vya Shule unapata maelekezo na toka kwa Afisa Elimu wa Wilaya kwa kuzielekeza Kamati za Shule kununua vifaa toka katika maduka waliyoteua wao na ambako ni dhahiri kuna mgao wao. Mfano hai ni hivi karibuni nilipokuwa nafanya ziara Jimboni, nilipopata malalamiko toka Uongozi wa Kamati ya Shule ya Mgambo (Buhingu) kwamba wanaelekezwa na Afisa Elimu wakanunue vifaa kwenye maduka mahsusi aliyoyachagua. Hii ni rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Elimu huyu alivuruga utaratibu wa kufanya mtihani wa Darasa la Nne. Mtihani huu ulikuwa ufanyike Novemba, 2005. Badala yake, kwa sababu ya uzembe wake na mipangilio yake kutafuta rushwa, mtihani huo ulifanyika mwaka 2006 Januari. Hivi Wizara haina taarifa ya hili? Ni sababu zipi watakazoweza kuzitoa za kuridhisha zilizofanya mtihani wa Taifa ufanyike tarehe tofauti na sehemu

nyingine nchini? Nitaomba Mheshimiwa Waziri anijibu hili wakati wa majumuisho. Ahsante.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa kuonyesha uwezo, umakini na uadilifu katika kipindi kifupi walichofanya kazi.

Naipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kuanzisha *MMEM* na *MMES* kwa kusudi kubwa la kufufua na kuendeleza elimu kama nyenzo muhimu ya kupambana na umaskini.

Nawapongeza wananchi wa Mkoa wa Kagera kwa *MMEM* na *MMESS* na kuifanyia kazi na mafanikio ni makubwa. Wanawake walionyesha mwamko mkubwa sana na hivyo walishiriki kikamilifu kuchangia fedha na nguvu zao, hivyo, nami katika ziara zangu nilichangia katika miradi hiyo kwa kuunga mkono nguvu za wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya *MMEM* na *MMES*, Serikali imekuwa ikichangia fedha kwa kiwango sawa bila kujali jiografia ya nchi yetu. Fedha hiyo ilikusudiwa kununua vifaa vya ujenzi vinavyotengenezwa viwandani kama mabati, saruji, misumari na kadhalika ili wananchi nao wachangie vifaa vinavyopatikana katika maeneo yao kama mawe, matofali, mchanga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za bidhaa za viwandani ni ghali sana katika Mikoa iliyo mbali na viwanda ambavyo vipo Dar es Salaam, Tanga na kadhalika tofauti na Mikoa iliyo karibu na viwanda. Kwa Mkoa wa Kagera, natumaini ni mfano mzuri. Kwa fedha hizo zilizokuwa zikitolewa, ziliweza kununua vifaa kidogo kutokana na bei kuwa kubwa ukilinganisha na Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na mingineyo iliyo karibu na viwanda. Hata hivyo, ilikuwa ni nafuu kidogo kwa maeneo ya Mijijini kuliko zile zilizo mbali na Miji kutokana na gharama za usafiri na usafirishaji wa vifaa.

Naiomba Serikali ifikirie kurekebisha ili fedha inayotolewa na Serikali iendane na maeneo husika, vinginevyo katika baadhi ya maeneo ubora duni wa majengo unaweza kujitokeza.

Naiomba Wizara iishauri Serikali kuboresha Shule za Sekondari za Kata kwa kuziwekea umeme pale inapowezekana au umeme wa Solar ili ziweze kukidhi hali na haja ya kuzifanya zivutie watumiaji, Walimu, wanafunzi na hata wananchi wanaozizunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha na mimi nichangie hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mungu, sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyoitoa pamoja na kitabu chake cha hotuba ni

cha aina yake. Pia, niwapongeze Manaibu Waziri pamoja na Watendaji wote waliomsaidia Waziri kutengeneza Kitabu hiki na Uandishi wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hotuba hii kwa kifupi hasa kwa kuwa mengi yamekwishachangiwa na wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie Baraza la Mitihani Tanzania. Naipongeza Wizara kwa marekebisho makubwa ya Watendaji katika Baraza la Mitihani. Kwa habari niliyoipata ni kwamba, Wizara imefanya uhamisho wa Watendaji hawa na kupelekwa sehemu nyingine. Kama hayo ni kweli, naiomba Wizara itafute na maeneo mengine yanayoleta kero na kama sio kweli naomba marekeisho ya haraka yafanyike katika Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii imetupa taabu sana wazazi wakati wanapoiba mitihani na kuwauzia wanafunzi na baadaye wanafunzi wanafutiwa mitihani yao wanapobainika kuwa wamepata majibu ya mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwauzia wanafunzi mitihani ni kuwapotosha na kuwaharibia. Kwa sababu kuna wanafunzi ambao wamefutiwa mitihani walikuwa na uwezo wa kufaulu mitihani hiyo, lakini joto la mtihani limepanda na kusababisha kumfuata shetani. Kwa hiyo, nazipongeza juhudi hizi za kusafisha Baraza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya juhudi hizo, ningeiomba Serikali kupitia Wizara kubadilisha adhabu iliyowekwa ya mwanafunzi anayethibika ameiba mtihani ibadilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumzuia mwanafunzi kukaa muda mrefu wa miaka miwili kutofanya mtihani ni kumkomaza na kumharibia maisha yake ya baadaye kwa sababu kuna wenye uwezo na wengine hawana uwezo na kuamua kuacha kabisa masomo. Kwa hiyo, suala hili liangaliwe upya na badala yake waruhusiwe kufanya mitihani inayofuata wakati mwanafunzi ana uwezo wa kufanya mtihani huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwa imani aliyonayo atalishughulikia kwa ari mpya na nguvu mpya kwa sababu Waswahili wanasema mtoto akinyea kiganja cha mkono, mama haukati mkono bali huusafisha na kuendelea kumlea mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Bajeti ya Wizara hii. Ni nzuri na ipo wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nachingwea lina Shule hususan 11 za Sekondari ambazo zina wastani wa Mwalimu mmoja kwa kila Shule. Kuna tatizo kubwa la Walimu katika Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo pia tatizo hilo hilo la ukosefu wa Walimu katika Shule za Msingi. Nashauri Walimu wanaomaliza pale Nachingwe *TTC*, wengi wapangiwe kufundisha Nachingwea na Wilaya nyingine za Mkoa wa Lindi na Mtwara. Hawa wapo kule tayari na wamezoea hali ya maisha ya kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ijifikirie kuifanya Shule ya Sekondari ya *Farm 17* kuwa ni ya Kidato cha Tano na Sita kwa ajili ya kuhudumia Shule zote za Sekondari za Kata zote 26 za Nachingwea. Wilaya za Nchingwea, Liwale na Ruangwa zote zinaandaa Sekondari katika kila Kata, lakini hakuna hata Shule moja ya Kidato cha Tano na Sita. Sasa hawa vijana wakimaliza *Form Four* watakwenda wapi? Naomba Waziri atolee maelezo/ ufafanuzi mapendekezo haya.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa pamoja na Viongozi wote walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Chama cha Mapinduzi. Ni matumaini yangu kuwa utazidi kuimarisha Chama chetu na kusimamia Ilani ya Uchaguzi ili kuleta maisha bora kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Manaibu Mawaziri pamoja na Watendaji wao kwa kasi mpya waliyoanza nayo kuboresha elimu kupitia *MMEM* na *MMES* hasa kwa kuboresha mtaala wa elimu. Ni matumaini yangu kuwa kiwango cha elimu kitapanda na Wizara itazidi kubuni na kusimamia mipango ya uboreshaji elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila elimu Taifa haliwezi kuendelea. Hivyo, ni jukumu la Wizara kushirikiana na wananchi kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata elimu iliyo bora ili kuondoa ujinga, kwani wananchi wakielimika watondokana na maradhi hata umaskini uliokithiri katika jamii.

Pili, napenda kuzungumzia Shule Maalum za watoto wenye mtindio wa akili. Katika Mkoa wa Mtwara, tunazo Shule hizi hususan Wilaya ya Masasi Kata ya Lukuledi. Shule hii ipo katika eneo la Shule ya Sekondari Lukuledi na ina majengo yaliyorithiwa toka kwa Wamisionari na kukabidhi kwa Serikali kuwa Shule ya Msingi Lukuledi ambayo ndiyo yenye mkondo huu wa Shule maalum. Baadaye majengo haya yalikabidhiwa kuwa Sekondari na Shule ya Msingi kuhamia eneo lingine ambalo wananchi hawakuweza kujenga vyumba vya madarasa na mabweni kwa watoto wa Shule Maalum, hivyo, kubakia katika majengo yaliyopo eneo la Shule ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni dogo, majengo ni chakavu, Walimu hawana nyumba bora, kwani wanaishi katika eneo hili ili kuwa pamoja na watoto hao. Kwa kweli mazingira ni magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ione umuhimu wa kusaidia ujenzi wa madarasa, mabweni, nyumba za Walimu katika eneo la Shule za Msingi ambapo pana eneo la kutosha na Shule ya Msingi Lukuledi ndio Shule Mama na Shule Maalum ni

mkondo wake. Ninaomba ombi hili kwani Shule hii inachukua watoto wa Mkoa huu na nje ya Mkoa pia. Hivyo, ni muhimu Wizara kuona umuhimu wa ujenzi wa Shule hii. Upungufu wa Walimu ni kero kubwa katika Shule za Mkoa wa Mtwara za Sekondari na Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa huu watumishi wanafanya ni Mkoa wa kupatia ajira, wanakuja kuanza kazi na hatimaye kuhama nje ya Mkoa bila sababu za msingi. Hivyo, naomba Wizara iwe na mpango maalum wa kuwapeleka Chuoni wanafunzi wanaomaliza Sekondari watokao Mkoa huu ili wakimaliza mafunzo wabaki katika Mkoa wetu ili kuepuka Walimu watokao Mikoa mingine kuhama bila utaratibu na kutuachia upungufu mkubwa katika Shule zetu.

Mwisho, napenda kupongeza ujenzi wa madarasa ya *MMES* na *MMEM* unaoendela nchi nzima ili kuondokana na tatizo la upungufu wa vyumba vya kufundishia na nyumba za Walimu. Hii imeleta changamoto kubwa kwa jamii, kwani kimekuwa kivutio kikubwa katika kuandikisha watoto, hivyo kuwa na ongezeko kubwa katika Shule zetu. Ni matumaini yangu kuwa, mpango huu ukiendelea, tunaweza kupunguza idadi kubwa ya wasiojua kusoma.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote wawili kwa uteuliwa katika nyadhifa zao. Nawapongeza kwa kazi nzuri ambayo wameanza kufanya. Aidha, nawapongeza Watendaji wote wa Wizara pamoja na Walimu wote nchini, kwa jitihada zao kuwa za kuboresha elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuwaajiri Walimu moja kwa moja mara wanapomaliza au kuhitimu Vyuo bila kusailiwa. Kwa uamuzi huu, natumaini Wizara itaongeza kasi ya kuiba mapengo ya upungufu wa Walimu katika Shule za Sekondari zinazojengwa na wananchi. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Ileje, tuna Shule za Sekondari kumi, tano za zamani na tano mpya zilojengwa na kufunguliwa mwaka huu 2006, lakini kuna upungufu mkubwa wa Walimu. Barua yetu Kumb. Na. 1/3/114/VOLII/6 ya tarehe 17 Mei, 2006, inaonyesha upungufu wa Walimu 98 kulingana na masomo. Naomba Wizara itufikirie kipekee wananchi wa Ileje kutokana na mazingira ya Wilaya yetu, pamoja na mafanikio mazuri ya matokeo ya mitihani ya Darasa la Saba kwa miaka ya hivi karibuni.

Tusaidiwe ili tuendelee kufanya vizuri zaidi katika Elimu ya Sekondari kwa kupewa Walimu wa kutosha na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada ya kupunguza upungufu uliopo wa Walimu katika Shule mpya ya Sekondari, tunatafuta na kushawishi Walimu kuja Ileje. Kwa mantiki hiyo, naiomba Wizara itoe kibali kwa Mwalimu Emecka M. Bernard (E/PF16770) aliyepo Shule ya Sekondari Ipande (Kyela), ahamie Shule mpya ya Sekondari Mbebe (Ileje). Katika Shule zote Wilayani, wananchi wanajitahidi kujenga nyumba za Walimu na kuborehsa mazingira ili Walimu wafanye kazi kwa usalama na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wamekwishahamasika kujenga Shule za Msingi na Shule za Sekondari katika maeneo yao, tunaomba Wizara iendelee kutekeleza wajibu wake chini ya *MMEM* na *MMES*, kwa wakati na kwa ukamilifu. Serikali ikitekeleza na kutimiza wajibu wake, wananchi wataendelea kuhamasika zaidi na kushiriki kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuchangia kwenye maeneo machache sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Waziri kuhusu madeni/ madai ya Walimu, bado ningependa kupata ufafanuzi kuhusu madai ya Walimu wa Wilaya ya Mbozi. Walimu hao wanadai jumla ya Shilingi milioni 154. Hata hivyo, hivi karibuni Halmashauri ya Wilaya ilipunguza deni hilo kwa kulipa Shilingi milioni nane, baki ni Shilingi milioni 146. Naomba maelezo yatakayowaridhisha Walimu wa Wilaya ya Mbozi ambao pia ni wapiga kura wangu. Ni lini watalipwa pesa zao hasa ukizingatia kwamba madai hayo ni ya tangu mwaka 2004?

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashuari ya Wilaya ya Mbozi ina jumla ya Shule za Msingi 207, mahitaji halisi ya Walimu ni 3,730, lakini waliopo ni 2,225, pungufu ni Walimu 1,505. Hali hii hairidhishi hata kidogo na kwa kweli kuna Shule nyingine zina Walimu kati ya mmoja hadi watatu, katika hali hii tunategemea miujiza gani? Pamoja na mipango mizuri ya Serikali kutatua tatizo la Walimu, naomba Waziri atueleze/awaeleze wazazi wa watoto wanaosoma Shule ni lini tatizo hili kubwa la upungufu wa Walimu litatatuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubora wa majengo yaliyojengwa chini ya mpango wa *MMEM* na *MMES*, bado majengo mengi yamejengwa chini ya kiwango. Ushauri wangu, naomba Serikali kupitia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iweke viwango vya majengo vitakavyofuatwa kabla ya Shule kufunguliwa. Wakati huo huo usimamizi uimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwa dhati ya moyo wangu kabisa kwamba naipongeza Wizara kwa kuliona hili, kwani katika ngazi ya Wilaya kulikuwa hakuna *Coordiantion* kabisa ya Shule za Sekondari. Naishaukuru sana Wizara. Ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 9 Machi, 2006 Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza - Naibu Waziri wa Wizara yetu hii alitembelea Jimboni kwangu. Alipokelewa vizuri sana na kupewa taarifa nzuri sana za kila aina kutoka kwa wadau mbalimbail wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nililazimika kutofautiana nao kwa sababu hawakueleza ukweli wa mambo kuhusu Ruangwa. Mimi nilimweleza mbele ya Kikao hicho, maana ya Ruangwa kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kitaaluma Ruangwa ilikuwa ya sita katika Halmashauri sita za Mkoa wa Lindi. Maana yake ni ya mwisho.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika matokeo ya mtihani wa Shule za Msingi mwaka 2005, Ruangwa ilikuwa ya 114 kati ya Wilaya ya 118 za Tanzania. Manaa yake ni *very poor and extremely poor performance*.

(c) Katika matokeo ya kimkoa, Shule ya mwisho kimatokeo ilikuwa Najaru, ambayo imetoka Ruangwa. Je, hii inaridhisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya inazo taarifa kuwa Ruangwa ni kinara wa vifo vya watoto wa akina mama kwani watoto 250 hufa kabla hawajafika mwaka kati ya watoto 1000 wanaozaliwa. Pia akina mama karibu 200 nao hufa. Tishio hili la vifo linalo jina maalum katika kabila la wenyeji wa eneo hili ambao ni Wamwera, wanaitwa kuwa ni *Kuutanda*. Maana yake ni kufa wakati anajifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani kwa maelezo mengi sana haya. Lakini nilikuwa na maana ya kuwaeleza kuwa *education level* ya wananchi wetu kule chini kabisa. Wilaya nzima ina Sekondari za kusuasua mbili tu, nazo ni Nkowe na Mbekenyera. Mandawa na Mbekenyera Ruangwa zipo mbioni kuanza taratibu hizo za kusuasua.

Mimi naomba tufikiriwe sana ili tuzinduke. Leo ninachoomba ni kimoja tu. Nipatiwe kiongozi yeyote yule toka Wizarani ili twende naye kule tukawasikilize Waalim, wadau wa elimu, wanafunzi na wazazi tupate chanzo chake na tuandae mwelekeo mpya kwa spidi muafaka. Naomba hilo tu. Simu yangu ni 0784495213.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuunga mkono hoja. Nakiri kuwa Wizara inafanya vizuri. Pamoja na utendaji wake mzuri, naomba Wizara inapopeleka pesa za *MMES,* zifuate utaratibu wa *MMEM.* Bado Wakuu wa Shule *(Heat Masters)* hawakubali kushirikisha Kamati za Shule za Ujenzi, matokeo pesa zinapotea.

Naomba majibu kwa Shule ambazo zimesababisha upotevu wa pesa za *MMES*. Walimu Wakuu hao wamechukuliwa hatua gani?

Nasikitika kusema Viongozi wa Shule hizo bado ni Wakuu na wanadhihaki wananchi kuwa watawafanya nini? Wakuu hao ni Mkuu wa Shule ya Sekondari – Bukori na Mkuu wa Shule ya Sekondari Butundwe. Hatuelewi kwa nini Wizara haitupi ushirikiano katika tatizo hili. Wabunge wote watatu tumekwenda pale tukakuta kuna ubadhirifu na nimeieleza Ofisi ya Wizara. Naomba nielezwe kuna nini?

Naunga mkono hoja, lakini naomba nielezwe kwa nini Walimu Wakuu walioharibu kama hao bado Wizara inawakumbatia?

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa matumaini kwa maendeleo ya elimu nchini. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kuwa maendeleo endelevu ya elimu yanahitaji kuwepo kwa Walimu wa kutosha katika Shule zote. Hili suala ni muhimu hasa leo ambapo wananchi wanajitolea kujenga Shule za Msingi na Sekodnari kwa wingi. Matagemeo yao ni kuwa, Serikali itashughulikia suala la upatikanaji wa Walimu.

Wananchi wa Kyela wamepata mwamko mpya katika kujenga Shule. Katika kipindi hiki kifupi tu cha nusu ya mwaka huu, Shule nne mpya za Sekondari zimejengwa kwa nguvu za wananchi, Nkuyu, Mwaya Masukila na Kajunjumele. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi waishio Kata za Ngana Mwaya, Kajunjumele na Kyela kwa kufanikisha ujenzi wa Shule hizo.

Tatizo linalotukabili ni la upungufu la Walimu. Hadi sasa Shule hizo mpya hazina Walimu kabisa na hali hiyo tayari imeleta hali ya kuwakatisha tamaa wananchi wasijitolee kujenga Shule zaidi. Naiomba Wizara iipe Wizara ya Kyela kipaumbele kwani hata Shule chache za zamani zilizopo zinakabiliwa na tatizo hilo hilo.

Aidha, nimetiwa moyo sana na mipango ya Serikali na kuendeleza elimu ya ufundi nchini. Naiomba Wizara itakapoanza kutekeleza mkakati wa uanzishaji wa Vyuo vya Ufundi Stadi kila Wilaya, nguvu ya mwanzo ielekezwe kwenye Wilaya zenye vijana wengi wanaoishia Darasa la Saba na ambao hazina Vyuo vyovyote wala viwanda vya kuwameza vijana hao. Kyela iko katika hali mbaya sana. Zaidi ya asilimia 80 ya vijana wanaomaliza Darasa la Saba wamekuwa wanashindwa kwenda Sekondari kutokana na uhaba wa Sekondari Wilayani kwa miaka mingi huko nyuma.

Pili, Kyela haina viwanda wala vyuo vya kuendeleza vijana wa aina hiyo. Matokeo ni jeshi kubwa la vijana wenye nguvu wanaozagaa Wilaya nzima. Naiomba Wizara itupe kipaumbele katika ujenzi wa Vyuo vya ufundi stadi. Naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii niliyoipata ya kuchangia hotuba ya Bajeti hii. Pia, napenda kumpongeza Waziri pamoja na Manaibu wake wote wawili na watalaam wake wote kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, urithi pekee kwa watoto wetu kwa sasa ni elimu peke yake. Hivyo, tuna kila sababu ya kuelekeza nguvu zetu katika suala hili la elimu kwa watoto wetu. Napenda kutoa pongezi kwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuhamasisha Viongozi pamoja na wananchi katika ujenzi wa madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madarasa yamejengwa, ila madarasa bila kuwa na Maabara na vitabu kwa ajili ya wanafunzi, hayo madarasa hayataweza kutusaidia kuwa na elimu bora ambayo tunaihitaji sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ujenzi wa madarasa, kuna tatizo kubwa sana la nyumba za Walimu hasa huko Vijijini ambako wananchi wana hali mbaya ya

kipato na hawana uwezo wa kuchangia kujenga nyumba hizo za Walimu, hivyo, kufanya maeneo hayo kukosa nyumba na Walimu wanaokwenda huko kufundisha.

Tunaiomba Serikai itazame maeneo hayo ili iweze kusaidia upatikanaji wa nyumba hizo za Walimu ili watoto wetu waweze kupata elimu bora. Naamini nyumba hizo zikipatikana, Walimu watakwenda kufundisha huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana kwa Walimu wetu, hasa inapofika mwisho wa mwezi wa kupata haki yao, yaani mishahara. Kwa kweli inasikitisha ukiwaona Walimu hao wanavyohangaika kupata hiyo mishahara huwalazimu Walimu hao kusafiri kutoka huko walikokwenda Wilayani kufuata mishahara yao. Kibaya zaidi, wakifika huko, wanaambiwa mishahara haijafika na wakati mwingine huwalazimu kukaa zaidi ya siku mbili mpaka tatu kusubiri mishahara yao. Wakiwa huko gharama zote ni juu yao kwa malazi na usafiri. Katika hili, ningependa gharama hizo zilipwe na Wizara kwa sababu sio kosa la Walimu wetu na tukumbuke Walimu wanapokuwa huko, watoto wetu wanapoteza vipindi vyao vya masomo. Pia, tungeomba Wizara itafute utaratibu mwingine ambao utawawezesha Walimu wetu kupata mishahara yao bila usumbufu ambao wanaupata sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuipongeza hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa dhati kabisa na moja kwa moja nakwenda katika kuchangia hoja kwa maandishi kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba, bila elimu hakuna maisha bora na yenye mwelekeo kwa wananchi wa nchi yoyote ile. Kwa maana hiyo, Wizara ya Elimu ni mhimili muhimu katika nchi yoyote ile duniani. Iwe ni nchi iliyoendelea au nchi inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa nchi yetu imekuwa ni moja ya nchi zinazoendelea ambazo zinaifanya kila liwezekanalo kupandisha kiwango cha elimu na hasa nikichukulia hapa nchini kwetu jinsi Wizara ya Elimu inavyojitahidi kwa wakati huu wa Awamu ya Nne ya hali mpya kasi mpya na nguvu mpya lakini utakuta kuna baadhi ya Watendaji wanatumia vyeo vyao kukwamisha ukuaji wa elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo la kusikitisha. Mimi kama Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Gairo, ambaye niko katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, nasikitika sana na hata kufikia kukosa imani na Wizara hii kutokana na Watendaji wake walioko Wilayani Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara na Serikali kwa ujumla kujua kuwa kuna upungufu mkubwa wa walimu na fedha, lakini Serikali imejitahidi kutuletea Walimu 51 katika Wilaya ya Kilosa.

Kama Mbunge niliwasiliana na Afisa Elimu wa Wilaya ya Kilosa na kumwuliza kuhusu mgao wa Walimu, alichonijibu ni kuwa atahakikisha katika Majimbo matatu ya

Wilaya ya Kilosa atawapangia Walimu hao wageni kwa usawa na aliniahidi kuwa Gairo imepata Walimu 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza nilipta malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu upungufu wa Walimu katika Shule karibia zote katika Jimbo langu. Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro amefanya ziara katika Jimbo la Gairo na kuona hali mbaya ya kutisha ya upungufu wa Walimu Jimboni Gairo. Nikaamua kumwandikia barua Afisa Elimu wa Wilaya kuulizia ule mgao alioniahidi kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Afisa Elimu kuonekana haelewi hata mgao ulivyokwenda, kwa shida akanipatia takwimu sahihi aliyonayo yeye inayoonyesha Jimbo la Gairo katika Walimu 51 tuliopewa na Wilaya Gairo imepata tisa tu. Hili ni jambo ambalo ni la kusikitisha, sio kushangaza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kilosa, Jimbo lenye Shule nyingi za Msingi ni Gairo, leo iweje kila wakati ipate mgao mdogo wa Walimu kuliko Majimbo yenye Shule chache kwa mfano Shule ya Dumila yenye wanafunzi 524 tu, ina Walimu zaidi ya 28 katika Jimbo la Kati; Shule ya Chanjale Gairo wanafunzi 750, Walimu wawili tu na Shule ya Chakwale ambayo ipo katika Kata ya Chakwale na ipo karibu kabisa na barabara ina wanafunzi 1800 Walimu 11 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni baadhi ya mifano michache mno katika Jimbo la Gairo na kuwa minong’ono isiyo na uhakika kuwa hupangiwa Walimu katika Shule yako mpaka utoe chochote ambayo inawakuta Walimu Wakuu wa Shule. Je, Wizara haioni kwa hali hii hata kama sio kweli, lakini inafanya watu sasa tupate mashaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, sitapenda kulumbana na Wizara, lakini Wizara isiachie Halmashauri lawana kwamba zitakuwa Wilayani, hivyo Wizara itakuwa imejidanganya. Wizara yenye Waziri na Manaibu wawili ni wajibu wake ifuatilie suala hili kwa umakini sio kutupia Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka majibu ya kina kuhusu suala hili kabla sijalitolea tamko. Nategemea nitapata majibu ya kutosha litakalowasaidia wananchi wa Taifa hili na hasa wanaopata taabu ya kukosa elimu ambayo ni haki yao ya msingi. Wenu katika ujenzi wa Taifa.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kumteua Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Manaibu Waziri wake Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila ambao ni wakereketwa wakubwa wa maendeleo ya Sekta ya Elimu, nampongeza sana na wasaidizi wake kwa mwanzo mzuri katika Wizara hii. Katika kipindi hiki cha miezi sita, pamoja na mambo mengine, wameweza kusaidia Serikali kuanza kutatua migogoro ya maslahi ya Walimu na kurejesha mpango wa Shule za Mchepuo wa Ufundi na Biashara. Nawapa hongera sana.

Lakini bado kuna changamoto kubwa mbeye yao. Tatizo la upungufu wa Walimu hakuna budi litatuliwe kama ilivyoonyeshwa kwenye viambatanisho *"A"* na *"C"* vya hotuba ya Wizara katika kipindi cha mwaka 2002 hadi 2005 idadi ya Shule zote imeongezeka sana. Vile vile, idadi ya wanafunzi imeongezeka. Lakini ongezeko la Walimu haliendi sambamba na ongezeko la wanafunzi wale na ongezeko la Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lipo tatizo la upungufu wa vitendea kazi katika Shule za Msingi na Sekondari. Vitabu havitoshi na kwa baadhi ya Shule hata madawati hayatoshi. Ingawa Walimu ni wachache, lakini hakuna nyumba za Walimu za kutosha, Walimu wengi hawana mahali pa kuishi, hivyo, hata utendaji wao wa kazi mzuri na matokeo yake wanafunzi hawafaulu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kutambua umuhimu wa ukaguzi wa Taasisi zote za Elimu kwani Walimu wasiokaguliwa hasa kule Vijijini kwa kusongwa na mazingira mabovu, hawakai madarasani. Baadhi yao wanapoteza muda wao kwenye ulevi wa pombe za kienyeji ambazo zinapunguza uwezo wao wa kutenda kazi.

Lakini bado najiuliza, iwapo kwa mujibu wa kiambatanisho *"C"* mwaka 2005/2006 wizara ilipanga kutekeleza kaguzi 805 za Shule za Sekondari, wakatekeleza asilimia 98 za lengo. Vile vile, walilenga kaguzi 7,018 za Shule za Msingi, wakaishia na kaguzi 5,018 sawa na asilimia 72. Sio vibaya, lakini mwaka huu wamelenga kutekeleza kaguzi 7,164 za Shule za Msingi na kaguzi 1,032 katika Shule za Sekondari wakati ajira ya Walimu mwaka 2005/2006 ilikuwa chini ya 3,000. Watawezaje kutimiza azma hii bila kuathiri utoaji wa elimu yenyewe mashuleni?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inayo changamoto nzito ya kuhakikisha kuwa maeneo yaliyo nyuma sana kielimu, yanapewa kipaumbele. Hapa nawapatia hali halisi katika Jimbo langu la Kisarawe. Wilaya yenye ukubwa wa kilometa za mraba 3,500 Vijiji vilivyosajiliwa 76 na vinavyosubiri kusajiliwa nane, Kata 15, lakini zina Shule za Msingi 75 tu na Sekondari za Serikali/wananchi saba tu. Nafahamu kuwa zipoWilaya zenye Shule za Msingi ziadi ya moja katika kila Kijiji na Sekondari zaidi ya moja katika kila Kata. Sasa usawa uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya Walimu inasikitisha. Tunahitaji Walimu wasiopungua 800. Lakini waliopo ni chini ya 600. Kwa hiyo, kuna upungufu wa Walimu zaidi ya 200 ili kuwezesha hizo Shule chache zilizopo zitoe elimu inayostahili.

Hali ya nyumba za Walimu katika Jimbo la Kisarawe inatisha. Zinahitajika nyumba 832 lakini zilizopo ni 202 tu tena mbovu wala hazifai kwa maisha ya Walimu. Hali hii, kama nilivyosema kwa Taifa, inawafanya Walimu wasiwe watulivu, wanashindwa kufundisha vizuri. Wengi wao hulazimika kutafuta sababu za kuhamishwa wapelekwe kwenye Wilaya zenye mazingira mazuri, wanapokataliwa kuthubutu hata kuacha kazi. Matokeo yake, Jimboni kwangu pamoja na uchache wa Shule, zipo Shule kadhaa ambazo zina Walimu wasiozidi watatu. Baadhi ya Shule zina Walimu wawili tena ni mume na mkewe. Hali hii inatisha. Naomba irekebishwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuona ni kuamini. Ili Mheshimiwa Waziri aweze kupata picha halisi ya elimu katika Wilaya ya Kisarawe, nashauri aje Kisarawe nimtembeze Wilayani athibitishe ninayoyaeleza. Ingefaa pia Manaibu wake nao wafike ili kwa kuwa hataweza kufika kila mahali, nao wamsaidie kuona maeneo mengine.

Naunga mkono hoja hii kwa kutegemea kuwa kilio changu kitasikilizwa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri yenye ufafanuzi mzuri. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpango wa *MMEM* umefanikiwa vizuri sana kwa kujenga madarasa huko Vijijini na hivi sasa wanafunzi wanasomea katika mazingira mazuri ya kuwa na vyumba vya madarasa ya kutosha, tatizo kubwa hivi sasa ni nyumba za Walimu na madawati. Walimu wanaishi katika mazingira magumu sana huko Vijijini. Serikali iweke mikakati/mipango ya kujenga nyumba za Walimu kwa kutenga fedha za kutosha pamoja kutengeneza madawati ya kutosha ili wanafunzi wasikae chini.

Mishahara ya Walimu kuchelewa na pia Walimu kupoteza muda mwingie kufuata mshahara Makao Makuu ya Wilaya, hii inaathiri kwa kiwango kikubwa taaluma katika Shule za Msingi kwa vile wanaacha kufundisha na kufuata mishahara na wengine hutumia wiki moja kufuata mishahara kutokana na umbali na matatizo ya usafiri. Walimu walipwe posho ya mazingira magumu, madai yao ya uhamisho, matibabu, Walimu wkopeshwe vyombo vya usafiri kama pikipiki baiskeli na kadhalika ili kurahisisha hali ya usafiri huko Vijijini. Shule ya Msingi ya Pwaga Wilayani Mpwapwa imeshika nafasi ya kwanza kitaifa katika matokeo ya mtihani wa Darasa la Saba 2005. Je, Serikali imejiandaa vipi kuipongeza Shule hiyo wakiwemo Walimu wa Shule hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Mpwapwa *(Mpwapwa High School)* imefanya vizuri sana katika mtihani wa Kidato cha VI – 2005 na kushika nafasi ya pili kitaifa: Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ya Shule hiyo kwa kukarabati majengo ya Shule hiyo, kuboresha vifaa vya kufundishia zikiwemo *computers, internet,* kuboresha vifaa vya kufundishia wanafunzi wasioona *(Blind Students),* kujenga uzio wa Shule hiyo kwa ajili ya ulinzi na usalama wa Shule. Tunaomba usafiri wa gari kubwa. Wilaya ya Mpwapwa tumejenga Shule za Sekondari na kila Kata. Hivi sasa kuna Shule 19, tatizo ni Walimu na majengo ya Maabara kivitendo. Bwalo la Shule lifanyiwe ukarabati mkubwa.

Mwaka 2005 Serikali iliajiri Walimu wa Shule za Sekondari. Kuna baadhi ya Walimu hawajalipwa mishahara yao hadi sasa. Ni lini Serikali itawalipa mishahara na malimbikizo ya mishahara yao? Walimu wapewe mikopo ya vyombo vya usafiri. Shule nyingi za Sekondari hakuna nyumba za Walimu katika mpango wa *MMES,* Serikali itenge fedha za kutosha kujenga nyumba za Walimu. Shule za Sekondari zitengewe fedha za kutosha na kuboresha huduma katika Shule za Bweni hasa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufanyike ukarabati wa Shule za Sekondari Mpwapwa, Kilakala na Dodoma na kujenga uzio kwa ajili ya ulinzi na usalama wa Shule hizo. Naomba haya yafanyike katika Bajeti hii ya 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ualimu cha Mpwapwa kina historia ndefu na nzuri. Chuo hiki kilianzishwa mwaka 1926. Wapo watu maarufu waliosoma Chuo hiki cha Ualimu. Lakini Chuo hiki kinakabiliwa na matatizo yafuatayo: Majengo mengi ni ya zamani, yanatakiwa ukarabati mkubwa na hasa mabweni, *Assembly Hall*, madarasa, Bwalo la Chakula, usafiri wa uhakika wa gari kubwa jipya unatakiwa kuboresha vifaa vya kufundishwa na vya kisasa kama vile *computers, internet* na kadhalika?

Pia, nashauri Chuo cha Ualimu cha Mpwapwa kipanuliwe pamoja na kufundisha Walimu wa *Diploma,* pia kinaweza kufundisha Walimu wa shahada na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Serikali iwe na mipango ya baadaye ya kukifanya Chuo hicho kiwe Chuo Kikuu kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lipo eneo kubwa la kuongeza majengo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa haotuba yake yenye dira ya maendeoleo ya elimu. Kwa kuwa elimu ndio ufunguo wa maisha, Serikali iangalie upya elimu sasa kwa lugha ya Kiingereza ianzie Darasa la Kwanza ili kujenga Msingi mzuri kwa watoto wanaoingia Sekondari. Kuwepo kwa *Academy Schools,* kumeifanya elimu iwe na tabaka mbili za mtaala wa elimu na wengine wapate elimu bora na wangine wanapofikia Darasa la Nne ndio wanaanza somo la Kiingereza. Hii ni kurudisha nyuma elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie uboreshaji zaidi wa elimu kwa walemavu. Kuna watoto walemavu ambao wana uwezo wa kusoma, lakini wazee wao hawana uwezo wa kuwafikisha Shuleni ili wapate elimu kutokana na ulemavu wao. Aidha, Serikali iongeze Shule za bweni au iwawekee usafiri maalum ili kupata elimu na waandaliwe mazingira kutokuwa na ulemavu wao mfano madarasani na vyooni.

Suala la kuwepo kwa taarifa ya Shule moja ambayo ina watoto 300 kusimamiwa na Mwalimu mmoja au watatu, hii inaonyesha wazi jinsi gani watoto wanavyokosa haki haki yao ya kielimu. Nashauri Walimu waongezwe ili kukidhi hoja ya mashule.

Somo la Elimu ya Uraia, sasa ndio wakati muafaka kwa kutoa elimu hii katika mashule yetu kuanzia msingi. Suala la kujenga Maabara katika Shule zetu ni muhimu kwa kuwa madarasa mengi yamejengwa. Naipongeza Serikali kwa hilo, sambamba na nyumba za Walimu. Sasa Serikali iangalie kwa karibu kuweka vitendea kazi na mishahara Walimu wapate kwa wakati. Vile vile, iangaliwe ni kwa nini Walimu hawaripoti katika maeneo waliopangiwa ili lipatiwe ufumbuzi kuwashawishi Walimu wapende kazi zao.

Suala la usafiri wa wanafunzi wa Jiji la Dar es Salaam, Serikali iangalie upya kurudisha tena mabasi ya wanafunzi ili kuondoa unyanyasaji unaofanyika na baadhi ya mabasi ya daladala kwa wanafunzi. Pia, Serikali iwashauri wazazi ambao, mfano mtoto wa Darasa la Kwanza anatoka Ubungo kuja kusoma Upanda au tokea Gongolamboto kuja kusoma Muhimbili wawaandikishe katika maeneo yao wanayoishi ili kupunguza usumbufu kwa watoto. Naomba kuwasilisha.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri na Manaibu wake kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya katika Wizara hii. Jitihada naona ni nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vibali vinavyotolewa utumishi na Halmashauri kupata Mwalimu ambaye alipata kibali hicho, nashauri kwamba kilio na mwenywee. Suala hili ni kukaa na Wizara husika, maana elimu ndiyo inashuka sana kuona ucheleweshaji wa Walimu na maendeleo ya Vijana wetu yanarudi nyuma kielimu. Hili ni la kuongelea katika Baraza la Mawaziri na kutafuta njia ya kulitatua haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *VETA* inafanya kazi vizuri na ina maana ya kuwasaidia vijana wengi, tatizo *VETA* ina na magari machache ya kuwasaidia vijana kujifunza udereva, haipa pesa na kukaa hata miezi miwili hawajaanza. Hiyo ni nini? Tunaomba Idara hii sasa iboreshwe hasa *VETA* Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa juhudi nyingi na busara na pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwani mwanamke ni mkombozi wa Watanzania. Elimu ni maendeleo.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Margareth Sitta na Manaibu wote wawili, sisi wanawake wa Mkoa wa Mwanza tumefarijika sana kumpa mama ambaye anasimamia dira ya maendeleo ya watoto wetu. Tunamuahidi tutakuwa wote pamoja katika malezi bora ya watoto kuanzia Shule za Awali hadi Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sitta alikuwa mstari wa mbele kabla ya ya kuwa Waziri kwa kuwatetea Walimu ambao ndio tegemeo kubwa juu ya malezi ya watoto wetu wakiwa Shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri kwa kukusudia kupunguza kabisa madai ya marupurupu ya Walimu na wengi wamelipwa, mambo sasa ni shwari kabisa. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua kuwa Waziri kushika Wizara hii, anaimudu kwa asilimia mia moja. Naomba madeni yaliyobaki yalipwe kama ilivyo katika ukurasa wa 76 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti sana, tunamwombea afya njema ili adui ujinga atokomee kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2006/2007 ni mazuri hasa ukurasa wa 20 (g) naomba nitoe ushauri wangu. Wanafunzi 45,873 watalipiwa na Serikali, naomba twende Vijijini, kuna watoto wa kike kule wanafichwa na wazazi ili waolewe tu. Huyu Afisa wa Elimu wa Wilaya awe makini kupita katika Shule za Msingi zote za Wilaya, ajue watoto waliofaulu na hali ya wazazi ni duni, ili wasome.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba MheshimiwaWaziri amsaidie kulipa deni la umeme la Shule ya Sekondari ya *Bwiru Girls* ya Mwanza. Ni tatizo zito ambalo limesababisha mashine ya maji kutofanya kazi, hivyo wanakunywa maji yasiyo salama. Ni Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bwiru na Sekondari ya Wavulana ambazo ziko karibu zote zinatumia mashine moja. Kwa kuwa Shule mbili za Sekondari zina wanafunzi wengi sana wanahitaji maji salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili Waziri alifanyie ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii sina pingamizi nayo kabisa, *MMEM* tumefanikiwa sana, ninatarajia sasa *MMES* tutafanikiwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri atusaidie watoto wa kike, wanapewa mimba kwa bahati mbaya ili sababu zijulikane, basi tuombe wakishajifungua warudi waendelee na Shule, ila ithibitishe ni bahati mbaya tu, wala sio wahuni na wanazaa ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini uboreshaji wa ujenzi wa Hosteli za Wasichana itapunguza kabisa hali hiyo. Naomba Wizara isisitize Shule zote za Sekondari ziwe na Hosteli za wasichana ili mtoto wa kike apate elimu anayostahili, itapunguza vishawishi vinavyowapa watoto wa kike wananchi washirikishwe katika kuchangia ujenzi wa Hosteli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia, apewe fedha zote.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa zinazoendelea kufanyika za mapinduzi ya elimu (imeboreshwa sana). Ttatizo la Maabara ni kubwa kwa kuwa Shule nyingi hazijifunzi kwa vitendo na kiasi cha Maabara zinazojengwa haziwiani na Shule hizo. Naiomba Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa Maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye utaratibu wa kupima viwanja vya Shule visimamiwe na wakazi, vinginevyo italeta vurugu kwa wananchi kuja kuondolewa baadaye. Ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri na Wizara yake ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi siyo tu kwa hotuba yake ya Bajeti, lakini kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. *I have nothing but admiration; it is probably the best presentation so far. Please keep it up!*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba nami nisisitize tatizo la upungufu wa Walimu, suala ambalo limetajwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengine. Jimboni Kalenga tatizo hilo liko namna mbili.

Kwanza katika Sekondari. Nina Sekondari kumi zinazoendelea na 3-5 zimo katika hatua mbalimbali za ujenzi na zote hazina Walimu wa kutosha. Najua hatua zinazochukuliwa. Niomb tu kwamba Mheshimiwa Wziri asisahau Jimbo la Kalenga katika migao mbalimbali itakayofuata.

Pili, kuhusu Shule za Msingi, upufungufu wa Walimu kwa kiwango fulani ni *artificial* kwa maana ya kwamba Walimu wengi hutumia uwongo na njama mbalimbali ili wabaki Mijini au karibu na barabara kuu badala ya Vijijini. *Concentration* ya Walimu Mijini/barabarani inasababisha Shule hizo kuwa na Walimu wengi zaidi kuliko mahitaji na kuvikosesha Vijiji Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri suala hili litazamwe kwa lengo la kurekebisha. Shule za Sekondari za Serikali Jimboni kwangu Idunda, Kalenga na Isimila, zina matatizo makubwa la *liquidity* na wamelibikiza madeni makubwa ya chakula kwa wanafunzi. Naomba suala hilo lichunguzwe na kurekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri na ninamwahidi ushirikiano wangu katika Jimbo langu.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, haipendezi hata kidogo Mwalimu ambaye ameshalitumikia Taifa kwa miaka mingi na akafika wakati wa kustaafu au akafariki yeye mwenyewe au warithi wake wakahangaishwa katika kupata haki zao za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo inavunja moyo na inashusha hadhi ya kada hii muhimu ya utumishi. Mfano hai ni wa Mwalimu huyu ambaye ni Marehemu. Anaitwa Shah B. Shah, *TSC No. 511702, EDPF 22156, CN NO 8702883,* Shule ya Sekondari Usagara - Tanga, alifariki mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika,mpaka ninavyochangia hotuba hii bado warithi wa Marehemu huyu hawajapata malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri atakapojumuisha hotuba yake anipatie jawabu kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni ulimwengu wa saynasi na teknolojia, kwa hiyo, elimu yetu iendane na mwenendo huo. Leo nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la

wahitimu wetu katika masomo ya sayansi kwa mfano Hisabati, Elimu ya Viumbe *(Biology),* Elimu ya Kemia *(Chemistry)* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchache wa wahitimu wa sayansi unatokana na ukosefu wa Maabara na vifaa vya Maabara. Elimu ya Sayansi inasomeshwa zaidi kwa nadharia kuliko vitendo. Hivyo ipo haja Wizara kuwa na sayansi kwa kujenga Maabara na kuwa na vifaa vinavyostahili kwenye Maabara hizo. Vinginevyo, vizazi vyetu vitakuja kukuta havina elimu ipasayo kwa maisha yetu ya leo na baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo cha kutegemea katika elimu ni mitihani. Kuvuja mitihani mitaani ya Kitado cha Nne inatia aibu na wasiwasi mkubwa. Kwa mtindo huo unaweza ukapata wahitimu wenye viwango vya juu kumbe vimepatikana kwa njia ambayo sio sahihi. Ipo haja ya Wizara kunieleza tatizo hili litadhibitiwa vipi na je, wako ambao wamekamatwa na suala hilo? Kama wapo, wamechukuliwa hatua gani? Ahsante.

**MHE. FATMA ABDALLA TAMIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuandika hoja yangu hii. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri pamoja na Watendaji wao wote kwa uwasilishaji wao mzuri wa hotuba hii.

Nikianza mchango wangu, nawapongeza Walimu kwa kazi waliyonayo, kwani Ualimu ni kazi ngumu, ni kazi isiyo na malipo, malipo ni kwa Mwenyezi Mungu, atawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu ni kioo cha jamii katika maisha yetu, wanahitaji kuangaliwa na kutunzwa kwa stahili zote. Naomba Walimu watakaoingia Chuoni kwanza na wao wapewe Elimu ya Dini zao ili wapatikane Walimu watulivu, wawe ni kigezo kwa watu wengine ili watakapoanza kusomesha wawe Walimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, atakapopatikana Mwalimu huyo niliyemtaja, ninaamini watapatikana wanafunzi wazuri wenye nidhamu na wasiofanya mambo machafu kutokana na Mwalimu huyu aliyetayarishwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kazi nzito, ni Ualimu na daktari. Mwalimu huyu anahitaji kutunzwa kimaisha ili apate kutulia, afundishe vyema kazi zao ili wasipate usumbufu, wafundishe vyema na watoto wamsikie. Lakini atakapokosa huduma hizo wanafunzi hawatamsikia na pia hawatamfahamu na mazingira aliyokuwanayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ijitahidi kuchukua Walimu na Mikoa yao wanayotoka ili kupunguza tatizo la Walimu kutafuta uhamisho na kukimbia sehemu zao walizotoka.

Kuhusu tatizo la Ukimwi na madawa ya kulevya walimu washirikiane na wazee katik malezi ya watoto, kwani Mwalimu peke yake hawezi kuyatatua matatizo ya

wanafunzi. Bila ushirikiano na mzazi, Mwalimu atamjua mwanafunzi tabia zake pindi Mzee atakapojenga tabia ya kupita mara kwa mara Shuleni, naamini atajua matatizo ya mwanafunzi na pindi ameanza kuharibika ni rahisi tu kumwelewa mwanafunzi huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ukimwi, naomba somo hili liwe maalum mashuleni na somo hili naomba lisisitizwe na Walimu watakaofundisha wawe Walimu wanaokubalika katika jamii ili wawe mfano na kigezo kwa wanafunzi. *Condoms* ziondolewe, kwani zinakithiriri. Wanaona *condom* zipo za kuzuia, kwa hiyo hawashtuki hata wakiambiwa Ukimwi unaua, lakini pindi hizi *condom* zitakapoondolewa na somo litasomeshwa na kusisitizwa na filamu zikawazinaoneshwa mtu anavyougua, naamini watakapoona hali hiyo ya kutisha watapata hofu na woga na kuogopa kukfanya tendo hilo kwa uwezo wa Mwenyenzi Mungu naamini Ukimwi utapungua au kutoweka kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa juhudi zao wanazochukua, kwani kitabu hiki kila mahali unaposoma, lakini Walimu inaonyesha ni tatizo kidogo. Walimu waongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa juhudi wanazochukua kufaulu kwa wingi wanafunzi, kwa hiyo nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kazi nzito, ngumu ya Taifa hili. Kwa nini kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha za *MMES*? Mwaka 2005/2006 Wilaya ya Nzega ilipata mgao mara moja tu. Kwa kuwa Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Nzega haina Sekondari za kutosha, kwa kuwa wananchi wamejitokeza kuchangia ujenzi na madarasa, inawezekana kupewa fedha zaidi?

Kwa kuwa katika Wilaya ya Nzega kumejengwa Shule za Sekondari, lakini bado kuna matatizo. Hakuna Walimu wa kutosha, hakuna Maktaba na Maabara. Je, Serikali itaondoa lini matatizo haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 Chama kiliahidi kujenga Vyuo vya *VETA* kila Wilaya Chuo kimoja. Je, ni lini Vyuo vya Ufundi hivyo vitajengwa? Serikali imekwishaanza kuandaa mkakati wa utekelezaji wa azima hii katika mwaka huu wa fedha.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kitabu cha Bajeti kilichotengenezwa kialimu na kitaalam. Aidha, naipongeza Serikali kwa mafanikio makubwa kwa mipango ya *MMEM* na *MMES*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya kuandikisha watoto wengi kwenda Darasa la Kwanza hata kupita malengo kwa miaka yote mitano 2002 – 2006, kumeonyesha kama sera ikieleweka basi, matokeo yatapatikana na ya kuridhisha. Lakini watoto hawa wanamaliza Darasa la Saba wakiwa miaka 13/14 na umri huu ni mdogo mno kukabili hali halisi ya maisha katika dunia hii ya ushindani na utandawazi. Takwimu za Wizara ukurasa wa 85 inaonyesha kwamba mwaka 2005 kiwango cha

kushinda mtihani wa Darasa la Saba ni asilimia 61.76. Aidha, mpango wa *MMEM* na *MMES* ni endelevu (ukurasa wa 75) wa hotuba. Kuma haya yapo, sioni kwa nini Serikali isiweke wazi kabisa kwamba *Basic Education* ni mpaka Kidato cha IV.

Faida za kutamka Sera ya *Basic Education* kuwa *Secondary School* itasaidia kuhamasisha jamii kujitahidi kujenga *Secondary School* kwa kila *Primary School* na hili linawezekana. Aidha, kwa kukaa kimya, halafu jambo hili lifanywe kidharura kama lilivyofanywa mwaka huu wa 2006 kwa shinikizo la Waziri Mkuu, lina madhara makubwa sana kibajeti kwa upande wa Halamshauri na kwa viwango na ubora wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa *Secondary Schools,* juhudu mwaka huu zimefanywa vizuri katika Mikoa mingi na Shinyanga ni moja ya Mikoa iliyoamka mwaka huu kwa msukumo wa Waziri Mkuu. Ukiangalia hotuba ya Bajeti, lengo ni kujenga madarasa 1,637 mwaka 2006/2007, lakini kama tumeandikisha watoto 1,632,141, mwaka 2002 basi mwaka 2008 watoto hawa watamazlia Darasa la Saba na watahitaji vyumba vya madarasa 40,000. Kwa mpango huu wa 1,637 kwa mwaka 2006/2007 mwaka 2008 kutakuwa na *crisis* kubwa ya kuwapa watoto hawa nafasi ya Kidato cha Kwanza. Ninaishauri Serikali kwa Bajeti ya mwaka 2007/2008 itoe Shilingi bilioni 500 kwa ujenzi wa vyumba zaidi vya madarasa ya Sekondari. Tumeweza mwaka huu kupata karibu Shilingi bilioni 450 kwa ajili ya nishati. Tukiamua inawezekana. Kutegemea wazazi tu kujenga kiasi hiki cha madarasa ni kujidanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari zilizo nyingi pamoja na kuitwa ni Shule za Serikali, lakini ukweli ni kwamba Shule hizi zimejengwa na wananchi na Halmashauri *i.e. these are Community Schools* kwa mwaka huu kama Bariadi, Halmashauri imepeleka Walimu wa *Primary School* kwenye hizi Shule. Kwa misingi hii, Halmashauri ndizo ziko karibu sana na Shule hizi na kwa hiyo, utawala wa Shule hizi ni vyema ukawa katika Halmashauri na siyo *Central Government*. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kushusha madaraka ya Sekondari kwa Halmashauri (ukurasa wa 74 58(d)) jambo hili limefanywa kidharura, kwani sasa Walimu wanafika kwenye Halmashauri na Mkurugenzi hana *OC* za kuwahudumia Walimu na Shule hizi. Mpango wa kupeleka fedha *MMES* moja kwa moja kwa *Headmasters* uachwe mara moja ili kuzingatia utawala bora wa fedha na kupunguza hoja za *CAG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi maalum ya Bariadi.

- Walimu wa *Primary* katika *allocation 106* ni *64* tu ndio walifika. Tunaomba wafike.

- Shule nyingi zina wanafunzi zaidi ya 1600. Idadi hii ni kubwa mno kwa utawala na ubora wa elimu.

- Upungufu wa Walimu wa Sekondari ni mkubwa mno. Tuna Sekondari mpya 15 na zote hakuna Walimu, tumepeleka Walimu wa *Primary School.*

- Bariadi haina *high school* na kwa kuwa tumeongeza *Secondary School* ni vyema tukapata angalau Shule moja Bariadi ipandishwe mpaka Kidato cha Sita.

- Sekondari ya *Nanga Boardking* mwaka 2005 mtoto mmoja likufa kwa moto kwenye bweni kwa kuwa hakuna umeme. Tunaomba *generator* kwa Shule hii ili kuzuia watoto kutumia koroboi na kuungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba haya yazingatiwe na ninawaahidi ushirikiano wangu kwa miaka yote ili tupate elimu ambayo ni ufunguo wa maisha.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Elimu na mafunzo ya Ufundi kwa hotuba yake nzuri. Naomba kutoa mapendekezo yafuatayo katika hotuba hii. Kubadilisha muda wa masomo katika Shule za Msingi, Sekondari hadi Chuo Kikuu kutoka muundo wa 7 – 4 – 2 – 3 (msingi miaka saba, Sekondari miaka minne, "*A" Level* miaka miwili na Vyuo vya Elimu ya Juu miaka mitatu) kwenda katika muundo wa 8 – 4 – 4. Mapendekezo yanatokana na ukweli kwamba katika muundo wa saba, watoto wanamaliza Elimu ya Msingi wangali wadogo sana na hivyo kushindwa kuingia katika maisha ya kujitegemea. Ikumbukwe pia kuwa idadi ya watoto wanaobaki baada ya kutochaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza ni wengi sana. Kundi hili ndio linalojiunga na *Vocational Educaiton* ambapo kwa umri mdogo wanaomaliza, wanashindwa kuwa makini katika kupata *skills* ya kuwawezesha kuingia kwenye Sekta isiyo rasmi.

Kuhusu Shule za Mchepuo wa Ufundi, yaani *Technical Secondary School* Serikali iweke mikakati ya kufufua Shule hizi, hasa ukizingatia tamko la Waziri katika Bunge lililopita la kurudisha michepuo hii katika mitaala. Mikakati ionyeshe wazi wazi kufufua Shule zilizopo, kujenga mpya pamoja na maandalizi ya Walimu. Hotuba ya Waziri haijagusa kabisa eneo hili muhimu la ufundi ngazi ya Sekondari. Ikumbukwe kwamba, wanafunzi wa *Technical Secondary School* ndio wanaoingia katika Vyuo vya Ufundi, yaani *Technical Colleges* ambao wanakuwa mafundi wazuri sana baada ya kumaliza mafunzo haya. Wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne katika mikondo ya Ufundi ni rahisi sana kwao kuingia kwenye Sekta isiyo rasmi kwa kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala ya Vyuo vya Ufundi Stadi, yaani *VETA* ipitiwe tena kwa kuiongezea masomo ya Hisabati na Kiingereza. Kufanya hivyo kutafanya mitaala hii ivutie vijana wengi kuingia *VETA* kwani kufanya vile kutawawezesha wahusika kuwa na sifa za kuendelea na masomo ya juu pale wanapohitaji, yaani *curriculum* ziwe na *vertical progression* katika Vyuo hivi vya *VETA*. Vyuo hivi pia vinaweza kutimiza azma ya *role* ya Shule za Sekodanri za Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila Wilaya kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi uzingatie sana vipaumbele vya uchumi wa Wilaya na mataizo ya Wilaya. Hapa ningeomba Wilaya ya Makete ambayo ina matatizo makubwa ya Ukimwi, ipewe kipaumbele kwa kuwajengea Chuo cha Ufundi Stadi ambacho kitawezesha vijana kupata *skills* za kuwawezesha kujiajiri na hivyo kupunguza tatizo la ajira na maambukizi ya Ukimwi. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wa Makete watakuwa tayari kuchangia Chuo hiki wanachoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ione uwezekano wa kujenga Shule ya Kidato cha Tano na sita katika Wilaya ya Makete. Mpaka sasa Wilaya hii haina Shule hata moja ya "*A" Level,* hii itasaidia vijana wanaomaliza *"O" Level* Makete kupata nafasi kwa wingi katika Shule hii (wale waliofaulu). Kuhusu kuboresha Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo Wizara ikae na wadau wote na hasa Walimu wa ngazi zote kujadili namna ya kuboresha elimu hii katika mitaala. Walimu ni wadau namba moja wanaojua sana matatizo ya kiini cha kuporomoka kwa kiwango cha elimu nchini. Hivyo ni vyema wakashirishwa katika kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED A. ABDUL AZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia na kutoa ushauri katika maeneo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na utaratibu wa *MMEM* ambao pesa zilikuwa zinasimamiwa na Shule husika, mpango wa *MMEM* ulipata mafanikio makubwa sana. Mpango wa fedha za *MMES* kusimamiwa na Shule jirani unapunguza sana kasi ya maendeleo ya mpango huu. Nashauri Kamati za Shule husika ambazo zimeanza ujenzi wa Shule hiyo. Nashauri Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya wapatiwe fedha hizo na kuziwakilisha moja kwa moja kwenye Kamati ya Shule husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la utoro wa wanafunzi hasa wa Shule za Msingi. Tatizo ni kanuni na sheria haziwabani Walimu na Viongozi wa Kata kuwajibika ipasavyo. Nashauri zipangwe taratibu na kanuni zinazoeleweka za kuwabana kisheria viongozi wa Shule za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza suala la ujenzi wa Chuo cha *VETA* Lindi lifanyike kwa haraka. Lindi ni miongoni mwa Mikoa iliyo nyuma kielimu. Kupatikana kwa Chuo cha Ufundi kutaharakisha sana maendeleo ya elimu katika Mkoa wa Lindi. Naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongea Waziri wa Elimu kwa hoja aliyoitoa kuhusu elimu. Hongera sana. Pili, naishukuru Wizara ya Elimu kwa kutupatia watu wa Mkoa wa Lindi Walimu wapya wa Sekondari. Ninasema ahsante sana. Baada ya kusema hayo, sasa nichukue nafasi hii kuchangia hoja kwanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu yoyote inayotolewa duniani ni ukombozi wa wananchi wake, kwani elimu ni ufunguo wa maisha. Kuendeleza elimu katika nchi yoyote ni ufumbuzi wa maisha ya wananchi husika. Kwa hiyo, mbinu au mikakati yoyote inayowekwa ili kuendeleza elimu katika nchi ni jambo la maendeleo. Kwa maana hiyo, nichukue nafasi hii kupongeza Wizara kwa kuanzisha mfumo wa *MMES* na *MMEM.* Suala hili liendelee mpaka nchini, kwani linatusaidia sana kuendeleza elimu. Mpango wa *MMES* usaidie kwanza katika Mikoa ile ambayo haina Walimu wa kutosha na Shule za kutosha na Sekondari za kutosha kama Mkoa wa Lindi. Shule za Sekondari

ni chache mno.  Wilaya zijejenga Shule kwa kujitolea, kwa mfano Ruangwa wamejenga Shule 14 na zimefikia usawa wa *renter,* lakini sasa hawana uwezo wa kumalizia. Tunaomba Wizara itusaidie sana.  Vile vile, tuangalie upya mpango wa kupeleka pesa za *MMES* kwani mtindo wa sasa hautusaidii, unaleta kero na wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa Shule ni muhimu sana katika Shule zetu. Taaluma haiwi bora kama haikaguliwi.  Ukaguzi wa taaluma haiba ya Walimu maandalizi ya Shule kwa ujumla ni muhimu kukaguliwa.  Lakini Kitengo cha Ukaguzi hakina zana za kufanyia kazi/magari na mafuta. Bahati nzuri magari angalau yamepatikana lakini sasa Wakaguzi hawana mafuta ya kuendeshea magari. Kwa hiyo, wasaidiwe mafuta pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Wizara kuwa na mpango wa kuwa na Shule za *VETA,* kila Mkoa ni mzuri sana.  Mimi ninashauri Mikoa ile ambayo haina *VETA*; wajengewe wao kwanza kabla ya kujenga *VETA* za Wilaya.  Imetajwa Mikoa ambayo itajengewa *VETA* ambayo ni Singida, Arusha Manyara, Pwani, Dar es Salaam na Lindi.  Tunaomba Wizara ianze kujenga Lindi tafadhali.  Mikoa ya pembezoni ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wana matatizo na kero mbalimbali zinazowakabili.  Baadhi ya kero wenzangu wamezitaja, mimi nitaje chache tu.  Nyumba za kuishi, kupokea mishahara mbali na Kituo cha Kazi kwani Wilaya nyingine hazina Benki. Kama Wilaya ya Ruangwa; madai ya Walimu ya marupurupu wengine hawatalipwa kutokana na karatasi yao kupotezwa na Ofisi; Walimu wenye kesi kusubiri muda mrefu bila kupata hukumu zao, hivyo kusababisha Walimu kuzurura.  Kwa hiyo, tunaishauri Wizara iangalie matatizo hayo.

Baada ya kusema hayo, ninawashukuru Waziri wa Elimu na Naibu Waziri kwa kututembelea Mkoa wa Lindi.  Ahsante sana.  Naomba kuunga mkono hoja.  Ahsante sana.

**MHE. HAZARA P. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kupongeza sana jitihada za Mheshimiwa Waziri katika kupanga shughuli za Wizara yake pamoja na Waheshimiwa Manaibu Waziri wawili wa Wizara. Maoni ya Kamati husika na Maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze sana jitihada za Serikali kuendelea kukuza elimu ikiwa ni pamoja na kuanzisha Chuo cha Elimu kama Mkwawa na Mazengo na vingine.

Aidha, hii ni dalili tosha kuwa Serikali inazingatia na kuona kuwa ni kero kubwa. Ipo haja pia ya kuendelea na jitihada zifuatazo kama ninavyoshauri.  Maslahi ya Walimu yaangaliwe, *qualification* za Walimu pia zitiliwe mkazo.  Elimu ya Watu Wazima hasa Vijijini ni muhimu, wataalam wapelekwe.

Suala la Walimu Wastaafu kupewa kazi kwa Mkataba ni muhimu sana na linapaswa kupongezwa na kutekelezwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo shida kubwa sana ya ujinga miongoni mwa wananchi wetu jambo ambalo linaweza likatatuliwa kwa kupewa elimu hasa ya ufundi. Ipo haja ya Serikali kuendeleza Vyuo vya Elimu hasa maeneo ya Makete ambako kuna tatizo kubwa *HIV.* Naiomba Serikali ianzishe Chuo cha Ufundi (*VETA)* au Chuo chochote ili wananchi wapate elimu na kujikwamua na umasikini na hatimaye *HIV*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wetu ni lazima wawe wenye uwezo mkubwa ili wanafunzi nao wawe na uwezo mkubwa kwani Walimu legelege huzaa wanafunzi legelege.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu elimu imeanza kupewa umuhimu na sasa inaingia katika Sekta huria, Shule nyingi zimeanza kuwa na gharama kubwa sana za ada hasa kwa *International Schools* na matokeo yake, Walimu hawataki kufundisha Shule za Serikali, wanakimbilia Shule binafsi. Hivyo, naiomba Serikali itupie jicho gharama za Elimu katika mashule binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maoni yangu haya, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi kwa Waziri wa Elimu na Manaibu wake wote kwa hotuba nzuri ya Wizara ya Elimu. Naomba nichangie upande wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekondari za Wasichana Mkoa wa Mwanza za kitaifa (Nganza na Bwiru) zisiendelee kuchukuliwa *"O" Level* na kubakiza *"A" Level* tu bila kwanza kuandaa ni wapi watoto wa *"O" Level* watachukuliwa. Pia naomba watoto yatima wapewe elimu ya bure toka Shule ya Awali hadi Chuo Kikuu. Hii itawaondolea mawazo potofu ya kuwa nchi yao imewatelekeza na kumbe sio kosa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ukaguzi uwepo kwenye Shule hizi za Sekondari. Ukaguzi huu pamoja na kuwa wapo kwenye Kanda, lakini kuwepo na ufuatiliaji wa karibu na mara kwa mara toka Taifani (rejea ufuatiliaji uliofanyika Dar es Salaam hivi majuzi na Shule nyingi kufungwa). Hizi Sekondari ni zile za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kugawa Walimu wasambazwe mashuleni kitaaluma. Nina maana ya kuwa Walimu wenye kufundisha masomo mbalimbali (yote).

Mashindano ya Shule na Shule kitaaluma, michezo, nyimbo yafufuliwe. Hii inaleta tija kwa kuweza kujua maendeleo ya ushindani wa Shule hizi. Kwa kuwa *"O" Level* inatolewa katika Sekondari za *boarding,* basi kuwepo na mikakati maalum ya kujenga *Hostel* kwenye Shule hizi za kutoa kwa wale wanafunzi wa kike na wakiume watakaotoka mbali kama ikigundulika. Kuweko mkakati maalum wa fungu maalum kwa ajili ya ununuzi wa madawati mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu katika Shule za Sekondari Mkoa wa Mwanza hawatoshi kabisa. Tunaomba Walimu na hasa Shule zilizoko katika Kata za Vijijini. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ubora wa elimu unatokana na maandalizi mazuri ya wanafunzi kuanzia Kidato cha Kwanza pamoja na mambo mengine, ni vyema walimu wa Sekondari wawe bora, wenye elimu na taaluma ya Ualimu. Kuendelea kutumia watu ambao sio Walimu, pamoja na vijana waliomaliza *Form VI* kunaleta athari kubwa kwa wanafunzi na athari hiyo nionavyo mimi ni *irreparable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi isifanye mpango kuagiza Walimu kutoka nje, hata *volunteers*, ili watusaidie kuziba mapengo wakati Serikali inajitahidi kufungisha Walimu wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama bado kuna adhabu zinazotolewa zikielekezwa katika kazi za kilimo, naomba suala hili liangaliwe kwa umakini. Kilimo kisiendelee kutafsiriwa na wanafunzi na jamii nzuri kuwa ni kazi ya suluba. Kazi ya mashamba/kilimo Shuleni zisitolewe zikiambatana na dhana ya adhabu, badala yake, taaluma ya kilimo iongezwe katika mashamba ya Shule hasa kwa Shule zenye mashamba makubwa kama ile ya Weruweru Sekondari, Moshi.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa kuweza kuongoza Bunge hili kwa kiwango cha *speed* na umahiri mkubwa pamoja na wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Manaibu Waziri na Kamati yake na Washirika wote waliotoa mchango wao katika kutunga hii hotuba hii, ni nzuri na inastahili kupewa pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naanza kuchangia hotuba hii. Elimu ni mkombozi wa binadamu. Kama binadamu hana elimu, huyo hajakamilika, kwani hata fundi Seremala ikiwa hana elimu hawezi kuunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Serikali kwanza kwa kujua hilo kwa kuweza kutoa kipaumbele kwa Wizara hii kwa kuweza kuongeza madarasa ya kusomea kuanzia Shule ya Msingi hadi Sekondari kwa nguvu za wazazi na Serikali. Lakini la kusikitisha ni uhaba wa Waalimu na madawati katika Shule hizo na moja linalowaangusha wanafunzi katika masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, mshahara wa walimu ni mdogo sana kwa hiyo, mshahara waongezwe. Kwa kweli Walimu wana kazi kubwa kumwelimisha bubu hata akasema, kipofu akaona, kiziwi akasikia na sote hapa Bungeni tusingekuwepo leo lakini ni nguvu za Walimu. Walimu walioko Vijijini waangaliwe kwa kupewa nyumba za kuishi au wajengewe wasiwe na hali duni kama ilivyo hivi sasa na wale wanaokaa mbali na wao wapewe usafiri japo wa baiskeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile la kusikitisha, wanafunzi wa kike wanaopata mimba, wanafunzi hao hufukuzwa na wanafunzi hao hupata shida sana na wengine bado wanao uwezo wa kumudu masomo yao, kwa nini watoto baada ya kujifungua hawamruhusu kuendelea kusoma kwa wale watakaoendelea? Naomba jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Hawa ni watoto wetu, kama wanakosea, tayari ameshaona kosa lake, aende wapi huyu? Serikali iliangalie suala hili.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika Bungeni na kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Manaibu wake kwa mipango mizuri kama Mwenyezi Mungu atawawezesha kuitekeleza, naomba Mwenyezi Mungu awasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najikita katika hoja husika ya elimu. Kuhusu usafiri kwa wanafunzi, Serikali iweke mikakati ya usafiri wa wanafunzi ili wawapunguzie kudhalilika. Wanafunzi wanapata taabu sana kuhusu usafiri hasa wa Jiji la Dar es Salaam. Ikiwezekana, Serikali iweke mabasi maalum ya wanafunzi ambayo yatakuwa ya bei nafuu kwa mfano *UDA*. Kwa vile Shirika hili ni la Serikali, basi lingefanywa mahsusi kwa ajili ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu wanafunzi walemavu. Kuna wazazi wengine wakishazaa watoto walemavu huona wale watoto hawana haki ya jambo lingine lolote isipokuwa kula na kunywa, hivyo kuwakosesha haki yao ya msingi hasa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi hao hushindwa kuwapeleka watoto Shule, kwa hiyo, naiomba Serikali iwatazame watoto wa aina hiyo kwa jicho la huruma kwa kuwajengea Shule pamoja na *boarding* (hosteli) waweze kupata elimu na kwenda kwa pamoja ili mtoto asijihisi mnyonge na kuathirika kisaikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi sana kujenga Shule, lakini tatizo ni Walimu na vifaa na ubora wa elimu hupimwa kwa Walimu, sio kwa wingi wa Shule bila vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri yenye mchanganuo wa kina. Vile vile, nawapongeza Manaibu Waziri wote wawili kwa kazi nzuri wanayoifanya wakishirikiana na Watendaji wote wa Wizara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Dar es Salaam, hali ya idadi ya Shule za Sekondari hazikidhi mahitaji kutokana na idadi ya watu waishio Mkoani humo kuwa

kubwa. Inakadiriwa kuwa na watu milioni tatu na nusu. Vile vile, mwamko wa kujitolea kujenga Shule au kuchangia masuala ya elimu kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhimiza ujenzi wa Shule za Sekondari, hatimaye tatizo hili limepungua kidogo ingawaje Mkoa huu bado tatizo halijakwisha.

Ombi langu kwa Serikali ni kwamba, kama litawezekana itoe tamko maalum kwa Mkoa wa Dar es Salaam litakalohusu ujenzi wa Shule za Sekondari kwa kila Kata na kwa muda maalum usiozidi mwaka mmoja. Ikiwezekana, itoze kodi hata kwenye Mechi kubwa za Mpira wa Miguu au Tamasha la Muziki kwa madhumuni ya kusaidia vijana wengi kuzurura Mitaani kwa kukosa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na Mpango maalum wa kuelimisha wananchi kupitia Vyombo vya Habari kama *television, Radio* vijarida mbalimbali ili kuwajenga wananchi kisaikolojia waondokane na mawazo kwamba kila kitu Serikali itafanya, hususan Mkoa wa Dar es Salaam. Wengi hawana moyo wa kujitolea, lakini inatokana na kutoelimishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ucheleweshaji wa Serikali Kuu kupeleka posho za Walimu kwa wakati, ambapo inapelekea Halmashauri kutumia pesa kwa kuwalipa Waalimu ambazo hazikuwa kwenye mpango au Bajeti kwa ajili ya posho za Walimu. Hii inarudisha nyuma mipango ya Halmashauri hususan Halmashauri ya Manispaa ya Ilala Mkoani Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za mpango wa *MMES* uende kwenye Kamati za Shule kupitia Halmashauri kama ulivyokuwa Mpango wa *MMEM* au Serikali iwaelimishe wananchi kuhusu kusuasua kwa mpango wa *MMES* ambapo inasababisha hisia mbaya kwa kutokuelewa mpango mzima wa *MMES*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Watu Wazima iendane na elimu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kushukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia hoja iliyo Mezani. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mwalimu Margaret Sitta kwa namna alivyoandaa kwa mpangilio mzuri Bajeti yake hii, ambayo ina *layout* nzuri, mpangilio wa taarifa mbalimbali nzuri sana, *quality* ya kitabu chenyewe na michoro, *graphs* mbalimbali na picha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama *graphs* nyingi zilizotolewa, unapata kabisa picha ya Elimu ya Darasa la Kwanza hadi Kidato cha Nne ilivyo nchini. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Elimu ndiyo roho ya maendeleo ya nchi na ndiyo dira ya maendeleo, ndiyo maana Serikali iliibua Sera ya *MMEM* na *MMES*. Tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza *MMEM* na mafanikio tumeyaona katika kupanua Shule, kuongezeka kwa Walimu, vitabu vya kiada, maliwato, kiwango cha kufaulu na kadhalika. Kama tunavyojua, neema hii imetuletea tatizo la kukosa Shule za kutosha za Sekondari. Kwa hiyo, ni lazima zaidi ya kujenga na kuimarisha Shule za Sekondari *MMES* ni lazima ikazaniwe zaidi kwa namna ile ile tulivyofanya *MMEM*. Serikali isichoke kuhamasisha wananchi kujitolea nguvu zao katika ujenzi wa mwanzo wa Shule/madarasa. Kuna haja pia ya kuweka mkazo zaidi wa uhamasishaji katika maeneo yaliyo nyuma kielimu. Maeneo haya hayataendelea kwa kulalamikia wale walioendelea tu, bali nao ni lazima wajitoe na kuwa *aggressive* katika kuhakikisha kuwa watoto wao wanakwenda Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari zinakosa sana vifaa vya Maabara. Hii ni karne ya sayansi na teknolojia na kwa kweli dunia haitarudi nyuma, kwa hili. Kwa hiyo, ni muhimu na kwa dharura, Serikali ijitahidi kuweka vifaa japo vya msingi wa Maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa idadi ya Walimu ni kubwa, pia hali ya UKIMWI ni kubwa. Wizara ni lazima iendelee kutoa elimu ya kinga, lakini zaidi ihakikishe kuwa Walimu wanapata dawa za kurefusha maisha na bila ya urasimu mrefu. Elimu hii pia itolewe kwa kadri itakavyoonekana inafaa kwa marika tofauti ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma miaka ya 1960 tulilazimishwa kutumia wino wa kidau na nibu. Nafikiri hii ilikuwa ni kwa nia nzuri ya kuimarisha mwandiko/hati ya wanafunzi au ilikuwa ni kwa sababu gani? Kwa nini hili limeondolewa? Sasa hivi wanafunzi wanatumia *ball points* moja kwa moja. Hii maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Ufundi ni elimu muhimu sana nchini. Ni kutokana na elimu hii ndiyo nchi itaweza kupata tabaka la ngazi ya kati *(middle income earners)* na vile vile tabaka la *artisans* na wafanyakazi wenye stadi/*skills* mbalimbali na hivyo kuchangia katika kukuza uchumi na kutoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri sana Serikali, ijitahidi wanafunzi hawa wakimaliza wapewe vifaa vya stadi waliyohitumu, hata kama ni kwa mkopo ili mara watokapo Chuoni waweze mara moja kuanza kazi. Hii ina maana, kwa mfano mafundi cherehani watapatiwe/wakopeshwe vyerehani, useremala – vifaa kama randa, misumeno na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Ufundi ni muhimu sana vishuke ngazi ya Wilaya. Ni bora visiwepo Vyuo vya Mkoa, lakini vikawepo vya Wilaya. Huku ndiko wananchi na watoto wengi waliko. Huku ndiko vile vile kunakotakiwa kuwa na mazingira mazuri ambayo yatawafanya watu/watoto wasikimbilie Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, miaka ya 1960, wanafunzi walikuwa wanapata maziwa Shuleni, kila wakati wa mapumziko. Ninakumbuka maziwa hayo yalitolewa kwa msaada wa *USAID*. Ninajua kwa sasa Shule na wanafunzi wameongezeka sana na ni gharama kubwa. Lakini suala la lishe tena lishe bora kama *protein* – maziwa ni muhimu. Kwa nini Serikali isiombe Wafadhili, *USA* wakaendelea na *gesture* hii muhimu? Tena kwa sasa wao *USA* walishaanza kuzungumza kuhusu lishe/mlo wa watoto? Nitaomba Mheshimiwa Waziri aseme baadhi ya hoja hizi.

Ninampongeza tena Waziri na timu yake kwa Bajeti nzuri sana na ninaunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ambayo imewasilishwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo, Mheshimiwa Margaret S. Sitta. Niwapongeze pia Manaibu Waziri wote wawili, Kamati ya Bunge inayoshughulikia huduma ya jamii pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii waliofanikisha kwa njia moja au nyingine hotuba nzuri na yenye mchanganuo mzuri wa wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za pekee zimwendee Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne kwa ubunifu wake makini wa kuanzisha Wizara hii ambayo ni mpya na iliyojaa au kusheheni mambo ya elimu na mafunzo ya ufundi. Mheshimiwa Rais pia ameipangia Mawaziri watatu (Waziri na Manaibu Waziri wawili) Wizara hii kwa maana ya kuonyesha nia yake katika utendaji mzuri kwenye Sekta hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ninaomba Mawaziri wa Wizara hii wasituangushe na pia wasimwangushe Mheshimiwa Rais, wafanye kazi kwa kushirikiana pamoja na maelewano na wananchi (wadau) ambao wana imani kubwa sana na uongozi wa Awamu hii ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitakuwa na mchango sana, kwa sababu kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kimejitosheleza kwa kiwango kikubwa sana cha maelezo ya utekelezaji kwa kipindi kilichopita na kipindi kijacho utekelezaji wake pia umepangwa. Kitabu hiki pia kina vielelezo vya kutosha kiasi kwamba kimepunguza maswali kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mapendekezo tu kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu ni Mafunzo ya Ufundi hasa kuhusu mipango mizuri ya kukuza Elimu ya Msingi *(MMEM)* na Sekodnari *(MMES)* inayofanywa huku Tanzania Bara.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Waziri wa Elimu na Amani kwa upande wa Zanzibar, mipango hii na mingine mizuri ifike hata huko Zanzibar. Kwa maana nyingine ni kwamba, umefika wakati mfumo mzima wa elimu Tanzania kuanzia Shule ya Msingi hadi Vyuo Vikuu uwe ni mmoja, isiwe vipande vipande kama ilivyo sasa Zanzibar, wana utaratibu tofauti na Tanzania Bara hasa kwenye mipango ya Elimu ya Msingi.

Mheshmiwa Naibu Spika, suala la Mafunzo ya Ufundi ni muhimu sana kwa vijana wetu ambao huwa hawapati nafasi ya kuendelea na elimu ya juu. Kule Zanzibar, Serikali imeanzisha mafunzo ya Elimu ya Amali ambayo inafanana sana na hii ya

Tanzana Bara. Kwa hiyo, upo umuhimu pia wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kuanzisha Vyuo vya *VETA* angalau viwili huko Zanzibar ambapo kimoja kikajengwa Ujunga na kingine Pemba. Vyuo hivi viwe vya kitaifa ambapo wanafunzi wanaweza ama wakatokea Tanzania Bara au Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili litasaidia sana katika kuimarisha umoja wetu wa Muungano ukizingatia kuwa hivi sasa uhusiano kwa Sekta ya Elimu ya Msingi hadi Sekondari wa kubadilishana wanafunzi hatunao, tulionao ni ule wa Vyuo vya Elimu ya Juu tu ambao nao huenda ukazorota kufuatia kuanzishwa Vyuo Vikuu huko Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya Baraza la Mitihani la Taifa Tanzania *(NECTA)* ndilo lililopewa uwezo wa kuendesha mitihani ya kitaifa ya kumaliza Elimu ya Msingi Tanzania Bara, Elimu ya Sekondari Kidato cha Nne na Sita, Ufundi, Ualimu Daraja "A" na Stashahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 64 na ule wa 68 wa kitabu cha hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kimeelezea orodha ya utekelezaji wa malengo ya Baraza hilo katika mwaka 2005/2006 na malengo ya mwaka 2006/2007 kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya utekelezaji wa malengo hayo ni kuendesha mitihani ya Cheti cha Ufundi Sanifu na Stashaahda ya juu ya Uhandisi kwa niaba ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu mimi, Baraza hili kwa miaka mingi sana limekuwa likiendesha mitihani ya namna hiyo kwa Cheti na Stashahada ya Juu ya Uhandisi kwa Vyuo ambavyo viko chini ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana na migogoro mingi sana kwa wananchi wanaotahiniwa na Baraza hili kwa upande hasa wa Stashahada ya Juu ya Uhandisi kwamba hawatendewi haki kabisa na Baraza hili kwa vile Baraza huwa halizingatii hali halisi ya maswali inayoyatunga kuwa katika kiwango cha elimu hiyo. Mtahiniwa kuulizwa swali la miaka miwili nyuma, mfumo ambao hauko kwenye Vyuo vingine hapa hapa nchini, kwa mantiki hiyo wanafunzi wengi sana wamekuwa hawafaulu mitihani hiyo na hivyo kupoteza wataalam wengi kwa utaratibu huo mbaya wa mitihani ya Baraza hilo. Je, ni kwa nini sasa Baraza halioni haja ya kuendelea kuwatungia mitihani Wahitimu wa Uhandisi wa Stashahada ya Juu na badala yake mitihani yao itungwe na Taasisi zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumbukumbu zangu ni kuwa, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia imefuta Cheti cha Ufundi Sanifu na badala yake imeanzisha Shahada ya Uhandisi, lakini kwenye malengo ya mwaka 2006/2007 ya hotuba ya Waziri kifungu *"C"* ukurasa wa 68 Wizara yake kupitia Mamlaka ya Baraza la Mithani ya Taifa, nina lengo hilo la kuendeleza mitihani ya Cheti chaUfundi Sanifu *(FTC).* Je, Wizara yake

itaendeleza mafunzo katika ngazi ya Cheti hicho? Kama ndio, ni Chuo kipi kitakachotoa mafunzo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Baraza la Mitihani la Taifa huendesha mitihani mbalimbali kama ilivyoainishwa ukurasa wa 66 kifungu 52 cha Kitabu cha hotuba ambapo pia vielelezo vya matokeo ya kufaulu kwa wanafunzi yameambatanishwa kwenye viambatanisho, lakini bado matokeo ya kufaulu kwa wanafunzi waliofanya mitihani ya Taifa kupitia *NECTA* kwa Cheti cha Ufundi Sanifu na Stashahada ya Juu ya Uhandisi hayajaambatanishwa ili kulinganisha ufaulu wa Wahitimu hao. Je, ni kwa sababu zipi viambatanisho vya matokeo hayo kwa ngazi hizo (*FTC* na *ADE*) havikuambatanishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara pia kuwa, ikiambatanisha matokeo ya kufaulu mitihani ya Taasisi za nje inazozisimamia, Baraza la Mitihani la Taifa kama vile ile ya Chuo Kikuu cha *London Linclonshire Institute of Purchasing and Supply Chartered Institute of Marketing, The Royal Institute of Chartered Suveryors* na kadhalika ili wananchi wafahamu ni Watanzania wangapi wanaofaulu mitihani hiyo.

Nnashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutolishirikisha Baraza la Mitihani la Taifa *(NECTA)* kuendelea kutunga mitihani kwa Wahitimu wa Stashahada ya Juu ya Uhandisi, kwani linachangia sana kuwapoteza wataalamu wetu waachie Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia watafute namna yao. Vinginevyo, Stashahada ya Juu ya Uhandisi ifutwe mpaka pale Wizara husika itakapopata muafaka au suluhisho la kudumu kwa mafunzo hayo ya utoaji wa Stashahada ya juu ya Uhandisi baada ya kuharibu fedha za Umma na kupoteza muda mwingi kwa Wahitimu ambao wengi huwa hawafaulu mitihani hiyo inayotungwa na *NECTA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasilisha na ninaunga mkono hoja tena. Ahsante.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa uwezo wa leo kusikiliza Bajeti ya Wizara nyeti kama hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nampongeza Waziri wa Elimu na Manaibu wake pamoja na wote waliotoa mchango wa fikra, maandishi na hata kuchapisha vijitabu ambavyo vimeendana naWizara yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu kwa kweli ni Wizara ambayo kila mmoja wetu alipitia elimu kwa namna yoyote ile na bila kuelimika huwezi kupata maisha bora. Jamii yoyote yenye kaya ya vijana walioelimika, maisha ya wazee husika hubadilika na kuwa maisha mazuri na wale ambao hawakupata bahati ya kupata elimu, maisha ya kaya hizo huendelea katika umasikini mpaka milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Walimu ambao ndio hasa wanaohitajika. Bila Mwalimu hakuna elimu. Walimo wetu kwa kweli wanakosa moyo wa kusomesha kwa dhati kwa sababu ya Serikali kupoteza kabisa dhamana ya kuwaenzi Walimu, hawapatiwi mishahara ya kuwawezesha kuishi kwa raha, mpaka wanajihusisha na

vibiashara vidogo vidogo wanapokuwa kwenye Vituo vya kazi, yaani mashuleni ili waweze kuokoteza visenti vya kuweza kuwasadia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu hawaandaliwi kielimu, wanatolewa moja kwa moja kutoka mashuleni bila kupitia kwenye Vyuo vya Ualimu na kwanza kusomesha, hawaelewi taratibu za ualimu, kwani Mwalimu lazima awe na uwezo wa kulea pia. Mwalimu ajue jinsi ya kusomesha wenye akili nzuri na wale ambao akili zao hazishiki mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi kwa wanafunzi, yaani watoto wetu, elimu hawaitilii maanani hata kidogo, watoto wanazaliwa kwenye umasikini uliokithiri hasa wale wa Vijijini ambao ndio walio wengi, maisha yao tangu asubuhi ni ya kutafuta, wazee hawana uwezo wa kuwapeleka Shuleni, ukianzia tangu sare za Shule na ukizingatia leo lazima madaftari awe nayo mwenyewe, Serikali haisaidii hata penseli, kwa hiyo, wazee wanajikuta hawana uwezo, wanaacha watoto bila ya elimu na umaskini unaendelea kama nilivyokwishaeleza huko nyuma. Kwa wale wanafunzi walio Mijini walio wengi, hata kama wanataka kusoma Mijini, kuna kila vishawishi, Shule ziko mbali na nyumbani, usafiri wa shida, wanachelewa kurudi majumbani, wanajikuta kuingia kwenye makundi mabaya na kupoteza hamu ya kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba:-

- Walimu waandaliwe kwa kupatiwa elimu iliyo bora na kurudishwa mpango wa kufanya majaribio kabla ya kuanza rasmi Ualimu;

- Walimu wapatiwe motisha ya kuwawezesha kumudu maisha yao na kupatiwa nyumba bora za kuishi karibu na maeneo yao ya kazi;

- Walimu wapatiwe mishahara yao kwa wakati na wasisumbuliwe kuifuata maeneo ya umbali na pale anapofanya kazi;

- Elimu itolewe kwa wazazi hasa wale wa Vijijini waeleweshwe kwamba kumpeleka mtoto Shuleni ni jambo la lazima na sheria ya kutokupeleka watoto Shuleni kwa muda unaohitajika ifanye kazi, ikibainika mzazi hajampeleka mtoto Shuleni hatua kali ichukuliwe;

- Serikali ijitahidi kupata fedha ya kusaidia wanafunzi wapatiwe madaftari na vitabu vya kiada hata kama vitabu hivyo vitakusanywa baada ya kazi;

- Serikali ijitahidi kusaidia upatikanaji wa usafiri kwa urahisi ili wanafunzi wanaosoma mbali na nyumbani warudi mapema (hasa Mkoa wa Dar es Salaam);

- Serikali irudishe Elimu ya Dini mashuleni ili watoto wetu wapate muda wa kuelewa dini zao kwani wanakaa Shuleni muda mwingi tangu asubuhi na kukosa muda wa kupata Elimu ya Dini zao. Inachangia kukosa maadili;

- Masomo yawe na ratiba iliyozingatia siku ili wasiendelee kubeba mizigo ya madaftari yote na kumfanya mtoto kubeba mizigo kila siku;

- Elimu ya Sekondari iendane na vipaji vya stadi za kazi ili akitoka pale aweze kujiajiri; na

- Masomo ya upishi, ufundi cherehani yaani mshoni, kazi za mikono kama kufuma na kusuka vikapu na mikeka, yarudishwe mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali haijatenga fungu la ujenzi wa Maabara. Katika Bajeti yake ya mwaka 2006/2007, ni sifuri, nashindwa kuelewa madarasa ya Sekondari tuliyojenga itakuwaje bila Maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, natanguliza shukurani. Naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Viongozi wote wa Chama cha CCM na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliochaguliwa na kuteuliwa ndani ya Serikali hii ya Awamu ya Nne. Nampongeza kipekee Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta kwa uteuzi wake katika nafasi hii ya Uwaziri wa Eimu na Mafunzo ya Ufundi. Tangu ateuliwe na kuanza kazi, kwa kweli ameonyesha uwezo mkubwa sana katika uongozi na hasa katika utumiaji wa mbinu shirikishi katika kuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niwapongeze Manaibu wawili, Mheshimiwa Ludovick Mwanzila na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, kwa kujipanga vyema ndani ya Wizara hii na hasa kwa majibu yao ya ufasaha wanayoyatoa hapa Bungeni kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Nimalizie kwa kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara chini ya Katibu Mkuu Dr. Dihenga na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Yusufu O. Mlaki, Wakurugenzi na wengine wote. Jamani poleni na kazi na hongereni kwa kazi yenu nzuri. Mimi ni mwenzenu na najisikia vizuri sana leo ninapowasilisha Bajeti ya Wizara yenu ambayo imenilea kwa zaidi ya miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uzoefu huo wa miaka 30, kama Mwalimu na pia kama kiongozi katika Vyuo vya Ualimu, ninayo machache ya kuchangia hotuba hii nzuri sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Idara kwa utekelezaji mzuri wa kuandaa kupeleka vifaa hasa vya watoto wasioona mashuleni. Hata hivyo, kwa kuwa Vyuo vyetu vya Ualimu mathalan Butimba *TTC* huchukua hata vijana wasiiona, ni vyema Idara iwe na mikakati ya kupeleka vifaa hivyo katika Vyuo vinavyojikuta vina wanachuo wa aina hiyo. Hii itasaidia kuweka mazingira mazuri kwa vijana hao kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachuo hawa ambao tumewatumia ku-*remedy* hali ya uhaba wa walimu mashuleni waandaliwe mazingira mahsusi ya kupatiwa kazi ya Ualimu ya kawaida ili kuwaongeza uwezo wa kitaaluma na pia ili tuweze kuwa-*retain* baada ya miaka yao miwili ya kufundisha kwa leseni, nashauri wapelekwe *DUCE* (Chang'ombe) au *MUCHE* (Mkwawa) au hata Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na Stashahada za fani zitolewazo sasa Butimba *TC,* nashauri Serikali irejeshe pia kozi za Cheti ili wale wasiokidhi sifa za Stashahada na wana-*interest* au vipaji vya fani hizo, basi wapate fursa hiyo na waweze kwenda Chuo Kikuu cha Dar es Salam kuendelea na fani kama awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii muhimu sana pamoja na Manaibu Waziri wake kwa kuandaa Bajeti hii na kuiwasilisha hapa Bungeni. Niende kwenye mchango wangu moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana la kukosekana kwa Walimu wa kutosha kwenye Shule zetu za *Primary* na hata *Secondary* na hasa maeneo ya Vijijini. Aidha, Serikali imehamasisha sana wananchi kuchangia kwenye ujenzi wa Shule kwenye ngazi mbalimbali kuanzia Vijijini, Kata, Tarafa hadi Wilaya. Wito huo umepokelewa vizuri na wananchi wameweza kujenga Shule nyingi lakini hakuna Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wengi ambao wanapangwa Vijijini wamekuwa wanakataa na wengine kuacha kazi pale wanapopelekwa Vijijini au kuhamishiwa huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati muafaka sasa Serikali ichukue juhudi za haraka kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Walimu huko Vijijini na pia Wizara iandae utaratibu wa kutoa motisha *(incentives)* kwa Walimu wanaopangwa Vijijini ili kuvuta Walimu kwenda huko na hivyo kusaidia watoto wa huko Vijijiji kupata elimu bora kama watoto wanaoishi Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ucheleweshaji wa mishahara ya Walimu na adha wanayoipata walimu hao wakati wa kufuatilia mishahara yao. Walimu wanasafiri kutoka Vijijini hadi Wilayani kufuatilia mishahara yao, wakifika Wilayani wanaambiwa mishahara haijafika na kwa kuwa hawana nauli za kurudi kwenye Vituo vyao vya kazi, wanalazimika kusubiria kwa siku tatu hadi tano. Pale hana chakula wala makazi, anaishi kwa taabu kubwa. Hili limepelekea Walimu kujiingiza kwenye vitendo vya kihuni ili wapate huduma pale wanaposhindwa na hivyo kuchangia sana Walimu kuathirika na ugonjwa wa hatari wa UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itambue mchango wa Walimu kwa Taifa hili na hivyo kuwaboreshea mishahara yao na kurahisisha upatikanaji wa mishahara yao bila bughudha kama wanazopata sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu Serikali haijatoa umuhimu wa kutosha kwenye Vituo vya Ufundi ambavyo ni muhimu sana kujengea vijana uwezo wa kuweza kujiajiri. Vituo hivi sasa vinaendeshwa na watu binafsi maeneo mbalimbali na vingine kwa sababu ya kukosa pesa za kutosha, vinatoa elimu isiyokuwa bora na hivyo vijana kushindwa kupata ujuzi mzuri na maarifa ya kujitegemea pale wanapomaliza masomo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni umuhimu wa kutoa msukumo wa kutosha kwa Vituo hivi vya masomo ya Ufundi na kusaidia Vituo Binafsi kwa kuwapatia Walimu wenye uwezo mzuri ili vijana wetu waweze kupata mafunzo na ujuzi wa kutosha kujiajiri pale wanapomaliza Vyuo vya Ufundi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naishauri Serikali kurudisha mafunzo ya ufundi kwenye Shule za Sekondari zilizokuwa zinatoa elimu ya nadharia na vitendo ambavyo utaratibu huo uliondolewa kwenye mitaala *(syllabus)* ya Sekondari katika awamu iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante sana.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kabla ya yote, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuingia madarakani baada ya ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuonyesha umahiri mkubwa katika uwasilishaji wa Bajeti yake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya yote hayo, mimi binafsi kwanza naipongeza Serikali katika mipango yake ya *MMEM* na *MMES.* Mpango huu umeipelekea Wizara hii kupata sifa kubwa katika kuusimamia kikamilifu hatimaye *impact* yake imeonyesha kukubalika kikamilifu nchini. Kwa upande wangu, wanafananisha kukubalika kwake sawa na *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Wizara hii kwa kurudisha hadhi ya elimu nchini kwani hivi sasa idadi ya wanafunzi wanaopelekwa nchi jirani kwa masomo imepungua sana, hivyo hii inathibitisha Watanzania sasa wanathamini elimu inayopatikana nchini.

Mheshmiwa Naibu Spika, elimu ya amali ni jambo la msingi sana litakalopelekea watoto wetu kuweza kujitegemea baada ya kuhitimu mafunzo hayo. Hivyo, naomba kusisitiza mipango ya baadaye, kila Mkoa wawe na mikakati ya Elimu ya Amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii siyo Wizara katika Muungano, lakini mimi napendekeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ziwe na *Syllabus* moja kitu ambacho kitapelekea kuwa na kiwango cha Elimu inayofanana. Naamini mpango huu kama utakubalika, utaiwezesha nchi yetu kuwa katika mustakabali mzuri kwa maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado napendekeza kwamba, kwa kuwa elimu ni suala la msingi sana duniani na katika kutafuta elimu sio suala la kulionea aibu, basi mipango ifanywe kupitia *UNICEF* tupatiwe Walimu wa *volunteer* kutoka nje ili kukidhi na kujenga mazoea kwa wanafunzi katika uwanja wa kimataifa ndani ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la malalamiko ya Walimu hasa kuhusu mishahara, lazima yaondolewe. Kero hii inatia aibu kubwa siyo tu Wizara bali hata nchi kwa jumla, iweje mwajiriwa akae miezi 131 bila kulipwa? Serikali ya Awamu ya Pili ililivalia njuga sana likapungua kwa kiasi kikubwa sana, basi Awamu hii ya Nne ilimaze kabisa.

Mwisho, *hostel* za wasichana ziongezwe maradufu ili maadili ya dada zetu yaboreke. Ahsante. Naitakia kila la heri Bajeti hii.

**MHE. JOHN P. MAGUFULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta – Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri ya Bajeti yake. Nampongeza pia Naibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara yake. Ukweli, pongezi nyingi sana ziwafikie wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi yafuatayo: Ninaomba nipatiwe walimu katika shule zilizo ndani ya Jimb langu. Shule hizo ni pamoja na *Chato Secondary School, Katende Secondary School, Zakhia Meghji Secondary School, Busilayambo Secondaryy School, Buziku/Sumaye Secondary School, Makurugusi Secondary, School, Nyamitembe Secondary School, Buselesele Secondary School* na *Ilemela Secondary School.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule hizi zina upungufu mkubwa wa Walimu. Naomba Wizara hii wakati ikipanga Walimu, Shule husika zitazamwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Maabara inayojengwa katika Shule ya Sekondari Chato ikamilike, kwani sasa ni zaidi ya miaka mitano na Maabara bado haijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii, hata kupitia Bunge hili kutoa tamko la kuzipongeza Shule zilizofanya vizuri katika matokeo ya *Form IV* na *Form VI.* Hii ni *motivating agent* kwa maadili ya Ualimu, hii ni pamoja na *Chato High School* ya Wilayani. Chato iliyoshika nafasi ya tatu kitaifa kwa ushindi kwa Shule zenye idadi ya wanafunzi *less than 30* wengi wanafikiri Shule hii ni *Seminary* wakati sio hivyo. Shule hii ni ya Serikali chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nampongeza tena Waziri, Mheshimiwa Margaret Sitta, Naibu wake Mheshimiwa

Ludovick Mwananzila na Mwantumu Mahiza, Katibu Mkuu wake na Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na wafanyakazi wote wa Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana na ninaunga mkono hoja.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mashaka sana na jinsi Wizara na mikakati yake ya kukabiliana na mapungufu ya utekezaji wa mipango ya *MMEM* na *MMES* hasa katika kukabiliana na upungufu wa Walimu yaani:-

(a) Kwa walimu wa Shule za Msingi, kupunguza muda wa Walimu wa Shule za Msingi kusomea mwaka mmoja badala ya miaka miwili; na

(b) Kuwapa kozi ya mwezi mmoja vijana waliomaliza *Form Six* ili wakasomeshe Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba Ualimu ni fani inayohitaji ujuzi na hivyo basi sio kila aliyesoma hata iwe katika kiwango cha *Ph.D.* anaweza kuwa Mwalimu bila kusomea Ualimu na akawa Mwalimu *effectively*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maamuzi (a) na (b) ya hapo juu, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba anaishushia hadhi kazi ya Ualimu na kunaweza kusababisha Walimu kuikimbia kazi hiyo kwa kuonekana aliyekwenda Shule bila ya kusomea Ualimu anaweza kuwa Mwalimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulielezea Bunge lako Tukufu anaposema mkakati huo ni wa muda mfupi, ni lini anategemea mpango huo utasita na wanafunzi wetu watasomeshwa na Walimu wenye fani ya Ualimu, akizingatia kwamba mkakati huo unaathiri ubora wa elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimestushwa na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusiana na wanafunzi wa Shule za Msingi wa jinsia ya kike ambao huacha Shule kwa tatizo la kupata mimba, kwa mfano katika mwaka 2005 Mkoa wa Morogoro peke yake ni karibu wanafunzi 400. Je, Mheshimiwa Waziri analiahidi nini Bunge hili katika kukabiliana na tatizo hili ili wanafunzi wa kike wasikose haki yao ya msingi ya kupata elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iwape adhabu kali wanaohusika na kuwapa mimba wanafunzi ili kukomesha tabia hiyo mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu mimi utaifa wetu ni pamoja na Tanzania Bara na Zanzibar, yaani utaifa wa Tanzania. Nafahamu kwamba suala la Elimu na Mafunzo ya Ufundi sio suala la Muungano. Lakini kwa nia njema kabisa ya kujenga utaifa wetu, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza ni vipi wanafunzi wa Zanzibar na

wa Tanzania Bara wanaweza kukunganishwa kwa kutumia Shule na kuimarisha umoja wa kitaifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri na Manaibu Waziri kwa hotuba nzuri yenye kukidhi. Naomba nichangie ili kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya elimu ilivyo sasa *(crisis)* inaonyesha mipango yetu ina walakini, kwa mfano wananchi wamehamasishwa kujenga Sekondari kila Kata na wameitikia vizuri Same.

Matatizo ni fedha za kuchangia majengo hayo kama Serikali ilivyoahidi hazijatolewa na Walimu ni haba sana. Kama mipango ingekuwa safi wakati wananchi wamehamasishwa, *training* ya Walimu pia ingekuwa inafanyika. Naiomba Serikali inapochukua hatua mbalimbali ifikirie/ishirikishe Idara/Wizara mbalimbali kwa mfano kama lengo ni kuongeza idadi ya wanaoingia Sekondari, basi pia kila anayehusika aangalie jinsi atakavyohusika kumpata Mwalimu, inachukua muda gani, kujenga Sekondari inachukua muda gain, *placement* inachukua muda gani, mishahara ina sera ipi na Bajeti gani na vifaa vya elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadilishaji wa mitaala, pia huathiri sana elimu yetu. Napendekeza kwamba Vyuo Vikuu vyote viwe na Idara ya Ualimu ili wanafunzi wanaotaka kuchukua *option* ya Ualimu wafanye hivyo. Kwa kweli ifanyike kazi ya kuwahamasisha. Kwa namna hiyo, tutapata walimu wenye fani mbalimbali. Hii pia ina *incentive* kwa sababu eneo hili ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wilaya ya Mbinga, wananchi wa Mbinga wameitikia kwa kiwango cha juu sana kuhusu kujenga maboma na katika Jimbo langu, kila Kata imejenga Sekondari mahali pengine mbili. Naomba fedha ipelekwe ili wananchi wasikate tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mbinga ina *High School* moja tu ya Kigonsera. Tunaleta maombi Sekondari zifuatazo ziwe *High School,* Itagati, Ruanda na Lundu. Dhana ya kusema *High School* ni za Taifa, naielewe sana. Mimi naangalia faida zake kwa mlengo mpana zaidi. Naomba Wizara ifikirie maombi haya na iidhinishe hizo *High Schools.*

Mwisho, mipango ya Wizara 2006/2007 inaelekea kuiacha mbinga kabisa. Naomba jambo hilo liangaliwe na kurebishwa. Naomba magari kwa *Mbinga day*, Ruanda na *Matiri Secondary Schools.*

Naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia hotuba ya Wizara hii nikizingatia yale matatizo yanayokabili Wilaya yangu ya Kibondo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Wilaya ya Kibondo inakabiliwa na tatizo kubwa la upunguvu wa Walimu kwenye Shule zote. Tatizo linalojitokeza ama sababu zinazotolewa ni kwamba hata kama Walimu wangepatikana, bado lipo tatibo kubwa la nyumba za kuishi Walimu kwenye mashule hayo.

Walimu wa kujitolea *Form IV* katika *Sekondary Schools* hawakidhi mahitaji kwa maana ya kuwa na uwezo mdogo. Hali hii inasababisha kushindwa mtihani kwa vijana mashuleni, anashinda kwa kiwango kidogo *(below standard)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu iliahidi upendeleo maalum katika Sekta ya Elimu kwa Mikoa iliyoachwa nyuma katika Sekta ya Elimu ikiwemo Kigoma. Je, ni hatua zipi hasa Wizara imechukua kusaidia Mkoa wa Kigoma kifedha? Naomba maelezo yatolewe kuhusu tatizo hili. Ikumbukwe kwamba Mikoa inayosemekana kuendelea imetumia fedha nyingi za Taifa ambazo ni za wananchi wote. Ili kuimarisha Sekta ya Elimu, Mikoa ya Kigoma na kwingineko ambayo bado ipo nyuma, lazima kuwe na uamuzi wa makusudi kuiinua katika Sekta ya Elimu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nimpongeze pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Bakary Mahiza, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa Maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara. Bajeti imegusa maeneo yote muhimu. Pamoja na hayo, naomba nipewe ufafanuzi wakati wa majumuisho kwa haya yafuatayo:-

Mpango wa *MMES* umepokelewa vizuri na wananchi wapo tayari kufanya kazi kwa kuhakikisha mpango huu unafanikiwa, lakini ni vigezo vipi vinavyotumiwa na Wizara katika Serikali *(Wizara)* kuweka nguvu zake? Wananchi wanasimamisha maboma lakini maboma hayo yanaachwa bila utekelezaji katika kuyamaliza kwa kipindi kirefu, lakini maeneo mengine yanadaiwa tangu awalai na kukamilishwa na Serikali yenyewe. Lakini ni ajabu Jimboni kwangu Shule ya Sekondari Kaselya imejengwa na kukamilika kwa muda mrefu (kwa nguvu za wananchi), lakini pamoja na juhudi hizo, Serikali imekaa kimya bila kuweka nguvu zake, haieleweki ni kwa zababu zipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho, basi anieleze ni sababu zipi zinazofanya Serikali kutokuunga mkono juhudi hizo za wananchi ambapo wamekamilisha madarasa mawili, jengo la utawala na nyumba moja ya Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini inapoanzishwa Shule mpya ya Sekondari bado ulezi unatolewa kwa Shule za Sekondari iliyo karibu ili kuhudumia ile mpya? Hii ikiwa ni pamoja na fedha zote zinazohusu maendeleo ya Shule hiyo mpya. Huo wote ni urasimu na unaleta ubadhirifu na hata ucheleweshaji wa kazi yenyewe. Hivyo basi,

utaratibu urekebishwe, fedha zipelekwe moja kwa moja kwa Bodi ya Shule iliyochaguliwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba *Head Master/Miisstress* wasipewe madaraka makubwa na maamuzi kwa kila jambo likiwemo la matumizi ya Shule, kwani mara zote maamuzi yao sio endelevu na yanayolenga maslahi binafsi. Mfano ni *Head Master* wa Sekondari ya Kizaga ambaye amefuja fedha za ujenzi wa Shule zikiwemo za mabweni ya wasichana. Fedha hizi zilikuwa za wafadhili wa Japan. Kadhalika alikula fedha zilizotolewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa kiasi cha Sh. 500,000/=. Mwalimu huyu hakuna hatua zozote zilizochukuliwa za kinidhamu dhidi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hilo, *Head Master* huyo bila aibu ameanzisha Shule ya Sekondari binafsi umbali wa kilometa mbili kutoka ile ya Serikali, hivyo yeye na wenzake kupora wanafunzi kuingia Shule yake iitwayo *EDCOM* Sekondari na hivi sasa yupo mbioni kukamilisha taratibu za usajili wa Shule yake binafsi. Inasadikika fedha za kuanzisha Sekondari hiyo binafsi ni zile zinazotokana na michango ya wapiga kura wangu wa Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipewe ufanuzi juu ya hatua ambazo Wizara imezichukua kwa Mwalimu huyu. Kadhalika wapiga kura wangu hawako tayari kuona Shule binafsi ya Sekondari inafunguliwa ubavuni mwa ile ya Serikali huku aliyefanya hivyo wakiwa wanamwona na ni mtumishi wa umma. Kitendo hicho hakitavumiliwa na kamwe hatutaki kuona Shule hiyo ikiendelea na kupata usajili ndani ya Jimbo langu la Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu fika umuhimu wa elimu na hata uhaba wa Shule za Sekondari ndani ya Jimbo langu la Uchaguzi, lakini hatupo tayari kwa Shule ya aina hiyo ambayo inaonyesha uhalifu wake ukibarikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari Kizaga, Shelui, Ndago, Kisiriri, zipewe umeme kwani zote zipo kwenye *grid* ya Taifa. Kadhalika zikamilishwe kujengewa Maabara yenye vifaa vyote na sio Maabara kwa jina kama ilivyo sasa. Namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake aeleze bayana ni lini kazi hiyo itakamilika ili sasa watoto wetu wapate elimu bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa Walimu wa Shule za Msingi, Walimu, wanafunzi wanaochukuliwa wasianzie mwaka 2002 tu, bali ianzie mwaka 1995, kwani umri wao bado unaruhusu na bado taaluma wanayo. Naomba nipewe ufafanuzi. Naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wote wawili kwa hotuba yao nzuri ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuchukua fursa hii kupongeza mafanikio ya *MMEM* kama yaliyoainishwa kwenye hotuba na kama ilivyoainishwa na Kitabu cha *Poverty and Human Development Report 2003/2005* ambayo inaonyesha kwamba *Primary Net Enrollment Reform* imeongezeka toka asilimia 59 mwaka 2000 mpaka asilimia 90 mwaka 2003 *target* ikiwa ni asilimia 100 mwaka 2010. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo ya *Enrolment Reform* hali ya matokeo ya kufeli Darasa la Saba (*PSLE – Primary School Leaving Examination)* imekuwa ni ndogo sana kwa mujibu wa ripoti husika licha ya kwamba zaidi ya asilimia 85 ya watoto wenye umri wa kuanza Shule wanaanza Shule, ni asilimia 70 tu wanaofika Darasa la Saba na asilimia 20 tu wanaofanikiwa kuingia Kidato cha kwanza na katika hao ni asilimia 12 tu wenye umri wa kuingia Sekondari *(i.e. only 12% of the relevant age group entered Secondary School)* ndio wanaopata fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa kuangaliwa ni kwa kiasi gani kunakuwa na uwiano kati ya watoto wanaoingia Darasa la Kwanza, wanaomaliza Darasa la Saba na wanaoingia Sekondari. Hatuwezi kusema tumefanikiwa kwenye elimu wakati asilimia 90 wanaanza Darasa la Kwanza, asilimia 22 wanaingia Sekondari (kati ya hao ni asilimia 12 ya vijana/watoto wenye umri wa kuanza Sekondari wanaingia Kidato cha kwanza). Ningependa kufahamu mkakati wa Serikali kuhakikishwa kwamba Umbwe huu unazibwa au kupunguzwa japo kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa hivi karibuni (hii ni kwa mujibu wa ripoti tajwa hapo juu) inaonyesha kwamba *Curriculum* nyingi tulizonazo zimepitwa na wakati na haziendani na dunia ya sasa ya utandawazi. Inasemekana kwamba hali hii imeathiri sana soko la ajira kwa vijana wetu wa Tanzania ambao wanajikuta wakishindwa katika usaili *(interviews)* mbalimbali kutokana na kutokuwa na *general knowledge,* kukosa utaalam katika uchambuzi wa mambo na utatuzi wa matatizo *(Analytical and Problem Solving Skills, Entrepreneurships)* na elimu ya teknolojia ya habari *(Education and Information Technology Competence).* Kwa msingi huo, ningependa kufafanuliwa, Serikali ina mango gani wa kuboresha mitaala ya Shule za Serikali ili kuwajengea uwezo vijana wetu kuweza kupambana na soko la ajira ambalo linazidi kuwa gumu kutokana na mfumo wa Soko Huria?

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa tunajivunia mafanikio yaliyopatikana, Shule za Msingi hali inaonekana kuwa mbaya sana. Kwa Shule za Sekondari (hii ni kwa mujibu wa ripoti ya Mkukuta ya mwaka 2005 *(National Strategy for Growth and Reduction of Povert (NSGRP 2005))*

Kama nilivyoainisha, ni asilimia 12 ya watoto wanaoingia Sekondari. Kati ya wanafunzi watatu ambao wako Kidato cha Sita ni mmoja tu ambaye ni mtoto wa kike *(only one in three students is female)* na kwa mujibu wa ripoti, inazidi kuwa mbaya tokea mwisho wa miaka ya 1990.

Ninependa kufahamu, kuna mikakati gani maalum kwa Wizara kuhakikisha kwamba *gap* lililopo biana ya wanafuni wa kike na wa kiume inapunguzwa? Huo ndio mchango wangu kwa uchache. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote wawili na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoanza kuifanya katika kipindi kifupi cha Uongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kwa maelezo katika maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ujenzi wa vyumba vya madarasa mwaka 2005/2006 Serikali lilitoa ruzuku kwa ujenzi wa vyumba 2,692 vy madarasa kwa mwaka 2006/2007 kiasi hicho cha ruzuku kimepungua kwa ujenzi wa vyumba 860 tu. Je, hii inatokana na utafiti sahihi wa mahitaji ya vyumba au ni kutokana na ufinyu wa Bajeti?

Pili, hivyo hivyo, kama ujenzi wa vyumba vya madarasa kupungua, nyumba za Walimu pia zimepungua toka mwaka 1956 mwaka 2006 hadi 500 mwaka 2007, punguzo la zaidi ya nyumba 1,356; Je, hii nayo inatokana na kupungua kwa mahitaji ya nyumba za Walimu? Sidhani kwamba hilo ni sahihi hasa ukilinganisha na ongezeko la Shule za Msingi na Ongezeko la idadi ya Walimu Shule za Msingi. Ni vyema wananchi wakajua sababu ili wasije wakadhani kazi imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Shule mpya ya Msingi kati ya mwaka 2005 na 2006, Shule mpya 443 za Msingi zilijengwa. Lengo kwa mwaka 2006/2007, hakuna mpango wa ujenzi wa Shule mpya hata moja. Sidhani itakuwa sawa, hasa kwa kuzingatia kwamba, bado watoto wengi wanatembea mwendo mrefu kufuata Shule ya Msingi ilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado vipo Vijiji vingi vinaendelea kuandikishwa mwaka 2006/2007 na Vijiji hivyo vitahitaji Shule zao mpya. Bado kuna msongamano mkubwa katika Shule hasa za Mijini na hivyo kuhitaji Shule mpya. Zipo Wilaya mpya zimeundwa mwaka 2005/2006 na zitahitaji ongezeko la Shule mpya. Kwa kuzingatia hayo, ni muhimu Wizara ikatenga fedha kwa ujenzi wa Shule mpya badala ya kuegemeza jukumu hilo kwa wananchi peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko la ujenzi wa Shule za Sekondari mwaka 1945, mwaka 2005 hadi 2,289 mwaka 2006 ongezeko la Shule 544.

Hata hivyo, Serikali imefungua Shule za Sekondari 488 hadi Mei, 2006 katika Mikoa yote. Tangu mwaka 2002 – 2005 nimekuwa nikilalamika kwamba Wilaya ya Muheza haina hata Shule moja ya Sekondari ya Serikali Wizara imekuwa ikiitikia kilio hicho bila ya kujali kutekeleza ombi langu kwa muda wote licha pia ya kujenga Shule 488 Mikoa yote. Je, Mkoa wa Tanga umepata Shule ngapi na zipi? Kwa nini Wilaya ya Muheza haikupewa hata Shule moja?

Hivyo hivyo, ndiyo fadhila kwa Wilaya ya Muheza ambayo ndiyo iliyokuwa na Shule ya kwanza hapa nchini na kutoa wasomi na Walimu wengi kitaifa? Ni matumaini yangu kwamba Wizara hii kwa Awamu hii ya Nne itasikia na kutekeleza kilio cha Wilaya ya Muheza na Wilaya mpya ya Mkinga iliyokuwa ndani ya Wilaya ya Muheza juu ya kuomba Shule ya Sekondari ya Serikali.

Mwaka 2005/2006 Serikali ilijenga Maabara nane katika Shule za Sekondari za wananchi kati ya zaidi ya Shule 2000 ambazo bado hazina Maabara. Mwaka wa Fedha 2006/2007 Serikali inamalizia ujenzi wa Maabara tatu tu, Mangaka, Tuyonga na Kilangalanga. Kiasi hiki cha sifuri hakiridhishi ukilinganisha na idadi ya Shule zilizopo ambazo hazina Maabara. Serikali na Wizara ione upungufu huu kubwa na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa matumizi ya fedha za *MMES*, uamuzi wa Wizara ya Elimu kuondoa usimamizi wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa madarasa kutoka kwenye Kamati za Ujenzi wa Shule za wananchi na kukabidhi majukumu hayo kwa Halmashauri, kumewakatisha tamaa wananchi? Hawana mamlaka na fedha hizo, hawapewi tathmini ya gharama za vifaa vinavyoletwa, vifaa havikabidhiwi ipasavyo kwa Kamati za Ujenzi, vifaa vinapopungua kukamilisha kazi, wanajibiwa kwa ufupi tu, fedha zenu zimekwisha. Gharama za kusafirisha vifaa kwenda Vijiji zinazokuzwa na hivyo fedha kutotosheleza na wananchi hawana kauli na fedha hizo.

Ni wakati gani na hatua gani ya ujenzi, msaada wa fedha unahitajika? Ni jambo muhimu. Mara nyingi wananchi wanakuwa na tofali za kutosha, mchanga mawe na hata kokoto, lakini hawana sementi, mifuko 200 ya kuweka jamvi na kujengea. Majengo mengi yanasimama hapo. Fedha za *MMES* zitatolewa, wakifikisha jengo kwenye lenta. Tutoe fedha katika hatua hiyo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshimia na taadhima napenda kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mwalimu anapohamishwa kutoka Wilaya hadi Wilaya nyingine au Mkoa hadi Mkoa mwingine, Mwalimu huyu analipwa kiwango ambacho kimepitwa na wakati. Kiwango hiki ni kidogo mno. Mwalimu anapohamishwa analipwa kiwango cha mizigo cha tani moja na nusu, kwa wakati huu hakuna Mwalimu ambaye ana mizigo ya tani moja na nuzu, kiwango cha chini ni tani tano na wengine hata ziadi ya hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na malipo madogo ya kusafirisha mizigo, wengine huviacha vyombo vyao pale wanapohamishwa na huwafanya wakanunue vyombo vingine kitu ambacho kinaongeza ukata na ukali wa maisha ya Mwalimu.

Baadhi ya Walimu hugoma kuhama kutokana na adha ya kupoteza vyombo vyao kutokana na fedha ndogo ya kusafirishia mizigo. Wengine pia huziacha familia zao na kuhama bila familia na huko aendako akaanze maisha mapya na familia nyingine bila kupenda na matokeo yake ni gonjwa hatari la Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na karne hii ya sayansi na teknolojia, masomo ya Hisabati, Sayansi na lugha, yapewe kipaumbele. Nikizungumzia kuhusu

lugha, zaidi napenda kuzungumzia lugha ya Kiingerza. Wanafunzi wetu wanapoanza Kidato cha Kwanza, wanapata taabu ya kuzungumza na kuiandika lugha hii ya Kiingerza. Lugha ya Kiingereza ni muhimu katika kuchota hazina ya elimu iliyomo katika mtandao wa *internet* ambapo asilimia 90 ya tovuti zote zinatumia lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ruzuku kwa Shule za binafsi, kwa kweli mzazi anapoamua kumpeleka mtoto wake katika Shule binafsi, ni kuwa uwezo wa kumlipia anao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, naomba ruzuku hiyo, kama ipo, isitolewe kwa wanafunzi wa Shule binafsi. Fedha hizi zielekezwe kwa wale watoto ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwalipia Shule za Sekondari ili waweze kuendelea na masomo hadi watakapomaliza Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Shule zinakaa muda mrefu bila kukaguliwa na kupelekea hata Walimu wa Shule hizo kujisahau kuhusu uwajibikaji wao. Naomba Wizara ihakikishe angalau kila muhula Shule zinakaguliwa ili mapungufu yatakayoonekana yatafanyiwa kazi kwa wakati na taaluma itaweza kuimarika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia maoni machache kwenye hoja hii kwa sababu ya imani yangu na hakika ukweli kwamba elimu ndio ufunguo wa mlango utakaotuingiza katika ile nchi ya ahadi, nchi inayotawaliwa na uelewa, nchi yenye maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ambayo Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Sitta ameiwasilisha kwa umahiri, ufasaha na kwa muda aliopangiwa na hakika alimaliza hotuba yake kabla ya kengele ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika hoja hii utajikita zaidi kwenye elimu ya Sekondari nchini. Elimu ya Sekondari ni pana. Hivyo basi, nitachangia leo kwenye suala la Maabara ya Shule zetu za Sekondari, hasa Sekondari zilizoanzishwa kwa juhudi za wananchi na hatimaye kuendeshwa na Serikali katika kujenga Shule hizi katika Jimbo la Rungwe Mashariki na hakika Wilaya nzima ya Rungwe, wananchi wamejenga Maabara au niseme nyumba za Maabara. Baada ya kujenga, haitegemewi wananchi na Kamati zao, hata wakipata *layout* za ndani za Maabara, au hata orodha ya vifaa wakaweza hata kwa msaada wa Walimu wenye taaluma wakaweza kukamilisha Maabara hizi. Katika moja ya mambo muhimu ambayo msaada (hakika wajibu) wa Serikali unahitajika ni ujenzi na pale nyumba zimejengwa na kukamilisha Maabara. Baada ya kuzungumzia suala hili, ushauri tunaopewa ni kwamba Mamlaka ya Elimu Tanzania unaweza kusaidia. Lakini fikiria Shule zilizo Vijijini, kilometa hamsini na zaidi toka Makao Makuu ambako hata mawasiliano ni shida, waweze wakajua halafu kufuatilia uwezekano huo. Kwetu sisi tunaamini hili ni jukumu la Wizara na Serikali moja kwa moja. Kama tulivyochukulia changamoto ya upungufu wa Walimu, tunahitaji mpango kabambe au programu mahsusi ya ujenzi na ukamilishaji wa Maabara.

Hili ni vyema tukalivalia njuga kitaifa. Katika uliwengu ambao tumo na dunia tunayokwenda ya ushindani bila msingi wa masomo ya sayansi, tutapata matatizo makubwa. Kuna wakati Benki ya Maendeleao ya Afrika itasidia ujenzi wa Maabara. Tunahitaji mpango huo na uhakika mkubwa zaidi ya huo kuhusu Maabara za Shule za Sekondari.

Mwisho, nina ambi moja kwa niaba ya wananchi wa Rungwe Mashariki ili wao pia wasaidie Taifa kuendeleza elimu. Shule ya Sekondari ya Ntaba ina eneo kubwa, wamehamasika kujenga majengo ya zaidi ili kuanzisha Kidato cha Tano na cha Sita. Tunaomba Wizara ikubaliane na ombi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Viongozi wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Elimu. Tusaidiane kuzifanya Taasisi, Shule za Sekondari na Shule za Msingi, Vyuo vya Ualimu ili sehemu ziwe Vituo vya Mazingira na Upandaji Miti. Ahsante.

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi kwa hotuba nzuri sana ambayo imegusa kila kona ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama takwimu zinavyoonyesha, ni kwamba Wilaya ya Ulanga inaongoza kwa mdondoko katika Mkoa wa Morogoro (2004/2005 – wanafunzi 124) mwaka 2005/2006 hadi Juni, wanafunzi 90 kwa Mkoa wa Morogoro na 45 ni kutoka Wilaya ya Ulanga. Hali halisi ndiyo ilivyo.

Mheshimiwa Waziri, naomba kufikiriwa kupewa bweni katika Shule ya Sekondari Ilonga ambayo ipo pembezoni mwa Wilaya, Shule hiyo iko mpakani mwa Wilaya ya Liwale Mkoani Lindi. Shule hiyo itahudumiwa Kata nane. Pia, mazingira ya Shule hiyo, wanafunzi wanatembea umbali mrefu kufika Shuleni. Hadi sasa wananchi wamejenga madarasa matatu jengo la utawala na wameshafyatua matofali laki tatu kwa ajili ya ujenzi wa mabweni matatu ya kuanzia. Nitashukuru iwapo tutasaidiwa kuongezwa nguvu ili tupate kujenga mabweni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa ajili ya Maafisa Elimu wa Wilaya na Maafisa Elimu wa Kata, kama nilivyotangulia kusema, Wilaya ya Ulanga ni kati ya Wilaya zenye mazingira magumu, hata Walimu huwa hawapendi kupangiwa huko. Ukiangalia ukurasa wa 50, mafunzo kwa Maafsia Elimu wa Wilaya, Wilaya ya Ulanga haipo. Pia, ukurasa wa 52, mafunzo kwa Maafisa Elimu wa Kata (Mratibu) Wilaya ya Ulanga pia haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya motisha kwa wafanyakazi walioajiriwa kwenye Wilaya zenye mazingira magumu, naomba Wilaya ya Ulanga iwekwe kwenye orodha ya ukurasa wa 50 na 52. Naomba kuwasilisha.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimwia Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba Walimu kwenye Shule ya Sekondari ya Igalula hususan Walimu wa Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimweleza Mheshimiwa Waziri sio mara moja, naomba leo anipe maelezo ni vipi Walimu watapatikana ili wananchi waone umuhimu wa kuanza Shule hiyo. Tusikatishe tamaa wananchi kwa Shule walizojitolea kujenga majengo hayo sehemu za Vijijini, ni suala la kufa na kupona kuwa na majengo na kuwa na Walimu. La sivyo, yatakaa magofu, kwani wanafunzi hawawezi kuvulika kwenda Shule na kwenda kucheza tu. Uone tofauti iliyoko kati ya Shule za Mjini na Vijijini. Hotuba ni nzuri sana hasa nikiona ni mara yake kuandaa hotuba ya Bajeti, lakini yeye ni Mwalimu, sishangai sana kuona hayo aliyoyafanya. Naomba jibu la Walimu kwenye Shule ya Igalula.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia machache katika hoja hii. Lakini kabla sijaanza kuchangia, nichukue fursa hii awali ya yote kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza na Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa ujumla kwa kuandaa hotuba nzuri sana. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kuiomba Serikali iharakishe kulipa malimbikizo ya madai mbalimbali ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ambayoyamekuwepo kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamekuwa wakichangia, kuchelewesha malipo haya ni kuwavunja moyo Walimu wetu, matokeo yake ni kuathiri ubora wa elimu wanayoitoa kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kielelezo cha malimbikizo ya madai ya Walimu wa Shule ya Msingi katika nchi yetu ni yale ya Wilaya ya Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ya Sengerema ina malimbikizo yanayofikia kiasi cha Sh.256,191,509/= ambayo uchanganuzi wake ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Posho ya usumbufu | Sh. 27,859,188.00 |
| (ii) | Posho ya Kujikimu | Sh.115,629,049.00 |
| (iii) | Masomo | Sh. 42,984,996.00 |
| (iv) | Matibabu | Sh. 33,866,642.00 |
| (v) | Likizo | Sh. 742,850.00 |
| (vi) | Ajira mpya | Sh. 26,265,000.00 |
| | **Jumla** | **Sh.256,191,509.00** |

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Walimu wa Shule za Msingi wako chini ya TAMISEMI, naiomba Wizara hii ifuatilie haraka iwezekanavyo kwa kushirikina na TAMISEMI pamoja na Hazina ili malimbikizo haya yalipwe. Barua zote na taarifa zote zinazohitajika katika madai haya, zilishawasilishwa TAMISEMI kwa utekelezaji tangu mwaka 2005. Cha kusikitisha ni kwa nafasi yangu, nimekuwa nafuatilia pale

Hazina bila mafanikio. Tafadhali namwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko leo kwamba, ni lini madai hayo yatalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninalopenda kuchangia ni ombi kwa Wizara hii. Jimbo langu la Sengerema tunaiomba Wizara hii itusaidie fedha kwa ajili ya kumalizia maboma mawili ya vyumba vya madarasa ya Shule za Sekodanri za Kata ili tuweze kukamilisha na kuwasajili wanafunzi 80 waliofaulu, lakini hawakupata nafasi ya kuendelea Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukimalizia kuwapeleka Sekondari vijana hawa 80, sisi Wilaya ya Sengerema tutakuwa tumetimiza lengo la asilimia 100 kwa kupeleka watoto Sekondari kwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia zote.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Bajeti yake iliyoandikwa na kuwasilishwa kwa umahiri wa pekee. Nawapa hongera pia Naibu Waziri, Mwantumu Mahiza na Naibu Waziri Ludovick Mwananzila na Katibu Mkuu, Prof. Hamis O. Dihenga. Hotuba iliyowasilishwa ni nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa hatua ya kijasiri ya kupunguza tatizo la Walimu katika Shule za Sekondari. Hatua hizi, pamoja na *programme* ya kuwasomesha Walimu kwa mwezi mmoja na kuwapeleka Shuleni ni hatua nzuri ya kuondoa uhaba wa Walimu. Hatua ya Wizara kuwasomesha Walimu hawa kwa *distance learning* kupitia Chuo Kikuu Huria, ni mpango mzuri sana. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Mei, 2005, Mheshimiwa Waziri wa Elimu wa wakati ule (Mheshimiwa Joseph Mungai) alikuwa mgeni rasmi katika Tamasha la Kuchangi Ujenzi wa Shule katika Wilaya ya Mwanga. Katika Tamasha letu, Mheshimiwa Waziri aliahidi kusaidiana na wananchi wa Mwanga katika kuendeleza Shule ya Sekondari ya Nyerere iliyoko Lembeni, Mwanga kuwa na Kidato cha Tano na Sita. Aliahidi kuwa wananchi wakiwa tayari, Wizara itachangia madarasa mawili na Hosteli ya wasichana na wavulana wa *Form Five* na *Six*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hatua hiyo, Halmashauri ya Wilaya ilichukua hatua ya kupima eneo la Shule, kuchora ramani na kukamilisha zoezi hilo. Baada ya zoezi hili, Halmashauri imepeleka maombi rasmi ya kuomba Wizara iruhusu Shule ya Sekondari Nyerere iendelezwe ili kufikia Kidato cha Tano na Sita.

Nichukue fursa hii sasa, naomba kwa heshima na taadhima kuwa Wizara ipokee ombi letu na isaidiane na Halmashauri yetu kuendeleza Shule yetu. Aidha, tunaiomba Wizara sasa itekeleze ahadi yake. Shule ina eneo la hekta 90. Inafikika kwa barabara ya lami na huduma ya maji ndiyo inayohitaji iimarishwe. Ahsante sana.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninasema naunga mkono hoja. Aidha, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Manaibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya hadi kuleta hoja hii nzuri ndani ya Bunge lako Tukufu. Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ni nzuri na inawapa matumani Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni mdogo tu, nao unahusu Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mkoa wa Shinyanga na husuan Wilaya ya Kahama. Wilaya ya Kahama yenye watu karibu 700,000, una Shule za Sekondari zisizozidi 20. Kufuatilia *program* ya ujenzi wa Sekondari inayoendelea hivi sasa ambapo kila Kata inatakiwa kujenga Shule mbili za Sekondari, kwa maana nyingine ni kwamba, hadi kufikia Desemba 31,2006 Wilaya ya Kahama itakuwa na Shule ya Sekondari 68. Tatizo kubwa lililoko mbele yetu ni Walimu, ujenzi wa Sekondari nyingi unaendelea Wilayani hivi hauendi sambamba na idadi ya Walimu wanaoajiriwa? Hili ni tatizo kubwa! Bila ya kutatua bado Mkoa wa Shinyanga utaendelea kubaki nyuma katika maendeleo ya elimu. Kama hali hii itaendelea, kutakuwa na Shule nyingi za Sekondari, watoto wengi lakini hawana Walimu.

Pia tatizo kubwa ambalo linakwenda sambamba na hilo la kwanza ni Laboratories ujenzi unaeondelea katika Shule karibu zote hivi sasa ni wa madarasa na nyjmba za walimu tu. Hivyo ni maon yangu kwamba ni muhimu kwa Serikali kuchangia au kusaidia jitihada za wananchi kwa Serikali kujenga Laboratories katika Shule zote zinazoendela kujengwa.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni msingi wa maendeleo na adui mkubwa wa ujinga, maradhi na umaskini. Tukielimika na tukiwa na elimu bora, tutajenga Taifa bora na lenye uwezo wa kuendesha nchi yetu kwa misingi iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa elimu bora hauji tu kwa dhana, bali ni kuwa na nyenzo muhimu ya kwanza ambayo ni Walimu. Walimu bado ni tatizo sugu, hawatoshi kulinganisha na idadi ya wanafunzi, Walimu wenyewe pamoja na uhaba, bado wanafundisha katika mazingira magumu, mishahara midogo hata nyumba za kuishi hawana, hata vitabu vya kufundishia havitoshi. Ni budi Wizara itatue tatizo la Walimu ili tupate Walimu bora ili kupata mwanafunzi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi anahitaji mahali pazuri ili kupata elimu. La kushangaza, madarasa hayatoshi, madawati hayatoshi, mwanafunzi anakaa chini na vitabu vyenyewe havitoshi kwa mwanafunzi. Ni bora kuyaboresha haya ili kupata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la utoro na mimba za utotoni nalo linaathiri elimu kwa vijana wetu kwa hivyo nalo linahitaji kutazamwa kwa mtazamo wa jicho la huruma na wakati huu wa maambukizo ya *HIV/ AIDS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora pamoja na vitabu, majengo mazuri madawati, Walimu, mitaala na mitihani ni kigezo cha kutosha kupata elimu iliyo bora. Kwa hiyo, naomba Maabara ziimarishwe ili kupata elimu kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *MMEM* umefanikiwa kuhamasisha wananchi, idadi ya Shule imeongezeka na wanafunzi wamekuwa wengi zaidi na matokeo yameonekana kuwa mazuri. Ni jambo zuri, ni matarajio yangu kuwa mpango wa *MMES* nao utakuwa tayari kuwapokea wanafunzi wengi waliyoifanya vizuri kutoka kwenye mpango *MMEM.* Kwa hiyo, naiomba Serikali mpango huu uende sanjari ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ijitahidi kuviendeleza Vyuo vyote vya Walimu na Vyuo vya Ufundi ili kufikiwa lengo la madhumuni ya Wizara. Ahsante.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri yenye umahiri mkubwa na mchanganuo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Nianze kwa kuchangia katika kitabu cha hotuba ukurasa 55-55. Nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kuitambua *TEWW* na kupanga mipango mizuri ya kusaidia Taasisi hii ili iweze kujitosheleza na angalau kuifufua, katika kipindi kilichopita kwa kweli hawakuweza kupewa ruzuku ya kutosheleza mahitaji ya kuendeleza masomo hayo ambayo yako chini yake.

Kwa kiasi kikubwa, wao kwa kweli wametoa huduma chini ya Serikali ingawa limeitwa Shirika, kwa kweli katika Mashirika yanayofanya kazi katika mazingira magumu ambayo hawana majengo wala usafiri ingawa wako nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuishauri Serikali iangalie upya mgao wa ruzuku ili angalau aweze kuwalipa Walimu wa *part time* kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ukiangalia ada zao ni kama za Serikali, kwani hawawezi kuongeza zaidi ya Sh.20,000/= kwa kusomesha wanafunzi ambao wapo kwenye mpango na wale wazazi wao hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie upya kwa kuleta mitambo mipya ya uchapishaji ili waende na wakati kutenga fungu maalum kwa Walimu wanaosahihisha masomo hayo. Kuendelea kutoa elimu hiyo, kuna matangazo ndani ya Vyombo vya Habari, kama hawatapewa fedha za kutosha itakuwa vigumu kujiendesha na kukamilisha matakwa ya kutoa elimu hiyo kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isiadie kuitangaza Taasisi *(TEWW)* katika Wizara mabazo zina watumishi ambao wako chini ya mahitaji ya elimu kwa

kufikia Kidato cha IV angalau kwa kufungua madarasa maalum na kuruhusu wafanyakazi hao kwa zamu kuliko ilivyo sasa.

Mhshimiwa Naibu Spika, kumeruhusu wanafunzi hao kusoma kwenye madarasa yaliyopo kwenye maeneo hayo, hususani Vijijini ambako *TEWW* haiwezi kukodi vyumba vya kusomea kwani ikumbukwe kwamba wako chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Vituo (wakufunzi) na Taasisi hii hao wapewe vitendea kazi, kama vile *computer*, magari ili kurahisisha mawasiliano na Vijijini, kwa nini idadi ya magari matano hayawezi kukidhi mahitaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia magari yaliyopo hivi sasa ndani ya *TEWW* yauzwe ili fedha itakayopatikana iongezewe ununuzi wa magari mapya. Hata baadhi ya vifaa muhimu ambavyo havitumiki na angalau vina hali nzuri, ni vyema vikauzwa kama vile Vifaa vya mashirika, meza, viti, vilivyokaa muda mrefu imekuwa kama uchafu katika maeneo mengi hata magari yaliyopo kwenye mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TEWW* ikiandaliwa vyema, itasaidia kufuta ujinga au kutokomeza kabisa masuala ya Watoto wa Mitaani katuoakana na wazazi wao kutokuwa na uwezo na kuwaacha tu na kukata tamaa ya watoto kwenda Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TEWW* ipewe majukumu ya kuendesha mafunzo ya Wlaimu kama walivyoweza kufundisha *UPE* kwa miaka ya nyuma ambapo waliweza kusimamia vizuri na ndio wengi wao waliopo, uzoefu huo wanao ili kuondoa tatizo la upungufu wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iangalie uwezekano wa kutatua tatizo la Walimu wa Shule za awali, kwani kuna upungufu mkubwa kiasi kwamba wanaofundisha hawana uwezo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Manaibu Mawaziri na Wataalamu wote wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora inazo Shule za zamani kama vile *Tabora Boys School, Tabora Girls School* na Milambo *(St. Marys).* Baadhi ya majengo ya Shule hizi yamechoka sana na huduma zifuatazo haziridhishi. Upungufu wa maji safi na salama kwa wanafunzi na Walimu. Upungufu wa Walimu wenye sifa, upungufu wa vitabu vya marejeo katika Maktaba, upungufu wa nyumba za Walimu hasa Milambo, kutokuwa na ukuta wa ulinzi hasa Milambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri hatua za haraka zichukuliwe kutatua matatizo haya. Aidha, fedha zitengwe kwa ajili ya kuchimba visima virefu katika Shule hizi. Matatizo niliyoyataja hapo juu, yanazikabili Shule nyingine za Sekondari na za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ucheleweshaji wa malipo kwa Wazabuni wa Vyakula na huduma nyingine katika Shule zetu. Nashauri Wizara iharakishe malipo ya

nyuma ili wanafunzi wasije kuathirika kwa kukosa huduma muhimu za Wazabuni za vyakula na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zinafanywa kuwahimiza wananchi kushiriki katika ujenzi wa Sekondari kila Kata. Wananchi wanaitikia wito huu angalu kwa kasi toafuti baini ya Kata na Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara iwe tayari kutoa sehemu ya mchango wa Serikali kwa kasi kubwa kuliko ilivyo sasa kila inapohitajika kufanya hivyo. Utaratibu wa sasa una urasimu sana. Tupunguze urasimu. Vile vile, upatikanaji wa Walimu na vitendea kazi vingine katika Shule zetu upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa uadilifu wa baadhi ya Walimu na Watendaji katika Wizara kama unavyojidhihirisha katika uvujaji wa mitihani na wanafunzi wasichana kupewa mimba na Walimu wao vinahitaji kupigwa vita kwa nguvu zetu zote. Nashauri adhabu kali zitolewe kwa wahusika katika makosa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kukarabati na kuyasanifu upya majengo ya Chuo cha *VETA* – Tabora. Aidha, naiopongeza pia Serikali kwa kukipanua Chuo hicho na kukipatia mashine/mitambo ya ziada ili Chuo kiweze kutoa mafunzo ya stadi nyingi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu uwe kasi, ari na nguvu mpya. Tuepukane na tabia ya kusuasua katika utekelezaji wa miradi ambayo tayari Serikali imekwishaamua kuitekeleza. Aidha, ni vizuri wanafunzi wanaohitimu katika Vyuo vyote vya *VETA* wawezeshwe kupata vitendea kazi kwa mikopo nafuu ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu spika, baada ya kukihamisha Chuo cha Nyuki Tabora Mjini ninapendekeza/ ninaomba Serikali iyatoe majengo haay kwa Manispaa ya Tabora ili yatumike kama Shule ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja nakuongeza ujenzi wa Maktaba nchini nakuzipatia vitabu. Napendekeza Serikali iweke huduma za *internet* katika Maktaba zetu zote. Elimu nyingi zinapatikana kwa urahisi na haraka zaidi kwa njia ya *internets* kuliko vitabu pekee.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha siku ya leo kufika hapa Bungeni kwa miguu yangu bila kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu ya shukurani sasa naomba nianze kutoa mchango wangu katika Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha fasaha ya mwanadamu, ambaye ana akili timamu Wizara ya Elimu aipe umuhimu wa kuipa jina la sifa "moyo." Maisha ya leo ni elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inapaswa kuipa kipaumbele katika Bajeti ya Serikali. Matatizo yanayowakabili Wizara hii ni makubwa sana na ukiitazama Bajeti yao utakuta hata nusu ya matatizo haiwezekani kutatuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiw Lowassa kwa kutamka hapa Bungeni kuwa elimu yakilimo ndio wizara zilizopewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu pamoja na mahitaji yao kuwa makubwa, lakini ina haki haya walio na uwezo nayo yanaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kama ubora wa elimu, hii kipimo chake ni mitihani. Wizara inapaswa hili walijue na wawe wazi kumpima wanafunzi kupitia huo mtihani, Wizara igundue siri ya kuvuja mitihani. Haki ya kumpima mwanafunzi iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda Wizara inijulishe ni utaratibu gani unaotumika katika kuandaa mitihani Walimu wa *subjets* pamoja na mitaala ya mashuleni Wizara ni msimamizi wa yote haya, lakini sio hivyo inavyofanya. Wizara ikishirikiana na Baraza la Mitihani ni kuandaa mitihani na sio kujua mtahiniwa jinsi alivyofundishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa Kidato cha Nne, mitihani yao ni ya kitaifa kati ya Unguja na Tanzania Bara. Baadhi ya Shule hazina Walimu wa somo ambalo Wizara inapeleka mtihani. Ni nani mwenye makosa? Mwanafunzi ama Wizara? Pemba kuna baadhi ya Shule hadi leo hazina baadhi ya Walimu hasa wa masomo ya Science. Vipi mwanafunzi aukabili mtihani? Wizara itajibu ni lini itahakikisha masomo yote yana Walimu wenye sifa katika mashule zote. Kupasi kwa mwanafunzi kunahitaji Walimu wazuri. Hili likikosekana, Wizara ikubaliane nami ndio mkosa kwa watoto wetu wa kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo kwa wanafunzi, Serikali inafaa kushukuriwa kwa jitihada zake za kumwezesha mtoto wa kimaskini naye kusoma. Pamoja na jitihada hizi, suala kubwa lililopo ni kwa nini Wizara iwatengee wanafunzi maalum mikopo hiyo? Hivyo wanafunzi wengine haki hiyo sio yao. Serikali inajua fika kwamba imeshindwa kukidhi haja ya watoto wa kitanzania kielimu na badala yake Mashirika ama Shule Binafsi ndio inayookoa watoto wetu kielimu. Hivyo basi, kwa nini Serikali haiwawezeshi hawa wanaolazimika kujiunga na Shule hizi ambazo ni za malipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa Elimu, Wizara ilipaswa ifahamu na kutoa jibu, watoto wanapofikia Darasa la Saba (Elimu ya Msingi) kuwa ni elimu sio sahihi. Iko haja baada ya Serikali kujua uhaba wa Walimu upo, ndio chachu ya maamuzi

kumfikiria mtoto wa kimaskini kufeli katika elimu ambayo haiwezi kumsaidia hata kuuza pipi dukani. Elimu ya Msingi ingefikiriwa kuboreshwa katika kuongezewa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa Walimu nchini unatokana na nini? Serikali ni lazima ijue na itoe jibu. Ukiangalia kwa wazi, utakaloliona ni Walimu kutopewa umuhimu katika nchi. Ukiangalia Wizara imelijua hili mapema, lakini mpaka leo Walimu pamoja na kazi ngumu zinazowakabili bado posho yao ni ndogo. Sababu hii ndio ikaleta kuwepo kwa uhaba wa Walimu. Kwa ufupi, mazingira yote ya Walimu sio mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuishukuru Serikali kwa jitihada zake za kuazimia kujenga Chuo Kikuu hapa Dodoma. Naitakia Wizara mafanikio mema katika Bajeti yao.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Wataalam wa Wizara na Walimu wote nchini kwa kazi nzuri. Bila kusita, naunga mkono hoja. Nina hoja na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya Ilani ya *"A" Level* wastani wa Shule ngapi za *"O" Level* zitahitaji Sekondari moja ya *"A" Level*?

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Ilani ya CCM utatuwezesha kuwa na angalau Sekondari moja kila Kata. Je, Wizara iko tayari kuzitumia Sekodnari za Kata ziwe Vituo vya kuwaendeleza kielimu Walimu wa Shule za Msingi zinazozunguka Sekondari husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule nyingi za msingi zinajikuta zina wanafunzi wachache wa Darasa la Saba. Je, Serikali iko tayari kuruhusu wahitimu wa Darasa la Saba warudie Darasa hilo katika Shule zenye nafasi kwa utaratibu utakaowekwa na Wizara ili kujaza nafasi zote za Darasa la Saba?

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, Naibu waziri wote wawili, katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzoya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sote tunavyoelewa kuwa Elimu ya Msingi ni ufunguo wa kila kitu, bila elimu hakuna maendeleo, sio kwa mtu mmoja mmoja tu, hata Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi linanigusa sana suala la mitaala ya Shule zetu baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kutofautiana hasa ukizingatia watoto (wanafunzi) wa nchi hii ni wamoja na zaidi ni kwa mitaala tofauti na mtihani ni mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mitaala ya Darasa la Kwanza mpaka la Tano isiwe mmoja (au iwe tofauti)? Darasa la IX – X isiunganishwe wakati wanafunzi wanafanya mtihani mmoja Darasa la XII hili sio sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani utashi wa watu binafsi hapa usitumike tena kuliongoza vibaya Taifa hili au Wizara hizi. Kama ujuavyo, Elimu ya juu ni suala la Muungano kikatiba, hawa wanafunzi watanunuaje mitihani na hata masomo ya darasani wakati viwango vyao sio vya kielimu bali hata wakufunzi (Walimu) wao wanatofautiana kiviwango, mitindo ya kusomesha, Vyuo wanavyojifunzia na kadhalika. Kwa nini Vyuo vya kusomeshea Walimu haviwi vya namna moja au navyo haviunganishwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dhuluma kabisa. Wakati huu dunia inaunganika kiuchumi, sisi Zanzibar tunatawanyika kwa sababu zisizo za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati *EDC*. Tuna mwelekeo wa kuona tunakuwa na kiwango cha pamoja, sisi Tanzania tunatengana. Maombi yangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, suala hili walishughulikie na Waziri mwenzie wa Zanzibar kuona kero hizi zinaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Meshimiwa Waziri ukurasa 53 amesema wanaendesha tafiti za elimu kwa kushirikiana na nchi za Malawi, Zambia na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind-up* anieleze kwa nini Zanzibar hakuitaja?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la mishahara kuchelewa kuwafikia Walimu na kuwa kuna wakati wanafuatilia mishahara na kuacha madarasa. Hili tunaomba lizingatiwe kwa kina, kwani ni mapungufu ambayo yanamgusa mwanafunzi, mtu ambaye hangehusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefikia wapi juu ya madai ya mishahara na *allowance* za nyuma za Walimu na kama bado haijalipwa Wizara inaeleza nini katika hilo? Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupendekeza, Serikali iangalie upya suala hili la uchelewaji wa mishahara hasa kwa Walimu wapya ambao wamekuwa wakikaa hata miezi sita bila mishahara.

Suala hili limekuwa likiwakatisha tamaa Walimu ambapo wengine wameamua kuacha kazi na kwenda katika Shule za Binafsi ambazo ndizo zimekuwa Soko la Walimu wanaoshindwa kuhimili uchelewaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwepo na muundo mzuri ambapo Mwalimu atapata mshahara mara tu baada ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kuhusu Maafisa Elimu Ufundi. Hivi karibuni kumedhihirika kuwa Maafisa Elimu ya Ufundi kwa kweli hawafanyi kazi zao kama inavyostahili, maana imedhihirika kwa kuona hali halisi ya usimamizi mbovu wa majengo mapya ya Shule za Sekondari zilizojengwa kwa nguvu ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Maafisa walioshindwa kufanya kazi yao inavyostahili wachukuliwe hatua kwani kuendelea kuwaachia kutasababisha wananchi kutokuwa na imani na Serikali na pia kuwavunja moyo wa kujitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Margareth Sitta (Waziri wa Elimu) kwa kufanya ziara ya kikazi katika Mkoa wa Shinyanga na kusaidia kuboresha hali nzima ya elimu kutokana na ushauri wa maagizo muhimu aliyoyatoa. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malengo ya mwaka 2006/2007, ukurasa wa 10 kifungu cha 11(c): “Kujenga nyumba za Walimu 500 hasa Vijijini ili kuboresha makazi ya Walimu.” Napenda msukumo uwe kwenye maeneo ya pembezoni mwa nchi, pamoja na Ludewa. Ni vyema Waziri aeleze vigezo anavyotegema kugawa msaada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgao wa *MMES* wa Shule mpya za Sekondari mwaka 2005 fedha ya namna hiyo kwa ajili ya Shule mpya ya Sekondari ya Kayao Shilingi milioni 24.6 zilirudishwa Wizarani baada ya kutumwa kwenye akaunti isiyo ya Shule kule Njombe. Tunaomba fedha hiyo itumwe mara moja kwenye akaunti sahihi ya Shule *NMB* – Ludewa Na. 6503000007 ili kurahisisha upatikanaji wa fedha hii. Nakala ya maandishi iwe inatumwa kwenye *Revenue Office* ya Halmashauri, kuliko kuwasiliana na Mkuu wa Shule tu bila taarifa Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malengo ya mwaka 2006/2007 kifungu cha 21 (g) ukurasa wa 20 “kugharamia elimu ya Sekondari kwa wanafunzi 45,873 wanaotoka … kulipiwa.” Je, hawa wanafunzi wanapatikana kwa utaratibu gani? Fedha hizo zinapatikana vipi? Wilayani Ludewa wanafunzi wa namna hii ni wengi, ningependa kuleta orodha yao wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa elimu wa Mikoa hawna usafiri wa uhakika ukilinganisha na wenzao wa wilaayni. Maafisa hawa wanategemewa wafanye ukaguzi Wilayani, awezeshwe ili wtimize wajibu wao ili wasitoe visingizio vya kukosa usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *High School Form V – VI* pale Ulayasi – Ludewa imejengwa na wananchi na kusaidiwa na Kanisa la Katoliki. Mwaka 2005 wanafunzi waliopangwa Shule hiyo hawakusoma kwa kukosa Walimu. Mwaka huu wa 2006 wanafunzi wameletwa, lakini tatizo la Walimu *(graduates)* liko pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika tunaomba mchepuo wa *Arts* ili wenyeji wapate fursa ya kupeleka watoto wao hapo. Kwa ukosefu wa Maabara katika *Form I – IV* vijana wa Ludewa hawategemewi kufaulu masomo ya sana na kungia *Form V* Ulayas. Matokeo yake, Shule inajaa wageni kutoka nje ya Ludewa na wananchi hawaoni faida ya kujenga Shule ile. Tusaidiwe mchepuo wa sanaa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii pamoja na kutoa mchango wangu kwenye Bajeti hii kwa kuzungumza. Napenda kukazia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wamekuwa wakiwajibika sehemu nyingi mfano TAMISEMI, UTUMISHI, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kadhalika. Hali ambayo inawachanganya sana Walimu hususan pale chombo chao *TSC* kilipoondolewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kupelekwa Tume ya Utumishi wa Umma na kupewa jina la *TSD,* yaani Idara ya Huduma kwa Walimu. Hali hii inaweza kuwapotezea Walimu *scale* zao na kutopanda madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, chombo hiki kiwe chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambako ndiko Walimu waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ina Watumishi wa Idara ama Taasisi mbalimbali wenye majukumu yanayotofautiana na muda wa kufanya kazi mfano Idara nyingi kufanya kazi kwa muda wa saa za kazi na kurejea makwao kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wamekuwa na majukumu mazito sana ya utendaji kazi, kwani hufanya kazi kwenye Vituo vyao kwa muda wa saa za Serikali huhamishia Ofisi zao nyumbani kwenda kusahihisha daftari za wanafunzi, kuandaa masomo ya kesho na kutengeneza zana za kufundishia kwa gharama zao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulinga na uzito huu wa kazi na gharama za ziada, naishauri Serikali iwarudishie Walimu fedha/posho za kufundishia *(teaching allowance)* kama ilivyokuwa zamani, yaani asilimia 50 ya mishahaya yao ili iwe motisha na changamoto ya kuipenda kazi yao na kuiacha tabia ya kuacha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ihakikishe kuwa kila Shule ya Sekondari ambayo haina umeme ipewe *generator* kwa matumizi ya Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, napenda kurudia tena kuwa naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja nikisubiri kwa hamu majibu ya Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yake.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja kwa kuandika. Mimi binafsi naunga mkono hotuba, ni nzuri. Nawapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Manaibu wake wote wawili.

Kuhusu Walimu wa Vijijini Amko barabara hipitiki na kuwafanya Walimu kutembea kwa miguu kwa muda mrefu kuja Wilayani kuchukua mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wanakosa kusomesha mpaka warudi Vijijini kwenye Shule, wanafanya wanafunzi kukosa masomo. Naomba Serikali kuliangalia hilo. Kuhusu Wakaguzi kwenda Vijijini, hawa hawaendi huko, kila mara naomba Wizara kuangalia hilo. Ukaguzi ufanyike mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora haiwezekani kupatikana kwa kupata Walimu wazuri wenye talaaluma, tuwe na madarasa mazuri, uhaba wa Walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu michezo mashuleni, napongeza mpango huu umerudishwa, nasisitiza mpango usisitizwe Vijijini ambako wanafunzi wanajali sana michezo kwa kuwa kwao mpira ni kama ndoto. Naomba sana. Michezo Vijijini ni muhimu zaidi.

Mhshimiwa Naibu Spika, kuhusu *drop out* (mdondoko) tatizo hili liko sana Mkoa wa Lindi. Naomba Wizara ilichukulie hatua kali kutokana na swali hili. Mafunzo yatolewe kwa wanafunzi na wazazi asilimia kubwa ya mndokoko ni wanafunzi wa kike. Naomba tuliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mpango wa kufundisha somo la *HIV/AIDS (PASHA)*. Mafunzo hayo ni mazuri na yananusuru Taifa letu hili lijalo. Ushauri nasaha unapatikana kwa wanafunzi wetu. Naomba kuwe na somo maalum kwa wanafunzi mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza miradi yote miwili ya *MMEM* na *MMES*. Kwenye *MMEM* tumefanya vizuri sana, naomba sasa tulenge kwenye Sekondari (*MMES).* Naona kuna upungufu wa Walimu wa Sekondari, Serikali ichukue hatua za haraka ili Sekondari zisikose Walimu wenye taaluma ili elimu bora ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja asilimia mia moja na kazi nzuri wanayoifanya. Ahsante.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza wote kwa kazi nzuri Wizarani, kuanzia Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani za pekee zimwendee Mheshimiwa Mahiza kwa kutembelea Mbulu. Aliona mazingira magumu ya Mbulu, hasa Bonde la Yeyeda, wanakoishi jamii maskini kabisa za wawindaji. Alipofika huko alikumbushwa ahadi mbalimbali za Serikali kwa watu hao na hasa ile ya Waziri aliyetangulia Mheshimiwa Mungai ya kuwa wananchi hao wachangie nguvu zao kuandaa mawe, kokoto na matofali na Serikali itakamilisha kazi ya ujenzi wa shule ya Sekondari katika nchi ya Wahadzabe. Tunaomba ahadi itekelezwe wananchi wametekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira magumu aliyoyaona Mheshimiwa Mahiza, Walimu hawayapendi. Binafsi ninajaribu kuwabembeleza Walimu ambao wanaelekea kupenda kwenda huko, lakini baadhi ya watumishi katika kurugenzi ya Sekondari wamekuwa kikwazo. Kwa mara nyingine nitakabidhi tena majina haya. Naomba msaada wa Viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya fedha za Elimu ya Sekondari ya ujumla, umbali uliopo kati ya Afisa Mhasibu (Katibu Mkuu) na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari inajulikana. Tumepokea kwa furaha nafasi ya Mwakilishi wa Wizara katika ngazi ya Wilaya, lakini iwapo dhamira Wizarani haitabadilika, Mwakilishi huyo hatasaidia. Mara nyingi taarifa za Viongozi na Wakaguzi kuhusu upotevu au matumizi mabaya ya fedha hazikushughulikiwa na Wizara.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Margaret Sitta kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi hasa ninapozingatia kuwa yeye ni Mwenyekiti Mstaafu mwezangu wa Vyama vya Wafanyakazi, yaani alikuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama nikiwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wafanyakazi wa Mawasiliano *[COTWU (T)]*. Namtakia uongozi wa Utumishi uliotukuka.

Aidha, nawapongeza Manaibu wote, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza kwa kuteuliwa kwao, lakini pia kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake wote wawili pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya Hotuba yao ambayo imeandikwa kitaalam sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameupokea vizuri mpango wa *MMES* kama walivyopokea mpango wa *MMEM*. Tatizo kubwa la mpango wa *MMES* ni utekelezaji hasa kutokana na Waraka wa Wizara ambao inasadikiwa unawapa madaraka makubwa Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari kiasi kwamba Walimu Wakuu nao katika ujenzi wa Shule/ madarasa na nyumba za Walimu hawataki kuwashirikisha Kamati ya Ujenzi, Bodi ya Shule na kadhalika.

Mfano ni Sekondari ya Sepuka Wilaya ya Singida Vijijini ambako kuna malumbano makubwa kati ya Mwalimu Mkuu wa Kamati ya Ujenzi pamoja na Bodi ya Shule kwa kutoshirikiana katika suala zima la ujenzi wa darasa na nyumba ya Mwalimu baada ya kupokea Sh. 27,000,000/=. Inasadikiwa kwamba, fedha zimekwisha, lakini madarasa yale mawili na nyumba ya Mwalimu haijamalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri waaraka ufutwe haraka na maelekezo mapya yatolewe yakizingatia suala zima la ushirikishwaji wa wananchi kupitia Kamati ya Ujenzi na Bodi ya Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpano wa *MMES* pia ulilengwa kujenga Shule mpya za Sekondari katika Wilaya ambazo hazina Sekondari za kutosha kama Singida. Shule ya Sekondari ya Wilaya ya Singida ya Serikali ni moja tu ambayo ni Mwenge Sekondari ambayo nayo *mission* wanaitaka irudi kwao ili wafungue Chuo Kikuu. Je, Wilaya ya Singida itajengewa lini Shule mpya ukiachilia mbali hizi Sekodnari?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 64 hadi 68, Mheshimiwa Waziri ameelezea shughuli za Baraza la Mitihani katika kifungu cha 53 ukurasa wa 67. Mheshimiwa Waziri anaeleza bayana kuwa Baraza limefanya kazi, mitihani ya Darasa la VII, Kidato cha Nne, Sita na Ualimu ikiendeshwa bila kuwako uvujaji wa mitihani.

Hata hivyo, baada ya uongozi mpya kuletwa pale hivi karibuni umeingia kwa makeke na kuwaondoa watumishi takribani 35/40. Amewahamisha na wengine kupangiwa kwenda kufundisha mashuleni wakati hawajafanya kazi zaidi ya miaka kumi. Nauliza, kwa nini watumishi wote hao waondolewe kwa pamoja na mara moja? Kosa lao nini? Mbona hawakuambiwa? Kwa nini wasichuliwe hatua kwa mujibu wa Sheria za kazi? Naomba maelezo. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na watalaamu wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri sana. Aidha, pia ninapongeza Wizara hii kwa utendaji mzuri. Ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu juhudi hizo ziendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndio mwanga. Ni lazima tukubali kwamba, Taifa hili tutalikwamua na adui ujinga, umaskini na maradhi kwa kuwapatia Watanzania elimu. Ndio maana tunasema elimu ni ufunguo wa maisha. Juhudi kubwa zilizoonyeshwa na Wizara hii katika kusomesha wananchi wa Taifa hili zinahitaji kuungwa mkono na kila mwanchi katika nchi hii. Hapa ninataka Serikali ichulie wazazi hatua kali kwa wale wote wanaozembea kusomesha watoto wao. Itungwe sheria maalum kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bila Walimu hakuna elimu. Kuna umuhimu wa kuwa na mpango wa makusudi kuongeza Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Wizara inahitajika kuwa na mkakati wa kuongeza Walimu hao. Baya zaidi, hata hao Walimu hatuwatumii vizuri.

Nashuari yafuatayo ili waweze kutumika vizuri. Lipo tatizo la Walimu wengi kusoma Vyuo au Vyuo Vikuu, kujiendeleza kiholela. Matokeo yake ni kwamba Shule nyingi zinakosa Walimu kwa idadi kubwa, kwenda kusoma bila mpangilio unaojulikana. Ninayo mifano hai. Shule yangu ya *Semkiwa Secondary Korogwe* Walimu zaidi ya sita wapo Vyuoni kwa ajili ya kujiendeleza na masomo. Kiikama, Shule inaonekana ina Walimu wanaostahili kumbe hawapo, wapo masomoni. Hali hii ipo nchi nzima. Mimi ninaomba nieleweke kwamba ninapenda Walimu wajiendeleze, kwani bila Walimu kujiendeleza watavia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuokoa hali hii, ninashauri kuwa na mikataba maalum ya kusoma. Haiwezekani kila Mwalimu anakwenda kusoma tu kiholela. Turudishe ule utaratibu wa zamani wa Mwalimu kufundisha kwanza miaka kadhaa halafu ndio aende kusoma. Utaratibu huo utasaidia kuwa na Walimu mashuleni. Walimu waende kwa zamu.

Mheshimiwa NaibuSpika, ni jambo la kusikitisha kwamba baadhi ya Wakuu wa Shule za Sekondari ni kero kwa jamii yetu. Utaratibu wa kuomba na kusailiwa sio mzuri. Wanapewa uongozi Waalimu wabovu. Zamani Mwalimu Mkuu alikuwa anachaguliwa toka Wizarani, baada ya kuchunguzwa mwenendo wa Mwalimu huyo kwa muda mrefu. Ninashuri sana utaratibu wa zamani urudishwe. Hali ilivyo na Sekondari zinavyozidi kuongezeka tunahitaji Wakuu wa Shule wenye sifa na waliochujwa vizuri. Njia inayotumika sasa haifai, ina kujuanajuana sana. Tunapata Walimu Wakuu dhaifu. Utaratibu wa zamani urudiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii ni nyeti, lakini haipewi umuhimu unaostahili. Haiwezekani Idara hii ikatengewa asilimia mbili ya Bajeti lakini baya zaidi hata fedha za Idara hii zinazopelekwa kwenye maeneo ya kazi Wilayani ni kidogo sana na hazipelekwi kwa wakati. Matokeo yake ni Maafisa Ukaguzi hawa wanafanya kazi kwa shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha, kumetokea wakati fedha kupelekwa mwishoni wakati Bajeti au mwaka wa Fedha unakaribia kwisha. Ninashauri sana wapewe fedha za kutosha na zipelekwe kwa wakati ili ufanisi upatikane. Bila Walimu kukaguliwa elimu itadorora.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri yenye picha halisi ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na Dira ya Maendeleo na Sera ya Elimu Nchini. Nina kila sababu ya kusema kwamba hii inathibitishwa na kila ukurasa, jedwali na *graph* iliyopo ndani ya kitabu cha hotuba yake.

Mheshimiw Naibu Spika, napenda pia niipongeze Wizara hii kwa hatua madhubuti iliyochukua katika kuhakikisha elimu itolewayo nchini inakidhi mahitaji yetu na pia ushindani wa kimataifa. Kutokana na hili, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, naomba nieleze hali halisi ya elimu Wilayani Mbozi, hususan Jimbo la Mbozi Magharibi ninaloliwakilisha Bungeni. Wilaya ya Mbozi ina jumla ya Shule za Msingi 207 zenye jumla ya wanafunzi 138,962. Kwa idadi hii ya Shule na wanafunzi, idadi ya Walimu hitajika ni 3,730 lakini waliopo ni 225 tu na hivyo kuwa na upungufu wa Walimu 1,505 ambao kwa kiasi, uko katika Shule zilizoko Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi, kwa takwimu za mwaka 2005 Jimbo hili lina Vijiji 70 vyenye jumla ya Shule 75 kati ya 207 zilizopo Wilayani Mbozi. Kwa bahati mbaya sana kutokana na sababu mbalimbali ni katika Jimbo hili ndiko kuna upungufu mkubwa wa Walimu katika Shule zote 75. Nyingi ya Shule hizo zimeshamiri Walimu wenye Elimu ya Darasa la Saba na pale ambapo wamejaliwa kuwepo na mbaya zaidi kuna Shule kadhaa zenye Mwalimu mmoja mmoja na pale anapobahatika, wakisaidiwa na Mwalimu mmoja wa kujitoela. Mifano hai ni Shule ya Kasinde na Isunda zilizoko kati ya Kapele Shule ya Isunda. Toka ifunguliwe mwaka 2002 hadi hii leo, ina Mwalimu mmoja tu hadi hii leo. Shule nyingi ni Shule ya Sante Kata ya Ivuna yenye Mwalimu mmoja tu anayefundisha wanafunzi 250. Walimu hawa wakiumwa au wakienda kufuata mishahara yao, Shule zinafungwa. Suala la likizo kwa Walimu hawa umebaki ni hadithi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya upufungu wa Walimu Shule za Jimbo la Mbozi Magharibi zina upungufu mkubwa wa madarasa, madawati, nyumba za Walimu na vifaa vya kufundishia. Hali hii inasababisha utoaji wa elimu duni inayodhihirishwa na idadi ndogo ya watoto wanaofaulu kuingia Kidato cha Kwanza. Kwa mfano tu, mwaka 2005 wanafunzi 10,145 walifanya mtihani wa Darasa la Saba, 1,606 tu wakiwa ni kutoka Shule za Jimbo la Mbozi Magharibi. Jumla ya wanafunzi waliofaulu mtihani huo walikuwa 5,480 na kati ya hao ni wanafunzi 785 tu ndio waliotoka Jimbo la Mbozi Magharibi ambao ni 429 tu walijiunga na Shule za Sekondari ambazo nazo ni tano tu katika Kata 11 zenye jumla ya wakazi wapatao 200,000. Kibaya zaidi, kati yao wasichana ni 142 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio kikubwa cha wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi ni kwa Serikali kuzipatia Shule zake 75 angalau Walimu watano kila moja wenye kumaliza Kidato cha Nne na kuwa na Vyeti vya Ualimu, kuteua Mratibu Elimu atakemwajibika kuleta ripoti za uwiano wa Walimu katika Shule zake, kuzipatia Shule za Jimbo hili vitabu vya kiada na ziada ili kuwapa fursa ya kupata elimu sahihi wanafunzi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi lenye eneo la kilometa za mraba 6,250 za Kata 11 zenye jumla ya wakazi 200,000 lina Shule za Sekodanri tano tu ambazo hakuna hata moja yenye Walimu wa kutosha licha ya kwamba hata wale waliopo nina shaka kama kuna aliye na shahada ya Chuo Kikuu na hata wenye stashahada hawazidi watano.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi wamejizatiti kuhakikisha kuwa ifikapo mwakani 2007 Shule za Sekondari nyingine saba zinafunguliwa ili kutoa fursa kwa kila Kata kuwa na Shule moja. Ombi lao ni kwa Serikali kuwapatia Walimu na misaada mingine muhimu ili kuziwezesha Shule hizo kuanza mapema mwezi Januari, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wao kwa kuandaa hotuba hii ambayo ina mwelekeo wa kuimarisha elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali yafuatayo ili kuinua kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba iwe ni muhimu kila Shule iwe na madarasa ya Elimu ya Awali ili kuwajenga watoto bado na umri mdogo wawe wanaithamini elimu katika makuzi yao kuliko ilivyo sasa kwani Shule nyingi hazina madarasa ya awali.

Vile vile, Walimu wapelekwe kwenye Vyuo vya Elimu ya Awali na kuwe na Vyuo vinavyotoa Elimu hiyo hadi kiwango cha *degree*. Vile vile, ningeomba kujua Vyuo vinavyotoa au kufundisha Walimu wa Elimu ya Awali, viko wapi na vinatoa Elimu ya kiwango gain?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Shule zina wanafunzi zaidi ya 60 katika madarasa ya msingi na kufikia watoto zaidi ya mia moja katika Shule, kwa mfano baadhi ya Shule za Manispaa ya Dodoma, Shule kama hizo zinahitaji ziongezewe madarasa ili watoto waweze kupata madarasa ya kusomea na kuwaondoa mbanano wa watoto madarasani na ndipo uboreshaji wa elimu. Kwa hiyo, Serikali itenge fedha za kutosha hasa katika Shule za Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu Walimu wanadai mapunjo ya mishahara na marupurupu yao. Tunaishukuru Serikali imetenga fedha za kulipa madai ya Walimu ila hazikutajwa fedha za kulipa mapunjo ya mishahara ya Walimu. Tunaomba Serikali iliangalie suala hili ili walipwe kwani mapunjo ya mshahara ni haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya mazingira magumu ya kazini itolewe kwa Walimu kwani Walimu hawana muda wa kufanya kazi ya kujiongezea kipato. Miaka ya nyuma Walimu walikuwa wakilipwa *Teaching Allowance* ambayo ilikuwa inawapa moyo wa kujituma kazi zaidi. Maadamu posho hii inatolewa kwa baadhi ya watumishi, basi posho itolewe hata kwa Walimu kwani hata mazingira ya kazi sio mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Ufundi, Wizara naipongeza kwa maandalizi mazuri. Naiomba Serikali ionyeshe utaratibu wa elimu hii mashuleni kwani hata zile Shule zilizo na Kitengo cha Ufundi, bado hakitoi elimu hiyo kutokana na ukosefu wa zana. Suala la Ufundi ni muhimu kwa motto, akishapata taaluma ya ufundi atakuwa au atajiajiri mwenyewe na ataweza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukru Serikali kwa hatua iliyochukua kuongeza idadi ya Walimu. Hata hivyo, upungufu bado ni mkubwa waangalie uwezekano wa kuongeza wanafunzi waliopata hata alama 30 katika mtihani wa Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimwia Margaret Sitta, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Mwananzila, Katibu Mkuu, Kamishna, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara wakiwemo Walimu wote nchini wa ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza umuhimu wa ujenzi wa hosteli za wanafunzi hasa wasichana maeneo ya wafugaji wanaohamahama na ambao hawajaona umuhimu wa elimu. Katika Wilaya ya Hanang tuna *hostel* mbili tulizojenga Shule ya Mulbadaw Nangwa na Endasak Sekondari. Wananchi walijitolea kwa kiasi kikubwa kwa kusaidiana na fedha kidogo za Wafadhili. Tunaomba Wizara isaidie kukamilisha ujenzi na kutoa vifaa kama vitanda, makabati, umeme na maji. Niliandika barua Wizarani, lakini hatujaona majibu ya Wizara. Tafadhali naomba tamko la Waziri kuhusu hili. Nitashukuru.

Kuhusu *MMES* tunahitaji kutekeleza ahadi ya Serikali kuhusu fedha zilizopangwa kwa kila darasa, nyumba za Walimu, Maabara, Bwalo, Maktaba na Vyoo kwa maboma yaliyojengwa na wananchi. Wilaya ya Hanang ipo nyuma sana kielimu, hivyo wananchi wamehamasishwa kujenga Shule katika kila Kata na karibu Kata zote 22 zimejitahidi. Tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri atupe jicho la huruma kwa hao ambao wapo nyuma. Ninaomba atembelee Wilaya nami nitakuwa naye Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. Nawapongeza sana.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwenyezi Mungu anijalie aniongoze katika mchango wangu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nianze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa iipe kipaumbele Wizara hii, kwani Wizara ambayo ni mategemeo ya Watanzania katika maisha yao kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ya Awamu ya Nne, hili imeliona kwamba watoto wa Kitanzania wanapotoka. Hii nasema pale Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake iliposema itajenga mashule Kata hadi Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi hii ya Elimu ina mawimbi mazigo ya matatizo. Nchi yetu ina ukosefu wa Walimu, Shule hazitoshi, hakuna zana. Haya yanahitaji fedha. Ukiangalia Bajeti ya Wizara utaona Wizara haiwezi kutatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaonekana kusahau idadi ya walemavu katika nchi yetu. Pia ni watu kama walivyo wengi wao Wizara inapaswa kujali hili kwamba kuna utofauti wa ulemavu katika mashule yetu. Wako walemavu wanaopaswa kuwa na Shule zao mahsusi na wako ambao wanaweza kukaa na wenzao wasio walemavu.

Mahitaji tu ndio tofauti. Mfano wa hili ni vyoo. Iko haja Wizara hili iwaondolee kero walemavu katika mashule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichunguza nchi yetu, ina ukosefu wa Walimu hasa Walimu wa Sayansi. Ni kwa nini? Njia moja ni ukosefu wa Maabara pamoja na vifaa vyake. Mwalimu wa Sayansi mara nyingi anaposomesha huhitaji kumfunza mwanafunzi kwa njia za uwazi, *practice* na sio kwa mfano *theory*. Ukosefu wa hili mwanafunzi na Mwalimu hawataridhika. Hili litaondoka lini nchini kwetu?

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari Shinyanga Mjini, naomba kibali kitolewe na Wizara kwa Shule ya Sekondari ya Rajani kuwa na Kidato cha Tano na Sita. Tulishawasilisha ombi kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule hii ina madarasa ya kutosha Kidato cha I – VI; Maabara ya kisasa iko tayari; umeme ulishafika Shuleni; nyumba za Walimu zipo; Jengo la Utawala lipo; eneo la michezo, maji ya Ziwa Victoria yanakuja na vyoo vya kutosha. Hivyo kibali kinastahili kutolewa mwaka huu wa 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za *MMES* zitufikie kwa muda muafaka ili tukamilishe ujenzi wa Shule za Sekondari zinazohitajika.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Naunga mkono hoja hii na pongezi kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Naomba kabla ya mpango wa pili wa *MMEM,* kwanza tathmini ifanyike kuhusu utekelezaji wa awamu ya kwanza.

Wilaya ya Njombe awamu ya kwanza ya *MMEM* hatukupata mafanikio kwa sababu ya makosa yaliyofanywa na Ofisi ya Elimu Wilaya. Walipeleka takwimu ambazo hazikuwa sahihi kuhusu upungufu wa madarasa. Walileta taarifa kuwa Wilaya ya Njombe kulikuwa na upungufu wa madarasa 250 badala ya 856 yaliyothibitishwa na *School Mapping*. Matokeo yake, Wilaya ilikuwa inapata moja ya tano ya 250 badala ya moja ya tano ya 856. Tulilalamika sana katika ngazi mbalimbali bila mafanikio yoyote. Hata TAMISEMI wanalifahamu hili. Nadhani tabia ya kufanya kazi kwa nidhamu ya uwoga kutoka Wilayani hadi Makao Makuu ya Wizara ndiko kulileteа kushindwa kuwasilisha takwimu sahihi.

Matokeo yake Wizara ile imeshindwa kukamilisha vizuri madarasa kwa sababu kwa kiasi kikubwa, mpango mzima umetekelezwa na wananchi kwa asilimia 95. Kwa sasa hivi, kama kuna madarasa ambayo yamekamilika vizuri ni machache sana.

Ndiyo maana naomba tathmini ifanyike kabla hatujaingia awamu ya pili. Awamu ya pili tuzibe mapengo ambayo yameachwa na awamu ya kwanza. Nashukuru sana uamuzi wa Serikali kuwa na awamu ya pili ya *MMEM,* vinginevyo tungebaki na magofu badala ya Shule.

Naomba niwakaribishe Jimbo la Njombe Kusini ili mwone haya ninayoyasema. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba, Tanzania inapambana na mambo makuu matatu, nayo ni ujinga, magonjwa na umaskini. Lakini ujinga ndio kubwa zaidi, kwani ujinga ndio chanzo cha maradhi na umaskini. Ukierevuka, basi mengine yote yanakwisha. Elimu maana yake ni kukomboka. Hivyo basi, elimu ni msingi wa yote. Nchi zote zilizoendelea zimeendelea kwa kuwa waliwapa elimu wananchi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Serikali kuwa na mpango wa *MMEM/MMES* mpango huu umekuwa na mapungufu ya kutokuwa na Walimu wa kutosha, elimu sio majengo ni walimu, wanafunzi na vitendea kazi kama *chalks* na *blackboard* pamoja na vitabu vya kiada. Lakini cha ajabu, Tanzania imeanza na majengo ya madarasa na kusahau hata majumba ya Walimu. Hii ni hatari sana.

Suala la wahitimu wa Kidato cha Sita kufundisha Sekondari, baada ya kozi ya mwezi mmoja ni cha kusikitisha sana kwani hii haina tofauti na *UPE* ambayo ilishindwa. Lakini ikumbukwe hawa ni vijana balehe (*adolescents*) na kwamba wako *sexually active* na *activeness* inazidi pale wanapoona vibinti vizuri. Sasa Wizara inajiandaaje kwa athari zitokanazo na ngono zembe na mimba?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ya namba ya wahitimu wa Darasa la Saba, lakini cha ajabu wanaokwenda Sekondari ni wachache. Je, hili kundi lote linalobaki linafanywaje, hasa ikizingatiwa wengi wao hata hawajui kuandika na kusoma? Hawa si wataishia kuwa watumishi wa ndani?

Pamoja na juhudi za *MMEM* na *MMES* za ujenzi wa Shule, madarasa yamekuwa ya *low quality* (hayana ubora) na wahusika wamekula fedha hizo. Je, Wizara imechukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu sio la masihara. Hivyo ni lazima Wizara ifanye mkakati wa kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu yao bila matatizo. Walimu ndio chanzo kikubwa cha wanafunzi kusoma. Cha ajabu, Walimu ni wachache mno. Je, Serikali haioni hili ni tatizo? Walimu ni watu muhimu sana na bila wao tutakuwa na Taifa mbumbumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu bila *allowances* mfano wamekuwa wakifuatilia mishahara yao na hawalipwi *per diem.* Serikali ianzishe *Mobile Bank* Vijijini, ila Walimu wabakie Mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Wizara ijitahidi kuwamotisha Walimu ili tutoe elimu bora siyo bora elimu. Nashukuru sana.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa, katika mwaka 2006/2007 zitajengwa Maabara 40 katika Shule za Sekondari, naomba sana katika Jimbo langu nipatiwe angalau Maabara

mbili katika Shule ya Sekondari ya Sepuka ambayo tayari wanalo jengo lakini hawana vifaa vya Maabara na vile vile Sekondari ya *PUMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuupatia Mkoa wa Singida walimu 197. Lakini hawatoshi, hivyo naomba tugawiwe tena Walimu wengine. Matatizo ya Walimu yaangaliwe. Madeni, posho ya uhamisho na kadhalika bado ni tatizo. Nyumba za Walimu ni tatizo kubwa. Naomba sana katika Jimbo langu nisaidiwe nyumba za Walimu idadi ambayo inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuwa kuna mpango wa kujenga Chuo cha *VETA* Mkoa wa Singida kama ilivyo katika ukurasa wa 71. Je, Chuo hiki kitaanza kujengwa hivi na kitajengwa eneo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ni muhimu kwa Taifa letu. Mashuleni ndio chimbuko la kuibua vipaji vya michezo kwa vijana wetu. Hivyo Wizara isiwe na kigugumizi katika suala la michezo mashuleni. Kitaalam, michezo sio mazoezi pekee, lazima ukishafanya mazoezi kwa kipindi Fulani, lazima pawe na mashindano ya kujipima. Ni busara kujipima na walio bora kuliko wewe. Hivyo, nasisitiza michezo ichezwe mashuleni na kisha washiriki katika mashindano. Narudia kusema kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukuhakikishia kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi , Manaibu wake wote wawili na Watendaji wote kwa jitihada kubwa wanayoifanya kuona elimu zote zinaboreka. Mimi binafsi nina imani nao kwa kupewa hii Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mapya, kwani hata nikiandika, mengi nitakuwa narudia. Mapya niliyonayo ni juu ya kuona uwezekano wa kupata Chuo cha Ufundi *(VETA)* japo kidogo kwa Wilaya ya Mafia. Mazingira ya Mafia yanaeleweka kijiograjia na kihisotira.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wetu wengi hasa wa kike wanaishia kuolewa na kuachika baada ya muda mfupi. Hawana ujuzi wowote wa kuweza kujisaidia wenyewe wala wazazi. Mbaya zaidi, vijana hawa wanaishia kudanganywa na wageni wanaokuja baadaye kuwaacha na mimba au pengine maradhi, ukiwemo Ukimwi. Kwa vijana wa kiume, wengine wanajiunga na vitendo ambavyo kwa Mafia sio kawaida, udokozi na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, suala la usafiri. Tunajua zamani kulikuwa na bei ya usafiri pungufu kwa wanafunzi wanapokwenda likizo. Sasa kwa Mafia kutokana na kuwa hatuna usafiri wa kutosha, bei za ndege ni kubwa na bahati mbaya ndio pekee unaoaminika. Hakuna kabisa upungufu wa bei kwa wanafunzi. Naomba sana Wizara ione namna haya Makampuni kusaidia wanafunzi.

Narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja. Nakutakieni kila la heri kwenye kazi zenu. Karibuni Pwani, karibuni Mafia.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kusema kwamba katika nchi yetu, Sekta ya Elimu bado hatujaipa kipaumbele kwa sababu bado tunasuasua katika kuboresha Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo kadhaa ambayo yanasababisha kuporomoka kwa kiwango cha elimu. Pamoja na mafanikio ambayo tunasema yamepatikana kwa kaisi fulani, bado sehemu kubwa ya watoto ambao wako mashuleni wanasoma katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira hayo ni pamoja na msongamano wa wanafunzi kwenye madarasa. Kama kweli tunataka elimu iwe bora, basi Serikali ihakikishe ujenzi wa madarasa ya kutosha ili wanafunzi wasizidi 30 katika darasa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Ualimu ni ya kitaalamu mbali na kufundisha kwa ujumla wake pia Mwalimu anahitaji kumhudumia mwanafunzi mmoja mmoja ili aweze kutoa msaada zaidi kwa wale ambao ufahamu wao ni mdogo *(slow learners)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi duni ya Walimu hulazimika zaidi kuhangaikia kujikumu kuliko kuzingatia kanuni za kazi zenyewe (ufundishaji). Walimu wetu wana maisha duni ukilinganisha na wafanyakazi wengine. Hivyo ili kuwapa thamani zaidi, basi tuboreshe maisha yao ili waipende kazi yao. Mwalimu asiyeipenda kazi yake, bila shaka ufanisi utakuwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi anayeingia darasani akiwa na njaa hawezi kupokea taaluma ya aina yoyote. Tunahitaji kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata lishe bora ili waweze kuopokea taaluma kwa maslahi ya Taifa letu na wananchi wenyewe. Hivyo basi, Serikali ijikite katika kuhakikisha kwamba, basi angalau Shule za Msingi zirejeshewe ule mfumo wa zamani wa kupikiwa watoto kule Shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ni maskini sana, hawawezi kumudu gharama za Shule na pia kuhakikisha kwamba mtoto wake anapata chai angalau ili aweze kuhudhuria vizuri darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa Walimu unachangia kwa kiasi kikubwa kuporomoka kwa elimu Tanzania. Sasa basi, ni muhimu kuona kwamba Walimu wa kutosha wanaajiriwa na wenye uwezo wa kutumia elimu (*materials*) waliyonayo ili kupata ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, somo la Sayansi na Hisabati uwekwe mkazo makusudi wa kupatikana walimu wa masomo haya kwani hayapendezi sana ndani ya vichwa vya wengi na hii itapelekea Taifa kurudi nyuma kwenye ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona msemaji wetu wa mwisho amekuwa *brief.* Sina matangazo ya ziada. Jana tuliletewa ki-*note* na Waheshimiwa Wabunge fulani hapa kwamba hotuba za Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi wengine hawakupata. Sasa sijui walikuwa wangapi hawajapata.

Kwa hiyo, tunashauri kwamba zinapotolewa hotuba hizi vijana wanaogawa hotuba wagawe kwa kila aliyekuwepo, kusudi wale ambao hawapo kama wanahitaji vitabu namna hiyo vinakwenda Ofisi ya Katibu kule chini kwa wale ambao wakati hotuba zinasomwa wanakuwa hawapo, basi unaenda ofisini kule chini jengo la zamani, pana ofisi yetu pale *store* unaweza ukapata nakala. Kwa sababu wengine jana walisema hawakupata. Upo uwezekano kwamba wengine walichukua zaidi ya moja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Wizara imeleta nakala kwa hiyo, kwa wale ambao hawakupata, naomba mfuate utaratibu huo.

Baada ya kusema hilo nilisema kwamba wazungumzaji wetu hawa ndiyo wamemaliza. Tunataka kumpa Mheshimiwa Waziri muda mzuri katika Kamati ya Matumizi.

Nadhani wengi tunapata ufafanuzi mzuri zaidi kipindi hicho kuliko ambavyo tunazungumza hapa na kwa ukweli Bunge kufanya uamuzi ni kipindi kile. Hizi hotuba tunazotoa ni mawazo mazuri kwa Wizara zinazohusika lakini maamuzi mazito yanatokea wakati wa Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, tumwachia muda mrefu.

Kwa hiyo, saa 11.00 jioni tutaanza kuwaita Naibu Mawaziri wanaohusika na mtoa hoja mwenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyoeleza asubuhi kwamba wasemaji kwa upande wa Wabunge tulishamaliza mchana kusudi tuweze kutoa muda wa kutosha hasa kwenye Kamati ya Matumizi.

Sasa nitawaita Waheshimiwa Naibu Mawaziri mmoja, mmoja, baadaye mtoa hoja tutampa nafasi lakini anapotaja yale majina mengi sana, haitahesabika kama ni sehemu ya kujibu hoja, kwa hiyo, sijui nani anaanza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuanza kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kusimama hapa ili nami

niweze kuchangia kwa kujibu hoja kadhaa za Waheshimiwa Wabunge, waliochangia katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kusema naunga mkono hoja. Baada ya hapo naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema na mapenzi mema kwetu sote. Namshukuru kwa neema zake na yote aliyonijalia katika utendaji wangu wa kila siku. Nazidi kumwomba mapenzi yake na mapenzi ya wote wanaompenda yeye atuzidishie uwezo wa kuwatumikia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki katika mchakato mzima wa uchaguzi ambao uliniwezesha kupata Ubunge wa Viti Maalum. Naomba shukrani maalum ziwafikia wanawake wa Mkoa wa Tanga kwa imani yao juu yangu, *inshallah* nawaahidi uwakilishi mwema. *(Makofi)*

Naishukuru sana familia yangu, hususan mume wangu Bakari Abdallah Mahiza, kwa kuridhia nijiingize katika masuala ya siasa. Aidha, nitakuwa mchache wa fadhila endapo nitasahau kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua na kunipa jukumu la kusimamia elimu kwa kushirikiana na wenzangu. Nitajitahidi kuifanya kazi hii kwa uwezo wangu wote kwa kadri mola atakavyonijalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa namna ambavyo amekuwa akituongoza kwa hekima na busara kubwa. Namshukuru pia Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kwa ushauri, mwongozo, maelekezo yao ambayo yamenisaidia sana kukuza uwezo wangu katika uwajikaji. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru kwa dhati watendaji wakuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, walimu wa shule za msingi na sekondari, waratibu wa elimu kata, wakuu wa vyuo vya ualimu na vyuo vya ufundi kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana pale nitakapokuwa nimeshindwa kukidhi haja na matakwa ya Waheshimiwa Wabunge, naomba ieleweke kuwa si kwa ujeuri wala kiburi, bali ni ugeni katika fani hii ya siasa. Mapendekezo yao na maoni yote tumeyapokea na tutayafanyia kazi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge wote kwa heshima na taadhima kwa kadri nitakavyojaliwa.

Maoni ya jumla yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ni ya kweli na yenye uzito mkubwa sana. Aidha, napenda nikiri katika programu hizi za *MMEM* na *MMES* kumekuwepo na mafanikio makubwa sana ambayo yametupunguzia kero kubwa zilizokuwa zinatukabiri hapo awali kwa kukosa nafasi za masomo. Hata hivyo uko pia udhaifu mdogo katika utekelezaji wake jambo ambalo limepoteza imani kwa baadhi ya

maeneo machache. Uwezo wetu wa kutembelea mikoa yote umekuwa mdogo na hivyo kusababisha kutopata uhalisia wa matatizo yatolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Napenda kupitia Bunge lako Tukufu kuwaahidi kuwa ni matarajio yote sote kuwa baada ya Bunge hili tutatembelea Mikoa mingine na kwamba kila Mkoa utapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali hoja za Wabunge ni nyingi na mimi nitajibu chache na wale ambao tutashindwa kutokana na muda tutawajibu kwa maandishi na kamwe hatutaacha kumjibu yeyote. Naomba nianze kwa kutoa hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Benedict Losurutia, ambaye alikuwa amezungumzia juu ya maendeleo ya elimu kushuka katika Jimbo la Kiteto. Tume ya kufuatilia maendeleo ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto imefanya kazi kuanzia tarehe 13 Mei hadi tarehe 26 Mei. Ufuatiliaji ulizingatia maeneo ya upatikanaji wa elimu bora, usawa katika utoaji elimu ya utendaji fanisi. Masuala kadhaa yamebainisha yakiwemo uwiano usioridhisha katika uandikishaji baina ya wavulana na wasichana uliotokana na matatizo ya elimu usioridhisha kwa elimu ya wasichana, upungufu wa walimu, miundombinu na vifaa, umbali wa shule na makazi na hivyo kuathiri maudhurio na umalizaji shule pamoja na udhaifu katika uongozi. Wizara imezingatia mapendekezo ya Tume na itayafanyia kazi kikamilifu ili pamoja na washirikishwaji wa wadau wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ili kuweka mikakati ya utatuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi iliyowakilishwa na Mheshimiwa George Simbachawene kuhusu sekondari ya Kibakwe na wakati wa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na masuala mengine. Ujenzi wa masuala ya mabweni ya hosteli ni mojawapo ya mikakati ya kupunguza kiwango cha wasichana kuacha masomo. Katika kuhakikisha kuwa suala la ujenzi wa hosteli unapewa umuhimu unaostahili. Serikali ilitoa mwongozo wa ujenzi wa hosteli na namna ya kuziendesha katika Waraka wa Elimu Na. 12 wa mwaka 2004. Hivyo wananchi wa maeneo ya Kibakwe wanashauriwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa na wadau wengine wakiwemo mashirika yasiyo ya Serikali na madhehebu mbalimbali kutafuta namna ya kujenga hosteli ya wasichana ili kuwanusuru katika katika mazingira yao hatarishi. *(Makofi)*

Hoja nyingine ya Mheshimiwa Gosbert Blandes, pamoja na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa Anastazia Wambura, wanasema michezo irudishwe mashuleni. Wizara yangu kama tulivyoeleza katika majibu mbalimbali haikufuta michezo shuleni, kilichositishwa ilikuwa ni mashindano, yalikuwa yanafanyika katika ngazi ya Taifa na kutumia muda mwingi wa masomo. Aidha, somo la michezo limo katika mitaala na linafundishwa shuleni. Kwa hali hiyo, mashindano yanaweza kufanyika katika ngazi ya shule. *(Makofi)*

Kuhusu uendelezaji vipaji walimu wanakuza vipaji vya wanafunzi kupitia ushiriki wao katika vyama mbalimbali kama vyama vya maskauti wa kike na kiume, kwaya, kongamano, uchoraji na uandishi wa insha. Elimu maalum bado ina matatizo mengi hoja hii imejadiliwa na Wabunge, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi,

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo na Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imepokea mawazo ya Wabunge na yote waliyoshauri yapo kwenye mpango wa kazi wa mwaka 2006/2007. Aidha, tathmini itafanyika katika shule zote ili kubaini mahitaji ya shule zote kwa utekelezaji ulio bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Mwibara kuhusu hatua zilizochukuliwa dhidi mwalimu anayetuhumiwa kwa kubaka. Kubaka ni kosa ambalo liko chini ya makosa ya jinai. Kulingana na sheria hiyo mtu yeyote hawezi kutiwa hatiani mpaka itakavyothibitishwa na mahakama kutenda kosa. Mwalimu wa shule ya msingi ya Mahiga, Kwimba anayetuhumiwa kubaka mwanafunzi ni mwajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mwanafunzi anayedaiwa kubakwa alikiri kuwa alikuwa mjamzito na alijifungua mtoto wa kike tarehe 9 Februari, 2005 kabla ya kujiunga na sekondari ya Ngudu tarehe 25 Februari, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, baba mzazi wa mwanafunzi alipogundua kuwa binti yake alikuwa mjamzito aliwasiliana na wakili wa kujitegemea wa Mwanza ambaye aliwasilisha suala hilo polisi na kufungua shauri namba *NGIR/655/2004.* Kwa mujibu wa taarifa kutoka Kituo cha Polisi Ngudu upelelezi wa shauri hilo bado unaendelea kwa sababu polisi wanasubiri majibu ya *DNA* ili kesi iweze kupelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo itathibitika kuwa mwalimu huyo ndiyo baba wa mtoto. Suala hili lilikwisha shughulikiwa na Wizara kupitia Ofisi ya Ukaguzi Kanda ya Ziwa kati ya tarehe 16 na 17 Juni, 2005 ambapo ilifikishwa polisi. Wizara yangu baada ya kupata taarifa na kuthibitisha kutoka kwa mwanafunzi mwenyewe ilichukua hatua za kumfukuza shule kwa kosa la kupata mimba. Aidha, kwa kuwa shauri hili liko polisi Afisa Elimu wa Wilaya ya Kwimba alikwishaagizwa kusimamishwa kazi mwalimu huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Manju Msambya, Mbunge Kigoma Kusini juu ya suala la mtihani kutofanyika darasa la nne na hatua zilizochukuliwa. Mkoa wa Kigoma una jukumu la kusimamia kuendesha na kuratibu mitihani ya darasa la nne ikiwemo kuchapisha nakala za kutosha kwa watahiniwa wote kwa kushirikiana na Halmashauri zake. Mkoa wa Kigoma una utaratibu wa kukasimu madaraka ya uchapishaji kwa Halmashauri moja kwa kila mwaka. Mtihani wa mwaka 2005 ulisimamiwa na Halmashauri ya Kigoma Vijijini. Mkoa wa Kigoma ulichelewa kuchapisha mtihani wa darasa la nne na kusababisha mtihani huo kutofanyika kwa tarehe zilizopangwa. Wizara iliufuta mtihani huo kwa barua yenye kumbu kumbu Na. *PYB/BC/109/1/98* ya tarehe 24 Novemba, 2005.

Kwa hiyo, mtihani haukufutwa na *RAS* wala *REO.* Aidha, Wizara ilifanya uchunguzi wa kina na kubaini kiini cha kutofanyika mkutano kwa wakati katika uchunguzi uliogunduliwa kulikuwa na ufuatiliaji hafifu na kwamba mtihani huo haukufanyika kwa wakati. Basi hata hivyo Wizara ilichukua hatua za kinidhamu kwa wahusika ikiwa ikiwa ni pamoja na kuwapa karipio kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja iliyowasilishwa kuhusu mrundikano wa wanafunzi katika madarasa. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuwa mrundikano wa wanafunzi darasani huchangia katika kuathiri ubora wa elimu. Kiwango cha Wizara cha kuhusu idadi ya wanafunzi kwa nadra katika shule za msingi ni wanafunzi 40. Wizara inaahidi kufanyia kazi suala hilo.

Halafu Mheshimiwa Martha Mlata, amezungumzia juu ya walimu wanaoiba fedha za *MMES.* Kiutaratibu Mkuu wa Shule kama mtumishi wetu wa Serikali akituhumiwa kwa kosa lolote, uchunguzi hufanyika na mhusika hupewa fursa ya kujitetea. Ikibainika kwamba tuhuma hizo ni za kweli huchukuliwa hatua za kinidhamu na sheria kutegemea aina na uzito wa kosa.

Halafu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, alizungumzia juu ya ujenzi wa maabara katika Shule ya Ganako, jibu, suala la majengo mbalimbali ambayo yalianza lakini hayajakamilika, limejitokeza katika majengo ya madarasa, nyumba za walimu na majengo ya utawala. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa kadri fedha zitakavyopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Margreth Mkanga na Mheshimiwa Nuru Bafadhili wamesisitiza juu ya michoro kwa ajili ya miundombinu ya shule za walemavu. Ni kweli kuwa michoro ya awali ya *MMEM* haikuwa na ramani za walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Wizara sasa imeshatayarisha michoro. Wizara inasisitiza wahandisi wote wa Halmashauri kuitumia vizuri miongozo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum amezungumzia juu ya maandalizi ya *MMEM.* Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ipo katika utekelezaji wa Mpango wa *MMEM* ambao una lengo la kuongeza nafasi zaidi ya elimu na sekondari. Hivyo utekelezaji wa *MMES* utasaidia katika kupokea wanafunzi watakaofaidika na kujiunga na shule za sekondari.

Aidha, kwa utaratibu wa kujenga shule za kutwa kwa kila Wilaya shule nyingi za sekondari zitafunguliwa na zitaendelea kufunguliwa na hivyo kupokea wanafunzi waliopo. Wizara ya Elimu iko tayari kwa maandalizi ambayo tumeshaeleza katika majibu yetu.

Halafu Mheshimiwa Lucy Mayenga, anazungumzia juu ya shule ya Ngaza na Bwiru kuwa ya *A level.* Katika kutafuta za shule *A level* wanafunzi wanaohitimu kidatu cha nne, baadhi ya shule zilikuwa na miundombinu inayostahili zaligeuzwa kuwa *A level*

tu. Shule ya Ngaza ni miongoni mwa shule zinazowaondoa taratibu wanafunzi wa *O level* hadi wanatakapoisha yaani tuna-*phaseout.* Shule ya Bwiru siyo miongoni mwa shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, anazungumzia juu ya gari la wakaguzi. Wilaya ya Kilwa ilikuwa na gari aina ya *Suzuki* ambayo ilibainika kuwa haifai kutumika kutokana na mazingira ya Wilaya hiyo na hivyo ikahamishiwa Wilaya nyingine. Kufuatia Wilaya hii itafuatiwa hali Wilaya ya Kilwa itapatiwa gari mpya aina *Toyota Landcruise Hardtop*. Gari hii ni kati ya magari 18 yaliyonunuliwa. Mheshimiwa Athumani Janguo anaomba walimu wakague mara kwa mara. Malengo yameongezwa kwa sababu kumekuwa na ongezeko la shule na vifaa vimeongezwa na kazi hiyo tunaahidi itafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu Mheshimiwa Riziki Omar Juma na Mheshimiwa Shally Raymond, jukumu la kutoa chakula kwa wanafunzi angalau mlo mmoja lipo mikononi mwa Halmashauri na jamii husika chini ya usimamizi wa kamati za shule. Hata hivyo Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani linatoa chakula kwa shule 330 katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Singida na Dodoma.

Kuna hoja ya kwamba elimu maalum bado ina matatizo mengi, hoja hii imechangiwa na Wabunge wengi. Wizara yangu imepokea mawazo ya Wabunge na yote waliyoshauri yapo kwenye mpango wa kazi wa mwaka 2006/2007. Aidha, tathmini itafanyika katika shule zote ili kubaini mahitaji ya kila shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliwasilishwa tathmini ifanyike kabla ya *MMES Phase II,* sasa ushauri wa Mheshimiwa Anna Makinda na Mheshimiwa Abdul Marombwa, umezingatiwa. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, umezingatiwa katika andiko la *MMEM* awamu ya pili, mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa aina ya kwanza yamezingatia. Aidha, kwa kuwa *MMEM* ni endelevu, itaendelea na kuzingatia na masuala yaliyojitokeza katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara ya kwanza kupata nafasi ya kuhutubia Bunge hili tangu nichaguliwe, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia kumaliza vizuri uchaguzi uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na hivi karibu kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, kwa kura zote kasoro moja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa ushindi alioupata na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti, Mheshimiwa Jenista Mhagama na

MheshimiwaJob Ndugai, kwa nyadhifa walizozipata, nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuingia katika Bunge hili jipya. *(Makofi)*

Nawashukuru wananchi wa Jimbo la Kalambo, kwa kuniamini na kunirejesha hapa Bungeni kwa mara ya pili, nitawatumikia kwa moyo wangu wote. Namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa namna ya pekee alivyoniamini na kuniteua kushika nafasi hii ya Unaibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, namshukuru kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kalambo, namshukuru pia Waziri wangu Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge kwa jinsi anavyonishirikisha katika uongozi wa Wizara hii. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mwantumu Mahiza, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano wao waliouonyesha kwangu, naishukuru sana familia yangu, kwa jinsi wanavyonipa moyo katika kazi zangu na namshukuru sana mke wangu Scollastica na watoto wangu wote. *(Makofi)*

Napenda kuwathibitishia Wabunge wote waliochangia katika hoja hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, hata wale waliochangia katika hotuba ya Waziri Mkuu kuwa tumeyapokea kwa unyenyekevu na tutajibu hoja zote kwa maandishi na kumpatia kila mmoja wetu. Hata hivyo kwa nafasi hii ndogo niliyopata, naomba niweze kujibu masuala haya machache yaliyoko mbele yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizozungumzwa na Wabunge ni nyingi, lakini hasa nazingatia zile hoja zilizozungumzwa kuhusu elimu ya walimu pamoja na *vocational training.* Kuhusu mgao wa walimu usioridhisha katika shule moja za msingi na nyingine hapa katika Halmashauri ya Kilosa, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby. Wizara hugawa walimu wa shule za msingi kwa ngazi za Halmashauri, ni jukumu la Halmashauri husika kugawa walimu waliopangwa kwenye shule hizo, kuzingatia kanuni ya *income* na upungufu uliopo, aidha, Halmashauri inahusika kurekebisha uwiano wa walimu miongoni mwa shule ndani ya Halmashauri, baada ya mabadiliko, kuhama au kustaafu. Uamuzi huu unazingatia kuwa Halmashauri kuwa ndio wanaofahamu mahitaji halisi ya shule moja, moja. Wizara itafuatilia katika Halmashauri, ikiwemo Halmashauri ya Kilosa, ili kuona hali halisi ilivyo katika Halmashauri hii na hasa shule za Gairo zipate walimu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuwatumia vijana waliomaliza kidato cha sita katika ufundishaji katika shule zilizoanza hivi karibuni. Mheshimiwa Felix Kijiko, alitoa hoja hii, jibu ni kuwa kutumia vijana waliohitimu kidato cha sita kufundisha katika sekondari muda mfupi tu, Halmashauri zinashauriwa kuwashirikisha Maafisa Elimu wa Mikoa ambao wanayo maelezo ya kuwahamisha walimu kutoka shule za sekondari zilizopo, ili waende katika shule zinazoanzishwa. Aidha, walimu wanaomaliza mafunzo ya stashada ya ualimu, wanapangwa kimkoa, ili Afisa Elimu wa Mkoa awapangie kituo kulingana na vipaumbele vya mkoa au na mahitaji ya kila shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Tatu Ntimizi, anaomba walimu na hasa walimu wa sayansi katika sekondari ya Igalula, Wizara inatambua upungufu wa walimu uliopo katika sekondari nchini ikiwemo shule hii ya Igalula. Kwa kuwa shule nyingi zimefunguliwa na maafisa elimu walishafikisha

Wizarani upungufu uliopo katika shule hizo, Wizara imewapanga kimkoa ili maafisa elimu wa mkoa wawapange katika shule zao kulingana na mahitaji ya kila shule.

Mheshimiwa Abdul Marombwa, alizungumzia kuhusu ikama ya walimu, utaratibu wa Serikali wa kupanga walimu, ni kwa uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45. Hata hivyo kwa kuwa mazingira ya nchi hii yanatofautiana, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge utafanyiwa kazi wakati wa kupanga walimu kwa sehemu zenye matatizo kama vile *delta.*

Mheshimiwa Mathias Chikawe, amezungumzia juu ya Chuo cha Ualimu Nachingwea kuwa wanaomaliza katika chuo kile wapangwe katika mkoa wa Lindi na hasa Wilaya ya Nachingwea. Vyuo vya Ualimu ni vya Kitaifa na hivyo huchukua wanafunzi kutoka nchi nzima, aidha, wanapohitimu hupangwa kwa kuzingatia mahitaji ya Kitaifa. Muhimu ni kila Wilaya iandae mazingira mazuri ya kuwapokea walimu wapya katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi walichangia katika suala hili la UKIMWI na jinsi ya kuweza kulishughulikia katika Wizara yetu ya Elimu.

Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Hasnain Daweji, wamelizungumzia hili suala la UKIMWI katika shule zetu. Wizara inaendelea kutoa elimu ya UKIMWI na stadi za maisha kwenye shule, vyuo vya ualimu na wafanyakazi wasio walimu. Wizara yangu pia itashirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili kuweza kuwasaidia watoto yatima. *(Makofi)*

Aidha Wizara itaendelea kutoa ushauri nasaha kwa walimu na wanafunzi ili kuwahamasisha katika upimaji wa hiari wa maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Upimaji huu utawasaidia kujua afya zao kupatiwa ushauri nasaha na kupewa dawa za kurefusha maisha kutoka vituo vya afaya kwa wale walioathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya *VETA,* hoja 18 zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali katika Kikao hiki na hoja zilizotolewa zimelenga katika maeneo mbalimbali yanayohusu *VETA.* Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu na Mheshimiwa Felister Bura, wamezungumzia kuhusu mipango mizuri lazima ielekeze fedha za kutosha kuendeleza mafunzo ya ufundi kwa vijana ni pamoja na Siraji Juma Kaboyonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya *VETA* na vya asasi zisizo za Serikali hupokea vijana wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne kwa ajili ya mafunzo ya ufundi stadi. Pamoja na mafunzo ya ufundi stadi vijana hao hupewa mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kujiajiri au kuajiriwa. Jumla ya shilingi bilioni 8 na milioni 554 zimetengwa katika bajeti ya *VETA* ya mwaka 2006/2007 kwa ajili ya kutoa mafunzo katika stadi mbalimbali. Serikali pia imetenga jumla ya shilingi bilioni 10.6 katika fedha za maendeleo kwa ajili ya kuendeleza ukarabati na upanuzi wa vyuo vya ufundi vya Shinyanga, Mpanda, Tabora, Kagera Mara, Arusha, Songea, Mikumi, Dakawa,

Ulyankulu na ujenzi wa vyuo vipya vya Arusha, Singida, Dar es Salaam ili kuongeza nafasi na mafunzo na fani za mafunzo za ufundi stadi. Hii ni sambamba na kufunga vifaa vya mafunzo katika vyuo hivyo na hasa Chuo cha Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya ufundi stadi kila Wilaya, waliochangia katika hoja hii ni Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Abdul Marombwa na Mheshimiwa William Shellukindo wa Bumbuli.

Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, mkakati unaandaliwa wa kuanzisha vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi katika kila Wilaya kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Abdul Marombwa pia amezungumzia juu ya suala hili la vyuo vya *VETA* vijengwe katika kila Mkoa, kila Mkoa uwe na chuo chake. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali itaanza kujenga vyuo vya ufundi stadi katika Mkoa wa Lindi, Pwani na Manyara, ili kukamilisha Mikoa yote kuwa na vyuo vya ufundi stadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, amezungumzia juu ya kutoa *Diploma* ya ufundi stadi katika vyuo vyetu vya *VETA*. *VETA* hutoa mafunzo katika ngazi tatu za cheti, ngazi ya Stashahada ya Ufundi, hutolewa na vyuo vilivyosalijiliwa na *NACTE*. Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mbunge wa Rorya amezungumzia juu ya mpango wa kuanzisha *polytechnics* katika nchi yetu ya Tanzania. Vyuo vya ufundi kama vile *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* ni sawa na *polytechnic*. Vyuo hivi viko chini ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na vinatoa fursa ya kuunganisha mafunzo ya ufundi stadi hadi ngazi ya juu. Unaweza ukafika chuo kikuu kwa kupitia mfumo huu wa *VETA* halafu unakwenda *DIT* halafu unakwenda chuo kikuu.

Mheshimiwa Wiliam Shellukindo, alizungumza kuhusu ajira katika kitengo cha hoteli Dodoma, utaratibu wa kuboresha kitengo cha mafunzo ya hoteli na mikutano *(Dodoma Course and Conference Centre)* unatekelezwa. Hii ni pamoja na kupitia muundo wa kitengo hicho ili kuweze kurekebisha kasoro zilizopo.

Mheshimiwa Salome Mbatia na Mheshimiwa William Shellukindo pia walizungumzia juu ya vifaa kwa wahitimu wa mafunzo ya ufundi wanapomaliza mafunzo wapewe vifaa vya kwenda kuanzia kufanyia kazi. Mpango wa kutoa vitendea kazi kwa wahitimu wa vyuo vya ufundi stadi umekwishaanza kutekelezwa katika vyuo vya *VETA,* vya Mikumi, Mbeya, Mtwara, Dakawa, Ulyankulu kwa kuwashirikisha wazazi. Utaratibu huo utaendelea kusambazwa katika vyuo vingine vilivyobaki hapa nchi.

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, amezungumzia juu ya mafunzo ya udereva. Katika mpango wa upanuzi wa mafunzo ya ufundi stadi, fani ya udereva ni mojawapo kati ya fani zilizopewa kipaumbele kulingana na mahitaji yanayojitokeza katika fani hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum amezungumza juu ya misaada kwa vyuo visivyo vya Kiserikali utaratibu wa kivijengea uwezo vyuo vya ufundi stadi visivyo vya Kiserikali ni kama ifuatavyo:-

Kugharamia mafunzo ya elimu na ufundi stadi, ipo katika mpango wa *VETA* na kutoa msaada wa vifaa vya mafunzo kwa ajili ya kuboresha karakana ya *VETA* na kutoa msaada wa vifaa vya mafunzo kwa ajili ya kuboresha karakana za mafunzo upo katika mpango huo.

Kwa mfano mwaka 2005/2006 jumla ya shilingi milioni 598 zilitolewa kwa ajili ya shughuli hizo nchi nzima kwa vyuo binafsi, wakuu wa vyuo hivyo hupewa mafunzo ya uongozi na vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Savelina Mwijage, alizungumzia juu ya Chuo cha Ufundi Gera katika Mkoa wa Kagera. Kuhusu Chuo cha Ufundi Stadi Gera, Ofisi ya *VETA* Kanda ya Ziwa ina taarifa juu ya matatizo ya chuo hicho na inawasiliana nacho ili kupata ufumbuzi wa matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya *VETA* kuwa vya Kitaifa lilizungumziwa na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu. Hoja ya kuvifanya vyuo vya Ufundi Stadi Tanzania Bara na Visiwani kuwa vya Kitaifa tumeipokea kama hoja na tutaifanyia kazi kwa kuanzisha ushirikiano kati ya *VETA* na Idara ya Mafunzo ya Amali Zanzibar umeshaimarishwa katika maeneo ya utayarishaji wa mitaala na utungaji wa mitihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, anazungumza juu ya mitaala ya *VETA* kurekebishwa. Mitaala ya *VETA* hivi sasa imefanyiwa marekebisho kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Hesabu, Kingereza, Sayansi, *Technical Drawing,* Stadi za Maisha, ujasiriamali na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, wamezungumzia juu ya Chuo cha Ufundi Stadi Singida na Tabora vitajengwa lini? Matangazo ya zabuni pamoja na uteuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa Chuo cha Singida na Tabora yatakamilika mwishoni mwa mwezi Januari, 2007, ujenzi wa chuo cha Singida utakuwa katika eneo la hivi sasa ambapo chuo kile kipo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo bado tunawasihi Waheshimiwa Wabunge kwamba hatuwezi tukajibu kila hoja, Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kujibu maswali mengine ambayo yamebaki lakini bado tutaandika ili kuweza kujibu na kuweza kuwapatia Wabunge wote nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa namwita Mheshimiwa mtoa hoja Waziri wa Elimu na Mfunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Sitta na kama nilivyosema majina haitakuwa sehemu ya majibu, ayataje yote siyo sehemu ya majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii ili nikamilishe kazi ambayo tuliinza jana ya kujibu hoja mbalimbali zilizowasilishwa au zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kutusaidia kuimarisha utoaji wa elimu hapa nchini, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea ningeomba kwanza nifanye sahihisho moja katika kitabu chetu cha bajeti tulichokigawa jana, tunashukuru mlikisifia na kweli tunakubali sifa mlizotupa isipokuwa kuna marekebisho mawili tu katika ukurasa wa 16 sehemu (b) mstari wa nne kutoka juu kama mtaona (b) pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavulana wanatakiwa wawe 10,776, wavulana imeandikwa 10,776 lakini isomeke 10,777, basi mta-*check* tu ni ukurasa wa 16 haitawapa shida sana. Aidha, wasichana 7,439 sasa isomeke 7,434.

Sahihisho la pili lipo ukurasa wa 84 kielelezo namba 10, ni uandikishaji wa wanafunzi kwa sekondari za Serikali mwaka 2006 tunaomba isomeke kama ifuatavyo.

**NAIBU SPIKA:** Ukurasa gani?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ukurawa wa 84, kielelezo namba 10. Katika shule za Sekondari za Serikali mwaka 2006 isomeke 18,211 na zisizo za Serikali mwaka 2006 isomeke 9,569 ni kwamba zilibadilishwa tu.

**NAIBU SPIKA:** Tunaomba urudie.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ukurasa 84 kielelezo namba 10 Uandikishaji wa Wananfuzi kwa Sekondari za Serikali mwaka 2006 isomeke 18,211 na zisizo za Serikali mwaka 2006 isomeke 9,569. ni kwamba zilibadilisha tu idadi ya Serikali ikapelekwa kwa zisizo za Serikali ni kubadilisha tu kidogo. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mmeelewa Waheshimiwa Wabunge?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii na mimi pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii adimu, namwomba Mwenyezi Mungu anipe nguvu niendelee kufanya kazi kwa lengo la kutumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Pili, nachukua nafasi hii kuishukuru familia yangu yote, imenisaidia kwa njia moja au nyingine na hususan Mheshimiwa Spika, Samuel John Sitta kwa kunilea kisiasa, hilo amefaulu lakini bado anaendelea kunilea katika *Standard and Speed* inayotakiwa, naomba asichoke aendelee kunilea tu. *(Makofi/ Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Wanasema imeonekana. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina wajibu wa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo namsumbua kwa kumuuliza maswali kila wakati, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu usichoke nikishabobea sitakusumbua sana. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wametuuliza maswali hapa na pale kwa kweli wametusaidia sana katika utendaji wetu, si leo tu katika Bunge lakini kila tunapokutana nao nje na ndani ya Bunge na wakati huo nichukue nafasi hii kuwashukuru watendaji wote kama nilivyosema jana lakini pia nina wajibu wa kurudia kwa namna ambavyo tunashirikiana mpaka kufikia hatua hii ya kuweza kuwasilisha hoja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba nizungumzie Waheshimiwa Wabunge waliochangia tunashukuru sana, tuna bahati tumechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 176, naomba niwataje lakini nashukuru Naibu Spika amesema hatahesabu dakika kwa kuyataja majina hayo,ni vizuri wakajisikia majina yao.

Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Omar Kwaangw' , Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Dr. Omari Nibuka, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Amina Mpakanjia na Mheshimiwa George Lubeleje.(*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Dunstan

Mkapa, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Ramadhani Maneno na Mheshimiwa John Shibuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa walichangia hoja za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupitia mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wapo pia waliochangia hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa njia ya maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Luhaga Mpina , Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir na Mheshimiwa Abbas Mtemvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Lucy Owenya. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji,

Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki na Mheshimiwa Diana Chilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa William Ngeleja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walioomba kuchangia bajeti na wakapata nafasi ka kuzungumza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Cynthia Ngoye. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Amina Mpakanjia, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niungane na Naibu Mawaziri waliozungumza kwamba si rahisi kujibu hoja kama mlivyoona idadi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia, kwa hiyo, naomba radhi kwa wale ambao hatutawataja majina kutokana na hoja walizozungumzia. Kwa hiyo, mtuwie radhi lakini tutaleta majibu kwa maandishi kwa kila mmoja kadri alivyouliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ingawa pamoja na kwamba liliulizwa na Mheshimiwa Mbunge mmoja tu lakini kwetu sisi kama Wizara tumeona ni kama changamoto nzuri sana. Nasema tuweke malengo mazuri yasiyozalisha matatizo, sisi tumelichukua kwetu kama changamoto kutokana hasa na masuala muhimu yaliyozungumzwa ndani ya Bunge hili kuhusu elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba mipango ya elimu inatayarishwa kitaalamu ikiwashirikisha wadau mbalimbali wa elimu na kamati za Serikali kufikiwa kwa baadhi ya malengo yaliyowekwa kabla ya muda uliopangwa kunatokana na msukumo wa Serikali na jamii kupata mwamko baada ya kuhamasishwa na hivyo kushiriki kikamilifu

katika maendeleo ya elimu kuliko ilivyotegemewa jambo ambalo tunaona ni la kupongezwa na kufurahiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo sasa msukumo wa Serikali na mwitikio wa jamii ndiyo unakuja kuona suala kubwa ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge 40 kuhusu upungufu wa walimu. Ningeomba nisiwataje tena ili tuendelee kwa sababu nimeshawaheshimu nimewataja wote ili tuokoe muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa walimu uliojitokeza katika Shule za Sekondari unatokana na mafanikio ya msukumo wa Serikali na mwitikio wa wananchi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekondari *(MMES)* wa mwaka 2004/2009. Mfano kati ya mwezi Januari, 2006 hadi Mei, 2006 shule 482 zilifunguliwa, shule hizi zilifunguliwa kwa wingi baada ya vijana wengi waliofaulu na kuhitimu mtihani wa elimu ya msingi kukosa nafasi ya sekondari. Serikali iliamua angalau nusu ya vijana waliobaki basi wapate nafasi ya elimu ya sekondari, kwa kufanya hivyo Wilaya zote za Mkoa kwa mfano Lindi wengi walikuja na kusema Mheshimiwa Waziri tupe pongezi sisi tumechukua wanafunzi wote, kwa mfano pia Igunga. Kwanza Mkoa wa Lindi umechukua wanafunzi wote, Igunga imechukua wanafunzi wote kadhalika Kiteko, Ruangwa na Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuchukua wanafunzi wote waliofaulu hili lingefikiwa mwaka 2009 angalau hata kwa 50% lakini hawa wenzetu wamechukua wanafunzi wote ndiyo hawa niliosema kwamba malengo yamefikiwa haraka sana kutokana na mwamko na wananchi kuhamasika kuongeza elimu. Mafanikio haya yamesababisha changamoto ya uhaba wa elimu na ili kupata ufumbuzi imebidi Serikali ichukue hatua zifuatazo kwa ajili ya wahitimu wa vyuo vikuu waliosomea ualimu, kwa ajili ya wahitimu wa vyuo vikuu wasio walimu, kuwaajiri kwa mkataba walimu wastaafu, kuwaajiri wahitimu wa stashada ya ualimu, kuendesha mafunzo maalumu ya ualimu kwa vijana waliohitimu kidato cha sita, kuwaajiri walimu wa kujitolea kutoka nje ambao tunategemea kuwapata mwezi Septemba na kuandaa mkakati maalum wa muda wa kati na mrefu ili kupata walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi zimewahi kutumika kwingineko si sisi tu Tanzania, kila panapokuwa na maendeleo Serikali inachukua hatua haraka sana, kwa mfano Zimbabwe nayo ilichukua hatua kama tunazochukua sisi na walitukaribisha tukajifunze kwao. Aidha, nchi yetu imepata kutumia njia za namna hii kukidhi mahitaji ya walimu kwa mafanikio kwa mfano Daraja "A" waliobobea kuna mwaka kati ya mwaka 1980 tulichukua walimu wa Daraja "A" ili kufidia upungufu wa walimu katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika katika vyuo vya Mkwawa na Korogwe tulichukua vijana waliomaliza kitado cha nne tukawapeleka kwa miaka mitatu tu wakasomea ualimu na pia wakasome kidato cha tano na sita wakawa walimu wa masomo ya Sayansi na hali kadhalika mafunzo ya Daraja "A" ili kukidhi mahitaji ya shule za msingi tumewapeleka kwa mwaka mmoja tu na mwaka wa pili pia wanapatia nje ya chuo. Yote haya ni katika kukidhi maendeleo yanayojitokeza kwa haraka kuliko ilivyotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wajibu wa kuwapa moyo vijana wetu wa kidato cha sita kwa kweli ningewaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla vijana wetu wanasoma asubuhi mpaka usiku ukienda huko shuleni ukakuta wanavyosoma, utafurahi. Sasa tunapolalamika jamani tusiwavunje moyo bali tuwape moyo tutawaendeleza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilikuwa ni kuongeza muda wa mafunzo kwa wanafunzi wa chaguo la pili, wengine wameanza hivi karibuni walikuwa wanafika Wizara ya Elimu kuomba usajili, tumewapa kwa sababu ya kuokoa vijana ambao wangebaki wanahangaika. Sasa tunachosema ni kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Meryce Emmanuel kwamba wamepoteza muda mwingi bila kusoma sasa tunasema ili wanafunzi waliochaguliwa awamu ya pili waende sawa kimasomo na wenzao Halmashauri na uongozi wa shule husika wanashauriwa kufanya taratibu za kufidia siku zilizopungua ili zifikie siku 194 za masomo kwa mwaka kama Waraka wa Elimu Na. 20 wa mwaka 1997 unavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Felix Kijiko, alizungumzia upungufu wa nyumba za walimu na sisi tunasema kwamba kweli upungufu wa nyumba za walimu upo, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya ujenzi wa nyumba za walimu kama tulivyosema mwaka huu wa fedha tutajenga nyumba za walimu 1,000 kwa uwiano wa madarasa mawili kwa nyumba moja ya mwalimu kulingana na fedha invyopatikana. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali Wizara inashindwa kutimiza azma yake hii. Kwa hiyo, natoa wito kwa wananchi wote kuendelea kujitolea kwa sababu mipango ya *MMES* na *MMEM* kwa sehemu kubwa inategemea nguvu za wananchi na kama nilivyosema kwenye bajeti kwamba tunategemea hata kwenye Maswali na Majibu tuliyokuwa tukitoa Bungeni kwamba tumeanza mazungumzo na *World Bank* na pia tumeongea na Serikali ya Ireland tukifanikiwa tutashukuru lakini kwa kiasi kikubwa tunategemea na nguvu za wananchi, kwa hiyo, tuendelee kujenga tu. *(Makofi)*

Hoja nyingine ilikuwa ni mazingira magumu ya kufanyia kazi ikiwemo upungufu wa nyumba za walimu kama hiyo niliyoizungumzia. Hiyo ilitolewa na wenzetu Wabunge saba ambao kama nilivyosema kwa ajili ya kuokoa muda kwa kweli nimewataja wote naomba nisirudie tena.

Hoja nyingine ilikuwa ni jinsi gani tunaweza kuwamotisha walimu wetu waweze kufanya kazi kwa bidii kwa kuwalipa madai yao ya malimbikizo. Katika hotuba yangu kwenye sehemu ya maamuzi muhimu tumezungumzia kwamba mwaka huu wa fedha 2006/2007 kwa Shule za Sekondari, Wakaguzi na Vyuo vya Ualimu waliopo chini ya Katibu Mkuu katika Kasma 46 wanalipwa fedha zao za malimbikizo. Wale walioko chini ya TAMISEMI naamini kabisa nao wana mpango wao wa kuwalipa walimu wa shule za msingi. *(Makofi)*

Hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu tofauti ya gharama za ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu katika mpango wa *MMEM* na *MMES,* tunachosema ni kwamba hii mipango kwanza imeanza kwa muda tofauti kwa mfano mpango wa *MMEM* ulianza

mwaka 2000 gharama zilikuwa tofauti na mpango wa *MMES* umeanza mwaka 2003 gharama tofauti, hilo ni la kwanza ndiyo limesababisha tofauti ya gharama.

Lakini hata hivyo tunasema mchoro wa darasa la sekondari chini ya mpango wa *MMES* una vipimo tofauti ukiangalia matofali yanatakiwa yalazwe halafu na vipimo pia ni tofauti kabisa, shule za msingi zenyewe tuliruhusu kwamba madarasa yake matofali yangeweza kusimamishwa.

Kwa hiyo, utaona hata utaratibu wa kujenga na wenyewe ni tofauti kabisa na kwa misingi hiyo tunasema bado tofauti ya gharama itakuwepo tu. Lakini hata hivyo kwa kuwa gharama za vifaa zinaendelea linaweza kuangaliwa na Wizara kwa kushirikiana na wadau.

Hoja nyingine ilikuwa Wizara ijenge maabara na kutoa fedha za vitabu, hoja hiyo imetolewa na Wabunge karibu nane, dhamira ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni kuhakikisha kuwa shule zote zinakuwa na majengo muhimu ikiwa ni pamoja na maabara na kuwa na vitabu.

Katika bajeti ya mwaka huu wa 2006/2007 tumesema kwamba tutajenga maabara 40 lakini tulikubaliana kwamba itakuwa maabara mbili kwa kila mkoa kwa hiyo itakuwa maabara 42, tutapeleka fedha wenyewe wataamua ni wapi maabara mbili hizo zijengwe.

Lakini hata hivyo tunaendelea na mazungumzo na *African Development Bank (ADB)* katika *Projet III* yaani Mradi wa Tatu wa Elimu ambayo tunategemea ukifanikiwa tutapata maabara 50 ambao pia tutaelekeza jinsi ambavyo tutasambaza.

Kuhusu vifaa vya kufundishia Serikali inatambua kuwa na umuhimu wa kuwa na vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika shule zetu hivyo Wizara inatoa ruzuku ya uendeshaji ili kuziwezesha shule kununua vifaa husika kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge tunatoa *capitation grant* ambayo ndiyo huwa inasaidia kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Hoja nyingine ilikuwa ni kwamba walimu wanafunzi kutolipwa kwa wakati posho zao, suala hili linafanyiwa kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, TAMISEMI na pia Tume ya Utumishi wa Umma kwa hiyo, naamini kabisa katika siku za hivi karibuni ufumbuzi utapatikana tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuongeza muda wa mafunzo kwa wanafunzi wa chaguo la pili ambalo hili tayari tumeshalizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine pia ilitolewa na Waheshimiwa Wabunge watano kuhusu umuhimu wa Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu umuhimu wa Elimu ya Watu Wazima katika kuwezesha washiriki kupata stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na pia kupunguza umaskini kwa haraka na kuimarisha demokrasia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia itazingatia ushauri iliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ili kufufua, kupanua na kuimarisha Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Juu na Elimu nje ya mfumo rasmi. *(Makofi)*

Aidha, Wizara yangu inakubaliana na mawazo yaliyotolewa kuhusu kuimarisha MEMKWA ili watoto wengi wa mitaami waliokosa elimu kuwa wanapata elimu kwa njia ya kujenga maadili mema na kuboresha maisha yao.

Ningependa pia kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba wawezaji wa MEMKWA wenye sifa hupatiwa nafasi ya kujiunga na Vyuo vya Ualimu na tumechukua wengi tu ili mradi tu wasiwe na zaidi ya *point 28* za ufaulu wa kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanapota mimba na uwezo kimasomo waruhusiwe kuendelea na masomo baada ya kujifungua, hili suala limejitokeza sana na kulingana na Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisho Na. 10 ya mwaka 1995 mwanafunzi anayepata mimba aidha wa shule ya msingi au wa shule ya sekondari anafukuzwa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tatizo hili sasa hivi ni la Kimataifa tutaliangalia na kulifanyia kazi zaidi kwa kushirikiana na Wizara kama vile Katiba na Sheria halafu pia na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kwamba Idara ya Ukaguzi wa Shule hutengewa fedha kidogo, fedha za *OC* na huchelewa kutumwa Wilayani, Wilaya hazina vyombo vya usafiri hivyo ukaguzi unaofanywa huwa hafifu, Maafisa Elimu wa Wilaya wawapatie wakaguzi usafiri na taarifa za ukaguzi wa shule haziletwi kwenye vikao vya Baraza la Madiwani ili kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kuwa Wilaya 56 kati ya Wilaya 122 hazina magari, Wizara yangu ina mpango wa kuzipatia Wilaya zote vyombo imara vya usafiri ili kuimarisha ukaguzi wa shule kwa awamu hii kutokana na fedha zilivyopatikana tutawapa Wilaya 18 magari, kwa kweli bila magari inakuwa ni vigumu sana kukagua. Kupitia Mpango wa *MMEM* na *MMES,* Idara ya Ukaguzi wa Shule itaendelea kupatiwa fedha zaidi kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito unaotolewa kwa Halmashauri ni kuwapatia Wakaguzi wa Shule usafiri na fedha hususan katika Wilaya ambazo hazina magari ili shule zote zikaguliwe kwa lengo la kuboresha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha kuona kwamba fedha cha *Other Charges* zinatolewa kwa wakati ili Wilaya zipate fedha hizo bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za ukaguzi wa Shule za Msingi zitumwe kwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri ambao ndio wenye shule, Afisa Elimu wa

Wilaya anatakiwa awasilishe taarifa za ukaguzi wa shule kwenye vikao vya Baraza la Madiwani hivyo Maafisa Elimu wa Wilaya wataelekezwa kuwasilisha taarifa za Ukaguzi wa Shule katika vikao vya Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Wakaguzi wa Shule ambao kiutaratibu siyo Wajumbe wa Baraza la Madiwani waalikwe basi ili waweze kuchangia nao katika vikao hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni viwango vya ada katika shule zisizo za Serikali, Waheshimiwa Wabunge wametoa malalamiko kwamba ada zinazotolewa katika shule zisizo za Serikali ni kubwa. Ni kweli lakini Serikali imetoa maelekezo ya viwango vya ada kupitia waraka wa elimu unaotoa kiwango cha ada kwa shule zisizo za Serikali katika Waraka Na. 9 wa mwaka 2002.

Kwa mfano, kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita katika shule za bweni ada ni shilingi 380,000/= kidato cha kwanza mpaka cha sita kutwa ni shilingi ada ni shilingi 150,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waraka wa Elimu wa Ada Wizara imetoa Waraka Na. 19 wa mwaka 2002 unaoagiza kuwa shule haziruhusiwi kuchangisha fedha nyingine ya aina yoyote kwa ajili ya kuendesha shule bila kibali cha Afisa Elimu Kiongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika kutoza ada, bado kuna matatizo. Ni suala ambalo bado linafanyiwa kazi, kwa sababu nao wanalalamika, wanatoa sababu mbalimbali. Kwa hiyo, bado tunalifanyia kazi ili tuweze kuangalia kwamba, kweli elimu haitolewi kwa njia ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine inahusu upelekaji wa fedha za MMES, ambayo pia imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi tu. Fedha za MMES zinatumwa katika Hazina ndogo Mikoani, ambapo Mkuu wa Shule akiwa na kibali cha Bodi ya Shule, anaweza kuchukua fedha hiyo kwa matumizi yaliyobainishwa na Wizara. Hivyo ndivyo matumizi ya fedha ya Serikali zinavyotakiwa kutumika na ndivyo tulivyokubaliana na Benki ya Dunia kuhusu fedha za MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapungufu yaliyoonekana katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango, yanayofanyiwa kazi, ikiwa ni pamoja na kuwa na Mratibu wa Shughuli za Elimu ya Sekondari katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaamini kabisa, baada ya kupata Mratibu wa Elimu ya Sekondari katika kila ngazi ya Wilaya, yaani kila Wilaya, watatusaidia sana kutuletea matatizo yote yanayojitokeza ili tuyafanyie kazi, ikiwa ni pamoja kuangalia matumizi ya fedha na pia kutupa taarifa kila wakati ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari. Lakini pia kuwa kiungo kati ya Wizara na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine iliyozungumziwa ya urasimu katika kusajili Shule za Msingi na Shule za Sekondari, zisizokuwa za Serikali. Usajili wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari zisizo za Serikali, ni mchakato unaoshirikisha wadau, wataalam, wakiwemo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Afya, Miundombinu, Ardhi na Serikalil za Mitaa. Aidha, mchakato huo unafanyika kwa Mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 na rekebisho lake Namba 10 la mwaka 1995, kwa lengo la kudhibiti viwango vya ubora. Kwa kuwa hatua hizi zinahitaji uthibitisho wa kisheria na kitaalam, kama vile umiliki wa eneo la Shule inakojengwa, uimara wa majengo na ubora wa majengo kiafya, ni vigumu kukwepa urasimu unaotokana na utaalamu au matumizi ya mamlaka ambazo haziko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, watakaoona dalili za rushwa, watoe taarifa ili tuchukue hatua. Wakati huo huo, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, kupitia Halmashauri, tusijenge shule tu zikawa nyingi, bila kuzingatia ubora, suala la ubora lizingatiwe. Hawa ni watoto wetu, wakae kwenye shule zenye viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali iangalie suala la wafadhili kutoa fedha pungufu kuliko wanazoahidi. Mimi ningependa kusema kwa uwazi kabisa kwamba, Mipango ya MMEM na MMES ili iwe endelevu, lazima itegemee nguvu za wananchi. Kwa sababu tukitegemea wafadhili, siku wakitoka hii mipango itakufa. Lakini kwa kuwa tunataka iwe endelevu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mtusaidie huko kuwahamasisha wananchi ili kwa sehemu kubwa, nguvu za wananchi zitumike. Halafu Serikali iongezee pale ambapo nguvu za wananchi zinapopungua, kufuatana na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni elimu kwa wasichana, nayo imezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana na wamesema kwamba, Sekondari za kutwa, haziwasaidii wasichana, zinawaletea matatizo na kusababisha pengine hata washindwe kuendelea na Elimu ya Chuo Kikuu.

Sasa ujenzi wa mabweni au hosteli ni mojawapo ya mikakati ya kupunguza kiwango cha wasichana kuacha masomo. Katika kuhakikisha kwamba, suala la ujenzi wa hosteli linapewa umuhimu unaostahili, Serikali ilitoa mwongozo wa ujenzi wa hosteli na namna ya kuziendesha katika Waraka wa Elimu Namba 12 wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga hosteli za wasichana ili kuwanusuru katika mazingira hayo, ni vizuri wananchi tukalizingatia suala hili kila tunapojenga shule za kutwa. Kwa mfano, tumekuta mahali pengine, shule nyingi sana ni za kutwa lakini zote hazikujaa. Lakini wangejitahidi wakajenga chache, halafu moja wakajenga yenye hosteli ili wasichana wawanusuru wakae mle, ingekuwa ni vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi, kwa kupitia Halmashauri katika kuamua kujenga shule, mliangalie sana suala hili ili zisiwe shule nyingi za kutwa, ambazo kama tulivyosema, kwa njia moja au nyingine, zina athari

kwa wasichana. Shule moja au mbili, mjenge hosteli, halafu Serikali itaongezea pale ambapo inaweza kuongezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine muhimu sana iliyotolewa ilikuwa ni ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tanzania Bara na Zanzibar. Sisi tunasema kwamba, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tanzania Bara na Zanzibar, wanashirikiana. Vikao na ziara mbalimbali zimeanza, juzi tu kundi zima la watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, walifurahi sana, kupanda meli kwenda Zanzibar. Nashukuru sana, walipokelewa vizuri wakawa na mazungumzo mazuri sana, ambayo yametusaidia kuona kwa jinsi gani tunavyoweza kuendelea kusaidiana katika siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za bweni kwa wafugaji, kwa kweli hata sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tunaona kuna ni muhimu sana kuwa na shule za bweni katika maeneo ya wafugaji. Kwanza, tunataka tuwapate wale wavulana na wasichana, lakini zaidi ya yote, wasichana ili nao waendelee. Kwa hiyo, tunazitilia kipaumbele hata zile hosteli tulizochagua, kama mmeona kuna hosteli tano, nadhani kipaumbele kitatolewa kwa shule ambazo ziko katika maeneo ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kurudishwa kwa masomo yaliyokuwa yameondolewa. Tunamshukuru Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na wengine waliochangia wengi tu, kwa kweli kumtaja mmoja itakuwa siyo haki kuwaacha wengine; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Prof. Feetha F. Banyikwa na Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba. Walitupongeza kuhusu kurudisha mitaala ya zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, alisema kwamba, wamejenga maboma 2,692 yanasubiri Serikali ipeleke fedha. Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, karibuni ofisini tuzungumzie juu ya hayo maboma 2,692, yote hayana mapaa na nyumba za walimu 1,858 yote ni maboma, karibu ofisini tuongee kwa kweli. Yeye amemaliza nadhani tatizo la nyumba za walimu katika Wilaya nzima, lakini jinsi ya kuezeka, nadhani tukubaliane uje ofisini tuongee kwa kweli ni mzigo mkubwa sana huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ilikuwa ni kufidia majengo yaliyotumiwa kwa ajili ya madarasa ya *High Level* katika Sekondari ya Njombe. Hili lilikuwa la Mheshimiwa Naibu Spika. Katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, fedha zimetolewa kujenga madarasa mapya katika shule mpya inayojengwa Njombe ili wanafunzi ambao watakuwa wamekosa kuingia katika Shule ya Njombe, wapate nafasi katika shule hiyo mpya. Serikali inaendelea kutoa ruzuku ya ujenzi wa madarasa katika shule za eneo hilo la Njombe. Ombi la matengenezo ya Shule ya Mbiji, ambayo ni ya Serikali, limepokewa na linafanyiwa kazi. Waambie tu Mheshimiwa Naibu Spika, unawatetea na tunakusikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ilikuwa ni watoto wa kike kufichwa na wazazi ili waolewe, licha ya kufaulu mtihani katika baadhi ya vijiji.

Kwanza, sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tunasema tunakilaani kabisa kitendo cha wazazi kuwaficha watoto wa kike ili waolewe licha ya kufaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi lazima nichukue nafasi hii kumshukuru mzazi wangu, Mzee Simwanza, kwa kweli hakunificha, ndiyo maana nimefikia nafasi hii. Sasa kwa nini wengine wawafiche nao wasifikie nafasi hii? Nadhani sisi wote tunakilaani kabisa kitendo cha watoto wa kike kufichwa, tuwaache wasome, baadaye ndiyo waolewe kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja ya deni la umeme la Shule ya Sekondari ya Wasichana Bwiru, linaathiri upatikanaji wa maji katika shule. Sasa hivi tumejizatiti kabisa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tumeweka Maafisa Wahasibu Maalum, kwa kujua hili tatizo kwa kweli ni baya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka nikiwa mgeni kabisa katika Wizara, niliona kwenye gazeti, Shule ya Sekondari ya Benjamin William Mkapa haina maji, vyoo vitafanyaje kazi, kwa kweli ilikuwa ni taarifa mbaya sana. Tukaenda kule tukakuta kweli hali ni mbaya. Kwa hiyo, kuanzia pale, tulishaweka sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Maafisa Wahasibu Maalum, ambao kazi yao tangu asubuhi mpaka jioni ni kulipa ankara za umeme na maji na kwa kweli shule ambazo zitakuwa zinakosa kulipiwa ankara hizo za umeme na maji, tutumieni taarifa mapema sana ili Wahasibu wanaochelewesha suala hilo kwa kweli wachukuliwe hatua. Tumeona ni suala la kiuzembe, kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua nafasi hii, kuwashukuru wote, waliofichua suala hili la kuwaficha watoto wa kike na hili suala la ulipaji wa ankara za umeme na maji. Kwa kweli haya masuala mawili ni ya maana sana, ambayo yanatuathiri sana kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja mbili tu za mwisho. Ya kwanza, ilikuwa tuweke malengo mazuri, yasiyozalisha matatizo na ningependa kurudia kusema kwamba, tuwe tayari tutakapo hamasishwa na Serikali, tuitikie yatakayotokea, tuyakabili, tusiwe waoga wa kuleta mabadiliko. Hata kama ni kwa kujikamua kwa kiasi gani, mabadiliko yoyote yatakayotuvusha kutoka hatua moja mpaka nyingine, tuyakubali na tunaendelea kuwashukuru wale wanaoitikia kwa manufaa ya Taifa letu.

La mwisho katika hoja za leo ambazo tumezitolea ufafanuzi ni mafunzo ya Maafisa Taaluma wa Wilaya, Vifaa na Takwimu na Waratibu wa Elimu Kata, wapewe mafunzo. Mafunzo kwa Maafisa Taaluma na Takwimu, kwa kweli na sisi tunaona ni jambo la muhimu sana. Kwa msingi huo, tunasema kwamba, mwaka huu tumeshatenga fedha kwa ajili ya Maafisa Taaluma wa Kata 2,300, watakwenda kupata mafunzo ili watusaidie kuendeleza taaluma mashuleni, lakini pia watusaidie kutuletea takwimu zinazohitajika kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba radhi kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia, ambao sikuwataja, Mheshimiwa Felister A. Bura, naomba uniwie radhi

ulichangia. Halafu na mwingine ambaye alichangia sikumtaja ni Mheshimiwa Ephraim N. Madeje. Naomba mniwie radhi, lakini nawashukuru kwa michango yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nirudie kutoa shukrani kwa wananchi wote, kwa niaba ya Serikali, kwa jinsi ambavyo wametusaidia sana katika Mpango wa MMEM na MMES, bila wananchi tusingeweza kufanikiwa. Ila ombi langu kubwa ni moja, tuzingatie ubora katika majengo tunayojenga, yawe yenye viwango kwa manufaa ya Taifa letu. Tusitoe elimu tu, bali tutoe elimu bora na sisi kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tutajitahidi kadri iwezekanavyo kuzingatia maoni yenu ili tusaidie kuboresha elimu ya nchi kwa manufaa ya Taifa letu. Tukijua wazi kabisa elimu tunayotoa ndiyo dira ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao na kama nilivyosema, naomba radhi sikutaja majina yote, lakini nawashukuru kwa michango yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 - *Administration and General* … … … Sh.25,744,678,200/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** wakati nachangia nilimwuliza Mheshimiwa Waziri, juu ya Sera ya *Secondary Schools. Sub-vote* 1001 na kifungu kidogo 250100, Mshahara wa Mheshimiwa Waziri, *issue* ya Sera. Wakati nachangia nilieleza kwamba, watu wengi tumehamasishwa Shinyanga. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuja akatuhamasisha na kweli tukagundua watu kama wa Shinyanga na sehemu nyingine, tulikuwa na matatizo makubwa sana ya *Secondary Schools*. Tunawashukuru wananchi, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, wamejitahidi. Kwa kweli tumejitahidi Bariadi sasa tuna shule karibu 20 hivi na karibu shule 15 tumezijenga kwa wakati huu mfupi, ambapo tumehamasishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikiangalia hili tatizo na nikiangalia takwimu ambazo ametupa Mheshimiwa Waziri, wameandikishwa watoto karibu milioni 1.6 kwa mwaka 2002, ndiyo kusema mwaka 2008 tutakuwa na watoto ambao watakuwa wanamaliza darasa la saba. Mungu awabariki. Tutahitaji vyumba vya madarasa karibu 40,0000 ili hao watoto waweze kupata nafasi ya Kidato cha Kwanza. Sasa tumeona kwamba, tukihamasishwa kwa kuamini Sera hii ndiyo inafaa na ujenzi unafanyika. Tumeamua watoto wetu wote, wataenda *Primary Schools,* fedha zimepatikana na *Primary Schools* zimejengwa na MMEM imefanya kazi vizuri na ninaishukuru Serikali imefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hatuna umeme, shilingi bilioni 450 zimepatikana na umeme unawekwa. Sasa kwa nini tusiamue leo ndiyo nasema la Sera kwamba, *Basic Education* ni *Secondary School*. Tukiamua kama *Baice Education* ni *Secondary School,* basi ndiyo kusema, kila mmoja atachacharika katika muda huu wa miaka mitano, kuhakikisha kwamba, kweli watoto wetu wote wanaoingia darasa la kwanza, wanaendelea na masomo ya *Secondary Schools.* Mpango wa sasa, Mheshimiwa Waziri hautufai, kwa mfano, kama Bariadi imebidi tufikie kasi kubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, naomba ukae chini kidogo. Pamoja na kanuni kusema ni kupata ufafanuzi, wewe unaanzisha hoja mpya kabisa ya kujadiliana, kwa sababu hapa tunasema yaliyoko hapa. Kilichopo hapa sasa hivi ni kwamba, *Basic Education* ya darasa la saba. Sasa ukianzisha *stage* hii mpaka *Secondary School,* itakuwa ndefu sana. Kwa hiyo, naomba sana tuna-*stick* hapa, hatuwezi kuingia kupanua Sera mpya kwenye kifungu hiki.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa umenitafutia maneno, nakubaliana na wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuuliza *specifically,* mwaka 2008 kutakuwa na watoto 1,646,000, ambao watakuwa wamemaliza darasa la saba. Kisera kuna utaratibu gani, ambao Wizara inafanya, kuhakikisha watoto hao wapata nafasi ya kuendelea na masomo? Kwa sababu ukiangalia kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, atajenga mwaka huu madarasa 1,646, ukilinganisha na takwimu za watoto watakaomaliza darasa la saba mwaka 2008, ni sawasawa itamchukua miaka 25 kuweza kuwapatia watoto hao madarasa ya *Secondary Schools* wanayohitaji. Kwa hiyo, tunataka sasa mtazamo ambao ni endelevu, ambao unatuonesha tutafika wapi. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilipokuwa nachangia *policy,* nilizungumzia juu ya *safety* ya watoto zaidi katika mabweni. Bariadi Shule ya Nanga, mwaka 2005 mtoto aliungua moto akafa, kwa sababu alikuwa anajisomea darasani, hakuna umeme. Sasa nasema, kwa nini *generators* zisiwe mojawapo ya *requirement* za kuhakikisha kuwa shule hizo zinapatiwa umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tunapouliza hapa ni dakika tano ndizo tunazokupa. Kwa hiyo, ni suala la kwanza na la pili. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa John M. Cheyo, kwa kuonesha jinsi ambavyo anajali elimu. Mimi nilikuwa nafikiri suala la umeme na *generator,* angelileta wakati wa kipindi cha maswali na majibu, tungemwandalia vizuri kabisa mipango gani tuliyonayo kuhusu hilo. Lakini kwa kipindi kama hiki, kwa kweli hatukuzungumzia suala la umeme wa *generator* katika Shule za Sekondari, ila tumezungumzia juu ya ulipaji wa *bill* za umeme. Uanzishaji wa matumizi ya *generator,* kwa kweli hatukulizungumzia, lakini tuko tayari kulifanyia kazi wazo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** La kwanza alilouliza ni kwamba, watoto walioanza darasa la kwanza, sasa itakuwaje baadaye?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja kubwa kama nilivyozungumza katika Mpango wa MMEM. Mpango wa MMEM na Mpango wa MMES ni endelevu, unaendelea na kwa sehemu kubwa nimesema itategemea Serikali, wananchi na Halmashauri. Naamini kabisa katika Mpango huu, kwa mfano, sasa hivi tumeleta Mpango wa 2006 – 2007, lakini pia tuko tayari kueleza Mpango wa tangu mwaka 2007 – 2008.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, avumilie tu tutaleta, kwa sababu hata sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tunaelewa wimbi kubwa la vijana linakuja. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa kutumia Serikali, wananchi na Halmashauri, tutaweza tu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nazungumzia Fungu 46, Programu ya 10, *Subvote* 1001, kifungu kidogo cha 280500. Nataka kupata ufafanuzi kwamba, hapa ndiyo *Subsidy* inayokwenda *VETA* inatoka au hapana? Lakini kwa vyovyote vile, nataka nipate uhakika kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kama alielewa hoja ambayo niliieleza. Kwa sababu kwanza, nilionesha masikitiko yangu kwamba, pale *VETA*, chuo kile kilikuwa chini ya Wizara ya Kazi, inayosimamia Sheria ya Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale pana uvunjaji wa Sheria ya Kazi, kuna vijana wanamaliza masomo yao vizuri, wanawachukua wanakaa miaka sita bila ajira. Sasa nilisema Mheshimiwa Waziri hilo ulishughulikie, kwa sababu Serikali itashindwa kukemea hoteli nyingine, ambazo zinafanya hivyo. Ni hilo tu kama alinielewa, sina hoja zaidi ya hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, unaweza kujibu wewe au wasaidizi wako wanaweza kukusaidia tu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala analolizungumzia Mheshimiwa William H. Shellukindo ni kweli tunapaswa kushughulikia ajira ya wafanyakazi waliokuwa *VETA* na hata leo hii mchana kulikuwa na barua nyingine ambayo tunaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa hivi tunashughulikia jinsi ya kufanya kazi pamoja na *VETA*. Kwa hiyo, tumepata mtaalamu, anayeandaa vizuri kabisa jinsi ya kuhuisha *VETA* na utaratibu mzima wa utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, usiwe na wasiwasi, wafanyakazi wanatendewa haki tu.

Kifungu alichokitaja Mheshimiwa Mbunge, sasa hivi kinachozungumzia *ADEM*, kile Chuo chetu cha Mafunzo na *Library,* pamoja na *NECTA*, yaani Baraza la Mitihani. Kwa hiyo, tutakapokuja kwenye vifungu vingine, ataona kabisa kwamba, *VETA*

imejitokeza peke yake, hata kwenye Kitabu cha Maendeleo. Tumelipokea hilo na tutalifanyia kazi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kupata ufafanuzi. *Vote 46,* Programu 10, *Subvote* 1001, kifungu kidogo 250100 - mshahara wa Waziri. Sina matatizo na Mshahara wa Waziri wangu, ndugu yangu na Mwenyekiti Mstaafu mwenzangu wa Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri, hakupata nafasi ya kunijibu kama alivyosema, hoja zilikuwa nyingi na sisi tuko wengi. Katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea matatizo yaliyoko katika Baraza la Mitihani. Kwamba, baada ya mabadiliko ya uongozi na kuja kiongozi mpya pale, amekuja kwa kishindo na makeke, kiasi kwamba, hata wafanyakazi hadi sasa siyo chini ya 35 na pengine wanakaribia 40. Sasa wameshaondolewa katika Baraza la Mitihani, bila kujali uzoefu ambao wameujenga katika Baraza lile, kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona hiyo ni hasara kubwa sana na inasemekana kwamba, nia ni kuondoa zaidi ya asilimia 50, kwa nini? Kwa sababu hataki kufanya kazi na wafanyakazi aliowakuta pale, yeye anataka aje na watu wake wapya. Sasa kama Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, angefanya hivyo, sijui ingekuwaje? Sasa nataka nipate maelezo kwa nini hali hii imetokea?

Lakini la pili, wafanyakazi katika kuondolewa, barua walizopewa zimeandikwa na Katibu Mkuu wa Wizara, wakati hawa wameajiriwa na Bodi ya Baraza la Mitihani. Bodi haina habari, lakini Katibu Mkuu wa Wizara, ndiye aliyeandika barua kwa mtu mmoja mmoja, Mohamed Missanga, Juma Hassan, kwamba wewe unaondolewa hapa nenda sijui wapi na kadhalika. Huo ndiyo utaratibu!

Lakini vilevile kama wana matatizo, Tanzania tunaheshimu Utawala Bora na Tanzania tunaheshimu haki za binadamu, haki za binadamu ni pamoja na haki za wafanyakazi. Kama wana matatizo, kwa nini wasiandikiwe barua wakaelezwa matatizo yao na mapungufu yao, wewe Mohamed Missanga, una tatizo moja, mbili, tatu, nne, tano, jieleze iende katika utaratibu unaojulikana kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wangu yeye ni mtaalamu kama nilivyosema, sisi sote tunatoka katika Vyama vya Wafanyakazi, tunajua Sheria za Kazi. Kwa nini hao wafanyakazi kama wana matatizo, wasifikishwe katika vyombo vinavyohusika na ikaamuliwa tu wote kwa pamoja, wafanyakazi 35 au 40 wahamishwe? Zoezi limesimama sasa kwa sababu ya kungojea Kikao cha Bunge kimalizike, kama si Kikao cha Bunge, wangeshafika wafanyakazi 80 na kadhalika na kadhalika. Kwa sababu kiongozi huyo, anataka akae na watu wake wapya, hataki wale wafanyakazi wa zamani. Napenda nipate maelezo, kwa nini hali kama hiyo imetokea?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nitoe maelezo kutokana na maswali mawili,

aliyoyatoa Mheshimiwa Mohamed Missanga kama ifuatavyo: La kwanza, amesema kwa nini imetokea, yaani kwa nini kumekuwa na mabadiliko? Kwa kifupi tu ni kwamba, ili kuleta ufanisi katika utendaji ndani ya Baraza. Baraza ni mahali nyeti sana, panahitaji kila wakati kuwa na amani. Kwa hiyo, yaliyofanywa yote ni kwa lengo la kuleta ufanisi katika Baraza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mohamed Missanga kwamba, nimefanya kazi kwa kushirikiana na Baraza. Mimi nikiwa mgeni pale Wizarani, kati ya wageni wa kwanza kuja kuniona ni Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Mitihani. Nakuhakikishia yote yaliyofanyika ni kutokana na ushirikiano wa Baraza la Mitihani. Ni kweli wana uzoefu, lakini nao walipoingia pale walikuwa hawana uzoefu, baadaye wakapata. Kwa hiyo, naamini kabisa wengi ni walimu. Walioingia pale ni walimu na walioingizwa pia ni walimu, naamini nao watapata uzoefu tu.

Halafu kitu kizuri ambacho ningekuongezea Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, wamekwenda na haki zao zote. Lakini mawazo yako mengine uliyoyasema tuendelee kufanya uchunguzi, tunayapokea na tutayafanyia kazi.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Ahsante Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Mimi wala sina tatizo, sana ni ufafanuzi tu. *Vote 46*, programu 10, *subvote* 1001 chini kabisa *item* 260200 - *Educational Materials, Supplies and Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka tu kufahamu katika hotuba ukurasa 32 na mimi mwenyewe nilichangia. Wizara au Serikali imeeleza kabisa kwamba, imejikita katika ununuzi wa vifaa vya mashuleni, hasa shule za watoto wenye ulemavu tena wa aina nyingi tu, hiyo ni hongera. Sasa niliuliza kwamba, je, ni kiasi gani cha fedha sasa katika hizi ndizo zote za hapa au ziko wapi za kununulia hivyo vifaa? Hicho tu basi, nataka kufahamu *amount* iliyotengwa kununulia vifaa hivyo.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ili nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, kama ifuatavyo:-

Vifaa vya Shule Maalum vitanunuliwa, kama tulivyosema hata miundombinu itatengenezwa. Naomba uvute subira, utaiona baadaye tutakapokuja kwenye Mpango wa MMES na MMEM.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Ahsante Mwenyekiti, programu ya 10, *subvote* 1001, kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri. Kwanza, naishukuru Serikali kwa hatua ambazo imeshachukua, kuhusiana na tatizo lililokuwa limejitokeza. Lakini pamoja na hilo, napenda nipate ufafanuzi kidogo zaidi. Je, endapo majibu ya *DNA* yatakuwa *negative,* mwalimu mtuhumiwa atakuwa amepona kosa la kubaka na hivyo kurudishwa kazini? Hilo la kwanza.

La pili, je, endapo majibu yatakuwa *positive,* nini itakuwa hatma ya mwanafunzi aliyebakwa?

Swali la tatu, je, Serikali itachukua hatua gani dhidi ya *DO*, aliyemhamisha mwalimu mtuhumiwa, mara baada ya kosa kufanyika badala ya kumchukulia hatua za kinidhamu?

Swali langu la nne, ni kwa nini imechukua zaidi ya miezi mitano tena mpaka kuja kupitia katika Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo Wizara imeweza kutoa majibu iliyoyatoa leo hii?

Ahsante Mwenyekiti. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ahsante Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi nitoe ufafanuzi wa maswali kama manne hivi, yanayohitaji ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Charles M. Kajege.

La kwanza, suala hili kama alivyosoma Naibu Waziri, katika kutoa ufafanuzi wa maswali yaliyohusiana na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba, hili suala liko Polisi, tayari limeshafunguliwa na jalada na alishasoma hata jalada namba ngapi. Kwa misingi hiyo, bado linafanyiwa kazi. Kwa hiyo, kama ni suala la jinai, litachukua mkondo wa kijinai huo huo. Kwa hiyo, tungojee lifanyiwe kazi, halafu tutajua, kwa sababu kama atapatikana na hatia, atachukuliwa hatua za kisheria kutokana na kosa lenyewe la kijinai. Lakini kama hatapatikana na ikathibitishwa kutokana na Sheria za Utumishi kwa taratibu za kazi ya ualimu, naye atachukuliwa hatua zinazopaswa, kwa sababu kuna Kamati katika maeneo yake. Mimi naomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira.

La pili, kuhusu hatma ya yule msichana, tumetoa taarifa, hatukutaka tu kutaja majina, tuna jina la mtoto. Yule msichana si kwamba, ilitoka mimba kama ilivyotolewa hapa, amejifungua mtoto tarehe 9 Februari, 2005. Jina tunalo ila hatutaki kutoa majina ya watoto wa watu. Kwa hiyo, sasa inakuwa ni suala, je, huyu msichana aliyezaa arudi shuleni? Labda hili ndilo suala la kuulizwa ambalo mimi siwezi kulitolea jibu. Kama nilivyosema, Sera ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 na Marekebisho yake Na. 10 ya mwaka 1995, bado hairuhusu msichana aliyejifungua kurudi shuleni. Sasa kama atachukuliwa kwa uzito wa pekee, suala hili Wizara ya Elimu italiangalia.

Lakini kisheria, ukichukua kama tu msichana aliyezaa hapaswi kuwa shuleni, nimesema hapa kwenye majibu yangu kwamba, tutafanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, pamoja na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Tutalifanyia kazi, lakini mpaka sasa hivi jibu ni kwamba, hawezi kurudi shuleni kwa sababu amejifungua na ana mtoto mzuri kabisa wa kike. Kuhusu yule *DO*, tayari amesha shughulikiwa, kwa kuandikiwa onyo kwa nini hakuchukua hatua wakati ule.

La mwisho la kusema kwa nini hukupata taarifa, nadhani labda hiyo ni kweli kwa sababu lilikwisha shughulikiwa mwezi wa sita. Suala lilikuwa ile barua kwamba, angepewa nakala Mbunge kwa taarifa. Lakini ilisha shughulikiwa tangu mwezi wa sita. Sasa hivi hata kama ungepata nafasi, karibu lipo hapa hapa ofisini tunalo. Ungeweza kuona barua ambayo kwa kizungu, ingetumia *authentic* kutoka kwenye wale waliofanya utafiti ule.

Naomba tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo, wakati mimi nimeku-*interrupt* dakika zako zilikuwa *considered.*

Halafu tunaposema wasimame watu, tunaandika majina, kama hukuandikwa hatuwezi kukupa nafasi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1001 – *Finance and Accounts* … …. ….. Sh. 562,495,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … ….. Sh.1,384,164,700/=

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 1003. Nimejaribu kutazama katika eneo lote, mahali ninapotaka kuulizia uweze kunisaidia ni kuhusu Elimu ya Watu Wazima. Nadhani labda itaingia kwenye eneo hili. Katika Elimu ya Watu Wazima, ambayo inasisitizwa kwa wakati huu, mafungu yanatolewa na yanalipwa, lakini tunatazama maeneo mengi na hasa kwangu, ingawa mafungu hayo yanalipwa, hakuna wanafunzi wa Elimu ya Watu Wazima wanaosoma, lakini fedha inalipwa. Nilikuwa naomba nifahamu haya madarasa ya Elimu ya Watu Wazima, Mheshimiwa Waziri yapo ama hayapo? Kama hayapo, kwa nini bado fedha zinaendelea kutolewa lakini bado Watendaji wetu wanaendelea kula hizo fedha? Mimi nina ushahidi kwenye Halmashauri yangu, ambapo fedha zimeliwa kwamba, wamewalipa walimu wanaofundisha Elimu ya Watu Wazima lakini hakuna darasa hata moja la Elimu ya Watu Wazima katika eneo langu la Nkasi. Ninaamini na maeneo mengine hali iko hivyo. Je, ni kwa nini fedha zinatolewa zinaliwa bure lakini madarasa hayapo? Naomba maelezo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii, nitoe ufafanuzi wa maswali yaliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Elimu ya Watu Wazima ina maeneo mengi, watu Wazima ambao ni wazee, lakini pia ukiita Elimu ya Watu Wazima ni pamoja na wale ambao wameshapita umri wa kuanza shule, yaani zaidi ya miaka 13. Wale nao wanaingia katika Mpango wa Elimu ya Watu Wazima, ambao ndio wanafundishwa kwa utaratibu unaoitwa MEMKWA na mwingine unaoitwa MUKEJA au MKEJA, ule ambao unasema unashirikisha jamii, Mpango wa Ushirikishaji wa Jamii katika kutoa elimu. Sasa hivi ndio tumetilia mkazo na ndio kifungu chenyewe hicho.

Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kwa suala lile la Elimu ya Watu Wazima, kama tulivyokuwa tumezoea kuiona miaka ya 1970, kwa sasa hivi ndiyo tumejitahidi hata Mkurugenzi wa Idara husika, anaandaa mkakati wa kufufua Elimu ya Watu Wazima kwa sura ile tuliyoizoea katika miaka ya 1970. Kukuta akinamama mahali labda wanapotengeneza pombe au wapi, unawakalisha pale chini ya mti. Huo ndio mkakati tunaotaka kuurudisha, ambao tuliona ulifanya kazi vizuri sana, mpaka tukafikia asilimia 95 ya watu wanaojua kusoma na kuandika. Lakini kwa sasa hivi, fedha zinazokwenda kwa ajili ya kulipia wale wa MEMKWA, ndizo hizo tunazoita Elimu ya Watu Wazima, ingawa pamoja na hivyo, katika fungu hili hili kuna ile Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, ambayo inasaidia wale wanaosoma nje ya Mfumo Rasmi, kwa utaratibu wa masafa, yaani *Correspondence* na taratibu nyingine. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge, kuonesha kwamba kuna haja kwa kweli ya kurudi nyuma na kurudisha ule mtindo wa ufundishaji wa zamani wa kuketisha wazee chini ya mti na ubao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu hayo mazuri na ya kuridhisha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Lakini naomba nifahamu, kwa vile tayari kwenye Halmashauri yangu madhara hayo yamekwishatokea. Hata yule anayesimamia huo Mradi na yeye hakufahamu, hizo fedha zimetokatokaje bila idhini yake. Baraza la Madiwani walipojaribu kuhoji baada ya mimi mwenyewe kutoa hoja hiyo kwamba, hizo fedha zimekwenda wapi, bado mpaka leo wameshindwa kutoa jibu sahihi na wamekiri kwamba, hizo fedha zilitumika kinyume na utaratibu. Kwa vile fedha hizo zinatoka kwenye eneo lako bila kujali ni nani, wa eneo lipi, aliyekula hizo fedha, ni hatua zipi zitakazoweza kuchukuliwa dhidi ya watumishi, ambao wanaweza wakachukua mafungu ovyo ovyo wakala wakati ambapo hawakufanya kazi?

Nimeridhika lakini naomba tu nijue mtafuatiliaje katika eneo langu la Nkasi na pengine maeneo mengine ya Halmashauri ili uzembe huu na ubadhirifu huu sasa ukome?

Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa tu maelezo ya ufafanuzi juu ya eneo ambalo Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami ameliulizia. Watumishi tulionao katika Halmashauri wako katika ngazi mbili. Tunaye Mkurugenzi, ambaye Mamlaka yake ya nidhamu ni Waziri mwenye dhamana au Waziri ambaye anasimamia eneo hilo. Watumishi wengine waliobaki, ikiwa ni pamoja na Wakuu wa Idara na wafanyakazi wengine wa ngazi za chini, wote hawa wako chini ya Mamlaka ya Halmashauri husika, kwa maana ya Baraza la Madiwani. Kwa hiyo, kama wako watu wabadhirifu wa aina hiyo katika Halmashauri yako ya Nkasi, jambo hili lisimamiwe moja kwa moja na Baraza la Madiwani, wawachukulie hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu katika eneo hili, Waheshimiwa Wabunge tusaidiane, maana tumelisema hili jambo mara nyingi, tumetoa na mwongozo

hivi karibuni wa kusaidia eneo hili, tusiwaendekeze wazembe hawa wakati taratibu ziko wazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Chief Education Officer* … … … …. Sh. 3,817,072,800/=
Kif. 2002 – *Inspectorate* … …. .... ..... ..... ..... Sh. 4,719,633,500/=
Kif. 3001 – *Basic Education* … … …. .... ..... Sh. 25,588,678,000/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – *Secondary Education* … …. … ... Sh. 62,281,866,100/=

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 46,* programu 40, *subvote* 4001, kipengele kidogo 250100 vile vile 260200.

Wakati tunachangia na mimi nilichangia, Wabunge wengi wameonesha wasiwasi kwamba, watoto wanaokaa kwenye Bweni wanakula chakula kibaya sana kiasi ambacho tuna wasi wasi kwamba, wameshapata utapiamlo na wengine wamevia akili. Serikali ilikuwa inatenga shilingi 862.47 ambazo zilikuwa hazipelekwi zote. Matokeo yake ni kwamba, watoto wanakula ugali na maharage tu. Tukauliza, kama Wakuu wa Shule sasa hivi wameshapeleka mapendekezo yao kwamba, angalau waongezewe wapewe shilingi 1,260 kwa kila mwanafunzi kwa siku. Kwa hiyo, angalau mtoto aweze kupata matunda mara moja kwa wiki na aweze kupata angalau na nyama mara moja kwa wiki, ambayo sasa hivi huwa wanakula siku ya *graduation* tu.

Sasa naomba nielezwe, kwenye kipengele hiki wanafunzi wa Shule za Bweni wametengewa kiasi gani?

Pili, tulichouliza ni kwamba, hawa Wakuu wa Shuleni jamani ambao kila Mkuu wa Shule unakuta ana *diploma,* ana digrii mbili au tatu, anapopewa Ukuu wa Shule, ni kazi tu haina *scale.* Nikawauliza Serikali kwa nini Wizara inapata kigugumizi kuutamka huu Ukuu wa Shule ukawa *substantive post,* badala ya kuwa *duty post,* ikaeleweka Mkuu wa Shule anapoajiriwa, ataanzia kwenye mshahara kiasi gani. Sasa hivi wanapata mshahara kuliko walimu walio chini yao, tunaendelea kuwa-*frustrate*.

Mwisho, tulisema walimu wanaoajiriwa katika Wizara ya Elimu, wanachukua mwaka hawajapata mshahara, hata vijana wa Kidato cha Sita walioajiriwa mwaka 2005, hawajapata mshahara mpaka sasa hivi. Kwa nini katika Wizara ya Elimu, mishahara inachukua *that long,* wakati katika Wizara nyingine, mtu akiajiriwa baada ya miezi miwili anapata mshahara? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, nitoe ufafanuzi kutokana na hoja tatu zilizotolewa na Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu chakula, ni kweli Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inatambua kwamba, kuna haja ya kuimarisha utoaji wa chakula shuleni na katika huu mwaka wa fedha, ukiangalia katika kifungu kile ambacho kipo hapa hapa 260200 - *Education Materials, Supplies and Services.* Katika hizo shilingi bilioni tisa ulizoziona hapo, shilingi bilioni 5.7 ni za chakula, lakini pia ukienda kwenye *SEDEP* kuna shilingi bilioni tano. Kwa hiyo, kuna kama shilingi bilioni 10 na zaidi, utakuja kukuta kwenye kifungu cha MMES pia kuna chakula. Kwa hiyo, ziko kama zaidi ya shilingi bilioni 10, ambazo zimetengwa kwa ajili ya chakula. Lakini kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana, tutaongezea, kwa sababu hawa ni watoto wetu.

La pili lilikuwa ni kuhusu *Scheme of Service*. Ni kweli lakini kama umesoma Mheshimiwa Mbunge kwenye kitabu, kwenye sehemu ya maamuzi muhimu, utaona tumeandika pale kwamba, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tunapitia *Scheme of Service* ya walimu katika maamuzi muhimu, ukisoma kwenye kitabu cha bajeti.

Halafu la tatu, lilikuwa ni kuhusu mishahara kuchelewa, napenda Mheshimiwa Mwenyekiti uniruhusu kabisa hapa kwamba, jana tulikuwa na kikao cha maana sana, kuzungumzia masuala haya chini ya Uenyekiti wa Waziri Mkuu. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni suala ambalo linafanyiwa kazi kwa muda mrefu na naamini kabisa katika muda mfupi ujao, hili suala la walimu kuchelewa kupata mishahara, hawa walimu wapya, litakuwa limekwisha. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ningependa kupata ufafanuzi. Nilitoa mchango wangu kwa maandishi. Programu ya 40, *subvote* 4001. Hapa nimetazama kipengele cha kukikamata nimekosa, lakini nataka kuzungumzia juu ya Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi napenda nishukuru kwamba, Serikali imetoa nafasi kila Kata iweze kuanzisha Shule yake ya Sekondari, ule utaratibu unaendelea vizuri. Kamati zinasaidia sana katika ujenzi. Lakini mara baada ya shule kuwa zimechukuliwa na Serikali, tunaendelea kupata tatizo la nani aendeshe shule. Shule inatakiwa isimamiwe na Kamati ama na Bodi. Nilikuwa napenda kupata maelezo hayo, kwa sababu mimi jimbo langu ni mojawapo, lenye shule nyingi za namna hiyo na shule nyingi zimeendelea kuwa chini ya Kamati, kiasi ambacho tunaendelea kupata matatizo. Napenda tupate ufafanuzi, nini ambacho kifanyike?

Lakini la pili, nalo pia Mheshimiwa Waziri anisaidie. Naipongeza Serikali kwa utaratibu wa kuongeza walimu, lakini kuna tatizo kubwa la nyumba. Walimu hawawezi kwenda kukaa mahali ambako hakuna nyumba na shule hizi tumezieneza karibu Kata zote nchi nzima. Nilikuwa napenda kufahamu kwamba, tunasaidiwa vipi kuhusu mchango wa wananchi na Serikali kusudi tuweze kupata nyumba ili walimu wetu wapate mahali pa kukaa waweze kufundisha watoto wetu?

**MWENYEKITI:** Napenda kujua Kamati gani inayoendesha shule?

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Kamati zinazohusika na ujenzi wa Shule za Sekondari za Wananchi, zikishakabidhi kwenye Serikali zinapenda ziendelee kung'ang'ania zenyewe kuendesha shule badala ya Bodi. Sasa nilikuwa napenda ufafanuzi tuendeshe hizi shule kwa Bodi au kwa Kamati.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nitoe ufafanuzi kwa hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, kama ifuatavyo:-

Kuhusu Kamati au Bodi, kwa mujibu wa Sheria ile Namba 25 ya mwaka 1978, Shule ya Msingi ndiyo inayoongozwa na Kamati ya Shule, lakini kwa upande wa Shule za Sekondari, zipo chini ya Bodi. Bodi inakuwepo na wakati wa ujenzi kunakuwa na Kamati ya Ujenzi, ambayo inatoa taarifa kwenye Bodi. Kwa hiyo, kazi ya ujenzi ikishaisha basi tena Bodi inaendelea na kazi zake.

La pili, kuhusu nyumba za walimu, kwenye kitabu cha bajeti, tumeonesha kabisa kwamba, mwaka huu wa fedha tutajenga nyumba za walimu 1,000. Kwa kweli ukiangalia nyumba 1,000 na idadi ya shule na hasa baada ya mwamko wa wananchi, si rahisi kufikia mahali popote. Nikatoa wito hapa na mimi ningeomba niendelee kutoa wito kwamba, Mpango wa MMEM na MMES, unategemea sana kwa kiasi kikubwa nguvu za wananchi, tusaidiane Waheshimiwa Wabunge. Tena nawaomba ninyi ndio muwe mstari wa mbele.

Nafurahi sana, nilipokwenda Musoma, Mbunge wa Musoma sijui yuko wapi? Nilikuta amejenga nyumba mbili yeye mwenyewe. Kwa kweli nilifuatilia, kwa fedha yake yeye mwenyewe, nikamsifu sana ingawa sitaki ninyi wote mjenge kwa hela zenu. Lakini ninachosema ni kwamba, muhamasishe. Kwa kweli nimemfurahia sana, nyumba nzuri, walimu wanafurahi, halafu amepanda na miti kuzunguka. Naomba mtusaidie Wabunge, Halmashauri zitenge fedha. Kama tulivyosema, madarasa mawili, nyumba moja na hata ukikisia mimi naomba nitumie nafasi hii Mwenyekiti, mnavyosema kwamba, tuwang'ang'anize walimu waje huko, tunaweza tukawapeleka hata tukawafikisha pale, baada ya siku mbili anakwambia narudia mizigo yangu. Cha maana ni kuweka mazingira ambayo yatakuwa kivutio na hasa kwa sehemu kubwa kama ninayosema ni nyumba. Nawasihi kwa manufaa ya nchi yetu na elimu kwa ujumla, tujenge nyumba za walimu ili walimu wakae wafundishe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – *Teacher Education* … … … .... Sh.9,865,489,500/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi, ingawa inawezekana kwamba na mimi nilishindwa hili niliweke wapi? Lakini nimeona hapa panapohusu mafunzo ya walimu basi niingize hapa na kama nitakuwa sahihi basi nizungumzie kifungu 260800 - *Training expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la kuwa na upungufu wa walimu mashuleni, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, limesababishwa kwanza na uwingi wa shule, kuongezeka kwa shule kwamba tumezijenga nyingi kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, inawezekana kuwa hatukuwa na mipango mizuri tangu mwanzo ya kuwaanda walimu mapema. Hii ndiyo iliyosababisha sasa kuwa na upungufu mkubwa kwenye shule zetu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia Hotuba ya Waziri Mkuu kwa maandishi, niliwahi kuzungumza kwamba, tuna upungufu mkubwa sana wa walimu katika Wilaya ya Mbozi na leo pia kwenye hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nilipochangia kwa maandishi, bado nimeendelea kusisitiza hili. Naomba nitoe takwimu chache, ambazo nilikuwa nimemwandikia Mheshimiwa Waziri kwamba, Mbozi tuna shule 207, lakini walimu waliopo ni 2,225 na mahitaji halisi ni 3,730. Kwa maana hiyo, tuna upungufu wa walimu 1,505. Sasa na hii wengi ambao wameangalia televisheni leo, sisi wa Mbozi tunasema si kwamba tumedhalilishwa, lakini tunashukuru pia walitoa ile picha. Kwa sababu wametoa picha ambayo inaonesha kuna shule ina mwalimu mmoja, Shule ya Namsinde kule Kapele. Sasa hata tukizungumza suala la elimu, tutafundisha watoto kweli, mwalimu mmoja atafundisha watoto wote, kama kuna madarasa yote saba? Ni kitu ambacho hakiwezekani.

Sasa ninachotaka hapa, ninaomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko. Kuna shule karibu tatu ambazo zina mwalimu mmoja au wawili, lakini zina wanafunzi zaidi ya 200 kila shule. Sasa Mheshimiwa Waziri, tunaomba atoe tamko kama ni kumwagiza Afisa Elimu wa Wilaya Mbozi, afaye utaratibu wa kuwahamisha walimu ndani ya Kata zile, kama sio kuwatoa nje. Agizo hilo litekelezwe mara moja ili shule hizo walau ziwe na walimu watatu au wanne ili hao watoto waweze kupata haki ya kufundishwa na kupata elimu ambayo tunaidai. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mimi naomba tu uondoe yale maneno kwamba, mipango sio mizuri. Wewe sema kuna upungufu wa walimu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuelezea kwamba, sio mipango mibaya. Ni kweli na mimi kwanza ningemshukuru, tungekuwa tuna muda mrefu wa kujibu kama walivyozungumza Mawaziri wenzangu waliotangulia, tungewataja majina wote mliochangia kwenye kila hoja. Ni kweli ulichangia Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, ila tu ni kwa sababu ya muda.

Ningependa kukwambia hata mimi mwenyewe, picha hizo nimeziona. Lakini nataka kusema kwamba, cha maana kama ulivyosema, mimi nimesikia, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, amesikia ni suala la kumwagiza *DO* tu aangalie jinsi ya kutoa mahali pengine, walimu awaweke pale. Kwa sababu kuna uzembe kwa kweli, shule kukaa na mwalimu mmoja kwa Shule za Msingi, naamini kabisa wengine wamesharudishwa. Kwanza, taarifa niliyonayo ni kwamba, baada ya zile picha zilizoonekana kwenye *TV*, tayari alishaagizwa achukue hatua. Tunavishukuru vyombo

vya habari, wakati mwingine vinatusaidia kuona vitu vya ajabu sana. Hatua zimeshachukuliwa na shule moja kati ya zile tumeshafanya *satellite,* ni shule ambayo inasaidia tu mahali ambako shule haijaanzishwa. Lakini hata hivyo na zenyewe zinapaswa kuangaliwa kwa sababu watoto wale pia ni Watanzania.

Kuhusu kifungu kile ulichokitaja, umekitaja tu, lakini sio kwamba, sisi tunategemea kufundisha walimu kwa hela hizo. Haya mafunzo unayoyaona, kwa mfano, haya tuliyopeleka sasa hivi shilingi bilioni nane ni tofauti kabisa, hiki kifungu ulichoona zenyewe ziko zinabebwa na Mpango wa MMES.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa nini nimesema hivi? Tulipoanzisha Mpango wa MMEM, watoto wengi walikuwa hawasomi, wakaletwa mara moja kwa wingi. Sasa walimu inachukua muda mrefu kuwafundisha, lakini watoto tuliwakusanya tu ilipotangazwa. Ndiyo nikasema tuseme kuna upungufu wa walimu. Hili ni kweli.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 –Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Elimu**

Kif.1001-*Administration and General* ...... Sh.643,999,000/=
Kif. 1003-*Policy and Planning* … … … … … Sh.13,730,082,100/=
Kif. 2001-*Chief Education Office* … … … … … Sh.2,040,000,000/=
Kif. 2002-*Inspectorate* … … … … … … … …Sh. 200,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001-*Basic Education* … ... … … … Sh. 30,794,631,000/=

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Fungu 46, kifungu 3001 - *Basic Education,* kifungu kidogo 4321. Nilichangia suala langu moja zaidi ya mara mbili, nakumbuka kwenye Bajeti ya Wizara ya Fedha sikujibiwa, nikajua imepelekwa mbele kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi nitajibiwa.

Lakini leo kwa kuona ili Mheshimiwa Waziri asije kusahau, kwa sababu ilikuwa ni nyuma kidogo, nikaamua kuchangia tena, lakini naona pia bado sijapata majibu. Kwanza, ningependa kujua hizi shilingi 27,226,493,600 zimetengwa hapa kwa ajili ya kitu gani, ninaomba ufafanuzi wa hizi pesa, zitatumika kwa ajili kitu gani?

Swali langu la pili ambalo nahitaji ufafanuzi, nilichangia sana kuhusu usafiri kwa wanafunzi hasa wa Mkoa wa Dar es Salaam. Wanafunzi wanapata matatizo ya kwenda shule, wananyanyaswa sana na makondakta wa mabasi ya watu binafsi na nilishazungumza wakati nachangia nilisema, sasa naiomba Serikali tuachane na mabasi

haya, kwa sababu wapo katika biashara na ni wakati wa biashara huria, wafanye biashara yao. Tuwaache wamiliki wa mabasi haya wafanye biashara zao. Lakini kama Serikali, ninaomba mtengeneze mpango mzuri wa kuweka mabasi ya wanafunzi, ambayo yatakuwa yanawasaidia wanafunzi hawa kufika shuleni mapema na pia kurudi majumbani mapema. Hii itawasaidia sana kama Serikali mtaamua kufanya hivyo.

Sasa swali langu ni kwamba, katika hizi shilingi bilioni 27 zilizoko hapa, je na mradi wa mabasi ya wanafunzi uko hapa ama haupo, kama haupo naomba majibu Mheshimiwa Waziri, uniambie hizo pesa ziko wapi au unafikiria nini. Ukizingatia kuwa Mheshimiwa Waziri ni mwanamke, najua una uchungu sana na watoto, ukizingatia wewe ni mama na una watoto nyumbani. Naomba utoe majibu ambayo yatawafurahisha wazazi wasiokuwa na uwezo wa kununua magari yao binafsi na kuwapeleka watoto shuleni na utoe majibu mazuri yatakayo waridhisha wanafunzi, ambao wanapata adha ya usafiri, ambao labda wanatuangalia sasa hivi kupitia katika *TV* ama watasoma kesho katika magazeti. Naomba ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nifafanue hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ameuliza hizi shilingi bilioni 27 zote ni za nini? Nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hapa ndiyo Mpango wa MMEM. MMEM ndiyo iko hapa na ukishasema Mpango wa MMEM, humo ndani ndiyo kuna *Capitation Grant. Capitation Grant* ndiyo zile fedha tunazopeleka za kununulia vifaa kama vitabu na kadhalika na humo humo ndani kila Mpango kwa mfano wa MMEM, pia kunakuwa na Mpango wa Kushughulikia suala la UKIMWI.

Halafu kama nilivyozungumza, kwenye kujibu hoja za Wabunge, kwenye upande wa ukaguzi wa shule za msingi, pia umo humu kwenye kifungu hiki. Kwa hiyo, hiki kifungu ndicho kinachoitwa MMEM kama nilivyosema.

Kutokana na swali lake alilouliza leo, nilipotoa shukrani mimi kwamba, tunawashukuru *DANIDA*, akasema ninyi mmeshukuru wahisani wengi, kwa nini msinyofoe fedha nyingine mpeleke kwenye usafiri wa wanafunzi. Namjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, wafadhili wanatoa kwa vitu maalum. Kwa hiyo, kwa mfano *SIDA,* atoe fedha kwa ajili ya kusaidia *ICT,* kwa upande wa vyuo vya ualimu, sasa wewe ukapeleka kwenye Mradi wa Magari Dar es Salaam, si watakushangaa. Kwa hiyo, wale wafadhili wote uliowaona kwenye kitabu hiki cha bajeti, wana malengo maalum pamoja na kwamba, mimi nina uchungu sasa na wale watoto kusema kweli. Nakuta watoto wameloana lakini nasikitika sana na mimi kama Waziri ninayesimamia Sera ya Elimu, ufikaji wa wanafunzi shuleni na mimi pia linanihusu.

Lakini ni suala ambalo linabebwa na TAMISEMI na Miundombinu. Mheshimiwa Peter Pinda yuko hapa, ana mikakati yake naye ya kushughulikia suala hilo pamoja na kwamba, mimi nina uchungu sana. Labda atanikaribisha tu kwenye kumpa mawazo, lakini ni suala la TAMISEMI na Miundombinu. Mheshimiwa Basil P. Mramba, anafurahi kwamba, suala lake limeguswa halafu pia na *SUMATRA*. Lakini mimi

nawatakia kila la kheri, mipango yoyote mizuri watakayoiweka ya kusaidia usafiri wa wanafunzi Dar es Salaam, nitaufurahia sana kwa sababu tutafanikisha Sera ya Elimu. Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia umenisaidia, natoa wito kwa wananchi kwa ujumla kwamba, wazazi wajaribu kadri iwezekanavyo, kupeleka watoto kwenye shule karibu na mahali wanakoishi, itasaidia sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, japo amesema kwamba, suala hili ni la TAMISEMI na Miundombinu. Mimi nimeona kwamba, hapa ni wakati muafaka kwa sababu linahusiana na wanafunzi kwenda shule na ndiyo maana nikalileta kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Labda kwa sababu wenyewe TAMISEMI wapo, Miundombinu wapo, wanipe tu tamko kwamba, wana mpango au wana mkakati gain? Kama si Wizara hii, sawa. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, wazazi wapeleke watoto katika shule ambazo ziko karibu. Tukumbuke kwamba, Dar es Salaam ina wakazi wengi sana, hata ukisema uwapeleke karibu, bado watakuwa hawatoshi. Kwa hiyo, tatizo litaendelea kuwepo palepale, hata ukisema uwapeleke wapi, nafasi ya kujenga hakuna, maeneo yamikwisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tafadhali naomba majibu ambayo yataniridhisha.

**MWENYEKTI:** Kwa suala hilo kuhusu usafiri, umesema kuna Wizara zinazohusika na Wizara katika Serikali, wanashirikiana katika kufanya kazi. Maana huyu akianza kupanga na mabasi, asomeshe na watoto, kwa uhakika haitawezekana. Kwa hiyo, nashauri kwamba, suala hili, Wizara zinazohusika zimesikia, lakini nina uhakika hawawezi kujibu sasa hivi. Wamesikia na hii ni mara ya pili

**MHE. ADAM K. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu nilitaka ufafanuzi kidogo, kuhusu mfumo huu wa mgao wa hizi shilingi bilioni 27. Nilikuwa napitia hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri na naomba niseme kabisa kwamba, ...

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. ADAM K. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeghafilika nisamehe. *Vote 46*, kifungu 3001 - *Basic Education, 4321 - Primary Education Program Support.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba, nilikuwa nimepitia kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri, kwenye kifungu hiki cha elimu ya msingi na kabla sijasema shida yangu, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri. Mimi binafsi na nina mategemeo makubwa sana kuhusu mambo yanayokuja huko mbele ya safari. Lakini ninaomba kuuliza kwamba, mgao huu wa shilingi bilioni 27, nimeona kuna masuala ya madawati, madarasa na kadhalika. Sasa nirejee aliposema Mheshimiwa Godfrey W. Zambi kwamba, mbali ya kuwa na tatizo la walimu, kuna matatizo pia ya madarasa na madawati, ambayo hayako sawa katika uwiano katika hilo. Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kunihakikishia kwamba, Wilaya ambazo zina matatizo kama Mkuranga

na Wilaya nyingine zenye uchache wa madarasa, zitapata *priority* katika *allocation* ya hizo shilingi bilioni 27? Ni hilo tu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu kilichoandikwa hapo cha 4321, kama nilivyosema ndicho kinashughulikia ugawaji wa fedha, kwa utaratibu wa *Capitation Grant* kusaidia vitabu, madawati na kadhalika. Lakini naomba kurudia tena, hiki kinachopatikana hakitoshi, ni wazi kabisa hakitoshi. Kwa hiyo, kama nilivyosema, tunategemea sana msukumo na mwamko wa wananchi na kupitia Halmashauri zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ningekuomba, huko uliko kama Diwani, tusaidiane tuone jinsi ya kuchangia madawati kwa sababu hata tukikupa hizi hazitatosha. Lakini la pili ambalo mimi naona ni jambo la kukufurahisha kukwambia wewe katika hatua hii ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Rais kwamba, katika kugawa fedha, tuwe tunazingatia maeneo ambayo kwa kweli yako nyuma sana kwenye maendeleo, ukiwemo Mkoa wa Pwani, naamini mtapata zaidi kidogo.

*(Kifungu kichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Chief Education Officer* … … … … … Sh. 2,040,000,000/=

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Kiti. Nilikuwa nafuatilia hiki kitabu naona tulikuwa tupo kwenye kifungu 4001, *Secondary Education.* Lakini Katibu kama nimemfuatilia, naona ametamka kifungu 2001, sasa sijakiona hapa sijui ni kifungu gani?

**MWENYEKITI:** Hebu eleza vizuri Ndugu Charles M. Kajege.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siitwi Mheshimiwa Charles M. Kajege, naitwa Mheshimiwa Juma H. Killimbah. Nimeeleza kwamba, nikifuatilia ule mtiririko tulipotoka katika hili kifungu 3001, kilikuwa kinafuatia kifungu 4001, ukurasa wa 52, Elimu ya Sekondari. Sasa Katibu alisema kifungu 2001.

**MWENYEKITI:** Sawa upo sahihi, Katibu soma tena.

Kif. 4001 - *Secondary Education* … … … … … Sh. 57,705,000,000/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu 46, *subvote* 4001, kifungu kidogo 4390 - *Secondary Education Development Program (SEDP)*. Kwa mwaka uliopita, najua kwamba, kulikuwa na fedha kidogo sana kwa ajili ya Mpango huu. Lakini kuna mafungu machache yalitolewa kwenye shule zinazojengwa, kuwasaidia wananchi kumaliza majengo yao. Katika Wilaya ya Ludewa, kulikuwa na shule kadhaa mojawapo ni shule inayoitwa Kayao na hili nimelitoa kwa maandishi kwenye mchango wangu. Fedha zake ambazo tulipata maelezo kwamba, zinakuja shilingi milioni 24.6, tulipofuatatilia tuliambiwa kumbe zilikosewa zilikwenda Njombe *NMB* na tulipofuatilia zaidi, tukaambiwa zimerudishwa Wizarani.

Kwa hiyo, mwaka 2005 mzima, tulikuwa tunafuatilia hizo hatukuzipata. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi, je, kwa mwaka huu sasa kwenye kifungu hiki, naona kuna fedha, hizo hela tutazipata kwa ajili ya shule hii na kama jibu ni ndiyo ni lini tutazipata tumalizie shule yetu? Asante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampa pole Mheshimiwa Mbunge, kwa usumbufu alioupata. Lakini pia ni kwamba, hizi fedha zinazotoka sasa hivi, ndiyo zile ambazo zilitakiwa zitoke Julai, 2005. Lakini hata hivyo, tutahakikisha kwamba, tunalifuatilia hili suala, tuone lilikwamia wapi na pia namkaribisha ofisini, tuongee tuone kwa undani. Lakini hata ukikosa nafasi, pia tunaweza kulifanyia kazi tukakuleta jawabu. Fedha za MMES kwa kawaida tunapeleka Mikoani na Wilayani, hasa Mikoani, ambako mnakaa wenyewe, mnaamua kwamba, Wilaya hii ipate nini na shule gani ipate, kutokana na matatizo ya maeneo husika. Hata hivyo, tutalifuatilia suala hili.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote 46, subvote 4001,* kipengele kidogo 4301 - *Construction of Labs and Supply of Equipment.* Wakati ninachangia asubuhi, nilisema huu Mpango ulioainishwa humu, hii bajeti ni nzuri sana, lakini itatekelezeka tu kama kutakuwa na fedha zilizotengwa na tukaendelea kuzungumza kwa kujua kwamba, sasa hivi Wizara ya Elimu inajiandaa kupokea watoto ambao wanatoka kwenye Mpango wa MMEM.

Kwa kujua kwamba, mwaka 2005 waliofaulu walikuwa ni wengi sana, ikabidi madarasa yaongezwe mwaka huu na kwa kujua kwamba, mwaka ujao, kwa maana ya watakaomaliza Desemba watakuwa ni wengi zaidi katika kujenga shule, sio madarasa tu, ni pamoja na maabara. Nikaonesha *my concern* kwamba, sasa hivi katika mashule wanafundisha sayansi kwa nadharia tu na mitihani wanafanya *alternative to practical*. Hebu kati yetu nani aliwahi kufanya *alternative to practical?*

Kama kweli tunataka kujenga na kuimarisha sayansi na teknolojia katika Tanzania, lazima tuwe *serious on this issue*. Nimesikitika kuona kwenye kipengele hicho hakuna hata senti moja, iliyotengwa kwa ajili ya kujenga maabara wala ku-*supply lab equipment*. Ina maana kwamba, tutaendelea kutengeneza wanasayansi, ambao wataendelea kujenga maghorofa yanayobomoka. Naomba maelekezo kwa nini hakuna hata senti moja hapa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, anafahamu vitu vingi sana, kwa sababu alikuwa *Headmistress,* nashukuru anatoa michango mizuri sana. Ningependa tu kukufahamisha au kutoa ufafanuzi kwamba, ile sehemu ambayo umeona 00, tulikuwa na mradi ulikuwa unaitwa *Education Two,* ambao umekwisha. Hata kwenye maelezo yangu katika maswali yaliyokuwa yanatolewa hapa Bungeni, nilijibu kwamba, tunaongea nao na inaonekana tunaweza kufanikiwa, tuwe na mradi wa tatu, *I mean, Education Project Three,* ambao watatupa fedha za kutosha kujenga maabara 40.

Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi hapo, kutokana na hiyo *Project Three* ambayo itasaidiwa na *Project* ya *ADB,* yaani *African Development Bank*, maabara 50 na tumefikia mazungumzo na hatua nzuri tu. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi hapo. Ni *project* ilikuwa ya *ADB*, lakini zile za maabara 40 zitatoka kwenye huo Mpango wa *SEDEP* na tumesema sisi kwamba, ili kurahisisha mgao tumesema zitakuwa maabara 42.

Lakini tunajua hata tukipata maabara 50 na tukipata maabara 40 zinakuwa 90, hazitoshi kwa sababu ya mfumko wa shule. Mimi bado narudi palepale, tunaomba Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane na kwenye suala hili, maabara ni za msingi sana na kwa kuwa tutapeleka Mikoani, tumesema kwamba, kila mkoa maabara mbili. Tunaomba hata kama inawezekana, mpeleke mahali ambako angalau shule nyingine ziko karibu na nyingine ambapo hata mwanafunzi wa shule nyingine, anaweza kufanyia mazoezi pale kwa utaratibu utakaowekwa vizuri.

Lakini bado tunarudi palepale, nilishauri katika Bunge hili hili na ningeomba nirudie ushauri huo huo kwamba, hawa *Tanzania Education Authority*, wanasaidia sana. Nimepata ushahidi mwingi sana, ujenzi wa maabara na hata vifaa. Wao labda wanaweza kuudhi kwa sababu wana taratibu zao, lakini ukizikamilisha wanasaidia sana. Pia naomba hebu tutumie hii Mifuko ya *TASAF*, wanasaidia sana katika masuala hayo.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wasiwasi wangu au nasemea sana suala la elimu, kwa sababu najua na wote tumekubaliana kwamba, *our priority number one* ni elimu. Sasa hivi hata ukiangalia kwenye bajeti yote ya maendeleo ambayo ni shilingi bilioni 105, wakati mwaka 2005 ilikuwa ni shilingi bilioni 109, hiyo ni moja. Lakini katika shilingi bilioni 105, shilingi bilioni 95 kitu ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, uwe *careful,* kama unazungumzia kifungu hiki usianze *debate*. Hiki cha maabara hakina fedha, fedha ziko kwenye *SEDEP* pale chini.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hicho hicho ninachokizungumzia

**MWENYEKITI:** Basi usianze *debate*

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Ninachozungumza ni kwamba, ukiangalia hizo hela zote, shilingi bilioni 94 zinategemewa kutoka kwa wafadhili, shilingi bilioni 11 ndiyo zinategemewa kutoka hapa. Nazungumzia *total budget*. Sasa kama Mheshimiwa Waziri, amenijibu kwamba, wanategemea wafadhili wakipata fedha ndiyo wajenge hizo maabara, je, zisipopatikana hizo fedha?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa ya pili ya hoja iliyoongezwa na Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine siyo vizuri kurudia sana lakini wakati mwingine pengine inabidi. Nilisema kwamba, hata kwenye taarifa zetu zilizomo kwenye kitabu cha bajeti, Mpango wa MMEM na MMES ni endelevu na kuita endelevu maana yake ni kwamba, tunajiandaa ili tujitegemee sisi wenyewe. Mimi ningeomba tulichukulie hivyo. Ukiangalia tena kwenye kitabu hicho hicho, tumewashukuru wananchi kwa nguvu, kutokana na mwamko, basi tunaomba hizo nguvu ziendelee.

Amesema kwamba watoto wanafanya mitihani kwa *alternative to practical*. Mimi naomba tuendelee kusaidiana kufanya kazi ili Mipango ya MMEM na MMES, iwe endelevu kwa kujitegemea sisi wenyewe. Niseme tu kwamba, kwenye kitabu ukiangalia kwenye changamoto, tumeweka wazi kabisa na tumesema kwamba, ya kwanza kuna pengo na pengo hili linatokana na mahitaji ni makubwa sana katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuangalia jinsi ambavyo tutapata fedha zaidi ili elimu iweze kutolewa vizuri. Kwa hiyo, naomba uvute subira tu lakini zaidi ya yote, tuendelee kuwahamasisha wananchi ili tufanikishe Mipango ya MMEM na MMES.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Subvote 4001*, kifungu kidogo 4390 - *SEDEP*. Kwanza, nataka kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa maamuzi muhimu ambayo anasema atateremsha hatua kwa hatua, utawala wa *secondary school* kwa Halmashauri. Natumaini hilo ni jambo zuri. Pia atatuletea katika Halmashauri mtu mmoja au wawili, ambao watakuwa kiungo cha Halmashauri na Wizara. Hayo ni mambo mazuri. Lakini labda kwa sababu hizi fedha za MMES, zinakwenda kwa shule zetu ambazo ni *community schools,* isingekuwa vizuri kama pia Waziri, unapopeleka hizi fedha Mikoani na Wabunge pia utuarifu ili tuweze kufuatilia kwa urahisi zaidi, hizi fedha zinakwenda wapi, hilo la kwanza.

La pili ni jambo ambalo kwa kusema kweli mimi linanikera, nimeona shule zangu kama mbili, tatu; Shule ya sekondari Nkoma nimekuta kuna darasa moja la MMES, hilo darasa la MMES limejengwa eti naambiwa kwa amri, hiyo michoro ya *World Bank* liwe na madirisha upande mmoja tu, upande mwingine matofali tupu na juu kama watoto wafungwa ndiyo kuna vidirisha viwili. Hii ni michoro ya wapi? Sisi wote tumesoma, tunajua kwamba kama kweli utataka ku-*concentrate,* lazima kuwe na *cross ventilation.* Sasa huu utaratibu wa kuwa hakuna dirisha upande mmoja ni *World Bank* gani hiyo, ambayo inatuletea michoro ya namna hii? Mimi ningeshauri kabisa kwamba, hili lingefutwa mara mmoja, tupate shule kama ulivyosema zilizo bora.

Lakini mwisho, majibu uliyotoa kwa leo, kuna moja ambalo lazima Serikali ilichukue. Hatujawa na mpango mahususi kabisa wa kutatua matatizo mengi kwenye elimu na kuna jambo moja tu, tuweke pesa kwenye elimu tutatatua mateso. Huyu mama utampatia kifua kikuu bure. Asante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupata taarifa za mgao wa MMES, nakuhakikishia au nalihakikishia

Bunge hili kwamba, fedha yoyote itakayotolewa kwa Mikoa yote, itawekwa wazi na kila Mbunge atapata nakala. Hata mgao wa MEMKWA, ambao unatupa shida sana, hela zitakazopelekwa kwenye Halmashauri zote, zitawekwa wazi ili mtusaidie. (*Makofi*)

Kwanza nakushukuru kwa ushauri na kuweka kila kitu wazi. La pili, lilikuwa ni madirisha. Kweli mimi nimekwenda Shinyanga nimekuta yale majengo halafu sasa wale wahandisi baada ya kuona lile jengo lililoporomoka pale Keko, walikataa kubadilisha, kwa sababu Kamati ya Ujenzi iliwashauri kushusha madirisha, kweli madirisha yako juu, wahandisi wakasema hapana. Lakini nasema hivi, ile ramani kosa lililotokea ni kwamba, hawakuandika pale chini. Ile ramani ilikuwa iende kwenye maeneo ya baridi, kama vile Lushoto, Mufindi na kwenye maeneo ya upepo mkali, bahati mbaya wakachukua Shinyanga. Tumeongea na wale wa upande wa michoro, leo hii asubuhi tulikuwa tunaongea na Mkuu wa Idara, wamesema wamerekebisha na naamini kabisa, wameweka kwenye maonesho pale nje. Tuwieni radhi, lakini tumeshabadilisha. Karibuni mchukue mchoro hiyo tunatoa bure tu. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nitazungumzia Fungu 46, kifungu 4001 - Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu hiki cha Fungu la Maendeleo, mimi sikuchangia kwa kuzungumza, nilichangia kwa maandishi na wakati nikichangia, nilieleza hali halisi hasa kuhusiana na fedha za Wafadhili. Fedha za Wafadhili ni fedha muhimu sana, ambazo tunatumia katika kuendeleza maendeleo hasa ya shule zetu za Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu, nilieleza kuhusiana na shule ya Sekondari ya Kizaga, iliyopata fedha za ufadhili kiasi cha shilingi milioni 36, ikiwa ni msaada kutoka kwa Wajapani, kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya watoto wa kike. Pili, ikapata shilingi laki tano za Kitanzania, tena hizi pesa zilitolewa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu. Pesa hizi zilikuwa ni kwa ajili ya kununua *screen,* kwa ajili ya maonesho mbalimbali na mambo mbalimbali kwa ajili ya mafunzo hapo shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, hivi ninavyoongea, wakati nachangia nimeeleza bayana, hali halisi juu ya pesa zile. Pesa zile kwa kutumia mamlaka, Mkuu wa Shule alizitafuna na zile pesa zimepotea, wananchi wanalalamika. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri katika majibu yake, anieleze ni hatua zipi zilizochukuliwa kuhusiana na huyo Mkuu wa Shule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi, mwizi yule ametoka amekaa pembeni, kaanzisha shule ya sekondari ya kwake binafsi na anaendelea sasa hivi anataka kuisajili kupitia Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri, angenieleza basi kwa sababu wananchi wa Jimbo langu la Iramba Magharibi, walikuwa wanategemea wasikie shule yao ambayo wamekuwa wakijitolea na wamekuwa

wakihakikisha kwamba, wanaiendeleza ili wapate Shule ya Sekondari, waweze kufanya maendeleo zaidi.

Lakini, leo anakuja mwizi mmoja tu, anaamua anafanya uhalifu shuleni, anaachwa na bado anaendelea kukaa ndani ya nyumba zilizojengwa mikononi mwa wapiga kura wangu. Jambo hili linanigusa sana. Kwa hiyo, ninaomba hili, Mheshimiwa Waziri, anipe ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilizungumzia kuhusiana na Shule za Sekondari za Kizaga, Ndaga, Shelui na Kisiriri, nikasema sisi tuna umeme wa gridi, nilieleza matatizo ya barabara huko unapita pale. Sasa nikasema zipate tu hata umeme hizo shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya hayo, tunazo tena shule nyingine ziko katika Manispaa ya Singida; Shule ya Unyamikumbi, Shule ya Mtipa, Shule ya Mugumaji, nazo vile vile zipate basi hata umeme tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nategemea katika majibu yake, Mheshimiwa Waziri, angenijibu na ili anieleze kwa udhati zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, nilielezea kuhusiana na shule ya Sekondari ya Tumaini. Shule ya Sekondari ya Tumaini ni ya muda mrefu sana na katika miaka ya nyuma, ilikubaliwa iwe *High School*. Hiyo mipango ilikubaliwa na Wizara hiyo hiyo yetu ya Elimu.

Lakini mipango hiyo mpaka sasa walimu wa *High School* hawapo, bado tunaendelea na *Ordinary Level* pale Tumaini. Sasa, yote haya nilitegemea katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri, ningepata majibu ili sasa na wananchi wa Jimbo langu la Iramba Magharibi, wajue kwamba wao wako katika mpango gani katika suala hili la maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, uwe *very brief.*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nimjibu Mheshimiwa Juma H. Killimbah, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu suala la mwizi anavyojulikana kwamba ni mwizi, naomba nilichukue suala hili tulifanyie kazi. Tutatuma *Auditors* kule kwenda kufanya kazi, lakini pia hapo hapo na Bodi iwe macho. Natoa wito kwa Bodi za Shule za Sekondari, hawezi kuwa mtu anaiba hela wakati Bodi za Shule zipo. Bodi ziwe kali, ndio wenyewe wangekuwa wa kwanza kufunga safari kuja hata Wizara ya Elimu kushtaki vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Bodi za Shule zetu za Sekondari, wawe makini katika ufuatiliaji wa masuala ya shule, lakini tumelichukua, tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme, tulikuwa tumependekeza kwamba, waende kuomba kwa Meneja wa *TANESCO*, tena hata Mheshimiwa Mbunge angesaidia kidogo kwenda kwa Meneja wa *TANESCO* pale akasaidia ku-*connect*. Mengine yote haya ni ya kuyafanyiwa kazi, tumeyapokea. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka *Vote No. 46,* kifungu 4001, kifungu kidogo 4390, *SEDEP*.

Katika maelezo yangu ya maandishi, nilikuwa nimeeleza suala la MMES kwamba, Mpango huu wa MMES ulipokuwa *introduced* kwenye Bunge liliopita na Mheshimiwa Joseph J. Mungai, moja ya maudhui ambayo walitushawishi sana ni kwamba, sisi ambao tuko nyuma kielimu, Singida ikiwa mojawapo, mpango huu pia unakusudia kujenga shule mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo tulivyoelezwa na hivyo ndivyo tunavyotazamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha hizi ambazo zimewekwa hapa, shilingi bilioni 57, je, Singida tutapata hiyo shule mpya kwa kuzingatia kwamba, sisi tuna shule moja ya Sekondari ya Mwenge na hiyo shule ilikuwa ya Misheni na tayari Misheni sasa wanaiomba hiyo shule irudi kwao ili wafungue Chuo Kikuu. Maana yake Shule ya Sekondari ya Serikali itakuwa hauna ukiacha hizi shule za wananchi.

Je, sisi tutafikiriwa kupata sekondari mpya katika shilingi bilioni 57 au namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nifafanue hoja za Mheshimiwa Mohamed H. Missanga kama ifuatvyo:-

Ni kweli kama nilivyosema mwanzo kwamba, iko mikoa ambayo iko nyuma na katika mgawo wa fedha za MMES wao pia wamepata upendeleo maalum na Mkoa wa Singida umo. Kwa hiyo, wataamua jinsi ya kuzitumia hizo hela. Mikoa mingine ni Tabora, Rukwa, Lindi, Mtwara, Pwani na Shinyanga kama nilivyosema.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 – *Teacher Education* … … … … Sh.572,920,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2006/2007, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa, Waheshimiwa Wabunge, naomba tulizingatie suala moja ambalo nadhani kwa muda mrefu tulikuwa hatulifuati vizuri. Kanuni 49(a) Kifungu kidogo cha (b): "Waziri anayetoa hoja au anayehitimisha hoja yake, ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 60."

Sasa tumekuwa tunafanya makosa kwamba, tunamjumuisha Naibu Waziri wa Wizara hiyo kama yeye ndiye mtoa hoja.

Kwa hiyo, dakika 60 badala ya kuwa yule mtoa hoja, tunampa Naibu Waziri na Naibu Waziri,wanagawana dakika 60. Kwa tafsiri sahihi ya kifungu hiki, tulikuwa tunafanya makosa. Dakika 60 zinatakiwa mtoa hoja mwenyewe.

Kwa hiyo, Naibu Mawaziri wanakuwa wachangiaji kama Wabunge wengine. Kwa hiyo, tumefanya makosa kwa kipindi chote kutafsiri hiki kifungu. *(Makofi)*

Kuanzia Bunge la kesho pamoja na Naibu Mawaziri, yule mtoa hoja atapewa saa yake, dakika 60. Nadhani tumeelewana. Kifungu 49(a), kifungu kidogo (b), tumekuwa tunachukua dakika 60, tunawagawia Naibu Mawaziri wote. Matokeo Waziri anayehusika

anabakiwa na dakika, kama leo, sijui nusu saa. Kifungu kinasema mtoa hoja na mtoa hoja ni mmoja, hata kama ana wasaidizi wake wengi.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, napenda kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.42 usiku, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 21 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*